**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Ishirini na Saba – Tarehe 21 Julai, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007.

**MHE. MARTHA M. MLATA – (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII):**

Maoni ya Kamati ya Huduma za Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara Hiyo kwa Mwaka 2006/2007.

**SPIKA:** Ahsanteni sana. Napenda nichukue nafasi hii, kuwapongeza Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu kwa sababu wanaendeleza ule Utamaduni mpya wa kuondoa ukiritimba. Siyo kila mara mtu kujitokeza wewe tu, ilimradi umepewa cheo basi wewe tu. Nashukuru sana. (*Makofi*)

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI:**

Maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, Pamoja na Maoni Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2006/2007.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaingia kwenye Maswali na Majibu kuna matangazo mawili tu Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji anaye mgeni hapo kwenye

*gallery* upande wa kulia nadhani ambaye ni Dr. Said Ghalib Bilali mshauri wa Elimu katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amani, Zanzibar. Yule pale anapunga mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Waziri Elimu ya Juu, Sayansi na teknolojia Mheshimiwa Kabaka anao wageni wake ambaye ni mdogo wake Veneranda Sagala na binti yake ambaye anakuja kujifunza kidogo mambo haya. Anaitwa Patricia Robi Kabaka. (*Makofi*)

Hawa wanafunzi huku sijaambiwa ni wa shule gani lakini labda baada ya maswali nitaweza kuwatambulisha. (*Makofi*)

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 251

### Mafao ya Wafanyakazi Waliopunguzwa Kazi

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID** aliuliza:-

Kwa kuwa wafanyakazi wengi waliokuwa wakitumikia Chama Tawala, wakati wa mfumo wa chama kimoja walipunguzwa kazi na wengine walikwenda kufanya kazi katika sekta nyingine wakati mfumo wa vyama vingi ulipokubaliwa hapa nchini:-

(a) Je, kwa wale wafanyakazi ambao hawakuendelea kufanyakazi mahali popote na walistahili kulipwa mafao yao ni wangapi kati ya hao walipata haki zao na ni wangapi mpaka leo hawajalipwa?

(b)Kwa wale ambao malipo yao hayajamalizika kulipwa. Je, ni lini Serikali itawakamilishia malipo yao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Mbunge wa Kwamtimpura, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa ni kweli Chama cha Mapinduzi (CCM), kilikuwa na wafanyakazi wengi wakati wa Mfumo wa Chama kimoja cha Siasa. Baada ya kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa, mwezi Julai, 1992 baadhi yao waliopunguzwa kazi katika utumishi wa chama hicho. Wote waliokabidhiwa barua zao za kujulishwa kuhusu hatua ya kukoma utumishi katika CCM, walilipwa mafao yao yote. Malipo hayo kwa wahusika, yalilipwa kupitia Shirika la Bima la Taifa ambao kwa wakati huo walikuwa ndio wanahifadhi fedha za mafao ya viongozi na watumishi wote wa CCM.

(b)Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba kumbukumbu zilizopo zinaonyesha kuwa hakuna watumishi

waliopunguzwa kazi wakati wa zoezi hilo, ambalo walistahili kulipwa na hawakulipwa mafao yao kabisa au walilipwa sehemu tu ya stahili ya mafao hayo. Kama yapo malalamiko, nitaomba nipatiwe majina ya waliohusika au yawasilishwe kwa Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi (CCM).

Na. 252

**Uchafuzi wa Mazingira unaosababishwa na Abiria wa Mabasi**

**MHE. JAKSON M. MAKWETTA** alijibu:-

Kwa kuwa, kuna tabia ya wasafiri katika mabasi kutupa makaratasi, chupa za maji, mifuko ya Rambo, maganda ya miwa na matunda kwenye barabara wanaposafiri na kwa kuwa tabia hiyo husababisha barabara zote nchini kujaa takataka sana:-

(a) Je, kwa nini Serikali isizuie wenye mabasi kuruhusu abiria kutupa takataka ovyo barabarani badala yake wawe na mapipa ya takataka ndani ya mabasi?

(b) Je, kwa nini Serikali badala ya kuajiri wafyeka majani kandokando ya barabara isiajiri watu wa kuokota takataka hizo kandokando ya barabara tu?

(c) Je, kwa nini Serikali isiwe na Juma la usafi ambapo watu wote watasafisha miji na vijiji vyao na vyombo vya habari vitumike kuelimisha umma?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA** alijibu:-

Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jackson Makweta, Mbunge wa Njombe Kaskazini na kaka yangu lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa mujibu wa Kanuni za Afya na Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 si ruksa kwa mtu yoyote kufanya kitendo chochote kinachotishia afya ya jamii na usafi wa mazingira. Halmashauri za Serikali za Mitaa, zimepewa mamlaka ya kutunga sheria ndogo na nyingi zimetunga sheria hizo zinazozuia uchafuzi wa mazingira.

Kifungu cha 114 cha Sheria ya Mazingira, kinawataka wafanyabiashara ikiwa ni pamoja na wenye vyombo vya usafiri kuweka vyombo vya kuhifadhia taka za aina mbalimbali. Aidha Mamlaka ya udhibiti wa usafiri wa nchi kavu na majini (*SUMATRA*) imetoa maelekezo yenye nguvu ya kisheria kwa vyombo vya usafirishaji katika kulinda na kutunza mazingira. Kuzingatia maelekezo hayo kunaweza kukapelekea wenye vyombo vya usafirishaji kukosa leseni.

(b) Mheshimiwa Spika, kazi za kuokota takataka na kufyeka majani kandokando ya barabara zote zinaweza zikafanywa kwa pamoja zote ni muhimu kwani zinasaidia

kuweka mazingira katika hali ya usafi na zinapunguza ajali. Wakuu wa Wilaya, wanatakiwa wasimamie Halmashauri zao katika utunzaji na uhifadhi ya mazingira ikiwa ni pamoja na usafi na uzuri wa mandhari wa Wilaya zao na Miji iliyomo katika Wilaya hizo.

(c) Mheshimiwa Spika, kila mwaka Tanzania hujumuika na nchi nyingine duniani kuadhimisha siku ya mazingira Duniani. Maadhimisho hayo huchukua wiki moja na kuhitimishwa tarehe 5 ya Juni ya kila mwaka. Wilaya, Majiji, Manispaa, Miji na Vijiji nchini, hutakiwa kufanya shughuli za kusafisha, kutunza na kuhifadhi mazingira. Kama ambavyo tunasisitiza tunaposherehekea wiki hiyo, kila wiki katika mwaka ni wiki ya mazingira na kila iwe siku iwe ni siku ya mazingira. Tuyatunze mazingira ili yatutunze kama tunavyosema mazingira ni uhai.

Mheshimiwa Spika, aidha nampongeza Mheshimiwa Jakson Makwetta, daima amekuwa mstari wa mbele katika kutoa mawazo na msukumo katika suala la mazingira tunamshukuru sana.(*Makofi*)

**MHE. HAROUB SAID MASOUD**: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa yeye mwenyewe ametamka kuna siku ya mazingira duniani je, haoni kwamba iko haja sasa ya kuzishindanisha Halmashauri au Wilaya ili siku ya sherehe kuwe na Wilaya maalum ambao inashinda kwa usafi wa mazingira ili ipewe zawadi Maalum kwa mfano kama Wilaya ya Moshi? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Halmashauri zote nchini hushindanishwa kwa maana ya usafi wa mazingira. Vile vile miji yote nchini hushindanishwa kwa maana usafi na hifadhi wa mazingira. Zawadi ya mshindi hutolewa siku ya mazingira duniani tarehe 5 Mwezi June. (*Makofi*)

**MHE. HASNAIN GULAMABBASI DEWJI:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kuweka kiwanda cha *recycle* cha *plastic* ili chupa zinazotupwa ovyo ovyo ziweze kutumika tena? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, kuna viwanda zaidi ya vitano nchini ambavyo pamoja na kutengeneza bidhaa za *plastic* za kawaida hufanya shughuli za kurejeresha na kutengeneza upya takataka za *plastic* hasa chupa au takataka ngumu za *plastic*. Kwa hiyo, hili jambo linafanyika na katika mkakati ambao tumeweka tulichosisitiza kwa kweli katika kupiga marufuku ni hii mifuko ya *plastic* laini ambayo hata kurejeresha inakuwa kazi ngumu. Kwa hiyo, hivyo viwanda vipo mojawapo ni kile kiwanda cha *Morogoro Plastic*. Ahsante. (*Makofi*)

Na. 253

**Kituo cha Utafiti wa Mifugo Mpwapwa**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:

Kwa kuwa Kituo cha Utafiti wa Mifugo (*LPRI*) cha Mpwapwa kilianzishwa mwaka 1905 na ndicho kituo kikubwa cha utafiti wa mifugo hapa nchini na kwa kuwa katika eneo hilo la kituo cha utafiti wa mifugo kuna Chuo cha Mifugo (*LITI)* Mpwapwa na Kituo cha Uchunguzi wa magonjwa ya mifugo (*Vertinary Investigation Centre*):-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kukifanya Kituo cha Utafiti wa Mifugo cha Mpwapwa kuwa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo ya Taifa *(National Livestock Research Institute?*

(b) Kama mpango huo upo, je, utekelezaji utaanza lini?

(c) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba Kituo cha Mifugo cha Mpwapwa kina watalaam wa kutosha na waliobobea katika sekta ya mifugo hivyo inafaa kituo hicho sasa kuwa taasisi ya utafiti wa mifugo ya taifa?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa George Lubeleje, kwa kuona mbali kwani anathamini utafiti kama muhimili mmojawapo muhimu wa maendeleo katika ya sekta ya mifugo nchini. Baada ya kusema hayo naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kwamba Kituo cha Utafiti wa Mifugo cha Mpwapwa, kilianzishwa mwaka 1905 na kituo hicho ni kati ya vituo vikubwa vya utafiti wa mifugo hapa nchini. Vituo vingine vikubwa ni pamoja na maabara ya magonjwa ya mifugo iliyoko, Temeke na taasisi ya utafiti wa Ndorobo na Malale (*TTRI*), iliyoko Tanga. Wizara inavyo vituo vingine vidogo vya utafiti wa mifugo huko Naliendele (Mtwara), *West Kilimanjaro*, Uyole (Mbeya), Tanga na Kongwa hapa Dodoma. Baada ya kuundwa kwa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo mwanzoni mwa mwaka huu, Serikali imeidhinisha kuwepo kwa muundo mpya wa Wizara ambao umekipa Kituo cha Utafiti wa Mifugo Mpwapwa, hadhi ya kuwa taasisi ya utafiti wa Mifugo ya Taifa. Taasisi hii itakuwa na jukumu la kufanya utafiti wa mifugo kitaifa na itawajibika moja kwa moja kwa Katibu Mkuu wa Wizara yangu badala ya kuwa chini ya idara kama ilivyokuwa awali.

(b)Mheshimiwa Spika, kulingana na maelezo niliyotoa hapo juu, mpango wa kukifanya Kituo cha Utafiti wa Mifugo Mpwapwa, kuwa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo ya Taifa tayari umeanza kutekelezwa, ikiwa ni pamoja na mchakato kutunga sheria ya taasisi. Aidha taasisi hiyo, itaanza kujipangia na kutekeleza mipango yake kuanzia mwaka wa fedha 2006/2007. Wizara yangu inalenga kuiwezesha taasisi hiyo kujitegemea kabisa katika kutekeleza majukumu yake katika siku za usoni.

(c)Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kuwa Kituo cha Utafiti wa Mifugo cha Mpwapwa, kina watafiti waliobobea wa shahada ya uzamivu (Udaktari wa Falsafa) 3 wa shahada ya uzamili 3, shahada ya kwanza ya sayansi 7, stashahada 15, astashahada 3 na watumishi wa kiungo (*Supporting Staff)* 39. Ni dhahiri kwamba idadi hii ya watalaam

inaridhisha kwa kiasi japokuwa watalaam zaidi wanahitajika kwa ajili ya kufanya tafiti mbalimbali za mifugo. Hivyo Serikali kupitia Wizara yangu itaendelea kuboresha taasisi hiyo kwa kuongeza watalaam na nyenzo za kufanyia kazi.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda niishukuru na kuipongeza Serikali kwa hatua zake za kupandisha hadhi Kituo cha Utafiti wa Mifugo Mpwapwa kuwa sasa Taasisi ya Kitaifa. Lakini kwa kuwa taasisi hii ina matatizo makubwa ya ukarabati wa majengo, uhaba wa fedha kwa ajili ya kuendesha taasisi hiyo, pamoja na upungufu wa watalaam hasa watafiti. (*Makofi*)

(a) Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba iko haja sasa ya kuhakikisha kwamba majengo yale yalianzishwa mwaka 1905 yanakarabatiwa kuongeza watalaam na kuboresha hali ya usafiri katika kituo hicho? *(Makofi)*

(b) Kwa kuwa katika eneo la taasisi la utafiti wa mifugo ya kitaifa kuna kituo cha uchunguzi wa magonjwa ya mifugo na kwa kuwa wanafanya kazi katika hali ngumu ya kukosa vitendea kazi. Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha hali ya utendaji wa Kituo cha uchunguzi wa magonjwa ya mifugo kwa kuwapatia vitendea kazi vya kisasa? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi ni azma ya Wizara yangu kuhakikisha kuwa inakipatia uwezo kituo cha utafiti kitakachokuwa taasisi ya utafiti wa mifugo nchini ili kuweza kupata fedha za kutosha ikiwa ni pamoja na watalaam wa kuweza kufanya utafiti. Kupata fedha ni upande mmoja lakini pia suala la watalaam ni upande mwingine muhimu sana. Ndiyo maana nimesema kuanzia mwaka huu wa fedha taasisi itaanza kupatiwa uwezo wa kujiendesha yenyewe lakini hatimaye Wizara itawezesha taasisi hii kuwa *semi autonomous* ili iweze kujipangia mambo yake kwa kuwa itakuwa na bodi yake na hivyo hata kubuni mikakati mingine ya kuweza kupata fedha za utafiti ikiwa ni pamoja na kuandika miradi ambayo itaiuza na kupata fedha za uendeshaji.Swali la pili, kuhusu kituo cha uchunguzi wa magonjwa *VIC* ni azma ya Serikali kupitia Wizara yangu, kuhakikisha kuwa vituo vyote vya uchunguzi vinakuwa na uwezo zaidi wa kuweza kuhudumia suala la uchunguzi wa magonjwa ya mifugo kila yanapojitokeza.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, namatumai Mheshimiwa Naibu Waziri, anafahamu kwamba katika nchi nzima ya Tanzania, hakuna maabara inayoweza kuchunguza ubora au kutokuwa na ubora wa dawa za kuogeshea je, Wizara ina mpango gani kuhakikisha kwamba utafiti unafanyika na kuweka kituo cha kuweza kuchunguza madawa haya kwamba yanafaa kuogeshea au hayafai?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kwa kumbukumbu nilizonazo tuna vyombo vingi sana hapa nchini vyenye uwezo wa kuchunguza ubora wa madawa yanayoingia nchini. *TBS* ni mojawapo na ndiyo yenye mamlaka ya kudhibiti ubora wa madawa. *Tropical pesticide research institute (TPRI )* iliyoko Arusha ndiyo yenye dhamana ya kuchunguza ubora wa madawa yanayoingia nchini iwe ni ya mifugo, iwe ni ya kilimo. Kwa hiyo, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kuwa tunayo taasisi iliyopewa dhamana hiyo na inafanya kazi nzuri sana hapa nchini. (*Makofi*)

**SPIKA:** Vazi alilovaa Mheshimiwa Selelii ndiyo vazi rasmi la mwambao kwa humu Bungeni. *(Makofi/Kicheko*)

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, *asalam allekum.* Kwa kuwa katika majibu ya Naibu Waziri wakati akijibu swali la msingi ameeleza vituo vingi vya utafiti wa magonjwa mbalimbali ya mifugo viko maeneo ambayo hayana mifugo. Ninapozungumzia mifugo ni ng'ombe. Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha vituo vya utafiti kama maeneo ambayo yana mifugo mingi kama Shinyanga, Mwanza, Tabora, Singida au Arusha? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu kuna kituo cha utafiti Ukiliguru, kimekuwa kina watalaam wa mifugo na kilimo, lakini Wizara kuanzia mwaka huu wa fedha ina mpango wa kujenga kituo cha utafiti wa mifugo kitakachokuwa chini ya taasisi ya mifugo kitakuwa Mabuki. Kwa hiyo, Wizara yangu inafahamu umuhimu wa kuwa na vituo vya utafiti kwenye maeneo yenye mifugo wengi. Kwa vyovyote vile Singida iko karibu na Dodoma. Kwa hiyo, itashughulikiwa ipasavyo.

Na. 254

**Madini ya Platinum Makete**

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI (K.n.y. MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Nne, imelenga kukuza utafiti katika sekta ya Nishati na Madini na kwa kuwa, katika Wilaya ya Makete, Kata ya Kitulo kumekuwepo na watafiti toka kampuni za Afrika Kusini, wanaotafiti Madini aina ya *Platinum* na kwa kuwa muda wa utafiti umekuwa mrefu kiasi kwamba, wananchi wa Makete wanaona kuwa kinachoendelea siyo utafiti tena bali kusafirishwa kwa madini hayo nje ya nchi:-

(a) Je, Serikali inatambua kuwepo kwa madini aina ya *Platinum* katika Wilaya ya Makete na hao watafiti kutoka Afrika ya Kusini?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa uchimbaji wa madini unasimamiwa na Serikali yenyewe ili Watanzania waweze kunufaika?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Binilith Satano Mahenge, Mbunge wa Makete, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwepo kwa madini aina ya *platinum* katika Wilaya ya Makete kutokana na utafiti wa kijiolojia uliofanywa na watalaam wa wakala wa Serikali wa (*Geological Survey of Tanzania)*, Wilaya ya Makete ina mfumo wa miamba unaojulikana kama *Usagaran system*. Mfumo huo katika baadhi ya maeneo

unayo miamba aina ya *Utramafic* yenye madini ya *Platinum*. Kijiolojia miamba ya aina hii inafahamika duniani kuwa na uwezekano mkubwa wa kuambatana na madini aina ya *Platinum*. Hivyo, kampuni zinapotafuta madini ya *Platinum* huenda katika maeneo yenye miamba ya aina hii, kama yale ya Wilaya ya Makete. Kwa sasa, kampuni ya Kitanzania ya *Warthog Resources Limited* inashirikiana na kampuni ya *Lonemin PLC* ya Afrika Kusini, kufanya utafutaji wa madini Wilayani Makete, kwa miaka miwili sasa. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kuwa, wawekezaji hao wanaofanya kazi katika eneo la Kitulo hawajaanza kuchimba madini ya *Platinum*, bali wanafanya utafutaji wa madini hayo. Utafutaji wa madini hufanyika kwa hatua mbalimbali na kuchukua muda mrefu.

(b) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge juu ya umuhimu wa Serikali kusimamia uchimbaji wa madini na ndivyo inavyofanyika na sheria ya madini ya mwaka 1998 na kanuni za mwaka 1999. Aidha, majadiliano yanayoendelea sasa kati ya Serikali na makampuni makubwa ya madini yana lengo la kuhakikisha kuwa Watanzania nao wananufaika ipasavyo na rasilimali yao ya madini.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya kuridhisha ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Kwa vile kampuni inayotafuta madini kule Makete, imekuwa ikipitisha mashine zake ambazo barabara na madaraja yaliyopo kwa sasa hivi yanashindwa kuhimili na mara nyingi huleta mtingishiko na *cracks* na kuleta uharibifu mkubwa kwenye madaraja na barabara hizo ambazo ni nyembemba. Je, Serikali inasemaje kuhusu hilo?

(b) Kwa vile kuna utaratibu wa kutaka kuipitia upya sera ya uchimbaji madini kwa nini Serikali, isisitishe kuwaruhusu hawa watu ambao wanaharibu miundombinu kwa sababu hakuna utaratibu unaowaelekeza vitu vya kufanya mpaka hapo sera itakapowekwa sawa sawa ili waweze kufanya kazi zao kwa utaratibu unaoeleweka? Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nilivyoeleza ni kwamba hivi sasa tunavyoongea kuna majadiliano ambayo yanafanyika kati ya Serikali na makampuni ambayo yanachimba madini hapa nchini. Suala hilo ambalo amelisema kuhusu uharibifu wa mazingira na barabara ambao unatokana na makampuni yakiwa yanafanya utafiti ni kati ya maswali ambayo tunaangalia hivi sasa na namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwamba tutaliangalia kwa ukamilifu katika urekebishaji wa Sera ya Madini hapa nchini.

Na. 255

**Barabara ya Mbalizi – Makongolosi**

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA** aliuliza:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne amedhamiria Serikali anayoiongoza kutekeleza ahadi zote zilizomo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 na kwa kuwa Mheshimiwa Rais akiwa Mbeya tarehe 29/8/2005 aliahidi kushughulikia barabara ya Mbalizi – Mkwajuni hadi Makongolosi ili ipitike kwa urahisi nyakati zote:-

(a) Je, ahadi hiyo itaanza kutekelezwa lini?

(b) Je, utekelezaji wa ahadi hiyo utakuwa ni wa kuzitengeneza barabara husika kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Guido Gorogolio Sigonda, Mbunge wa Songwe, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mbalizi – Mkwajuni hadi Makongolosi yenye jumla ya kilometa 116.6 ni barabara ya Mkoa *(Regional Road)* na ni ya changarawe na udongo inayohudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS)* Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekuwa ikiifanyia matengenezo barabara hii pamoja na madaraja kulingana na Bajeti ili iweze kupitika. Kazi ambazo zimekuwa zikifanywa ni pamoja na matengenezo ya kawaida, matengenezo ya sehemu korofi, matengenezo ya dharura na ukarabati wa madaraja. Jumla ya shilingi 435.9 milioni zimetumika kwa matengenezo haya katika kipindi kati ya mwaka wa fedha 2002/2003 hadi 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaanza kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais mwaka huu wa fedha kwa kuimarisha sehemu ya barabara hii kwa kiwango cha changarawe na tayari jumla ya shilingi milioni 140 zimetengwa kwa kazi hizo katika mwaka huu wa fedha wa 2006/2007. *(Makofi)*

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Nashukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Wakati Mheshimiwa Waziri Miundombinu wa sasa alipokuwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya alitumia nafasi yake nzuri sana ya kusimamia na kubuni mbinu ya kutengeneza sehemu ambayo ilikuwa ni korofi sana ya barabara hiyo, sehemu ambayo inaitwa Msangamwelu, akabuni mbinu na akaweza kutengeneza kwa kiwango cha lami sehemu hiyo ya kilometa 3.

Je, sasa hivi kuna sehemu korofi zaidi ya ile ambayo aliitengeneza, Mbala na Iseche. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza akatumia uzoefu huo huo wa angalau wakati huu tunaposema kwamba tutatengeneza hiyo barabara kwa kiwango cha changarawe

anaweza akatumia mbinu hizo hizo alizotumia kwa sehemu hii chache kuitengeneza hiyo barabara kwa kiwango ambacho kinaweza kikatumika wakati wote? *(Makofi)*

**SPIKA:** Naona hili la Mheshimiwa Waziri mwenyewe, kwa kweli.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, naomba tukutane Ofisini ili niweze kutumia uzoefu wangu na mapenzi makubwa niliyonayo kwa Mkoa wa Mbeya ambao walinitunza kwa miaka mitano mfululizo kuona namna ya kuwasaidia hawa wananchi wa eneo hili. Nawafahamu, Wilaya hii ya Chunya ni kubwa, barabara zake ni ndefu na ngumu. Kwa hiyo, niko tayari kuelewana naye zaidi ili tuweze kuona ni namna gani tunaweza kushirikiana. *(Makofi)*

Na. 256

**Ujenzi wa Barabara Kuu Mikoa ya Kusini**

**MHE. RAYNALD A. MROPE** aliuliza:-

Kwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kampeni za uchaguzi aliahidi kuwa barabara kuu iendayo Mikoa ya Kusini itakamilika ifikapo tarehe 31 Desemba 2006 na kwa kuwa, barabara hiyo ni kiungo muhimu sana kwa watu wote wa Mikoa ya Kusini na imekuwa ikisubiriwa kwa hamu kwa muda mrefu sasa:-

(a) Je, Serikali iko tayari kuthibitisha kwa vitendo kauli hiyo na inatoa matumaini gani kwa wananchi wa Mikoa ya Kusini?

(b) Je, ni kweli kwamba, sehemu korofi za barabara hiyo kuanzia Nangurukuru hadi Mingoyo itajengwa kwa kiwango cha lami katika kipindi hicho?

(c) Je, Serikali ina imani na Wakandarasi waliopo kuwa watakamilisha ujenzi huo kwa muda husika au kuna mpango wowote wa kuondoa baadhi yao ambao imeonekana kuwa wanalegalega?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Raynald Alfons Mrope, Mbunge wa Masasi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua sana umuhimu wa barabara hii kwa wananchi wa Kusini na kwa Tanzania kwa ujumla. Serikali inapenda kuwahakikishia wananchi wa Kusini na Watanzania wote kuwa itafanya kila iwezalo kuhakikisha kuwa

barabara hii kuu iendayo Mikoa ya Kusini inakamilika mapema iwezekanavyo na kwa viwango vinavyokubalika.

(b) Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara hii kuanzia Nangurukuru hadi Mingoyo unaendelea na upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama ifuatavyo:-

(i) Ni ujenzi wa sehemu ya Nangurukuru hadi Mbwemkuru yenye urefu wa kilometa 95 unatekelezwa na Mkandarasi *China Chongqing International Construction (CICO)* kwa gharama ya shilingi 39.239 bilioni. Hivi sasa mradi umefikia asilimia hamsini (50%) ambapo kilometa 40 zimeshakamilika kujengwa kwa kiwango cha lami. Awali mradi huu ulipangwa kukamilika mwezi *October, 2005,* lakini kutokana na matatizo ya Mkandarasi na mvua nyingi zilizonyesha juu ya viwango vilivyotarajiwa katika msimu wa mwaka 2003/2004 na 2004/2005 katika eneo la mradi, sasa inatarajiwa kuwa mradi utakamilika mwezi Februari mwaka kesho. Lakini kwa mujibu wa Mkataba, muda wa mradi umemalizika tarehe 19 Mei, mwaka huu baada ya muda wa siku 172 kuongezwa kimkataba, na kwa kipindi kilichobaki Serikali inamtoza Mkandarasi kwa mujibu wa Mkataba.

(ii) Sehemu ya pili ni ya Mbwemkuru hadi Mingoyo yenye urefu wa kilometa 95 tena na mradi huu unatekelezwa na Mkandarasi *M.A.Kharafi & Sons* kwa gharama ya shilingi 51.488 bilioni. Ujenzi wa mradi huu nao ulipangwa kukamilika mwezi *Oktober* mwaka jana lakini hadi sasa ujenzi umefikia asilimia 48 tu. Pamoja na suala la mvua na matatizo mengine ya Mkandarasi, mradi huu umekumbwa na tatizo la ziada la Mkandarasi kutaka kwenda kinyume na mkataba ili kujenga tabaka la mawe ya kusaga *(base course)* la barabara kwa kutumia mawe ya mwamba wenye ubora usiokubalika. Kwa upande wake Wizara imekuwa ikipinga matumizi ya kokoto hizo za mawe. Hadi sasa Mkandarasi amekamilisha kilometa 67 tu za tuta la barabara; kukamilisha ujenzi wa madaraja 12 na mengine 15 yanaendelea kujengwa. Kwa hali hii mradi umechelewa kwa zaidi ya miaka miwili. Hata hivyo Wizara yangu, kwa kutambua umuhimu wa kukamilisha barabara hii mapema imekuwa ikijaribu kutatua mgogoro uliojitokeza kati yake na Mkandarasi kuhusu suala hilo la kokoto na vipengele vingine vya Mkataba kwa njia ya mazungumzo. Tayari mkutano mmoja umefanyika tarehe 5/7/06 hapa Dodoma kati ya Uongozi wa juu wa Wizara na Uongozi wa juu wa Kampuni ya *M.A. Kharafi & Sons* na kikao cha pili kitafanyika tena tarehe 28 mwezi huu. Kama muafaka wa masuala yote yenye mgogoro likiwemo suala la kokoto za mawe, katika Mkataba utapatikana haraka, mradi huu sasa unategemewa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2007 au mwanzoni mwa mwaka 2008.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inachukua hatua za kimkataba kwa uangalifu mkubwa kwa lengo la kuwabana Wakandarasi hawa na hususan Mkandarasi wa sehemu ya Mbwemkuru hadi Mingoyo, ili akamilishe ujenzi kwa mujibu wa Mkataba na kama hakuna budi, tutavunja mkataba lakini baada ya kuzingatia kwa makini maslahi ya Serikali na ya wananchi wa Mikoa ya Kusini.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pia namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa jinsi alivyoelezea kwa kirefu jinsi Serikali inavyotaka kutatua mgogoro huu. Mimi swali hili nililiuliza kabla ya mkutano na kwa bahati nzuri wakati wa Bajeti Wizara imetueleza mikakati gani walikuwa nayo katika kutekeleza

mradi huu ingawa hatukuridhika. Lakini mimi sasa ningeomba zaidi Waziri atueleze ni mbinu gani anaweza kutumia katika miaka miwili hii anayoisema ili wafanye kazi walau usiku na mchana kumaliza kabla ya hiyo miaka miwili hili ndiyo tatizo letu kubwa. Mimi naomba sana watueleze jinsi gani wanavyoweza kujipanga upya ili kutimiza azma hiyo?

Swali la pili, ni kwamba kuna sehemu korofi za *divesions* zile ambazo ndiyo zinazoleta taabu sana sana kwa wananchi wa Kusini wakati wa masika. Kwa sababu hupelekea magari mengi kukwama na watu kukaa porini kwa muda mrefu kwa sababu ya barabara kuwa mbaya. Je, katika kipindi hiki cha miaka miwili Serikali itakuwa na mikakati gani ya kuhakikisha kwamba watu hawalali barabarani na pia kwa sababu tatizo siyo pesa hivi katika maeneo haya anayehusika watu wakikwama ni nani, ni *TANROADS* au ni Mkandarasi mwenyewe wa kuwakwamua katika shida wanazozipata?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwa kweli sehemu ya kwanza ambayo inajengwa na Wachina, nadhani kipindi walichotoa cha mpaka Februari mwaka kesho hakitakuwa na matatizo makubwa. Kwa sababu hakuna mgogoro mkubwa ni uchelewefu tu. Lakini kama nilivyoeleza tatizo kubwa liko katika sehemu ya pili la Mbwemkuru mpaka Mingoyo kwa maana ya yule Mkandarasi *M.A.Kharafi & Sons* na hapa kama nilivyoeleza tumekuwa na mgogoro huo wa kutumia mawe.

Sasa anasema ni mbinu gani ambayo tunaweza tukafanya ili iwe chini ya miaka miwili. Ninachoweza kusema ni kwamba cha msingi ni kwamba tumalize huu mgogoro ambao upo kati yetu na Mkandarasi na tumekuwa makini sana kuhakikisha kwamba tunafuata vipengele vya sheria. Lakini vile vile inabidi tuongeze mazungumzo na uhusiano. Kwa sababu Mkandarasi huyu si kwamba ni mkandarasi mwingine aliyeshindwa kazi, unamwambia, anasema samahani nitaongeza *speed* hapana, na yeye ana madai yake na kwa kweli ameshakwenda kwa msuluhishi. Kwa hiyo, lazima tuwe waangalifu sana. Tutumie vipengele vya sheria lakini vile vile tutatumia uhusiano na mazungumzo.

Kwa muda ambao unaweza kuwa ni mfupi kabisa wa kutekeleza mradi huo. Kama tutamaliza mazungumzo haya mapema, na *speed* ikaongezeka ni huo muda wa miaka miwili ambayo imeongezeka baada ya mkataba huo kuwa umekwisha. Nataka tumhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wote wa Mikoa ya Kusini kwamba Wizara yangu iko makini sana kuhakikisha kwamba barabara hii inajengwa. Na kwa kweli tutalazimika tu kwenda kwenye kuvunja mkataba kwa sababu uvunjaji wa mkataba, utatuletea matatizo mengi ya kuchelewesha mradi si ajabu miaka minne au mitano. Lazima tuendelee kujadiliana na tusilamishe kufikia huko. Mimi nina hakika kwamba tunaweza tukamaliza hili na kwa sababu ameonyesha nia kuzungumza na Wizara na kuendelea na mradi nina hakika suala hili litakwenda vizuri.

Kuhusu sehemu korofi za *divesions* ukweli hili ni jukumu la mkandarasi kusaidiana katika kuboresha *divesions* zile ili wananchi waweze kupita. Na mara nyingi panapotokea matatizo tumekuwa tunawasiliana nao na *TANROADS* wako pale kwa ajili

ya kushirikiana na Mkandarasi ili hizi *divesions* ziendelee kupitika na mnajua wakati mwingine zinakuwa mbaya hasa wakati wa mvua lakini jitihada zitaendelea kuwekwa ili kuhakikisha kwamba mkandarasi wakishirikiana na *TANROADS* Mkoa wa Lindi wanaboresha na wananchi hawakwami.

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kuwa utaratibu ulioanzishwa sasa na viongozi wetu wakuu kwa maana ya Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na baadhi ya Mawaziri wa kutembelea eneo la tukio na kupata suluhu pale pale umeonyesha kuzaa na tija. Je, Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu na Manaibu Waziri wataiga mtindo huu ili kuja kuona matatizo yanayotukabili haswa nyakati za masika badala ya kusubiri kuitwa na Mheshimiwa Waziri au Mheshimiwa Rais tu?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Nne na Mawaziri wote kwa kweli tumeiga mfano huu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu na ndiyo maana tumekuwa tukienda maeneo mbalimbali. Katika Bunge hili nadhani wengi mmeshuhudia Wabunge wakinisifu kwamba nimepita mikoa mingi kwa muda mfupi na huu ndiyo uwigaji wa viongozi wetu wakuu. Na Mheshimiwa Waziri wangu naye ametembelea maeneo mengi na tutaendelea kufanya hivyo na wala asiwe na wasi wasi.

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii niulize swali moja la nyongeza. Katika jibu lake la msingi ameeleza kwamba watakuwa makini katika kufuatilia ujenzi wa barabara ile ili wakandarasi wasiotimiza ahadi yao wafanye kazi vizuri.

Je, anaweza akatueleza ni utaratibu gani huo atakaoutumia, kutakuwa na Kamati Maalum ya kufuatilia ama Mheshimiwa Waziri mwenyewe ama utaratibu gani huo ambao utafuatilia ujenzi wa barabara hii ili wakandarasi hao wahakikishe kwamba barabara hiyo wanaikamilisha kwa muda uliopangwa?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, naomba Waheshimiwa Wabunge wa Mikoa ya Kusini waamini tunayosema kwamba kandarasi hii ngumu sana kwa sababu tuna mgogoro na Mkandarasi amekwishatupeleka sisi Mahakamani, Mahakama ya Kwanza. Mahakama ya Kwanza ni usuluhishi. Hivi sasa Serikali imepelekwa kwenye usuluhishi na kwa taratibu za usuluhishi uamuzi wa Msuluhishi una nguvu ya kisheria. Mwezi wa nane Msuluhishi atatoa jibu la kwanza. Kwa kutegemea uamzi wa msuluhishi huyo Serikali itabidi ifuate mkondo huo wa sheria ambao ni wa usuluhishi. Unaweza ukachukua miaka.

La pili, pamoja na kuelewa kwamba tuko kwa msuluhishi, sisi tumeendelea kufanya mazungumzo na Mkandarasi kwa utaratibu wa kisheria unaitwa, *Without Prejudice.* Kwa hiyo, ndiyo utaratibu huo wa tarehe 5 Julai, 2006 uliofanyika. Ni mimi mwenyewe nilikuwako kwenye mkutano huo. Tarehe 28 Julai, 2006 tutakutana tena pamoja na wadau wengine kutoka Canada wanaosimamia mradi huu, kama tukiweza kuelewana hapo kati kati kabla ya Msuluhishi kutoa hukumu, tutachukua hatua fulani. Isipowezekana na Msuluhishi atatoa hukumu, tutachukua njia fulani. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ningependa kuwahakikishia tu kwamba, la msingi ni kwamba sisi tunaumwa sana na tatizo hili kama vile watu wa Kusini wanavyouma. Lakini sheria ni sheria lazima tutii sheria na huku tunajaribu kutumia njia za kidiplomasia na za mazungumzo kuona wapi tunapoweza kupenya. Kwa hiyo, kusema hapa ni ipi itategemea mambo yatakavyokuwa wakati huo.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kusema kitu kinachofanana na hili hili kwa barabara ya Dodoma-Manyoni, Manyoni-Singida. Kuna wakandarasi wawili. Wa kwanza alishatupeleka kwenye usuluhishi, wa Dodoma-Manyoni na Msuluhishi ametoa hukumu nzuri kwa Serikali. Sasa tufanyeje, hata Msuluhishi akitoa hukumu hata asipotoa, barabara lazima itengenezwe. La maana ndiyo hilo. Barabara lazima itengenezwe. Kwa hiyo, katika Serikali itabidi tena tuzungumze, tunataka barabara, katika hali hii na iweje? *(Makofi)*

Yote haya tunayazungusha katika vichwa vyetu. Mimi nafikiri tutapata uchochoro ili barabara hizi ziweze kuendelea kutengenezwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mimi naamini kutokana na jibu refu la Mheshimiwa Waziri na hata kauli yake namna alivyoitoa kwa kweli ana uchungu na barabara hii. Tumpe muda. *(Makofi)*

Na. 257

### *Traffic* Kutoza Faini za Hapo kwa Hapo

**MHE. MOHAMED RAJAB SOUD** aliuliza:-

Kwa kuwa askari polisi wa usalama barabarani *Traffic* wa Tanzania Bara wanapothibitisha kuwa dereva amefanya kosa dogo la barabarani hutoza faini ya hapo kwa hapo:-

Je, mpango kama huo utaanza lini kwa *Traffic* walioko Tanzania Visiwani?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, napenda kumjibu Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, Mbunge wa Jang'ombe swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, baada ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar kupitisha Sheria namba 7 ya mwaka 2003, sasa ndani ya sheria hiyo kimo kifungu namba 181(1) ambacho kinatoa uwezo kwa Polisi wa Usalama Barabarani huko Zanzibar wa kutoa adhabu kutokana na makosa ya barabarani bila ya kufikishwa Mahakamani. Kwa kifungu hicho dereva anaweza kutozwa faini kwa kujaziwa fomu maalum.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sheria hiyo imepitishwa na Baraza la Wawakilishi na ipo chini ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar bado haijaanza kutekelezwa kwa kuwa Wizara husika inaandaa fomu maalum za kujaza na kuweka utaratibu wa wapi fedha zilipwe. Aidha, Wizara hiyo inatengeneza Kanuni *(Regulations)* itakayoelekeza utaratibu wa utekelezaji.

**MHE. MOHAMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na pia napenda nimpongeze SSP Mahmoud Juma kwa utekelezaji mzuri wa kikosi hiki cha Usalama Barabarani. *(Makofi)*

Lakini pamoja na hayo naomba niulize maswali mawili madogo kama ifuatavyo:- Kwa kuwa sheria hii imeundwa tangu mwaka 2003 na mpaka hii leo haijatekelezwa. Wizara yako inatoa msukumo gani ili iweze kutekeleza sheria hii?

Pili, kwa kuwa Mahakama zetu zimekuwa na msongamano mkubwa sana haoni ni vema ikasisitizwa sheria hii ikatumika ili kupunguza makosa madogo madogo yakahukumiwa barabarani badala ya kupelekwa Mahakamani?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sheria ile imetungwa na Baraza la Wawakilishi Zanzibar na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi ya Zanzibar ndiye mwenye dhamana ya kusimamia.

Sisi kwa upande wetu tutashirikiana na wenzetu kutaka wachukue jitihada ili taratibu hizi zimalizike na utekelezaji ufanyike ipasavyo. Hivi sasa Kanuni zile zipo kwa Mwanasheria Mkuu. Nategemea ya kwamba baada ya hapo utekelezaji utafanyika vizuri.

Hivyo naomba Mheshimiwa Mbunge avute subra tusubiri Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar akabidhi kwa Wizara ya Mawasiliano kanuni zile ili utekelezaji uanze.

Tungependa sote kuona kwamba tunapunguza msongamano kule Mahakamani na faini zinatozwa papo kwa papo hilo ni jambo zuri na ndiyo maana Serikali ya Zanzibar ikachukua hatua hizi.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza baada ya majibu sahihi ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Waziri alipokuwa anajibu swali mama amezungumzia jinsi ya mapato yanavyokusanywa na *Traffic* Tanzania Bara na pia ameliambia Bunge kwamba muda mfupi *Traffic* wa Zanzibar inatafutwa mahali pa kupeleka fedha hizo. Anaweza akaliambia Bunge hili je, kuna makubaliano yoyote kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ile ya Zanzibar katika kukusanya fedha hizo wakati Wizara ya Mambo ya Ndani ndiyo inayesimamia jeshi hili la Polisi?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika swali langu la msingi kwamba kuna utaratibu wa fomu maalum utakaoainisha fedha hizo wapi zipelekwe. Peza zote zitakazotozwa kwa adhabu ya Usalama Barabarani kule Zanzibar zitapelekwa kwa Wizara ya Fedha Zanzibar.

Na. 258

**Upandishwaji wa vyeo askari Polisi**

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA** aliuliza:-

Kwa kuwa kuna malalamiko juu ya upandishwaji vyeo katika jeshi la Polisi:-

(a) Je, kuna utaratibu maalum unaotumika kuwapandisha vyeo askari hao?

(b) Kama hakuna utaratibu maalum, kwa nini Serikali haipangi utaratibu maalum badala ya utaratibu wa sasa unaoleta malalamiko?

(c) Je, askari ambao wana kiwango duni cha elimu huwa wanapandishwa vipi vyeo?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, naomba kumjibu Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mbunge wa Micheweni, swali lake lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika jeshi la polisi, upo utaratibu maalum unaotumika kuwapandisha vyeo askari polisi. Utaratibu huu unatokana na mwongozo wa *Police General Orders (PGO)* na Kanuni za Utumishi za Jeshi la Polisi. Askari Polisi anaweza kupandishwa cheo kwa kuzingatia ukubwa kazini *(Seniority),* uadilifu uliotukuka *(merit)*, kiwango cha elimu, ujuzi wa ziada alionao ambao unaendana na mahitaji ya Jeshi la Polisi *(Prescribed qualifications)* na sifa nyingine kama ilivyoainishwa katika *Police General Orders* na Kanuni za Utumishi za Jeshi la Polisi *(Police Regulatoins).*

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika kipengele (a) cha jibu langu, jeshi la Polisi lina utaratibu maalum wa kuwapandisha vyeo askari wake.

(c) Mheshimiwa Spika, askari wenye viwango duni vya elimu nao pia wana haki ya kupandishwa vyeo kwani elimu ni moja tu kati ya sifa nyingi zinazomwezesha askari kupandishwa cheo kwa mujibu *Police General Orders (PGO)* na Kanuni za Utumishi katika Jeshi la Polisi *(Police Regulations).*

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii. Nina swali dogo tu la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kumwuliza ifuatavyo:-

Madhumuni ya cheo kwa aliyepewa ni kumpa maslahi ya hiki cheo chenyewe. Je, anayo habari kwamba hawa wanapandishwa cheo hasa askari wa chini wanachelewa sana kufaidika na hizo nyongeza zao na kama anazo je wanafanye katika kuondoa tatizo hilo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Khalifa umesema haraka sana na Waziri hakusikia vizuri. Hebu rudia tena swali lako.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Nitasema kidogo kidogo sasa. Nashukuru sana kwa majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Nina swali dogo tu la kumwuliza. Kwa kuwa msingi wa kumpandisha mtu cheo ni kufaidika na hicho alichokipata katika kupandishwa hicho cheo alichopewa.

Je, anazo habari kuwa hawa askari wa chini wanapopandishwa vyeo wanachelewa sana kufikiwa na hizo nyongeza zao kwa hivyo vyeo walivyopewa na kama anazo wanafanyaje katika kuondoa manung'uniko haya?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, ninazo taarifa za kuchelewa kwa baadhi ya askari wanapopandishwa vyeo kwa kupata mishahara yao kama inavyotakiwa. Tatizo hili hivi sasa linashughulikiwa na Serikali na katika kipindi cha Bajeti cha mwaka huu unaofuata matatizo hayo mengi yatakuwa tumeyaondoa. *(Makofi)*

Na. 259

**Viwanda vya Kubagulia Korosho**

**MHE. MARIAM KASEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa, zao la Korosho ndilo zao kuu la biashara Mkoani Mtwara:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Viwanda vidogo vya kubangulia Korosho ili wananchi waweze kuuza Korosho zilziobanguliwa kama Serikali inavyowahimiza wakulima hao?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia akina mama ambao wapo katika vikundi mikopo mikubwa yenye riba nafuu ili wawe na uwezo wa kununua korosho ghafi?

(c) Je, Serikali inawashauri Wakulima watumie dawa zipi za kuboresha zao la korosho kwani kuna madawa mengi ya kupulizia zao hilo yanayoingizwa nchini na wakulima hawapatiwi elimu ya kutosha?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mbunge wa Viti Maalum napenda kutoa maelezo ya awali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sera ya Serikali hivi sasa ni kuhakikisha kuwa mazao yanayozalishwa hapa nchini yanasindikwa kabla ya kuuzwa katika masoko ya ndani na nje ili kuyoangezea thamani na hivyo kuwapongezea kipato wananchi na Taifa kwa ujumla. Zao la korosho ni mojawapo ya mazao yaliyolengwa kufaidika na utekelezaji wa sera hiyo. Kuanzia mwaka 2004, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi nchini, inatekeleza mkakati wa kuhakikisha kwamba ifikapo mwaka 2008, sehemu kubwa ya korosho ianyozalishwa nchini inabanguliwa na kuuzwe katika masoko yanayohitaji korosho hizo na hivyo kuondokana na kutegemea soko la nchini India peke yake.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya awali napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Kasembe, lenye sehemu (a), (b) na ( c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mfumo wa uchumi uliopo hivi sasa unaongozwa na nguvu ya soko. Wajibu wa Serikali katika mfumo wa uchumi uliopo ni kuweka mazingira mazuri ili wajasiriamali wajitokeze na kujenga viwanda vikubwa, vya kati na vidogo vya kubangua korosho. Serikali inaendelea kuwahimiza wawekezaji walionunua viwanda vya korosho kuvikarabati ili vianze kubangua korosho haraka iwezekanavyo. Aidha, Serikali inahimiza wajasiriamali kuanzisha viwanda vidogo vya kubangua korosho ili kuongeza ubora. Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika, kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda Biashara na Masoko, itaendelea kutoa mafunzo ya mbinu bora na ushauri wa kiufundi juu ya mbinu bora za ubanguaji wa korosho.

(b) Mheshimiwa Spika, Tatizo la upatikanaji wa mahitaji na riba kubwa zinazotozwa na mabenki kwenye mikopo ya muda mrefu na mfupi ni baadhi ya changamoto zinazowakabili wananchi waliowekeza au wanaodhamiria kuwekeza katika usindikaji wa mazao ukiwemo ubanguaji wa korosho. Ili kuwasaidia wawekezaji katika ubanguaji wa korosho, Serikali kuanzia mwaka 2004/2005, iliamua kuanzisha Mfuko wa Kudhamini Mikopo ya Miradi Midogo na Kati (*Credit Guarantee Scheme for Small and Medium Enterprise*). Kiwango cha udhamini ni kati ya shilingi milioni tano na milioni 200 katika muda usiozidi miaka mitano. Serikali inahimiza akina mama walio katika vikundi mbalimbali kutumia fursa zianzotolewa na Serikali kwa kuibua miradi ambayo inaweza kuombewa fedha kutoka vyanzo mbalimbali vya fedha au miradi ya Serikali kama vile *PADEP*, *TASAF* na pia kutoka katika shilingi milioni 500 ambazo zitatolewa na Serikali kwa kila mkoa katika mwaka 2006/2007. Napenda kutoa wito kwa kina mama na wananchi wengine kujiunga katika vikundi na *SACCOS* na kuvisajili ili waweze kutumia fursa za uwezeshaji zinazotolewa na Serikali.

(c)Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2005/2006, Wizara ilifanya tathmini ya viwango vya mahitaji ya madawa ya kudhibiti magonjwa na visumbufu vya zao la korosho katika mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma. Kupitia tathimini hiyo, wadau walionyesha kuridhika na madawa ya Salfa ya Unga, *Bayfidan*, *Anvil* na *Thiovit Jet* kwa ajili ya kudhibiti ubwiri unga; na *Karate* na *Selecron* kwa ajili ya kudhibiti wadudu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2004/2005, Serikali ilitoa ruzuku kwa madawa ya korosho kwa lengo la kuwapunguzia wakulima gharama za ununuzi wa

madawa hayo. Madawa yaliyopatiwa ruzuku ni *Bayfidan*, *Anvil*, *Thiovit Jet*, *Karate* na *Selecron*. Aidha wataalam wa ugani walipatiwa mafunzo maalum ya matumizi ya madawa hayo ili wawashauri wakulima namna ya kuyatumia ipasavyo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, bahati mbaya muda wa maswali umekwisha, hasa ikizingatia nina matangazo mengi sana hapa. Kwanza kwa haraka haraka sana nitawatambua hawa wageni na wanapotajwa wasimame. Tunao upande wa kushoto, walimu watatu na wanafunzi 50 kutoka shule ya msingi Mlimwa B hapa Dodoma Mjini. (*Makofi*)

Nafurahi kuwafahamisheni Waheshimiwa kwamba tunaye mumewe Naibu Waziri Rita Mlaki, Bwana Theofil Mlaki. Mheshimiwa Col. Saleh Farrah, amefikiwa na Mgeni binti yake Ferima Farrah, ambaye kwa mujibu wa Mheshimiwa Mbunge anasema amekuja kujifunza ili ahamasishwe kuwa mwanasiasa. (*Makofi*)

Upo pia uongozi wa wanafunzi. Yupo Rais wa Serikali ya wanafunzi *CBTI* Tengeru, yupo Rais wa Serikali ya Wanafunzi Chuo Kikuu Mzumbe, yupo Rais wa Serikali ya Wanafunzi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, na wamefuatana na Serikali zao. Yaani kuna Mawaziri wao. Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, anawajulisha wajumbe kwamba kikao leo kinaendelea saa 4:30 asubuhi.

Mheshimwia George Lubeleje Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala anawatangazia Waheshimiwa kwamba, Waheshimiwa wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwamba kutakuwa na Semina ya Kamati hiyo ambayo itafanyika saa saba mchana, *Dodoma Hotel.*

Mheshimiwa William Kusila, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wa Kamati yake ya Ulinzi na Usalama kwamba leo saa tano asubuhi watakuwa na mkutano chumba Namba 133. Sasa kabla hatujamaliza eneo hili la matangazo, ninamwomba Naibu Waziri wa Habari, Uta maduni na Michezo, Mheshimiwa Joel Bendera atangaze kuhusu mbio za kesho. Hili ni tangazo maalum na mimi sina utaalam nalo. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. JOEL N. BENDERA):** Mheshimiwa Spika, nashukuru, naomba tu niwakumbushie Waheshimiwa Wabunge kwamba kesho tuna zile mbio za *VIP RACE* ambazo tunazifanya kila mwaka. Ndio tumeishatoa ratiba kwenye *pigeon hole* lakini kila mtu anayo ratiba yake na njia ambayo tutapita, naomba tu niwakumbushe leo saa 11 jioni tutagawa vifaa, tutagawa raba, tutagawa fulana pamoja na kofia. Tunaanza kesho mbio saa 12 asubuhi, saa moja kamili mgeni rasmi ambaye ni Waziri Mkuu Mheshimiwa Edward Lowassa atakuwa ameshafika na ameahidi kushiriki tutakuwa naye mwanzo mpaka mwisho. Tutakuwa na makundi nane, ya umri tukianzia na umri mdogo kabisa wa Mheshimiwa Amina Chifupa, miaka 24 - 30 mpaka tunafika wazee watu wazima. Tumeweka kipindi cha miaka mitano mitano kupishana ili wale wadogo wasiwaendeshe na watu wazima.

Kwa hiyo, tunawaomba wote kesho tuhudhurie kwa nia ya afya zetu nawashukuru ahsanteni. *(Makofi)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali ya mwaka 2006/2007
### Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia

**WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, pamoja na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, niruhusu pia niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu katika kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. Ushindi huu wa Kishindo alioupata Mheshimiwa Rais ni kielelezo tosha kuhusu imani waliyonayo wananchi kwake. Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, kwa kuteuliwa kwake na hatimaye kuthibitishwa na Bunge kuwa Waziri Mkuu. Nampongeza pia Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Mawaziri na Manaibu Waziri kwa nyadhifa zao mpya.

Vile vile nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Yusuph Rajabu Makamba, kwa kuteuliwa kwake kuwa Mbunge na Katibu Mkuu wa Chama Tawala.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote waliowezesha kutekeleza majukumu ya Wizara yangu kwa kipindi kilichopita, na ambao wamewezesha kuandaa mipango ya mwaka 2006/2007 na kuboresha hoja yangu ambayo naiwasilisha katika hotuba hii. Aidha, natoa shukrani kwa wananchi wote wa Tanzania kwa mchango wao katika kutekeleza majukumu ya Wizara yangu. Natoa shukrani zangu za dhati kwa Naibu Waziri wangu, Mheshimiwa Gaudentia Mugosi Kabaka, Katibu Mkuu Dr. Naomi B. Katunzi, Watendaji katika Wizara yangu pamoja na taasisi zilizo chini ya Wizara, mashirika mbalimbali ya ndani na nje kwa misaada na ushauri wao. Kwa namna ya pekee natoa shukrani zangu kwa Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii chini ya uongozi wa Mwenyekiti wake Mheshimiwa Omar Kwaang'w Mbunge wa Babati Mjini (CCM) kwa uchambuzi na ushauri wao. Aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA) ambaye ni msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu wizara yangu kwa ushirikiano wake na mchango wake katika kuboresha hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuwashukuru wananchi wa jimbo langu la Kilolo kwa heshima waliyonitunuku kuwa Mbunge wao. Napenda kuwathibitishia nia yangu ya kuwatumikia katika wadhifa huu kwa moyo wangu wote. Aidha, napenda kumshukuru kwa dhati kabisa Mheshimiwa Rais kwa kunipa dhamana ya kuiongoza Wizara hii ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia. Ninaahidi ya kuwa nitatumia uwezo

wangu wote kutekeleza majukumu niliyopewa ili kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa Watanzania.

Kwa namna ya pekee napenda tena kumshukuru Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania kwa juhudi kubwa anazofanya kuhakikisha kuwa Chuo Kikuu cha Dodoma kinajengwa katika kipindi hiki cha miaka mitano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, dira na dhima ya wizara, Dira ya Wizara yangu kufikia mwaka 2025 ni kuiwezesha Tanzania kuwa nchi yenye misingi imara yenye kuipa uwezo wa kuwa mshindani katika nyanja za Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia miongoni mwa Jumuiya ya Kimataifa. Aidha, Dhima ya Wizara ni kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera za Elimu ya Juu, Ufundi, Sayansi na Teknolojia ili kuwezesha upatikanaji wa nguvu kazi yenye uwezo wa kutumia rasilimali zilizopo ili kujiletea maendeleo. *(Makofi)*
Hii ni kutokana na kutambua kwamba watu, na hususan walioelimika na wenye afya bora ni rasilimali muhimu na nyenzo kuu ya maendeleo ya nchi kiuchumi. Kuna ushaidi wa kutosha juu ya hili ikiwa ni pamoja na kauli iliyotolewa na Rais wa Ireland Mheshimiwa Mary Mc Aleese alipolihutubia Bunge hili tukufu siku ya Alhamisi tarehe 22 Juni, 2006.

Mheshimiwa Spika, muundo na majukumu ya wizara. Wizara yangu imegawanyika katika Idara tano (5) ambazo ni: -

- Elimu ya Juu;
- Elimu ya Ufundi;
- Sayansi na Teknolojia;
- Utawala na Utumishi; pamoja na ile ya
- Sera na Mipango. Aidha, ipo Tume ya Taifa ya *UNESCO* ambayo inahusika na uratibu wa shughuli za *UNESCO* nchini. Vipo vitengo vitatu (3) ambavyo ni: Uhasibu na Fedha, Ukaguzi wa Ndani pamoja na kitengo cha Mifumo ya Habari na Mawasiliano. Wizara pia inasimamia Taasisi za elimu ya juu zikiwamo Vyuo Vikuu, Vyuo Vikuu vishiriki, Vyuo vya Ufundi, Mamlaka ya Elimu Tanzania, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Tume ya Vyuo Vikuu *(Tanzania Commission for Universities*) pamoja na Baraza la Elimu ya Ufundi (*National Council for Technical Education).*

Mheshimiwa Spika, Wizara ina majukumu makuu manne (4) ambayo ni:-

- Kuandaa na kutathmini matokeo ya Sera mbalimbali zikiwemo Sera za Elimu ya juu, Ufundi, Sayansi na Teknolojia;
- Kuratibu na kusimamia uendeshaji wa shughuli za Vyuo Vikuu, Vyuo vya Ufundi na Taasisi za Umma zilizo chini ya Wizara;
- Kuratibu shughuli za Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni (*UNESCO*) pamoja na mashirika mengine ya Kimataifa; na
- Kuratibu na kusimamia shughuli za *TEKNOHAMA.*

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya elimu ya juu, sayansi na teknolojia kati ya mwaka 1990 hadi mwaka 2006, Kama nilivyoeleza hapo awali, elimu ni nyenzo muhimu kwa ukuaji wa uchumi endelevu na katika kuboresha maisha ya binadamu. Tafiti nyingi zilizokwishafanyika zimedhihirisha kuwa mchango wa elimu, hususan elimu ya juu una uhusiano wa moja kwa moja na ukuaji wa uchumi endelevu. Tafiti hizi pia zimeonyesha kuwa uwekezaji wa kina na makini katika elimu ya juu kwa mwaka mmoja huongeza pato la Taifa kwa asilimia 0.63. Katika kutambua hali hiyo, Wizara yangu inalenga kuhakikisha kuwa taifa linakuwa na misingi imara yenye kuipa uwezo wa kuwa mshindani katika nyanja za sayansi na teknolojia miongoni mwa jumuiya ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1990 Taifa lilikuwa na vyuo vikuu viwili (2) na vyuo vya ufundi vitatu (3). Vyuo vikuu hivyo ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam sehemu ya Mlimani na Muhimbili, pamoja na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo. Vyuo vya Ufundi vilikuwa ni Chuo cha Dar es Salaam *(Dar es Salaam Technical College*), Chuo cha Ufundi Mbeya *(Mbeya Technical College)* na Chuo cha Ufundi Arusha (*Technical College Arusha*). Idadi ya wanafunzi katika vyuo vyote hivi ilikuwa wanafunzi 5,212 na hapakuwepo na chuo chochote cha binafsi. Nafurahi kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa hadi mwezi Mei, 2006 idadi ya vyuo vikuu pamoja na vyuo vikuu vishiriki vya umma na vya binafsi imefikia thelathini (30). Kati ya vyuo hivyo kumi na moja (11) ni vya umma na kumi na tisa (19) ni vya binafsi. Kwa upande wa Taasisi za Elimu ya Ufundi, hadi sasa kuna taasisi tano (5) moja ikiwa ni ya binafsi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, idadi ya wanafunzi wote katika vyuo vikuu vya umma na binafsi kwa sasa imefikia wanafunzi 51,657 kati ya hao wanafunzi 17,305 sawa na asilimia 33.5 ni wanawake. Kwa upande wa Taasisi za Elimu ya Ufundi na Taasisi zingine za Elimu ya Juu ambazo sio Vyuo Vikuu, idadi ya wanafunzi imefikia 16,372 kati yao wanafunzi 2,390 sawa na asilimia 14.6 ni wanafunzi wa kike.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sayansi, Teknolojia na Utafiti, Wizara imechukua hatua za kuhakikisha kuwa Sera za Sayansi, Teknolojia na Utafiti zinatayarishwa na kutekelezwa kwa lengo la kuwatoa wananchi katika lindi la umasikini. Aidha, utafiti huu unatekelezwa kwenye maeneo yanayolenga kuongeza uzalishaji, kutafuta nishati mbadala, kuhifadhi mazingira, uzalishaji wa maji safi na salama na ya bei nafuu. Utafiti shirikishi (*Participatory Research)* unahimizwa ili uwe endelevu na kuharakisha kupeleka teknolojia kwa wananchi. Mipango inabuniwa ili kuwapa motisha watafiti wenye uwezo kupata *Research Fellowships* katika maeneo maalumu.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa malengo ya mwaka 2005/2006, idara ya elimu ya juu, katika mwaka wa fedha 2005/2006, Idara ya Elimu ya Juu ilitekeleza yafuatayo:-

- Iliratibu uanzishwaji wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu.
- Iliratibu uanzishwaji wa Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania ambayo imechukua nafasi ya lililokuwa Baraza la Ithibati la Elimu ya Juu (*Higher Education Accreditation Council*).
- Ilianza kuhuisha Sera ya Elimu ya Juu ya mwaka 1999.

- Iliendelea kudhamini wanafunzi madaktari 1,427 katika vyuo vikuu nchini.
- Iliendelea kugharimia mafunzo ya wanataaluma themanini (80) katika vyuo vikuu vya umma.
- Iliratibu ukamilishaji wa kanuni za utekelezaji wa Sheria Na. 7 ya Vyuo Vikuu ya mwaka 2005 ambazo zimeanza kutumika baada ya kuchapishwa kwenye gazeti la Serikali Na. 39 la tarehe 21 Aprili, 2006.
- Ilielimisha wanafunzi na umma kwa ujumla kuhusu upatikanaji wa nafasi za elimu ya juu nchini na nje ya nchi.
- Ilielimisha wadau kuhusu upatikanaji wa mikopo kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu.
- Iliendeleza ushirikiano na Jumuiya ya Afrika Mashariki, Nchi za Jumuiya ya Madola na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*).

Mheshimiwa Spika, Idara ya Elimu ya Ufundi, katika mwaka wa fedha 2005/2006, Idara ya Elimu ya Ufundi ilitekeleza yafuatayo:-

Iliandaa na kuendesha warsha ya Wadau ili kuiboresha rasimu ya Sera ya Elimu ya Ufundi na mafunzo inayohuishwa. Iliendelea kugharimia mafunzo ya wanataaluma 23 na watumishi wengine wanne (4) katika vyuo na taasisi za ufundi. Ilikamilisha uteuzi wa wajumbe wa Bodi ya Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya na Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere. Ilidhamini wanafunzi elfu moja mia tano na moja (1,501) wa mafunzo ya ufundi sanifu katika vyuo/taasisi za ufundi.Iliratibu matumizi ya mitaala mipya ya *National Technical Awards (NTA* 4-6) katika ngazi ya ufundi sanifu katika vyuo na taasisi za ufundi.

Mheshimiwa Spika, idara ya sayansi na teknolojia, katika mwaka wa fedha 2005/2006, Idara ya Sayansi na Teknolojia ilitekeleza yafuatayo:

Iliandaa Nyaraka za Baraza la Mawaziri zenye lengo la kusimamia matumizi ya sayansi na teknolojia kwa maendeleo ya Taifa. Nyaraka hizo zilihusu: Kutunga Sheria ya Kuendeleza Sayansi na Teknolojia Tanzania. Kutunga Sera ya Taifa ya Bioteknolojia.

Kuridhia Mkataba wa Kimataifa unaohusu kujiunga na kituo cha Kiafrika cha Mafunzo ya Teknolojia (*The African Center For Technology Studies (ACTS*) kilichopo Nairobi Kenya. Mkataba huu unahusu kujiunga na Taasisi ya Kimataifa inayohusika na masuala ya Sera za Utafiti, mafunzo, ushauri na usambazaji wa habari za matokeo ya tafiti mbalimbali.

Kuridhia Mkataba unaohusu uimarishaji wa Mifumo ya Menejimenti na Uhifadhi wa Malighafi za Mitambo ya Nyuklia (*Convention on Radioactiove Waste Management and Spent Fuel*) zilizotumika pamoja na Mabaki ya Vifaa vya Mionzi Ayonisha (*Ionizing Radiation*). Kuendesha warsha za wadau kwa lengo la:

(i) Kuhuisha Sheria Na. 7 ya mwaka 1986 iliyounda Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania (*COSTECH*).
(ii) Kuhuisha Sera ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia ya mwaka 1996.
(iii)Kuandaa Sera ya Taifa ya Utafiti.

Kufanya majadiliano ya kuanzisha ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali za: Switzerland kwa lengo la kuendeleza miundombinu ya asasi za Utafiti na Maendeleo.India katika masuala ya uanzishaji wa vituo vya Sayansi na Teknolojia nchini. Iliendelea na maandalizi ya uanzishwaji wa Taasisi ya Kujenga Uwezo wa Maarifa na Kuendeleza Sayansi na Teknolojia nchini itakayojulikana kwa jina la Taasisi ya Nelson Mandela ya Sayansi na Teknolojia (Nelson Mandela *Institute of Science and T echnology).* Ilitoa elimu kwa umma kupitia Redio Tanzania Dar es Salaam Kuhusu umuhimu wa utumiaji wa sayansi na teknolojia katika kukuza uchumi na kuondoa umasikini. Vipindi 52 vilirushwa hewani. Ilifanya tathmini za usambazaji wa matokeo ya tafiti mbali mbali katika mikoa ya Kanda ya Mashariki. Mikoa husika ni mkoa wa Pwani, Morogoro na Dar es Salaam.

Lengo la tathmini hii ilikuwa kuangalia njia mbali mbali zilizotumika na Taasisi mbali mbali za Utafiti zilizopo katika mikoa hiyo kufikisha matokeo ya utafiti kwa walengwa.

Mheshimiwa Spika, ili kuwahamasisha wasichana wengi kujiunga na fani ya sayansi, teknolojia na uhandisi katika ngazi mbali mbali za elimu, wizara yangu ilitoa Tuzo ya Wizara kwa wasichana hamsini (50), wakiwamo kumi na mmoja (11) wa Kidato cha Nne, kumi na mmoja (11), Kidato cha Sita na ishirini na nane (28) kutoka Vyuo vya Elimu ya Juu (Umma na Binafsi) waliofanya vizuri na kuongoza kwa upande wa wasichana katika masomo ya sayansi ya msingi katika mitihani ya mwisho wa mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Sera na mipango, katika Mwaka wa fedha 2005/2006

Idara ya Sera na Mipango ilitekeleza yafuatayo:-

- Ilikamilisha utayarishaji wa Mpango mkakati wa Wizara (2006/2007-2009/2010).
- Ilikamilisha kuandaa Mpango wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2005.
- Iliratibu utekelezaji wa miradi ya maedeleo 27, kati ya miradi hiyo, 14 ni miradi ya ndani na 13 ni miradi ya nje.
- Iliratibu ukusanyaji, uchambuzi na uandaaji wa kitabu cha takwimu za Wizara kuhusu hali ya Elimu ya Juu na ya Elimu ya Ufundi nchini.
- Iliratibu zoezi la kupata kampuni elekezi (*consulting firm)* kwa lengo la kufanya upembuzi yakinifu wa Vyuo vya elimu baada ya Sekondari kwa ajili ya kuvihuisha (*Survey and Mapping of Post Secondary Education Institutions*).

- Iliandaa rasimu ya Programu nane (8) za uwekezaji katika elimu ya Juu na ufundi nchini.
- Ilianza upembuzi yakinifu wa Chuo Kikuu kipya ambacho kitajengwa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, idara ya utawala na utumishi, Katika mwaka wa fedha 2005/2006 Idara ya Utawala na Utumishi ilitekeleza yafuatayo:

Iliwalipia Watumishi hamsini na tisa (59) mafunzo ili kuwaongezea ujuzi, maarifa na ufanisi katika utendaji wa kazi. Watumishi 57 wamefanikiwa kupata sifa zinazohitajika katika miundo inayotawala kada zao za Utumishi.

Iliwapatia Watumishi sabini (70) mafunzo ya kompyuta na mifumo ya habari *(IT)* ndani na nje ya nchi.

Ilishirikisha Sekta binafsi katika utoaji wa huduma zisizo rasmi (*Non-Core Services)* katika Vyuo vya Ufundi vya Mbeya na Arusha hususan huduma za ulinzi, usafi na chakula.

Iliajiri watumishi hamsini na mmoja (51). Kati ya hao thelathini na tisa (39) ni kwa ajili ya Vyuo vya Ufundi vya Arusha na Mbeya na kumi na wawili (12) ni kwa ajili ya makao makuu ya Wizara.

Iiliratibu upatikanaji wa kibali cha kuajiri watumishi mia nne na tano (405) katika Vyuo Vikuu na Taasisi zake kwa lengo la kupunguza uhaba wa wafanyakazi.

Ilihuisha Mpango Mkakati wa elimu ya UKIMWI sehemu za kazi utakaotekelezwa na Wizara, Vyuo Vikuu na Taasisi zilizo chini ya wizara.

Iliendesha semina kwa watumishi mia moja na ishirini (120) kuhusu faida ya upimaji hiari wa virusi vya UKIMWI, lishe bora kwa watu waishio na virusi vya UKIMWI na jinsi wanavyoweza kupata dawa za kurefusha maisha kupitia mpango wa taifa ulioanzishwa.

Iliratibu utafiti kwa lengo la kuhuisha mitaala ya vyuo vya Elimu ya Juu kwa kuingiza elimu ya UKIMWI.

Iliwapatia watumishi wapya 16 mafunzo ya awali kuhusu utendaji kazi katika utumishi wa umma *(Public Service Orientation Programme*) na,

Iliendesha mafunzo kwa watumishi 130 kuhusu kutumia mfumo wa wazi wa kupima utendaji kazi kwa watumishi wa umma *(Open Performance Review and Appraisal System* (*OPRAS*).

Mheshimiwa Spika, Vyuo Vikuu, Chuo Kikuu cha Dar es salaam, katika mwaka wa fedha 2005/2006, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilitekeleza yafuatayo:-

- Kilidahili wanafunzi 4,702 ikiwa ni ongezeko la wanafunzi 634 sawa na asilimia 15 ikilinganishwa na idadi ya wanfunzi 4,068 katika mwaka 2004/2005.
- Kilifanya tathmini ya mitaala kwa lengo la kuiboresha ili iwiane na soko la ajira.
- Kiliimarisha ufundishaji kwa kutumia teknolojia ya mawasiliano *(ICT).*
- Kiliendelea kutoa mafunzo katika ngazi mbalimbali ili kuhakikisha chuo kinaendelea kuwa na wataalamu wengi wenye elimu bora.

- Kiliendeleza ushirikiano na taasisi za ndani na nje ya nchi katika kugharimia utafiti kulingana na sera ya chuo na vipaumbele vya taifa.
- Kiliendeleza juhudi za kuleta uwiano wa jinsia kwa kutoa masomo maalum kwa wasichana wanaotaka kujiunga na programu za Sayansi, Uhandisi na Teknolojia, Uchumi na Takwimu.
- Kiliendeleza ujenzi wa madarasa mawili makubwa yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi elfu moja kila moja.
- Kiliendelea na ujenzi wa awamu ya kwanza ya sehemu ya Buyu Zanzibar, ambako ndiko kutakuwa na makao mapya ya Taasisi ya Sayansi za Bahari.
- Kiliendeleza ujenzi wa mradi wa *"Mlimani City"* ambao ujenzi wake *"physical structure"* umefikia asilimia themanini (80). Uwekaji wa njia za umeme na maji unaendelea.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo,katika mwaka wa fedha 2005/2006 Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kilitekeleza yafuatayo:-

Kilidahili wanafunzi 830 wa shahada ya kwanza ikiwa ni ongezeko la asilimia 8 kutoka idadi ya wanafunzi 768 waliodahiliwa mwaka 2004/05.Idadi ya wanafunzi wa shahada ya kwanza imefikia2,260.

Kiliendelea na utafiti unaolenga kuboresha kilimo, mifugo na maliasili.

Kiliendelea kufundisha wakulima mbinu bora za kilimo, urutubishaji wa ardhi na hifadhi ya mazingira, mfano:

Mradi wa kilimo mseto katika kijiji cha Gairo wa miti kwa matumizi ya malisho, kuni na kurutubisha ardhi. *(Sesbania Seban, Grilicidia Sepium, Leucaena Leucacephala)*

Ufugaji wa mbuzi wa maziwa na udhibiti wa magonjwa ya kuku (mdondo) katika milima ya Uluguru.

Uvunaji wa maji ya mvua katika maeneo ya Same, Dodoma na Shinyanga.

Matumizi ya wanyamakazi kijiji cha Kisilo – Njombe.

Kudhibiti wadudu waharibifu wa mazao yaliyohifadhiwa ghalani. Maeneo yaliyohusika ni Handeni, Mvomero na Iringa.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu Mzumbe,katika mwaka wa fedha 2005/2006 Chuo Kikuu Mzumbe kilitekeleza yafuatayo:

- Kilianza ujenzi wa mabweni yatakayoweza kuchukua wanachuo elfu moja (1,000), ofisi kwa ajili ya wahadhiri mia moja (100) na ukumbi wa mihadhara katika Kampasi kuu ya Mzumbe.
- Kilikamilisha kuweka samani kwenye Kampasi ya Dar es Salaam na Mbeya. Masomo yalianza rasmi mwezi Oktoba 2005 Dar es Salaam na Januari 2006 Mbeya.
- Kiliendelea kusomesha Wahadhiri ishirini na sita (26) ngazi ya Udaktari wa Falsafa na sita (6) ngazi ya shahada ya Uzamili.
- Kilidahili wanafunzi 1,323 wa shahada ya kwanza, wanafunzi 309 wa shahada ya uzamili na wanafunzi tisa (9), shahada ya udaktari wa Falsafa.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania,katika mwaka wa fedha wa 2005/2006 Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kilitekeleza yafuatayo:

- Kilidahili wanafunzi 11,000 ukilinganisha na wanafunzi 2747 wa mwaka 2004/05.
- Kilianzisha shahada mpya ya Sayansi katika TEKNOHAMA, yaani Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (*Bachelor of Science in Information, Communication and Technology* (*BSc.ICT*).
- Kiliendelea kuimarisha huduma za vituo vya mikoa kwa kuvipatia majengo ya kudumu, maabara za kompyuta na maktaba. Vituo vilivyohudumiwa ni Mbeya, Singida, Iringa, Kilimanjaro na Ruvuma. Ufuatiliaji kwa ajili ya mikoa mingine unaendelea.
- Kilianzisha mchepuo mpya wa shahada ya Elimu ya Ualimu *(Bachelor of Education (B.Ed.)*
- Kilitunuku shahada ya kwanza kwa wahitimu 387

Mheshimiwa Spika, Vyuo Vikuu Vishiriki,Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi za Afya Muhimbili,katika mwaka wa fedha 2005/2006 Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi za Afya Muhimbili kilitekeleza yafuatayo:-

- Kilikarabati na kuongeza uwezo wa maktaba ili kiweze kuhudumia wanafunzi 600 kutoka uwezo wa sasa wa wanafunzi mia mbili (200).
- Kilipata ardhi yenye ukubwa wa ekari 3,800 eneo la Kisokwa (Kinondoni) na Mloganzila (Kisarawe) kwa ajili ya upanuzi wa chuo.
- Kiliendeleza ukarabati wa hosteli zilizoko Barabara ya Chole, *Oysterbay* zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 600.
- Kiliendeleza ujenzi wa kumbi mbili za mihadhara zinazoweza kutumiwa na wanafunzi 350 kila moja pamoja na vyumba 40 kwa ajili ya ofisi za wahadhiri.
- Kilidahili jumla ya wanafunzi 250
- Kiliboresha ufanisi wa Idara ya Uhasibu kwa kutoa mafunzo ya ‘Accounts Software’ kwa wahasibu wote wa chuo.
- Kiliendeleza wanataaluma 43 katika masomo ya juu.
- Kilidhamini wafanyakazi waendeshaji 89 katika mafunzo mbalimbali ya utendaji.
- Kilitunuku shahada ya kwanza kwa wahitimu 253, shahada ya uzamili kwa wahitimu 32 na stashahada kwa wahitimu 171.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ardhi na Usanifu majengo, katika mwaka wa fedha 2005/2006 Chuo Kikuu Kishiriki cha Ardhi na Usanifu Majengo kilitekeleza yafuatayo:-

Kilikamilisha utayarishaji wa Mpango Endelevu wa Kimkakati ambao utaongoza utekelezaji wa majukumu ya Chuo kwa kipindi cha miaka mitano (2005/2006 – 2009/2010).

Kiliendelea na matayarisho ya kukifanya kuwa Chuo Kikuu kamili ifikapo mwisho wa mwaka wa fedha 2006/2007.

Kilidahili wanafunzi 399 wa mwaka wa kwanza na kufanya jumla ya wanafunzi wa shahada ya kwanza kuwa 1120. Kati ya hawa wanawake ni asilimia 16.
Kiliendelea kuimarisha uhusiano na taasisi za kimataifa kwenye maeneo ya utafiti.
Kilishughulikia miradi ya ushauri 52 ya taasisi za umma na 72 ya taasisi za binafsi.
Kiliimarisha matumizi ya teknolojia ya mawasiliano katika shughuli za ufundishaji.
Kiligharimia mafunzo ya wafanyakazi kwa lengo la kuwatayarisha kwa ajili ya muundo mpya wa utumishi.
Kilianza ukarabati wa baadhi ya majengo ya Chuo.
Kilikamilisha ujenzi wa tanki la maji lenye mita za ujazo mia sita (600).
Kilikamilisha ujenzi wa jengo jipya la utawala lenye idadi ya ofisi ishirini na moja (21) na vyumba vya madarasa kumi na moja (11) vyenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 526. Jengo hilo limeanza kutumika.
Kilitunuku shahada ya kwanza kwa wahitimu 291, na shahada za uzamili kwa wahitimu kumi na saba (17).

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar s Salaam, katika mwaka wa fedha 2005/2006 Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam kilitekeleza yafuatayo:-

Kilifanya ukarabati wa jengo la utawala, madarasa, maabara, maktaba na kugeuza ukumbi wa chakula kuwa ukumbi wa mihadhara.

Kiliweka samani katika vyumba vya kufundishia na kujifunzia.
Kilidahili wanafunzi mia tano thelathini na mbili (532) katika fani za Sayansi, Sayansi ya Jamii na Elimu. Kati yao wanafunzi wanawake ni mia tatu na mbili (302) sawa na asilimia 56.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa, katika mwaka wa fedha 2005/2006 Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa kilitekeleza yafuatayo:-
Kilikarabati mabweni yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,400.
· Kilikarabati madarasa, na majengo mengine ya chuo.
· Kilianza ukarabati wa barabara na mifumo ya maji safi na maji taka.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Biashara-Moshi, katika mwaka wa fedha 2005/2006 Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Biashara-Moshi kilitekeleza yafuatayo:-

· Kilikamilisha ukarabati wa ukumbi wa mihadhara wenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 482.
· Kiliboresha miundombinu kwa kuweka mtandao wa kompyuta katika maktaba.
· Kilidahili wanafunzi 750 kati yao wanafunzi wanawake ni 264 sawa na asilimia 35.2.

- Kiliendesha mafunzo ya *SACCOS* kwa njia ya *TEKNOHAMA* kwa maafisa Ushirika, Wakaguzi na Waendeshaji wa Ushirika kutoka Kanda nne (4) za Mashariki, Kati, Kusini na Ziwa.
- Kilitunuku Stashahada kwa wahitimu 200.

Mheshimiwa Spika, Taasisi, Taasisi ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma, katika mwaka wa fedha 2005/2006 Taasisi ya Habari na Mawasiliano ya Umma ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

- Ilidahili wanafunzi tisini na tisa (99) wa mwaka wa kwanza wa shahada ya kwanza na kufanya idadi ya wanafunzi wa shahada ya kwanza kuwa 189. Wanafunzi wanawake ni asilimia 55.

- Iliimarisha kituo cha redio *(Redio Mlimani FM*) ili matangazo yake yasikike sehemu nyingi nchini.
- Iliendeleza utafiti na kutoa ushauri katika maeneo ya Habari na Mawasiliano ya Umma.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Teknolojia Dar Es Salaam, katika mwaka wa fedha 2005/2006 Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam ilitekeleza yafuatayo:

Ilianza kutumia mitaala mipya inayozingatia umahiri katika ngazi ya Ufundi Sanifu.

Ilidahili wanafunzi 50 wa programu mpya ya Shahada ya Uhandisi wa Kompyuta *(Bachelors Degree in Computer Engineering).*

Iligharimia mafunzo ya watumishi thelathini na saba (37), kati ya hao sita (6) mafunzo ya Shahada ya kwanza, 15 mafunzo ya Shahada ya Uzamili na kumi na sita (16) mafunzo ya Udaktari wa Falsafa.

Ilidhamini wanafunzi wanawake hamsini na tatu (53) katika mafunzo maalum ya kuwawezesha kujiunga na Taasisi kwa kushirikiana na Mamlaka ya Elimu Tanzania *(TEA).*

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya, katika mwaka wa fedha 2005/2006, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya ilitekeleza yafuatayo:-

- Ilinunua na kufunga mitambo yenye thamani ya shilingi milioni 306 kwa lengo la kuboresha mafunzo yatolewayo.
- Ilinunua vitabu vya kiada na rejea vyenye thamani ya shilingi milioni 28.
- Iligharimia mafunzo ya watumishi wawili (2) wa Shahada ya kwanza, kumi na wanne (14) mafunzo ya Shahada ya Uzamili, wanne (4) Mafunzo ya Udaktari wa Falsafa na mmoja (1) Stashahada ya juu ya Uhandisi.
- Ilikamilisha ujenzi wa jengo la hosteli ya wasichana lenye nafasi sitini (60) za kulala.

Mheshimiwa Spika, Vyuo, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, katika mwaka wa fedha 2005/2006 Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kilitekeleza yafuatayo:

Kilikamilisha mitaala mitatu ya Shahada ya Kwanza katika fani za Sayansi Jamii, Jinsia katika Maendeleo na Maendeleo ya Uchumi.

Kilipata ithibati kamili (*Full Accreditation*) katika kiwango cha kutoa tuzo mpaka *"National Technical Awards level 8" (NTA 8) (Bachelor degree)* kuanzia tarehe 30 Novemba, 2005.

Kilianza ukarabati wa jengo la Utawala na madarasa Manne (4).

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Ufundi Arusha, katika mwaka wa fedha 2005/2006 Chuo cha Ufundi Arusha kilitekeleza yafuatayo:-

Kiligharimia mafunzo ya watumishi wanane (8) kati ya hao mmoja (1) ni wa shahada ya kwanza, wanne (4) ni mafunzo ya stashahada ya Uzamili, mmoja (1) ni mafunzo ya shahada ya Uzamili na wawili (2) ni kwa mafunzo ya udaktari wa falsafa *(Ph.D.)*.

Kilikarabati majengo na kununua vifaa mbalimbali.

Kilinunua vitabu vya kiada na rejea.

Kilikamilisha upanunzi wa bweni moja lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 100.

Mheshimiwa Spika, Tume, Tume ya Taifa ya *UNESCO,* katika mwaka fedha 2005/2006 Tume ya Taifa ya *UNESCO* ilitekeleza yafuatayo:-

Iliendelea na utekelezaji wa miradi kulingana na maamuzi ya Kikao cha 32 cha Mkutano Mkuu wa *UNESCO* kilichofanyika Paris nchini Ufaransa.

Baadhi ya miradi hiyo ni:-

Kuboresha Maktaba ya Kituo cha Madini cha Kusini na Mashariki mwa Afrika (*Southern and Eastern Africa Mineral Centre*) kilichoko Kunduchi Dar es Salaam.

Kuimarisha ufundishaji wa Elimu ya Tiba ya Wanyama (*Veterinary Medicine*) kwa kutumia Teknolojia ya Mawasiliano (*ICT*) katika Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine.

Kuendeleza watumishi na miundombinu katika Taasisi ya Sayansi ya Bahari-Zanzibar.

Kujenga Utamaduni wa Ukarabati wa Miundombinu na Vitendea Kazi *Culture of Maintenance* katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (*DIT*). Mradi huu unaratibiwa na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam.

Kutoa Elimu ya UKIMWI kwa watumishi wa Tume ya Walimu Kanda ya Ziwa, kwa lengo la kupunguza kasi ya maambukizo.

Kuratibu mafunzo ya muda mrefu na mfupi chini ya ufadhili wa *UNESCO* kwa kushirikiana na nchi wanachama.

Kuandaa Programu na Bajeti ya *UNESCO* kwa kipindi cha 2006-2007 kwa kushirikiana na Taasisi za Serikali na zisizo za Kiserikali.

Kuwashirikisha wataalamu katika warsha, mikutano na semina zilizofanyika ndani na nje ya nchi zilizoandaliwa na *UNESCO* Paris zilizolenga

kuwaongezea taaluma na utaalamu katika nyanja za Elimu, Sayansi, Utamaduni na Habari.

Iliongoza ujumbe wa Serikali uliohusisha viongozi wa ngazi za juu Serikalini na wataalamu mbalimbali katika masuala ya *UNESCO*, kwenye Kikao cha 33 cha Mkutano Mkuu wa *UNESCO* kilichofanyika tarehe 3-21 Oktoba 2005 mjini Paris nchini Ufaransa.

Ilifanya mapitio ya Katiba ya Tume ya Taifa ya *UNESCO* na kuandaa Rasimu ya Waraka wa Baraza la Mawaziri (*WBLM*) unaolenga kutunga Sheria ya kuundwa Tume huru ya *UNESCO* nchini. Rasimu imewasilishwa katika Sekretariati ya Baraza la Mawaziri kwa hatua zaidi.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania, katika mwaka wa fedha 2005/2006 Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania ambayo kabla ya kupitishwa sheria namba 7 ya mwaka 2005 ilijulikana kama Baraza la Ithibati la Elimu ya Juu, ilitekeleza yafuatayo:

- Ilitayarisha kanuni na taratibu mpya za kusajili vyuo vikuu chini ya sheria Na. 7 ya Vyuo Vikuu ya mwaka 2005. Kanuni hizo zimetolewa katika gazeti la Serikali kwa tamko Na. 39 la tarehe 21 April 2006.
- Iliandaa na kuratibu maonyesho ya kwanza ya Vyuo Vikuu na taasisi chini ya Wizara ili kujitangaza. Baadhi ya mafanikio ya maonyesho haya ni udhamini wa wanafunzi wanane (8) chini ya Kampuni ya *CELTEL*.
- Ilikagua na kutathmini mipango ya kuanzisha au kuvipandisha hadhi ya ithibati vyuo vikuu nchini. Kutokana na tathmini iliyofanyika, Tume imetoa hati mbalimbali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo,katika mwaka wa fedha 2005/2006 Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kilitekeleza yafuatayo:

(i) Kuhuisha na kuongeza muda wa Hati ya Mamlaka ya Kuanzisha Chuo Kikuu cha *Bishop* Kisanji, Mbeya na Chuo Kikuu cha Kiislam cha Azad, Zanzibar baada ya vyuo hivi kushindwa kutekeleza masharti.

(ii) Kuidhinisha uanzishwaji wa Kampasi za Chuo Kikuu Mzumbe za Mbeya na Dar es Salaam.

(iii) Ilitoa Hati ya usajili wa muda kwa Vyuo vinne (4) ambavyo ni:- Chuo Kikuu cha Kiislam Morogoro, Chuo Kikuu Kishiriki cha Mwenge cha Chuo Kikuu cha Mt. Augustino, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ruaha cha Chuo Kikuu cha Mt. Augustino na Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Biashara, Moshi.

(iv) Ilitoa Hati ya usajili kamili kwa vyuo vikuu vitatu ambavyo ni:-Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi za Afya Bugando, Chuo Kikuu cha *Mount Meru* na Taasisi ya Elimu ya Juu ya Chuo Kikuu cha Aga Khan.

(v) Ilitoa Hati ya Ithibati kwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Tumaini, Iringa.

- Ilifanya tathmini ya vyeti kwa lengo la kuvichambua. Kati ya vyeti 82 vilipokelewa, vyeti 60 vilifanyiwa tathmini na kutambuliwa.

- Vyeti vilivyobaki havikutambuliwa kutokana na sababu mbali mbali zikiwemo ukosefu wa taarifa za ithibati ya Vyuo vilivyotoa vyeti hivyo pamoja na wenye vyeti husika kutotimiza masharti ya Kitanzania ya kujiunga na masomo ya Vyuo Vikuu.
- Ilielimisha umma kuhusu:-

(i) Elimu ya Juu nchini na nje ya nchi kupitia machapisho ya Mwongozo wa Elimu ya Juu Tanzania

(ii) Vigezo vya uanzishwaji wa vituo mahiri (*Centres of Excellence*)
(iii) Kutambua taasisi au vyuo mbalimbali duniani ambavyo havina ithibati ya mamlaka zinazohusika na utoaji wa Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka, Mamlaka ya Elimu Tanzania, katika mwaka wa fedha 2005/2006, Mamlaka ya Elimu Tanzania ilitekeleza yafuatayo:

- Ilielimisha wadau kuhusu umuhimu wa kuchangia Mfuko wa Elimu kupitia televisheni, redio na majarida. Mamlaka imekamilisha ziara za uhamasishaji kwa mikoa yote ya Tanzania Bara.
- Ilitayarisha sera ya kuwekeza katika vitega uchumi ikiwa ni hatua ya kuongeza vyanzo vya mapato vya Mfuko wa Elimu.
- Ilikamilisha taratibu za ushirikiano kati ya Mfuko wa Elimu na Halmashauri za Wilaya za Maswa, Karagwe, Kinondoni, Ilala na Musoma vijijini.
- Ilitoa ruzuku kwa taasisi za elimu na shule kwa lengo la kuleta mabadiliko ya haraka katika kuongeza ubora wa elimu na upatikanaji wake. Jumla ya Shilingi Bilioni 22.7 zimetumika kufadhili taasisi na shule 174.
- Ilifunga mtandao wa mawasiliano ya kompyuta kwa ajili ya kuimarisha uwekaji wa kumbukumbu.

Mheshimiwa Spika, Bodi, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu Ya Juu,katika mwaka wa fedha 2005/2006 Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ilitekeleza yafuatayo:

- Ilitoa mikopo kwa wanafunzi 42,729 katika vyuo vikuu na vya Elimu ya Juu nchini na nje ya nchi. Jumla ya Shilingi Bilioni 62.5 zilitumika.
  Mikopo ilitolewa katika maeneo yafuatayo:-
  Ada ya masomo;
  Chakula na malazi;
  Vitabu na viandiko;
  Elimu kwa vitendo; na
  Mahitaji maalum ya vitivo.
- Iliajiri Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu.
- Iliandaa mfumo utakaotumika kuwatambua wanafunzi wanaostahili kupewa mikopo na uwekaji wa kumbukumbu za wanafunzi waliokopeshwa (Loan Management System)

- Ilipitia Sheria Na. 9 ya mwaka 2004 ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi kwa lengo la kuihuisha.
- Ilihuisha fomu za mikopo na vigezo vitakavyotumika kuwakopesha wanafunzi watakaodahiliwa kuanzia mwaka wa masomo 2006/2007.
- Iliajiri watumishi ishirini na tisa (29) kati ya nafasi themanini na sita (86) zilizoidhinishwa.
- Ilinunua vitendea kazi vikiwemo kompyuta thelathini (30) samani za ofisi na jenereta ya umeme.

Mheshimiwa Spika, Tume, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia, katika mwaka wa fedha 2005/2006 Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia ilitekeleza yafuatayo:-

(i) Ilihawilisha teknolojia mbali mbali kama ifuatavyo:
(ii) Teknolojia ya matumizi ya makaa ya mawe yaliyoboreshwa kwa matumizi ya nyumbani katika wilaya ya Sumbawanga kwa kushirikiana na Kampuni ya "Upendo Group" yenye machimbo ya makaa ya mawe Wilayani Sumbawanga.

(iii) Kwa kushirikiana na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo Vidogo (*SIDO*) teknolojia ya kutengeneza jiko bora ilisambazwa katika mikoa ya Manyara, Mbeya, Shinyanga, Morogoro, Singida, Dodoma na Dar es Salaam.

· Kwa kushirikiana na *World Interlectual Property Organization* (*WIPO*) pamoja na "*Business Registration and Lincencing Authority*" (*BRELA*), Tume imeanzisha Kituo cha Haki Miliki na Huduma za Ushauri "*Interlectual Property and Advisory Services Centre" (IPASC)* kwa ajili ya kutoa elimu kwa umma kuhusu haki miliki. Kituo hiki kipo ndani ya jengo la Tume ya Sayansi na Teknolojia (*COSTECH*).· Iliandaa kongamano mbalimbali yakiwemo;

(vi) Kongamano la wanasayansi, wanateknolojia na watafiti 200 lililoambatana na maonyesho ya sayansi kwa vijana, iliyofanyika tarehe 24 – 26 mwezi Mei 2006 jijini Dar es Salaam.

(vii) Kongamano la kitaifa la wadau wa baioteknolojia kujadili uanzishwaji wa Chama cha Wanabaioteknolojia Tanzania (*Biotechnolgy Association of Tanzania)* lililofanyika Mhasibu *House*, Dar es Salaam tarehe 22 Machi 2006.

(viii) Kongamano la kitaifa kuhusu kutathmini athari zinazotokana na matumizi ya baioteknolojia lilofanyika Dar es Salaam tarehe 18 Aprili 2006.
· Kwa msaada wa Shirika la Maendeleo la Sweden (SIDA) Tume ilianzisha ushirikiano na Taasisi ya Anga ya Sweden *(Swedish Space Agency)* utakaowezesha upatikanaji wa mhimili wa mfumo wa *Internet* wa gharama nafuu (*Affordable Internet Bandwidth)* ili kuwezesha usambazaji wa *Internet* kwa bei nafuu kwa ajili ya vijiji zaidi ya mia moja (100). Kwa hivi sasa usambazaji wa majaribio unafanyika katika maeneo ya Bunda na Mugumu mkoani Mara, Wami na Chalinze mkoani Pwani.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania, katika mwaka wa fedha 2005/2006 Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania, ilitekeleza yafuatayo:-

· Ilitoa elimu ya kinga ya mionzi kwa njia za redio na *television*. Aidha, iliendesha semina tano (5), moja kati ya hizo ikiwa ni kwa watumishi wa mionzi (*Radiographers*), mbili (2) kwa ajili ya wafanyakazi katika migodi na moja kwa ajili ya watumishi walio mstari wa mbele (hasa Polisi) katika kushughulikia dharura za mionzi.

· Iliratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi minane (8) ya Kitaifa na Kikanda inayogharimiwa na Shirika la Kimataifa la Nguvu za *Atomic* "*International Atomic Energy Agency" (IAEA)* inayotumia tekinolojia ya mionzi hapa nchini. Shirika hilo lilizipatia taasisi husika zaidi ya Dola za Kimarekani 890,000 kama vifaa, mafunzo na ushauri wa kitaalamu ambapo kiasi cha dola za Kimarekani 100,400.00 zitatumika katika mradi wa kubaini na kutathimini upatikanaji wa maji katika bonde la Ruvu.

· Ilikusanya na kuvihamisha vyanzo vya mionzi vitano (5) toka Chuo cha Utafiti wa Mbung'o kilichopo Tanga "Tanga *Trypanasomiasis Research Institute*" (*TTRI*), Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road* baada ya kupatiwa msaada na shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki na kuvihifadhi katika maabara yake.

· Iligharimia mafunzo kwa wafanyakazi wawili (2) katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa mafunzo ya shahada ya Uzamili katika fani za Sayansi na Sheria.

· Iliimarisha Maktaba ya kupatia taarifa za Kimataifa na elimu ya nyuklia "*International Nuclear Information System" (INIS).* Maktaba hii imeanzishwa kwa kupitia mradi wa "*International Atomic Energy Agency" (IAEA).*

· Kupitia mradi wa Ushirikiano wa Wizara ya Nishati ya Marekani *(United States of America – USA Department of Energy – DOE),* Tume iliendelea kuimarisha usalama katika vituo vyenye vyanzo vya mionzi kwa kuweka vyombo vya kutoa tahadhari *(Security Alarm Systems* na *Radio Call).* Vituo hivyo ni "*Ocean Road Cancer Institute"* na *"Central Radioactive Waste Management Facility*" (*CRWMF*) iliyoko Njiro, Arusha.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi, katika mwaka wa fedha 2005/2006 Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi lilitekeleza yafuatayo:-

- Lilitathimini na kutoa ithibati kamili (*Full Accreditation*) kwa vyuo tisa (9).
- Lilitoa Ithibati andalizi (*Candidacy Accreditation*) kwa vyuo na taasisi ishirini na moja (21) za Ufundi.
- Lilitoa usajili kamili kwa vyuo kumi na viwili (12) na usajili wa muda kwa vyuo vinane (8).
- Liliidhinisha mitaala minne (4) ngazi ya shahada ya kwanza na mitaala kumi na minne (14) ngazi ya Cheti na Stashahada.
- Liliweka viwango vya mafunzo kwa programu nne (4) zifuatazo:-

Usimamizi Ardhi na Uthamini (*Land Management, Valuation and Administration).*

Urasimu Ramani (*Cartography*).

Uchapaji wa Ramani kwa komputa(*Graphical Arts and printing).*

Upimaji Ardhi (*Land Surveying*).

Mheshimiwa Spika, Malengo ya Mwaka 2006/2007, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia imejiwekea malengo yafuatayo.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Elimu ya Juu, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Idara ya Elimu ya Juu inatarajia kutekeleza yafuatayo:-

- Kuwadhamini wanafunzi shahada ya kwanza 1,500 katika programu ya udaktari (MD) katika vyuo vikuu hapa nchini.
- Kudhamini wanafunzi tisini (90) raia wa Uganda ikiwa ni kutekeleza utaratibu wa kubadilishana wanafunzi wa shahada ya kwanza katika vyuo vikuu vya Afrika Mashariki.

- Kudhamini mafunzo wanafunzi watano, raia wa China, ikiwa ni kutekeleza mkataba wa ushirikiano kati ya Tanzania na China.
- Kuendelea kuelimisha umma juu ya Sera ya uchangiaji gharama za elimu ya juu.
- Kukamilisha kazi ya kuhuisha Sera ya Elimu ya Juu ya mwaka 1999.

- Kudhamini mafunzo ya wanataaluma themanini (80) katika idara ambazo zina upungufu mkubwa wa wahadhiri, katika vyuo vikuu vya umma.
- Kutokana na ongezeko la udahili wa wanafunzi katika Elimu ya Juu kufikia idadi ya 68,029 mwaka 2006/2007, ushiriki wa Tanzania kwa lika husika kwa Elimu ya Juu umepanda kutoka asilimia 0.27 ya mwaka 1997 na kufikia asilimia 1.219. Ongezeko hili la ushiriki katika Elimu ya Juu unakwenda sambamba na ubora wa elimu itolewayo kwa kuhakikisha kuwa mitaala ya Elimu ya Juu inakidhi mahitaji ya soko la ajira pamoja na kujiajiri.

  Aidha, lengo la Wizara ni kuongeza ushiriki wa lika husika katika Elimu ya Juu kutoka asilimia 1.219 mwaka 2006/2007 na kufikia asilimia 2.0 ifikapo mwaka 2010.

  Wizara itaendelea kutekeleza agizo la Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete alipotembelea Wizara yangu tarehe 01 Februari, 2006 kwamba; **“**katika kupanua Elimu ya Juu Wizara na Wadau wengine wasigeuze Taasisi nyingine za Elimu ya kati na shule za sekondari kuwa Vyuo Vikuu, kwani umuhimu wa Taasisi hizo na shule za sekondari bado upo palepale.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Elimu ya Ufundi, katika mwaka wa fedha 2006/2007, Idara ya Elimu ya Ufundi inatarajia kutekeleza yafuatayo:

- Kudhamini mafunzo kwa wanafunzi 1,754 katika ngazi ya Ufundi Sanifu katika Vyuo na Taasisi za Ufundi zilizo chini ya Wizara.
- Kukamilisha kuhuisha Sera ya Elimu ya Ufundi ya mwaka 1996.
- Kugharimia mafunzo ya watumishi kumi na wawili (12) wa Chuo cha Ufundi Arusha na Makao Makuu katika ngazi ya udaktari wa falsafa (4), Shahada ya Uzamili (8).
- Kuratibu na kugharamia mafunzo maalum ya ualimu (Pedagogical Skills) kwa walimu wahandisi 23 watakaoajiriwa.
- Kuhamasisha wasichana katika shule za sekondari ili waweze kujiunga na Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa wingi.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Sayansi na Teknolojia, katika mwaka 2006/2007, Idara ya Sayansi na Teknolojia inatarajia kutekeleza yafuatayo:-

- Kukamilisha utungaji wa Sera ya Taifa ya Utafiti.
- Kukamilisha uandaaji wa Muswada wa Sheria ya Kuendeleza Sayansi na Teknolojia Tanzania.
- Kukamilisha uhuishaji wa Sera ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia na Sheria Na. 7 ya mwaka 1986 iliyoanzisha Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia.
- Kuendelea na uanzishaji wa Taasisi ya Kujenga Uwezo wa Maarifa na Kuendeleza Sayansi na Teknolojia nchini itakayojulikana kwa jina la Taasisi ya Nelson Mandela.
- Kuandaa mkakati wa uhamasishaji wa wanafunzi wa kike ili waweze kujiunga katika masomo ya sayansi, teknolojia na uhandisi katika ngazi mbali mbali za elimu.
- Kukamilisha uundaji wa Kamati ya Kitaifa ya Elimu ya Sayansi nchini.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Sera na Mipango, katika mwaka wa fedha 2006/2007, Idara ya Sera na Mipango inatarajia kutekeleza yafuatayo:-

- Kuratibu utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2005.
- Kuratibu utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayoendelea na ile itakayoidhinishwa katika kipindi cha mwaka 2006/2007.
- Kuratibu upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Chuo Kikuu kipya Dodoma.
- Kuratibu Uhuishaji wa Sera tatu (3) za Wizara, (Sera ya Elimu ya Juu, Elimu ya Ufundi na Sera ya Sayansi na Teknolojia)
- Kuratibu shughuli za Ushirikiano wa Kimataifa.
- Kukamilisha zoezi la uhuishaji wa vyuo vya elimu ya kitaalam (*Rationalization of Post Secondary Instituttions).*
- Kukamilisha program nane (8) za uwekezaji katika Elimu ya Juu na Elimu ya Ufundi.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Utawala na Utumishi, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Idara ya Utawala na Utumishi inatarajia kutekeleza yafuatayo:-

Kuajiri watumishi 14 kwa ajili ya makao Makuu na Chuo cha Ufundi Arusha.
Kugharimia mafunzo mbalimbali ya watumishi thelathini (30) ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi.
Kuendelea kutekeleza mkakati wa kuwaelimisha wananchi na watumishi kupitia vyombo vya habari kuhusu taratibu za kupata huduma zinazotolewa na wizara.
Kutekeleza mfumo wa uwazi wa upimaji utendaji kazi wa watumishi wa umma.
Kushirikiana na vyuo vya Elimu ya Juu katika kuhuisha mitaala ili kuingiza masuala ya elimu ya UKIMWI.

Kuendelea kushirikisha sekta binafsi katika utoaji wa huduma zisizo rasmi (non-core services) za ulinzi, mapokezi, usafi na chakula makao makuu ya wizara na Chuo cha Ufundi Arusha.

Kuendelea kuhamasisha watumishi kupima afya zao kwa hiari hususan virusi vya UKIMWI na kutoa huduma kwa wale watakaojitokeza kuwa wameathirika na VVU/UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, Vyuo Vikuu,Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam (Kampasi Kuu),katika mwaka wa fedha 2006/2007 Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinatarajia kutekeleza yafuatayo:

- Kudahili jumla ya wanafunzi 4,075.
- Kuendelea na utaratibu wa kuboresha mitaala kwa kuifanyia tathmini kila mwaka.
- Kuendeleza juhudi za kutumia teknolojia ya mawasiliano (*ICT*) katika ufundishaji na kujifunzia kwa kutumia kitengo cha "*Centre of Countinuing Education*" (*CCE*) kuwafundisha wahadhiri mbinu mpya na bora za kufundishia pamoja na kuimarisha mtandao wa ndani "*Local Area Network*" (*LAN*).
- Kuajiri na kutoa mafunzo katika ngazi mbalimbali kwa wataalamu kwenye idara zenye upungufu mkubwa wa wafanyakazi.
- Kuendelea kushirikiana na taasisi za ndani na nje ya nchi kugharamia utafiti kulingana na sera ya utafiti ya Chuo. Chuo kitaweka juhudi zake kuhakikisha kuwa matokeo ya utafiti yanasambazwa kwa walengwa.
- Kuendelea kutumia mikakati mbalimbali pamoja na kutoa mafunzo maalum kwa wasichana wanaotaka kujiunga na programu za sayansi, uhandisi na teknolojia, uchumi na takwimu; ili kuinua uwiano wa wavulana na wasichana.
- Kukamilisha ujenzi wa madarasa makubwa mawili yenye uwezo wa kutumiwa na wanafunzi 1000 kila moja kwa wakati mmoja.
- Kukamilisha ujenzi wa awamu ya kwanza ya Taasisi ya Sayansi za Baharini iliyopo Buyu Zanzibar.
- Kukamilisha ujenzi wa kitengo kitakachotumiwa na kituo cha ujasiriamali.

- Kuendelea na ujenzi wa awamu ya kwanza ya mradi wa *“Mlimani City”*.

- Kuendeleza majadiliano na Kampuni ya Simu Tanzania (*TTCL*) ili chuo kikabidhiwe rasmi majengo ya kilichokuwa Chuo cha Wafanyakazi wa Kampuni ya Simu eneo la Kijitonyama.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo,katika mwaka wa fedha 2006/2007 Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine kinatarajia kufanya yafuatayo:

- Kudahili jumla ya wanafunzi wa shahada ya kwanza 820 na 300 wa shahada za juu.
- Kuimarisha mafunzo ya shahada za kwanza, uzamili na shahada za Juu za Falsafa.
- Kuimarisha miradi ya utafiti unaoshirikisha wakulima.
- Kufanya warsha/kongamano za kisayansi ambazo wanataaluma na wadau ndani na nje ya nchi watajadili matokeo ya utafiti na matumizi yake.
- Kuendesha kozi fupi, warsha, mikutano na semina na kutoa huduma za ushauri wa kilimo, utunzaji na usimamizi wa mali ya asili, misitu na ufugaji kwa wakulima na wafanyakazi.

- Kuendeleza miradi ya maendeleo kama ifuatavyo:-

Kukarabati majengo, (mabweni 5 na nyumba 20) na mtandao wa mabomba ya maji.

Kuanza ujenzi wa chanzo mbadala cha maji katika Kampasi ya Solomon Mahlangu.

Kuendelea na ujezi wa vyumba viwili vya mihadhara, vyenye uwezo wa kukaa wanafunzi 500 kila kimoja kwa wakati mmoja.

Kununua samani kwa ajili ya maabara ya Zoolojia, Jengo la Ujasiriamali na Biashara, na Jengo la Maktaba lililopo Kampasi ya Solomoni Mahlangu.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu Mzumbe, katika mwaka fedha 2006/2007 Chuo Kikuu Mzumbe kinatarajia kufanya yafuatayo:

- Kudahili jumla ya wanafunzi elfu moja (1000)
- Kukamilisha ujenzi wa mabweni ya wanafunzi yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi elfu moja (1,000) pamoja na ofisi za wahadhiri.
- Kujenga maktaba yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,000 katika Kampasi ya Mbeya.
- Kujenga ukumbi wa mihadhara wenye uwezo wa kutumiwa na wanafunzi 300 katika Kampasi ya Mbeya.
- Kuendelea kusomesha wahadhiri 14 ngazi ya Shahada ya Udaktari wa Falsafa na 13 ngazi ya Shahada ya uzamili.

- Kukamilisha tafiti 5 maeneo ya Sayansi ya Jamii.
- Kununua kompyuta 100 kwa ajili ya matumizi ya wahadhiri.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kinatarajia kufanya yafuatayo:

- Kudahili jumla ya wanafunzi 5000.
- Kuendelea kuboresha ofisi za wafanyakazi makao makuu na katika mikoa ya Iringa, Kilimanjaro na Ruvuma, Rukwa, Mtwara na Manyara.
- Kuongeza idadi ya wafanyakazi wanataaluma na waendeshaji mikoani.
- Kuongeza maabara za kompyuta katika vituo vya mikoa na kuweka mtandao wa ndani "*Local Area Network"(LAN*) katika vituo 5 vya mikoa.
- Kuanzisha mafunzo ya ngazi ya cheti, stashahada na kozi fupi za ujasiriamali ili kuimarisha uwezo wa wananchi kushiriki kikamilifu kwenye "MKUKUTA".
- Kuanza utekelezaji wa mpango wa matumizi bora ya ardhi ya ekari 105 eneo liliko Kibaha.
- Kuendelea kuongeza idadi ya wanafunzi wa kike.
- Kuimarisha ushirikiano na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa lengo la kuongeza idadi ya walimu wanafunzi.
- Kuendesha mafunzo maalum kwa walimu wa masomo ya Sayansi, Hisabati na Teknolojia katika kituo cha "*Open and Distance Education Learning Centre"(ODEL Centre),* kilichopo makao makuu ya Chuo Kikuu Huria.

Mheshimiwa Spika, Vyuo Vikuu Vishiriki, Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi za Afya Muhimbili,katika mwaka wa fedha Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi za Afya Muhimbili kinatarajia kufanya yafuatayo:

- Kudahili jumla ya wanafunzi 300.
- Kukamilisha ukarabati wa hosteli za wanafunzi zilizopo Barabara ya Chole Dar es Salaam pamoja na kuweka samani.
- Kukamilisha ujenzi wa kumbi mbili (2) za kufundishia zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 350 kila moja kwa wakati mmoja na vyumba 40 vya ofisi.
- Kuanza kujenga barabara katika ardhi ya Chuo iliyopo Kisokwa na Mloganzila.
- Kukamilisha taratibu za kukipandisha hadhi kuwa Chuo Kikuu Kamili.
- Kuendelea na utafiti wa magonjwa ya binadamu hususan UKIMWI, Kifua kikuu, Malaria na magonjwa ya wanawake.
- Kuboresha mbinu za kufundishia wanafunzi kwa kutumia Teknolojia Mawasiliano.
- Kukamilisha upanuzi wa maktaba ya chuo kuitayarisha kuwa maktaba ya Taifa ya Sayansi za Afya ya Binadamu.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ardhi na Usanifu Majengo,katika mwaka wa fedha 2006/2007 Chuo Kikuu Kishiriki cha Ardhi na Usanifu Majengo kinatarajia kufanya yafuatayo:-

- Kuimarisha utawala wa Chuo ikiwa ni maandalizi ya kuwa Chuo Kikuu Kamili kwa kukamilisha *Charter* ya Chuo na kupata Mkuu wa Chuo na Makamu Mkuu wa Chuo.

- Kuongeza udahili wa wanafunzi kwa asilimia 50 baada ya kuongeza idara za taaluma kutoka 6 na kufikia 22.
- Kupanua shughuli za utafiti, ushauri wa kitaalamu na matumizi ya Teknolojia ya Mawasiliano.
- Kuendelea kutafuta wahisani mbalimbali kwa shughuli za utafiti na maendeleo.
- Kuendelea na ukarabati wa mabweni, ofisi, madarasa, barabara, mifereji ya maji na njia za umeme.
- Kukarabati jengo la zamani la utawala kuwa maktaba.
- Kuimarisha vifaa vya maabara
- Kuboresha huduma za wanafunzi ikiwa ni pamoja na

tiba na huduma za ushauri nasaha.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam, katika mwaka fedha 2006/2007 Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam kinatarajia kufanya yafuatayo:-

- Kudahili wanafunzi 500 wa masomo ya Sayansi na 1000 masomo ya Sanaa na Sayansi ya Jamii.
- Kuajiri walimu 106 na wafanyakazi waendeshaji 221 kati ya hawa walimu 75 ni kwa ajili ya shule za Awali, Msingi na Sekondari.
- Kupanua maktaba na kununua vitabu vya kufundishia na kujifunzia.
- Kununua vifaa vya maabara.
- Kuongeza walimu wa sayansi na lugha, na kuweka mkazo katika uzalishaji wa walimu bora na wa kutosha katika lugha za kiswahili, kiingereza na lugha zingine za kigeni.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Biashara – Moshi, Katika mwaka wa fedha 2006/2007 Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Biashara Moshi kinatarajia kufanya yafuatayo:-

- Kudahili wanafunzi 300.
- Kuendelea na mikakati ya kuimarisha mtandao wa kompyuta kwenye maktaba.
- Kuendeleza mafunzo ya wafanyakazi wanataaluma kumi (10) kufikia kiwango cha Udaktari wa Falsafa.
- Kuboresha shughuli za utafiti na uchapishaji.
- Kuendelea kuboresha kiwango cha huduma za uelekezi na ushauri.

- Kuandaa programu na mipango ya kujenga uwezo wa wanachama wa ushirika katika kuendeleza vyama vyao.
- Kupambana na maadui UKIMWI na rushwa.

Mheshiwa Spika, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa kinatarajia kufanya yafuatayo:-

- Kudahili wanafunzi 130 wa stashahada na 870 wa shahada ya kwanza.
- Kuendelea na ukarabati wa mabweni, madarasa na kuweka samani.
- Kuweka samani na vifaa vya maabara ya Kemia, Elimu Viumbe na Fizikia.
- Kukarabati na kupanua jengo la maktaba.
- Kuendelea na ukarabati wa zahanati.
- Kuanza ukarabati wa barabara, miundombinu ya maji safi na maji taka.
- Kutoa mafunzo maalum kwa wanafunzi wa kike katika masomo ya Sayansi ili kuinua uwiano wa wanafunzi wa kike na wa kiume.
- Kuajiri wafanyakazi mia moja na ishirini na saba (127) kati ya hawa Wahadhiri ni hamsini (50), na Waendeshaji sabini na saba (77).

Mheshimiwa Spika**,** Taasisi ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma, katika mwaka fedha 2006/2007 Taasisi ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma inatarajia kufanya yafuatayo:-

- Kudahili wanafunzi 120 wa shahada ya kwanza na 20 wa shahada ya uzamili, ukiwa mkupuo wa pili ngazi ya shahada.
- Kuongeza madarasa mawili (2) yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi sitini (60) kila darasa.
- Kuendesha *Radio Mlimani FM* na kuanza kuendesha kituo cha *Television* kiitwacho *Mlimani Television*.
- Kuendelea kutoa ushauri wa kitaalam katika masuala ya habari, mawasiliano ya umma, matangazo na utangazaji.

Mheshimiwa Spika, Taasisi, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, katika mwaka wa fedha 2006/2007, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam inakusudia kutekeleza yafuatayo:-

- Kudahili wanafunzi 647. Kati ya hao wanafunzi 25 katika fani za Kompyuta na (25) kwa ajili ya Mawasiliano ya Anga ili kupunguza pengo kati ya mahitaji ya soko na wataalamu wa fani hizo.
- Kuanza mafunzo ya Uhandisi Migodi *Mining Engineering* katika ngazi ya Ufundi Sanifu.
- Kukamilisha matayarisho ya mitaala na taratibu za programu ya mafunzo ya Shahada ya Uzamili ya Ukarabati (*Maintenance Management).*
- Kuendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu kwa wafanyakazi 43 wa Taasisi katika nyanja mbalimbali kwa lengo la kuongeza ufanisi katika kutoa elimu bora ya ufundi.

- Kutoa mafunzo maalum kwa wasichana ili waweze kujiunga na elimu ya ufundi katika Taasisi ya Teknolojia Dar er Salaam kwa lengo la kuongeza uwiano wa kijinsia.
- Kutayarisha mtaala wa kozi ya mafunzo ya Ufundi Sanifu katika fani ya *Multimedia Graphics and Animation.*
- Kuanza ujenzi wa jengo jipya kwa ajili ya kuongeza madarasa, maabara na ofisi za wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya, katika mwaka wa fedha 2006/2007. Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya inatarajia kutekeleza yafuatayo:-

- Kudahili wanafunzi 175.
- Kukarabati mabweni 2, mfumo wa maji taka na kuufanyia marekebisho mfumo wa umeme.
- Kununua na kukarabati mitambo, mashine na vifaa mbalimbali vya kufundishia na kujifunzia.
- Kuajiri walimu tisini na mmoja (91) na wafanyakazi hamsini na watatu (53) wengine kulingana na mfumo mpya wa Taasisi.
- Kuongeza udahili wa wanafunzi wa kike katika kozi za ufundi/uhandisi kwa lengo la kuongeza uwiano wa kijinsia.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, katika mwaka wa fedha 2006/2007, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kinatarajia kutekeleza yafuatayo:-

- Kudahili wanafunzi 120 wa shahada ya kwanza.
- Kuanza kuendesha programu ya shahada ya kwanza ya Siasa na Menejimenti ya Maendeleo ya Kijamii na Uchumi katika Maendeleo.
- Kuajiri wanataaluma 21 na watumishi wengine 20 ili kumudu majukumu ya chuo.
- Kukarabati jengo la Utawala, jengo la Uhuru, Jengo la Mihadhara na Jengo la Utamaduni.
- Kuendeleza wahadhiri kumi (10) na watumishi wengine watano (5) kitaaluma na kitaalamu.
- Kuandaa mpango Mkakati wa Chuo wa Miaka 10.

Mheshimiwa Spika, Chuo Cha Ufundi Arushakatika mwaka wa fedha 2006/2007, Chuo cha Ufundi Arusha kinatarajia kutekeleza yafuatayo:-

- Kudahili wanafunzi 418.
- Kununua na kufunga mashine na mitambo mbalimbali kwa lengo la kuboresha mafunzo.
- Kuanza ujenzi wa maktaba mpya ili kukidhi na kuboresha huduma ya maktaba.
- Kutoa mafunzo maalum kwa wasichana ili waweze kujiunga na matumizi ya elimu ya ufundi kwa lengo la kuongeza uwiano wa kijinsia.

- Kukarabati majengo, mitambo na vifaa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Tume, Tume ya Taifa ya *UNESCO,* katika mwaka wa fedha 2006/2007 Tume ya Taifa ya *UNESCO* inatarajia kufanya yafuatayo:-

- Kuratibu utekelezaji na kufanya tathmini ya miradi inayoendelea na ile itakayoidhinishwa na *UNESCO* kwa kipindi cha 2006/2007 kama ilivyoamuliwa katika Kikao cha 33 cha Mkutano Mkuu wa *UNESCO*.
- Kulishirikisha Taifa katika Maadhimisho ya kuutangaza mwaka 2008 kuwa "Mwaka wa Kimataifa wa Sayari Dunia" (*International Year for Planet Earth).*
- Kukamilisha mchakato wa kuifanya Tume ya Taifa ya *UNESCO* kuwa chombo huru cha Serikali.
- Kuratibu mradi wa *UNESCO* wa kuimarisha mafunzo ya walimu.
- Kuratibu utekelezaji wa mradi wa kujenga Utamaduni wa Ukarabati Miundombinu na Vitendea Kazi *Culture of Maintenance.*
- Kufuatilia ombi la Kuanzishwa kwa "*UNESCO Chair*" katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar ili kukiwezesha kupata kituo cha kumbukumbu za kihistoria (*History Resource Centre*).
- Kuandaa warsha ya kuhamasisha Mtandao wa Shule zilizoshirikishwa katika shughuli za *UNESCO* katika Kanda ya Ziwa Victoria (*UNESCO Associated Schools Project Network).*
- Kuratibu mradi wa kutunza na kuhifadhi kumbukumbu za ukombozi Barani Afrika *(Africa Liberation Movements Project*) (Mradi huu uko katika hatua za kutafutiwa fedha).

Mheshimiwa Spika, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania, inatarajia kutekeleza yafuatayo:-

- Kuratibu na kusimamia usajili na upatikanaji wa *Charter* kwa vyuo vikuu 5 na vyuo vikuu vishiriki 3 vya Serikali.
- Kuendelea kuboresha taratibu za udahili.
- Kuendesha warsha ya wadau wa ubora wa elimu ya juu, kuhusu mfumo wa tuzo za kitaifa (*National Qualifications Framework).*
- Kuandaa na kuratibu maonyesho ya pili ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia.
- Kuendesha semina za maadili na utendaji kwa wataalamu wanaoshirikishwa katika tathmini ya vyuo, programu na vyeti.
- Kuratibu uendeshaji wa semina za uongozi wa vyuo na ufundishaji.
- Kuimarisha Tume kwa kuajiri wafanyakazi watano (5) na kuongeza vitendea kazi.
- Kuendelea kutoa machapisho ya kuelimisha umma na kuhamasisha wawekezaji kuanzisha vyuo vikuu bora vyenye kutoa elimu inayozingatia mahitaji ya Taifa na soko la ajira.
- Kuimarisha mtandao wa teknolojia ya mawasiliano ndani ya Tume na wadau wake.
- Kuendeleza ushirikiano na mabaraza ya Ithibati ya Elimu ya Juu duniani.
- Kuendelea na mapambano dhidi ya UKIMWI na rushwa.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia, katika Mwaka wa fedha wa 2006/2007, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia inatarajia kutekelza yafuatayo:-

- Kuhawilisha tekinolojia mbali mbali kwa wananchi.
- Kufanya tathmini ya mahitaji ya teknolojia katika mikoa minne (4) nchini ikiwemo Dar es Salaam, Morogoro, Iringa na Mbeya.
- Kutoa elimu kwa wagunduzi na watafiti kuhusu umuhimu wa haki miliki *(Interlectual Property Rights)* na jinsi ya kutumia hataza (*patents*) kwa manufaa ya maendeleo.
- Kuandaa Benki ya Takwimu (*database*) ya wanasayansi nchini kwa ajili ya kubaini fani zao na kiwango cha elimu walichofikia na maeneo wanayofanyia utafiti kwa lengo la kusukuma maendeleo ya nchi kiuchumi na kijamii.
- Kuendelea kufadhili utafiti wa kisayansi katika maeneo ya kipaumbele ya taifa na kuwawezesha wanasayansi kubadilishana mawazo juu ya matokeo ya utafiti wao.

Kuimarisha mtandao wa taasisi za utafiti na mendeleo, kupanua Masjala ya utafiti, kustawisha matumizi ya mifumo ya mawasiliano na habari vijijini; na kuhamasisha wananchi kutumia sayansi na teknolojia katika harakati za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hili litatekelezeka kwa kuweka mkazo wa masomo ya Sayansi na Teknolojia katika ngazi zote za elimu kuanzia Elimu ya Msingi hadi Elimu ya Juu. Aidha, pamoja na kukamilisha uandaaji wa muswada wa sheria wa kuendeleza matumizi ya Sayansi na Teknolojia Tanzania, Wizara yangu kwa kushirikiana na Vyuo Vikuu inaandaa mkakati wa kufikisha Sayansi, Teknolojia na Ubunifu kwa wananchi kwa kutumia Mifumo ya Ubunifu (*Innovation Systems*), Uwatamizi *(Incubators)* ili kulea viwanda viweze kukua, Kongamano la Viwanda vidogovidogo vinavyoshirikiana kwa ajili ya maendeleo (*Clusters*), maeneo ya Sayansi (*Science Parks*) na Vituo mahiri (*Centres of Excellence*).

Tume ya Nguvu ya Atomiki Tanzania, katika mwaka wa 2006/2007 Tume ya Nguvu ya Atomiki Tanzania inatarajia kutekeleza yafuatayo: Kuimarisha huduma za matengenezo ya vifaa vya elektroniki, mashine za *X-ray*, kinga na upimaji wa mionzi katika vyanzo mbali mbali vya mionzi. Kuratibu utekelezaji wa miradi ya misaada na kikanda (Afrika) inayogharamiwa na Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki *Internationa Atomic Energy Agency* (*IAEA*). Kutoa elimu ya kinga dhidi ya madhara ya mionzi Ayonisha na isiyo Ayonisha kwa Waheshimiwa Wabunge. Kuimarisha na kutoa miongozo ya uendeshaji wa shughuli na majukumu ya Tume. Kukamilisha uanzishaji wa ofisi Zanzibar katika kutekeleza majukumu yanayohusiana na Sheria ya Nguvu za Atomiki ya mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Elimu Tanzania,katika mwaka fedha 2006/2007 Mamlaka ya Elimu Tanzania, inatarajia kutekeleza yafuatayo:-

· Kuendelea kuhamasisha na kuelimisha wadau kuchangia na kuwekeza kwenye miradi ya elimu na kupanua wigo wa uchangiaji katika Mfuko wa Elimu kwa kushirikisha wadau katika ngazi ya Wilaya.
· Kushawishi uanzishwaji na uendelezaji wa mifuko ya Elimu ya Halmashauri za wilaya mbalimbali. Aidha, mamlaka itaendelea kushawishi ushirikiano na mifuko hiyo ili kuchochea uchangiaji na maendeleo katika elimu nchini.
· Kuendelea kutoa ruzuku na mikopo kwa vyuo na shule kwa ajili ya miradi mbalimbali ya kuboresha elimu, kuongeza udahili na kuongeza usawa.
· Kuendelea kufanya ukaguzi wa miradi iliyofadhiliwa na Mfuko wa Elimu.
· Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi ili kuongeza ufanisi.
·Kuimarisha Mamlaka ya Elimu Tanzania kwa kuajiri wafanyakazi kulingana na mahitaji.
·Kuendelea na mapambano dhidi ya maadui UKIMWI na rushwa.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu inatarajia kutekeleza yafuatayo: Kuanza kutumia chombo cha elektroniki *(means Testing Software)* chenye uwezo wa kutambua wanafunzi wahitaji wa mikopo na kuweka kiwango maalum ambacho muhitaji anaweza kukopeshwa. Kuendelea kutoa mikopo kwa wanafunzi wahitaji wa elimu ya juu wanaostahili katika maeneo yafuatayo: Ada ya masomo, Chakula na Malazi,Vitabu na viandiko, Elimu kwa vitendo, Mahitaji maalumu ya vitivo

- Kuanza kukusanya madeni ya mikopo iliyotolewa toka mwaka 1994/95.
- Kushirikiana na vyuo vya elimu ya juu na taasisi zingine kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utoaji wa mikopo na ukusanyaji wa madeni kutoka kwa waliokopeshwa.
- Kutoa elimu kwa wadau wa mikopo – wanafunzi na umma kwa ujumla kuhusu dhana ya uchangiaji gharama za elimu na suala zima la mkopo na urejeshwaji wake.
- Kuendelea kuajiri wafanyakazi waendeshaji wa Bodi ya Mikopo.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi inatarajia kutekeleza yafuatayo:-

- Kukagua na kutathmini taasisi/vyuo vya ufundi 20 kwa ajili ya ithibati.

- Kusajili vyuo 15 vyenye uwezo wa kutoa elimu na mafunzo ya ufundi.

- Kuandaa na kuidhinisha mitaala ya programu za mafunzo 20 yenye kuzingatia mahitaji ya soko la ajira.

- Kuratibu mitihani ya ufundi ya kitaifa katika mfumo mpya wa *National Technical Award* (*NTA*) katika vyuo 17 ambavyo vinatumia mitaala mipya iliyoidhinishwa na Baraza.

- Kusimamia na kuhakiki ubora wa mafunzo katika taasisi/vyuo 30 vya ufundi.

- Kuandaa taratibu na kanuni za kuidhinisha programu za mafunzo ya ufundi kwa taasisi/vyuo vya nje zinazotaka kuendesha mafunzo hayo nchini.

- Kuimarisha ushirikiano na baadhi ya taasisi/vyuo vya ndani na nje vilivyo na majukumu yanayofanana na Baraza hili.

Mheshimiwa Spika, Maazimio na Mwelekeo wa Bajeti ya Mwaka 2006/2007, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Wizara inaazimia kutekeleza yafuatayo:-

·Kuendelea kuelimisha wadau wa elimu ya juu wakiwemo wanafunzi, wazazi walezi na jamii nzima kuhusu dhana nzima ya mikopo inayotolewa na Bodi ya Mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu.

· Kuimarisha utendaji wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kwa kuajiri watendaji wa kutosha. Kuwapatia vitendea kazi vya kutosha na vya kisasa. Kuanza kutumia mfumo wa kuwatambua wanafunzi wahitaji *(Means Testing)*

· Kurekebisha Sheria Na. 9 ya mwaka 2004 iliyoanzisha Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ili iwiane na Sera ya Elimu ya Juu ya mwaka 1999.

· Kuendelea kuongeza nafasi za masomo katika vyuo vikuu vilivyopo pamoja na kufanya maandalizi ya kuanzisha chuo kikuu cha Umma Dodoma.

· Kuanza kukusanya madeni kwa wale waliokopa kaunzia mwaka 1994/1995, ili wanafunzi wengi zaidi waweze kufaidika na mfuko huo.

·Kuanza kutumia mfumo wa kuwatambua wanafunzi wote wanaosoma katika taasisi za Elimu ya Juu nchini *Student Identification and Management Information System (SIMIS).*

· Kukamilisha uhuishaji wa Sera za Elimu ya Juu, Elimu ya Ufundi na Sayansi na Teknolojia.

- Kuandaa mpango endelevu wa kuwapata na kuwadumisha (*Retain*) Wahadhiri wa kutosha kwa ajili ya vyuo vikuu na vya ufundi nchini.

- Kuimarisha Tume ya Vyuo vikuu kwa kuongeza idadi ya watendaji na vitendea kazi, ili iweze kuratibu uanzishwaji na uendeshaji wa vyuo vikuu nchini kwa mujibu wa sheria Na. 7 ya mwaka 2005.

- Kuimarisha ukarabati wa vyuo vikuu vishiriki vya Dar es Salaam, Mkwawa pamoja na Vitivo vya Elimu vya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa lengo la kukidhi mahitaji ya walimu bora na wa kutosha wa sekondari.
- Kutoa elimu bora yenye ujasiriamali ili Wahitimu waweze kuwa washindani katika dunia ya utandawazi, waweze kujiajiri na hatimaye kuondoa umasikini.

Hitimisho, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wahisani na wadau mbalimbali kwa michango yao mikubwa katika Wizara yangu. Wahisani hao ni pamoja na: Marekani, Sweden, Norway, Uholanzi, Japan, Ubelgiji, Jamhuri ya Korea ya Kusini, China, Cuba, Algeria, Urusi, Poland, Benki ya Dunia na Umoja wa Mataifa.

Aidha, Mashirika mengine ni pamoja *UNESCO*, Jumuiya ya Madola, *International Atomic Energy Agency, Third World Academy of Sciences, International Foundation for Sciences* na Shirika la Kimaendeleo la Sweden. Naomba waendelee na moyo huo nasi tunaahidi kuendeleza ushirikiano huu kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha Wizara yangu kutekeleza mipango iliyojiwekea katika mwaka wa fedha 2006/2007 sasa naliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Sh. 209,859,163,000.00 kati ya fedha hizo Sh. 167,610,218,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Sh.42,248,945,000.00 ni kwa Matumizi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Mwisho kabisa napenda kukushukuru wewe binafsi pamoja na Bunge lako Tukufu, kwa kunisikiliza wakati nikiwakilisha hotuba yangu. Aidha hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara *www.msthe.go.tz*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitoewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia. Waheshimiwa Wabunge ninao wachangiaji 15 ni mmoja tu ambaye hajachangia ambaye ndiye tutaanza naye naye ni Mheshimiwa Nimrod Elirehema Mkono, waliochangia mara moja ni Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya ambaye ndiye atafuata, Mheshimiwa Esther Kabadi Nyawazwa, Mheshimiwa Margreth Agness Mkanga. Ah! Sijawaita Kamati kweli, nimeruka hizi *speed,* Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii karibu. (*Kicheko/Makofi*)

**MHE. MARGRETH A. MKANGA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI WA HUDUMA ZA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba nifanye masahihisho madogo katika taarifa yetu. Ukurasa wa 8 wa taarifa katika takwimu zifuatazo za Mamlaka ya Elimu ya Elimu Tanzania ninaomba radhi kwamba chini kabisa kuna mabadiliko ya miaka, mwaka 2004 – 2005 bajeti ya Serikali isomeke bilioni 1,757.8 chini yake zaidi tarakimu zisomeke mwaka 2005/2006 na tarakibu ya bilioni ya fedha zilizotengwa hapo ni sahihi.

Mheshimiwa Spika, Baada ya kusema hayo naomba nianze kutoa taarifa ya Kamati.Kwa mujibu wa Kifungu Na. 81(1) ya Kanuni za Bunge za mwaka 2004 naomba kuchukua fursa hii kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii kuhusu utekelezaji wa maagizo ya Kamati na malengo ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2005/2006 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa Fedha wa 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilijadili Bajeti ya Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia katika maeneo yafuatayo:-

(i) Dira, Dhima na Majukumu ya Wizara.

(ii) Taarifa ya Utekelezaji wa maagizo ya Kamati na Malengo ya Bajeti ya Wizara Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2005/2006.

(iii) Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, Malengo na Dira ya Wizara. Kamati imeridhika na dira ya Wizara inayolenga kufikia mwaka 2025 kuiwezesha Tanzania kuwa nchi yenye misingi imara yenye kuipa uwezo wa kuwa mshindani katika nyanja za Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia miongoni mwa Jumuiya ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaunga mkono dhima ya Wizara yenye lengo la kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera za Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia ili kuwezesha upatikanaji wa nguvu kazi yenye uwezo wa kutumia rasilimali zilizopo nchini ili kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa maagizo ya kamati. Kamati inaipongeza Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia kwa mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa maagizo ya Kamati na malengo ya Bajeti ya Mwaka 2005/2006.

Pamoja na hayo Kamati inatoa maoni na ushauri kwa nia ya kuboresha utekelezaji wa Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia katika kipindi cha mwaka 2006/2007 katika maeneo muhimu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kuanzishwa Chuo Kikuu Cha Dodoma. Kamati yangu inaipongeza Serikali kwa uamuzi muhimu wa kuanzisha Chuo Kikuu cha Serikali katika Manispaa ya Dodoma eneo la Milima ya Chimwaga katika azma nzima ya kuimarisha, kuboresha na kupanua sekta ya elimu ya Juu nchini. Aidha, Kamati inaridhika kuwa Serikali imefanya uamuzi huo kwa kuona mafanikio mazuri yanayoendelea kupatikana katika kutekeleza Mpango wa kuimarisha Elimu ya Msingi - MMEM na sasa inaendelea kutekeleza kwa kasi mpango maalum wa kuimarisha elimu ya Sekondari katika ngazi zake zote chini ya Mpango wa MMES na pia kwa kuweka maanani wito wa Serikali wa kuongeza idadi ya shule za sekondari.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaridhishwa na uamuzi na maandalizi yanayofanywa kupanua Vyuo vya Elimu ya juu kwa kuzingatia kuwa ingawaje nchi yetu ina idadi kubwa ya watu wapatao milioni 35, ina wanafunzi wachache zaidi katika vyuo vya Elimu ya Juu vya Umma na binafsi na bado inahitaji wataalam katika fani mbalimbali ikilinganishwa na wanachama wa Jumuiya ya Ushirikiano wa Nchi za Afrika Mashariki na nchi za kusini mwa Afrika - SADC ambapo Tanzania ni mwanachama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kielelezo kifuatacho kinaonyesha asilimia ya ushiriki wa wanafunzi katika vyuo vya elimu ya juu katika nchi za SADC na inadhihirisha kuwa nchi yetu ina idadi ndogo sana ya wanafunzi wa elimu ya juu kuliko nchi zote zilizoonyeshwa.

| **Nchi** | **% Ushiriki wa Wanafunzi** |
|---|---|
| Afrika Kusini | 9.11 |
| Kenya | 1.47 |
| Uganda | 1.23 |
| Lesotho | 0.98 |
| Malawi | 0.42 |
| Msumbiji | 0.33 |
| Tanzania | 0.27 |

Mheshimiwa Spika, pamoja na ushiriki mdogo wa wanafunzi katika vyuo vya elimu ya juu nchini, Tanzania imekuwa na wanafunzi wengi wenye sifa za kujiunga na elimu ya juu lakini wamekuwa wakiachwa kutokana na uchache wa nafasi katika vyuo vya elimu ya juu. Aidha, kielelezo kifuatacho kinathibitisha ukubwa wa tatizo ambapo wanafunzi wengi wenye sifa hukosa nafasi ya kuendela na Elimu ya juu.

Kielelezo kifuatacho ni mfano tu kwa Chuo Kikuu cha Dar es salaam.

| **Mwaka** | **Wanafunzi Wenye sifa** | **Wanafunzi Waliodahiliwa** | **Asilimia ya Waliodahiliwa** |
|---|---|---|---|
| 2000/2001 | 5325 | 2311 | 44.0 |
| 2001/2002 | 5340 | 2780 | 52.1 |
| 2002/2003 | 6251 | 3356 | 53.7 |
| 2003/2004 | 6103 | 3107 | 50.9 |
| 2004/2005 | 8698 | 4839 | 55.6 |

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa Serikali wa kujenga Chuo Kikuu Dodoma umepokelewa kwa furaha na wananchi wengi kutokana na changamoto kuwa, idadi kubwa ya watanzania wana mwamko wa kupata elimu ya juu, na pia ukweli kuwa jamii inahitaji wasomi wenye ujuzi katika fani mbali mbali kwa ajili ya kukidhi matakwa ya maendeleo ya milenia, sayansi na teknolojia, mahitaji ya kutokomeza umaskini, ujinga na maradhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilipata nafasi ya kutembelea eneo la Chimwaga na Jengo kubwa la Chimwaga. Kamati ilielezwa kuwa Serikali imetoa:-

(i) Jengo la Chimwaga kwa Chuo kikuu Kipya kitakachojengwa hapo Chimwaga.

(ii) Nyumba mpya 140 zilizoko eneo la Kisasa kwa ajili ya Wahadhiri.

(iii) Eneo la hekta 4,440 ambazo ni karibu sawa na ekari 11,100

Kamati inashauri kuwa, Serikali ianze kujenga majengo ya msingi ili Chuo kiweze kuanza mapema na kukamilisha mahitaji yafuatayo:-

- Mabweni ya wanafunzi ( *Hostel*)
- Bwalo la chakula ( *Cafeteria*)
- Ununuzi wa samani muhimu kwa ajili ya madarasa na ofisi za wahadhiri pamoja na zana za kufundishia
- Kurekebisha jengo la Chimwaga kwa ajili ya sehemu za maktaba, vyumba vya mihadhara, vyumba vya kufanyia semina na ofisi za walimu na kadhalika.
- Kuweka huduma za mawasiliano ya simu na mtandao wa kompyuta-(*internet*)
- Ununuzi wa vitabu na majarida kwa ajili ya maktaba ya chuo.

Mheshimiwa Spika, vyote vinahitaji fedha, Hivyo Serikali itenge fedha za kutosha kwa Chuo hiki kinachotazamiwa kuwa na wanafunzi 40,000 kitakapokamilika. Kamati inapongeza juhudi za Serikali na za Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete katika kutafuta wahisani watakaounga mkono juhudi zetu. Kamati yangu haina kipingamizi chochote endapo Serikali itawezesha kuanza kwa chuo hiki mapema iwezekanavyo hatua kwa hatua baada ya kukamilisha maandalizi ya msingi ikiwa ni pamoja na kuwa na Wahadhiri wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, Vyuo vya Elimu ya Juu. Kamati inapenda kuipongeza Serikali kwa kuhamasisha wadau mbalimbali wakiwemo Taasisi, watu binafsi, Mashirika ya Dini na kadharika kuanzisha Vyuo Vikuu ili kuisaidia Serikali katika kutoa huduma ya Elimu ya Juu nchini. Aidha pamoja na kuanzishwa kwa vyuo hivyo, Kamati yangu ina maoni yafuatayo-

(a) Kumekuwa na mtindo wa kuanzisha Vyuo vya Elimu ya juu kwa kutumia majengo ambayo yametumika kwa muda mrefu kutoa elimu ya Sekondari mfano Shule ya Sekondari Magamba – Tanga na Shule ya Sekondari Mazengo - Dodoma. Kamati inashauri Serikali isikubali kubadili Sekondari kwa nia ya kuanzisha Vyuo vya Elimu ya Juu, kwa sababu kwa kufanya hivyo kunapunguza upatikanaji wa nafasi za elimu ya Sekondari (waliokuwa wanaingia shule hizo sasa wako wapi?). Pia kwa kubadili majengo ya zamani ambayo yamejengwa kwa madhumuni tofauti ni gharama kubwa. Hivyo tunashauri ni vyema kabisa wale wote wenye nia njema ya kuwekeza kwenye elimu wajenge vyuo vikuu vipya na Serikali iwasaidie zaidi kuwapa maeneo ya kutosha.

(b) Tumekuwa na mipango ya kuanzisha Vyuo Vikuu na kusahau kuanzisha Taasisi za kufundisha mafundi yaani *Technicians* ambao kwa kawaida ndio wasimamizi wa kazi kwenye maeneo husika. Kamati inashauri kuwa Taasisi hizo ni muhimu na ziendelezwe kama tulivyoanzisha Taasisi ya Ufundi Mbeya *MIST*, Chuo cha Ufundi-Arusha na Taasisi ya Ufundi – Dar es Salaam *(DIT).*

Mheshimiwa Spika, Vyuo Vikuu vya Umma vimekuwa vikikabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(a) Mishahara na marupurupu ya wahadhiri wa Vyuo Vikuu Vyuo vikuu vya Serikali havitoi marupurupu ya kutosha kuwamotisha wanataaluma wanaotumia nguvu za akili *brain power* kama zinavyofanya nchi nyingine kuzuia wataalam wake wasiende nje ya nchi kutafuta maslahi bora zaidi *(Greener Pastures).* Kwa kuona tatizo hilo Kamati inashauri kuwa mishahara na marupurupu ya wanataaluma katika Vyuo Vikuu vya Umma (Wanataaluma na Waendeshaji) iangaliwe kwa makini ili Vyuo Vikuu viweze kuwavutia wafanyakazi na hasa ikizingatiwa kuwa wapo wahadhiri watakaostaafu.

(c)Mfumo wa pensheni kwa Vyuo Vikuu vya Umma – *"Senior Staff Superannuation Scheme"/ "Federated Staff Superannuation Scheme"* au (SSSS/FSSS) umepitwa na wakati na hautoi mafao ya kuridhisha, ikilinganishwa na mifumo mingine iliyopo hapa nchini. Hivyo Kamati inashauri kuwa Serikali ione umuhimu wa kuanza kutekeleza mapendekezo yaliyotayarishwa na Chuo kikuu cha Dar es Salaam na kuwasilishwa Serikalini tangu mwezi Mei 2000. Huu ni muda mrefu sana kwa Serikali kutekeleza au hata kuwajibu wahusika.

Mheshimiwa Spika, Bodi Ya Mikopo Ya Elimu Ya Juu. Kamati inaelewa kuwa mwanzo wa kazi kwa Bodi hii haukuwa rahisi lakini walijitahidi kufanya kazi katika mazingira magumu na kuwawezesha kutoa mikopo kwa wanafunzi 42,729 yenye jumla ya shilingi billioni 62.5.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza Bodi ya mikopo kwa kuanzisha mfumo maalumu wa kupima na kutambua uwezo wa mwombaji wa mkopo *"Means Testing"*. Mfumo huo utaiwezesha Bodi ya Mikopo kutambua wahitaji halisi wa mkopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu. Aidha Kamati inashauri kuwa ni vema huduma

zinazotolewa na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ziboreshwe zaidi ili ziweze kuwasaidia wahitaji wengi zaidi wanaohitaji kupatiwa huduma kupitia mfuko huu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaunga mkono Bodi ya Mikopo kwa hatua yake ya kutoa elimu kwa wadau wa elimu ya juu wakiwemo wanafunzi kuhusu huduma zitolewazo na Bodi. Kamati inashauri kuwa elimu hii iwe inatolewa kila mwaka mpya wa masomo unapoanza ili wanafunzi wapya ambao hawajui taratibu sahihi za Bodi hii waelimishwe katika muda muafaka ili nao wapate mikopo kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Elimu Tanzania *(TEA).* Kamati inapongeza Mamlaka ya Elimu Tanzania kwa kuhamasisha wadau mbali mbali kuchangia katika mfuko huu maalum wa kuendeleza elimu na pia kwa kutoa Mikopo kwa ajili ya kuendeleza miundo mbinu ya Shule, Vyuo na Taasisi mbalimbali za elimu.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na pongezi hizo Kamati yangu hairidhishwi na kiwango cha fedha kinachotengwa na Serikali katika Bajeti yake kwa ajili ya Mfuko huo. Pamoja na Sheria iliyoanzisha mfuko kutamka wazi kuwa Serikali itachangia kiasi kisichopungua asilimia mbili ya pato la Taifa baada ya kutoa gharama za madeni ya Taifa; asilimia ya Bajeti inayotengwa kila mwaka imekuwa inaushuka kama takwimu ifuatayo inavyothibitisha:-

| **Mwaka wa fedha** | **Bajeti ya Serikali(bilioni)** | **Tengo la fedha TEA ( bilioni)** | **Asilimia %** |
|---|---|---|---|
| 2001/2002 | 1,079.6 | 4.9 | 0.45 |
| 2002/2003 | 1,175.6 | 4.9 | 0.40 |
| 2003/2004 | 1,391.2 | 5.4 | 0.39 |
| 2004/2005 | 1,757.8 | 4.4 | 0.23 |
| 2005/2006 | 2,262.7 | 6.8 | 0.30 |

*Chanzo: Mamlaka ya Elimu Tanzania, Machi, 2006*

Mtiririko wa aina hii unatokana na kukosekana kwa ubainisho wa kiwango cha chini cha tengo kutokana na mgao wa bajeti ya Serikali kwa kuzingatia sheria ya Mfuko wa Elimu.

Mheshimiwa Spika, kwa mara ya tatu sasa, Kamati inapenda kuishauri Serikali kufanya marekebisho ya Sheria Namba 8 ya mwaka 2001, iliyoanzisha Mamlaka ya Elimu Tanzania na kuweka kiwango cha chini cha mchango wa Serikali katika Mfuko huu kisipungue asilimia mbili (2%) ya pato la Taifa baada ya kuondoa deni la Taifa. Kamati inataka kufahamu ni hatua gani zinachukuliwa ili kumaliza tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu Kishiriki Cha Ushirika na Stadi za Biashara cha Sua – Moshi (*Muccobs*). Kamati inaunga mkono hatua zilizofikiwa za Serikali kukipandisha hadhi chuo hiki kilichokuwa Chuo cha Ushirika na kuwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara cha *SUA* - Moshi. Kwa kuwa Chuo hiki kimepandishwa hadhi yake Kamati imegundua kuwa katika kipindi cha mwaka wa fedha

wa 2006/2007 Chuo hiki hakina kasma yaani *item Code* na hivyo Kamati iliambiwa kwa mdomo kuwa fedha kiasi cha shilingi Milioni mia mbili tu (200,000,000/=) zimetengwa kwa ajili ya ukarabati chini ya Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine *(SUA)*. Fedha hizi ni kiasi kidogo sana kufanya ukarabati ili kiweze kudahili idadi ya wanafunzi inayotakiwa. Kamati inashauri kuwa Chuo hiki kipewe kasma *item code* haraka iwezekanavyo na pia Serikali itafute fedha zaidi ili ukarabati na uimarishaji wa miundombinu uweze kukidhi hadhi ya Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Mambo ya Bahari – Zanzibar (Ims). Hadi kufikia Juni, 2006, Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia ilikuwa haijapokea shilingi bilioni 5.2 kutoka hazina kama sehemu ya fedha za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2005/2006. Kukosekana kwa fedha hizi kumesababisha madhara kwa ujenzi wa miundombinu katika Taasisi ya Mambo ya Bahari – Zanzibar ambapo mkandarasi alikwisha anza kazi ya ujenzi na kama hatalipwa mapema, ujenzi utasimama na Serikali itaingia kwenye matatizo ya mkataba wa ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Kukosekana kwa fedha hizo pia kumesababisha kusimama kwa ujenzi wa miundombinu katika Vyuo Vikuu vya Sokoine na Mzumbe. Kamati inaomba kupata maelezo kama kufikia wakati huu wa Bajeti; kama Serikali imekwisha toa shilingi bilioni 5.2 au sasa zipo tena kwenye Bajeti hii kwa ajili ya Taasisi zilizotajwa.

Mheshimiwa Spika, Vyuo Vikuu Vishiriki vya Ualimu - Chang'ombe na Mkwawa. Kamati inashauri Serikali kuwa, ili kukidhi mahitaji ya walimu wa Sekondari, Vyuo Vikuu vishiriki vya Chang'ombe na Mkwawa vipewe uwezo ikiwa ni pamoja na kuajiri wanataaluma kukidhi mahitaji yao. Aidha, Kamati inashauri kuwa Vyuo hivi vipewe kipaumbele katika kuvipa uwezo wa kukarabati miundombinu na kujenga nyumba za wahadhiri, mabweni na vyumba vya mihadhara vitakavyokidhi mahitaji ya wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, wote tunatambua kuwa Rasilimali Watu ndio nyenzo kuu ya maendeleo yote ya nchi na kwamba watu walioelimika ndio chimbuko la harakati zote za kukuza uchumi na kupunguza umasikini. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kuwa kwa kutotenga Bajeti ya kutosha kutekeleza mipango ya kuboresha elimu hasa ya Chuo Kikuu, Nchi itadidimia taratibu na matokeo yataonekana tu baada ya muda mrefu. Hivyo, tuzuie hali hii kwa kuwekeza kwenye elimu. Kamati inashauri kuwa upungufu uliotokea kwa mwaka 2005/2006 wa Serikali kushindwa kutoa fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge, usitokee kwa mwaka huu wa fedha wa 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa ni vema Serikali ikatafuta vyanzo vingine vya fedha ili kukidhi mahitaji ya Vyuo Vikuu Vishiriki vipya vya Chang'ombe, Mkwawa na *MUCCOBS* (Moshi) kwakuwa bajeti ya 2006/2007 ina upungufu wa fedha za matumizi ya kawaida wa shilingi bilioni 4.5 ukilinganishwa na bajeti ya 2005/2006. Upungufu huu utapelekea vyuo hivi vishindwe kutekeleza vema majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Shukrani. Naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Prof. Peter Msola na Naibu wake Mheshimiwa Gaudentia M. Kabaka kwa kuteuliwa kwao kuiongoza Wizara hii, ambao kwa mujibu wa Kanuni ya 87 (1) ni wajumbe wa Kamati wakati wanapowasilisha hoja zao. Ninawashukuru kwa ushirikiano wao mkubwa walioutoa katika kipindi chote ambacho Kamati ilikuwa ikijadili na kuchambua hoja na Bajeti ya Wizara hii.Aidha, namshukuru Katibu Mkuu wa Wizara hii Dr. Naomi Katunzi, pamoja na Maafisa wote wa Wizara hii kwa ushirikiano wao mkubwa na michango waliyotoa wakati wa kujadili Fungu 68 ya Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia.

Wajumbe wa Kamati hii walitoa mawazo na maelekezo mazuri kwa Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, napenda pia kuchukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati kwa kushiriki kwa makini katika kipindi chote ambacho Kamati ilikuwa kazini. Ni matumaini yangu kuwa michango na mawazo yao yatakuwa ni msingi wa ufanisi katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima naomba niwatambue wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii waliochambua Bajeti ya Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia – Fungu 68 kwa kuwataja majina ni Mheshimiwa Omari S.Kwaangw', Mwenyekiti, na Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Makamu Mwenyekiti.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, Mheshimiwa Nuru A. Bafadhili, Mheshimiwa Prof. Feetham F. Banyikwa, Mheshimiwa Hasnain G. Dewji, Mheshimiwa Meryce M. Emmanuel, Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mheshimiwa Hemed M. Hemed, Mheshimiwa Phares K. kabuye, Mheshimiwa Janeth B. Kahama, Mheshimiwa Mariam R. Kasembe, Mheshimiwa Sameer I. Lotto, Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo, Mheshimiwa Benito Malangalila, Mheshimiwa Margreth A. Mkanga, Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mheshimiwa Prof. Idris A. Mtulia, Mheshimiwa Omari A. Mzee, Mheshimiwa Khadija S. Ngozi, Mheshimiwa Sijapata F. Nkayamba, Mheshimiwa Usi Amme Pandu, Mheshimiwa Faustine K. Rwilomba,Mheshimiwa Mwanakhamisi K. Said na Mheshimiwa Fatma Abdulla Tamim. *(Makofi)*

Kwa namna ya pekee napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Katibu wa Bunge, Ndugu Damian S.L. Foka na Ofisi yake kwa huduma walizotoa wakati wa vikao vya kuchambua Bajeti ya Wizara ya Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia. Aidha, nawapongeza Makatibu wa Kamati hii Ndugu Theonist K. Ruhilabake na Ndugu Lina Kitosi, kwa kuratibu shughuli zote za Kamati na hadi taarifa hii kukamilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nina hakika Waheshimiwa Wabunge mtaungana nami kumpongeza sana Mheshimwia Mkanga ambaye kwa ufanisi mkubwa na ufasaha amewasilisha taarifa hii

ya Kamati ya Huduma za Jamii. Sasa naomba nimuite Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Sekta hii ya Elimu ya Juu Mheshimiwa Susan Lyimo.

**MHE. SUSAN A. LYIMO – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** Mheshimiwa Spika, Ninakushukuru kupata nafasi ya kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu Na. 43(5)(b)(c) na 81(ii) Toleo la Mwaka 2004. Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi zangu kwako kwa kuchaguliwa na Waheshimiwa Wabunge kwa kura nyingi kuwa Spika na Mheshimiwa Anne Makinda kuwa mwanamke wa kwanza Tanzania kushika wadhifa huo mkubwa wa naibu Spika.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia na Naibu Waziri, Mheshimiwa Gaudensia Kabaka na timu yao ya watendaji ikiongozwa na katibu mkuu Dr. Naomi Katunzi kwa kuwasilisha Bajeti yao hivi punde hapa Bungeni. Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa chama changu cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kwa kunichagua kukiwakilisha katika nafasi hii ya Ubunge Viti Maalum. Naahidi kuitunza imani ya chama changu na kwa Watanzania wote. Pia ninaishukuru Kambi ya Upinzani chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, pamoja na Mheshimiwa Dr. Slaa kwa kunituea kuwa msemaji Mkuu wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Juu. Katika dunia ya sasa ya ushindani unaoambatana na mapinduzi ya kiteknolojia na kifikira, elimu ya juu ni sekta nyeti na muhimu kwa kila taifa lenye dira thabiti ya kujiendeleza. Dunia yetu ya sasa si ya wenye kujua kusoma na kuandika tu bali ni ya wenye kuwa na upeo wa juu kimaarifa na kifikra.

Taarifa zinaonyesha kuwa baada ya miaka 45 ya Uhuru, idadi ya wanafunzi wa elimu ya juu ni 0.27% ya watanzania wote. Huku jumla ya Watanzania wakikaribia milioni 38. Yaani ni vijana elfu arobaini na nane (48,000) tu ndio wapo katika vyuo vyetu vya elimu ya juu. Uwiano wa wasomi na wasio wasomi katika nchi yetu ni 1:800.

Mheshimiwa Spika, La kusikitisha zaidi ni kwamba, majirani zetu wa Kenya idadi ya wanafunzi walio katika elimu ya juu ni asilimia 1.47% wakati Uganda ni asilmia 1.33%, Msumbiji 0.33%, Namibia 4.66% na Angola 0.44% nchi ambazo zimepata uhuru hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na idadi ndogo ya wanafunzi katika vyuo vya elimu ya juu mazingira mabovu yaliyopo katika vyuo hivyo yanawafanya wengi wao kuhitimu, wakiwa na vyeti tu vya shahada na stashahada lakini wakikosa sifa, ujuzi, fikira na utaalamu anaopaswa kuwa nao msomi wa chuo kikuu. Hii imepelekea vijana wetu kukumbana na ugumu katika soko huria la ajira.

Mheshimiwa Spika, Katika makadirio ya Wizara ya Elimu ya Mafunzo imeonesha kuwa wanafunzi 2,000,000 watakuwa shule za msingi ifikapo mwaka 2010 na wahitimu wa Sekondari wasiopungua 500,000 kila mwaka. Katika Shule za Sekondari za Juu yaani "A" Level" kutakuwa na wahitimu 250,000 kila mwaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kutokana na takwimu za Wizara ya Elimu na Mafunzo 2006/2007 katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kwa matokeo ya mtihani wa Kidato cha Sita mwaka 2005/2006 asilimia za ushindi kwa Div.I hadi Div.III ilikuwa 86.6% hivyo kama hali ikiendelea hivyo ni dhahiri kuwa kati ya wanafunzi 250,000 watakaomaliza Kidato cha VI, zaidi ya wanafunzi 130,000 watakuwa wanapaswa kuingia Vyuo Vikuu kila mwaka. Hadi hivi sasa vyuo vyetu vikuu vinachukua wanafunzi wapatao 35,000. Idadi hiyo ni ndogo sana na hivyo kufikia mwaka 2015 tunatakiwa kuwa na vyuo vikuu vya umma na binafsi 25 ambavyo kwa wastani vitatakiwa kuwa na uwezo wa kuchukua wastani wa wanachuo 20,000. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kama ilivyokuwa katika miaka mitano iliyopita chini ya Rais wa awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin Mkapa, Serikali ya awamu ya Nne imeonyesha nia kubwa ya kuongeza idadi ya wanafunzi wa vyuo vikuu nchini. Ni wazi kuna umuhimu mkubwa wa kutambua juhudi hizo za serikali katika vipindi vyote hivi kwa minajili ya kuhakikisha idadi ya vijana wetu wanaopitia katika vyuo vyetu vya elimu ya juu inaongezeka.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeamua kutumia mbinu ya kupandisha hadhi vyuo vya kawaida na kuvifanya vyuo vikuu na kuandaa mipango mbalimbali ya kuanzisha vyuo vikuu vingine. Hivi karibuni tumesikia kuwa kuna mpango kabambe wa uanzishwaji wa Chuo Kikuu cha Umma hapa Dodoma. Tena kinatakiwa kiwe tayari kuchukua wanafunzi wengi kufikia mwezi septemba mwakani. Nia kama hii pia inapaswa kupongezwa pia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Huku tukitambua umuhimu wa vijana wetu, kupewa haki ya kujiendeleza kielimu hasa katika ngazi ya vyuo vikuu, ni wajibu wetu kuhoji tunapoona juhudi hizo hazifanyiki kwa kufuata njia iliyo bora.

Mheshimiwa Spika, ni wazi mbinu zinazotumiwa na serikali kutatua tatizo la vijana wetu kukosa elimu ya juu hazilengi upatikanaji wa elimu bora ya usomi mahiri na makini kwa ajili ya kujenga Tanzania bora. Hii inatishia mustakabali wa taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kuanzishwa kwa vyuo vikuu vipya na kuongeza idadi ya wanafunzi wanaojiunga katika vyuo vyetu ni lazima kuendane na juhudi kubwa za kuboresha mazingira ya kazi ya wahadhiri na wasomi watarajiwa.

Vyuo vyetu vikuu hivi sasa, vile vya kihistoria kama chuo kikuu Dar es Salaam na vile vilivyozaliwa upya kama Chuo kikuu Cha Mzumbe, kwa miongo kadhaa sasa vimekumbwa na matatizo makubwa ya upungufu wa mahitaji muhimu.

Mheshimiwa Spika, mapungufu haya ni kama ifuatavyo:-

Upungufu, ufinyu na uduni wa vyumba vya mihadhara. Vyuo vyetu vimekuwa vikikumbwa na tatizo hili kwa miaka kadhaa sasa. Katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wanafunzi wanalazimika kukaa chini na wengine kusimama hadi milangoni kusikiliza mihadhara ya Wahadhiri wao. Hivi sasa wanafunzi na Wahadhiri wanalazimika kuwepo maeneo ya Chuo kuanzia saa moja kamili asubuhi hadi saa tatu usiku kutokana na upungufu na ufinyu wa vyumba vya mihadhara. Katika Chuo kikuu cha Mzumbe, hali ni mbaya zaidi, kiasi cha kulazimisha wanafunzi kuja Chuoni kwa mafungu.

Utawala wa Chuo hiki, umelazimika kuwarudisha nyumbani wanafunzi karibia wote wa mwaka wa kwanza isipokuwa wale wa shahada ya sayansi ya uchumi na wale wa shahada ya Sheria ambao wamelazika kuhamishiwa Mkoani Mbeya.

Mheshimiwa Spika, ukosefu wa vyumba vya kufanyia mitihani. Hali hii ambayo imekuwa ya kawaida katika Vyuo Vikuu vyetu kama Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambapo maeneo ya kula, yaani Cafeteria, yamegeuzwa kuwa vyumba rasmi vya kufanyia mitihani. Mitihani imekuwa ikiendelea sambamba na matumizi ya cafeteria hiyo. Kwa miaka kadhaa sasa Wahadhiri na wanafunzi wanalazimika kufanya mitihani yao nyakati za usiku, siku za sikukuu na siku na nyakati za ibada. Hii ni kuwanyima haki ya msingi ya kuabudu wanafunzi hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upungufu na ufinyu wa vyumba vya semina. Semina ni sehemu muhimu ya maisha ya kisomi kutokana na ukweli kwamba inawapa vijana wetu nafasi ya kujifunza kujieleza na kupanua wigo wa kifikira kwa njia ya mijadala. Kutokana na kuongezeka kwa idadi kubwa ya wanafunzi wanaoingia katika Vyuo vyetu kama pale Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Wahadhiri wanalazimika kusimamia na kuongoza semina hizo kwa wanafunzi wanaofikia hamsini hadi sitini katika vyumba vinavyopaswa kuchukua wanafunzi ishirini tu.

Hali ni mbaya kiasi kwamba ni kawaida kuwakuta wanafunzi kusimama nje huku wakichungulia madirishani kufuatilia semina hizo. Katika baadhi ya Vitivo Wahadhiri wameamua kuachana na mtindo wa semina ambao ni kigezo kimojawapo Kikuu cha ukamilifu wa Shahada za Vyuo Vikuu. Hii si haki kabisa. *(Makofi)*

Ukosefu wa maabara za utafiti na mawasiliano ya computer. Hali hii imepelekea wasomi wetu kuacha tabia za utafiti wa kisayansi na kulazimisha hata wanafunzi wetu kufanya mitihani inayopaswa kufanyiwa utafiti wa kimaabara kwa kutumia kifaa kimoja kwa watu zaidi ya kumi. Na wengine kutumia njia ya nadharia tu kukamilisha tafiti zao.

Upungufu, uduni na ukosefu wa maeneo ya makazi ya wanafunzi na wafanyakazi. Wanafunzi wetu wanaotakiwa kuwepo Chuoni saa moja asabuhi na kuondoka saa tatu usiku wanakumbana na majanga ya kutisha wanapokuwa wakielekea katika makazi yao mitaani. Matukio ya ubakaji na unyang'anyi kwa kutumia silaha dhidi ya wanafunzi wetu yamekuwa yakiongezeka kwa kasi na yamekuwa ya kawaida. Katika Chuo Kikuu cha

Dar es Salaam, chumba kimoja cha watu wawili kinapangiwa wanafunzi wanne na sehemu zingine zaidi.

Mheshimiwa Spika, wakati hali ikiwa mbaya kiasi hiki na bila ya kazi zozote za kuboresha hali ya mabweni hayo ya wanafunzi, tayari Baraza la Chuo limepandisha ada ya malazi kutoka shilingi 250 hadi 500 na shilingi 300 hadi 800 kwa kitanda kwa siku moja.

Mheshimiwa Spika, hali ya kule Mzumbe ndiyo ya kutisha na kukatisha tamaa kabisa. Mabweni na miundombinu kama ya maji na vyoo yapo katika hali mbaya kabisa kwa kukosa ukarabati kwa kipindi cha miaka mingi. Wanafunzi wengi wanalazimka kuishi katika vijiji vya jirani ambapo wengi wao wanaishia kuwa walevi na wavivu ukiachilia mbali majanga wanayokutana nayo huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukosefu wa Wahadhiri wa kutosha na walio na sifa za kutosha. Hivi sasa pale Chuo Kikuu Wahadhiri wengine wanalazimika kusimamia wanafunzi zaidi ya elfu moja kwa wakati mmoja. Katika baadhi ya Idara Wahadhiri wanalazimika kusahihisha zaidi ya karatasi za mitihani elfu mbili zenye majawabu zaidi ya elfu sita kwa mitihani ya muhula na maelfu mengine kwa mitihani ya majaribio. Hili limelazimisha Vyuo vyetu Vikuu kulazimika kutegemea usaidizi (*cheap labour*) unaotolewa na wanafunzi wa Shahada za Uzamili yaani *Post Graduate*.

Mheshimiwa Spika, wakati mwengine wanafunzi hawa wa Shahada ya Uzamili ndio wamekuwa wakipewa majukumu ya kutoa mhadhara kama hali ilivyojitokeza katika Chuo Kikuu Mzumbe. Yote haya yanatokea wakati vijana wenye vigezo vya kuajiriwa kwa kazi za Uhadhiri Saidizi *(Assistant lecturers)* wapo, lakini Serikali inashindwa kufanikisha zoezi la kuwaajiri, wengi wao hukimbilia sekta binafsi. Kutokana na msukumo wa kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi, sasa hivi kumejengeka tabia ya kuajiri wahadhiri ama wahadhiri wasaidizi wasio na vigezo vinavyotakiwa kiutaratibu. Wengi wao ni wale walio na shahada za kawaida, yaani Passes wakati kigezo cha mtu kuwa Mhadhiri wa Chuo Kikuu ni *1$^{st}$ Class* au 3.8 *points GPA* katika Shahada ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile kumekuwa na tatizo la kuajiri walimu waliopitia katika vyuo visivyo na sifa na hata wengine wakiwa na Shahada za Uzamili na zile za uzamivu *Ph.D.* zinazopatikana kwa njia ya mawasiliano ya *internet (online degrees).* Shahada za aina hii inawezekana hazina tatizo kutumika kisiasa, lakini inapokuja suala la ufundishaji hasa katika Vyuo vyetu Vikuu linapaswa kudhibitiwa kwa nguvu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maslahi duni kwa Wahadhiri na wafanyakazi wa kawaida. Ingawa kuna juhudi zinazofanyika, hali ya kimaslahi kwa wasomi wetu imekuwa ikiendelea kutoridhisha. Hili linasababisha wasomi wetu wengi kuamua kuhamia nchi zingine ambako taaluma yao inathaminiwa na kupewa umuhimu wa hali ya juu. Wengine wameamua kukimbia *Campus* zetu na kukimbilia katika sekta binafsi na wengine kuamua kuwa wanasiasa. Hapa tunapenda kutoa pongezi kubwa sana kwa wasomi wetu

walitukuka ambao wameweza kuthibitisha uzalendo wao kwa Taifa letu, kwa kuendelea kulitumikia Taifa letu katika mazingira magumu wanayokumbana nayo kififikira na kimaslahi, wakati ambapo wangeweza kwenda kufanya kazi hizo katika nchi zengine ambazo Serikali zinathamini mchango wao kwa dhati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la mafao ya wafanyakazi waendeshaji katika Vyuo vya Elimu ya Juu ni lazima liende sambamba na lile la Wahadhiri kama walivyoahidiwa hapo mwanzoni na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ukosefu wa Fedha za Usimamizi wa Elimu ya Vitendo (*Practical Training and Teaching Practices*). Kwa Elimu ya Chuo Kikuu kukamilika ni lazima wanafunzi wapitie mafunzo kwa vitendo kwa muda usiopunguwa wiki nane. Hivi sasa tunavyotoa hoja yetu hii, ni kwamba wanafunzi wa mwaka wa kwanza na wa pili wa Chuo Kikuu cha Dare es Salaam wanaochukua mafunzo ya ualimu wamekosa usimamizi wa Wahadhiri wao katika vituo walivyopangiwa kufanya elimu ya vitendo yaani *assessment*. Hii ni kutokana na ukosefu wa fedha na Serikali mpaka sasa hivi bado haijawapatia fedha hii. Hii ni kinyume na mahitaji ya kitaaluma ambayo itapelekea wanafunzi kurudia kufanya zoezi hilo mwakani kwa gharama nyingine za Serikali kwani bila ya hivyo, hawatakuwa wamefikia viwango vya kuhitimu. Wanafunzi wengie wa Kitivo cha Sayansi ya Jamii nao pia watalazimika kusimamiwa wakiwa nje ya vituo vyao kwani hadi sasa Serikali haijatoa posho za kutosha kwa wahadhiri wao kuwafuata huko walipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nielekee kwenye Bodi ya Mfuko wa Mikopo kwa Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu (*the Higher Education Student Loan Board*)

Mheshimiwa Spika, mnamo mwaka 2004 Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria ya *The Higher Education Students Loans Board* kwa ajili ya Vyuo vya Elimu ya Juu.

Hili lilifanyika wakati wanafunzi wa Vyuo Vikuu nchini hasa vile vya Umma wakiandamana kuishinikiza Serikali kutambua busara za kutofanya hivyo kwa wakati ule. Serikali na Wabunge walio wengi humu ndani waliamua kuziba masikio na kuipitisha sheria hiyo kwa umahiri mkubwa. Sasa ni miaka miwili imepita tangu sheria hiyo kupitishwa.

Mheshimiwa Spika, mpaka hivi sasa sheria hiyo imeonyesha kuwa na mapungufu mengi ambayo yamepelekea kusababisha usumbufu mkubwa kwa wadau wote wa elimu ya juu, yaani wanafunzi, wazazi, Wahadhiri, wafanyakazi na watanzania kwa ujumla. Mapungufu hayo yamo katika Sheria yenyewe na maamuzi ya kiutekelezaji.

Mheshimiwa Spika, miaka ya hivi karibuni Serikali iliamua kuanza kutekeleza rasmi matumizi ya sheria hii kwa kutoa nafasi kwa vijana wote waliopata nafasi za kuingia katika Vyuo vya Elimu ya Juu nchini kote kupewa mikopo.

Ni wazi uamuzi huu unabaki kuwa mfano hai wa maamuzi mabovu yenye kulenga maslahi ya kisiasa tu bila ya kujali uwepo wa mazingira ya kutosheleza utekelezaji wa maamuzi hayo. Vijana wengi, wanafunzi wa kweli na wanafunzi hewa wakubaliwa na kupokea mikopo hiyo kwa mwaka wa taaluma wa 2005/2006. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ilihusisha hata wale waliokuwa tayari wanalipiwa na wazazi wao kwenye Vyuo vya Umma na vya binafsi. Idadi ya waliopewa mikopo ikaongezeka na kukidhi matakwa ya wakati ule. Hivi sasa tunajikuta tupo katika mkanganyiko usio na kifani kutokana na mabadiliko ya kimaamuzi. Mabadiliko ambayo yanasababisha vijana wengi wa kitanzania waliojiunga na Vyuo mbalimbali nchini kutokana na ahadi hiyo kulazimika kukatiza masomo yao. Hawa ni wale wa Vyuo binafsi na waliopo katika Vyuo vya Umma ambao mwanzoni walipaswa kulipiwa na wazazi wao.

Mheshimiwa Spika, linapokuja suala la viwango vya posho ambayo sasa ni mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu, Serikali imekuwa ikikwepa kukubali ukweli wa hali ya kimaisha inayowakumba wanafunzi wetu. Ni ajabu kuona Serikali yetu inakataa kuwapa wanafunzi wetu mikopo ya fedha katika kiwango kinachoendana na mahitaji halisi ya maisha kwenye maeneo ya Vyuo vyetu.

Mheshimiwa Spika, kushuka kwa thamani ya shilingi imepelekea mfumuko wa bei za bidhaa nyingi hususan vyakula. Kutokana na kupanda kwa bei za vyakula, tafiti zinaonyesha kuwa gharama za kujikimu ni kama ifuatavyo:-

| **CHUO** | **USAFIRI** | **B/FAST** | **LUNCH** | **DINNER** | **MALAZI** | **JUMLA** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| UDSM | 800 | 500 | 1000 | 1000 | 800 | 4100 |
| UCLAS | 800 | 500 | 1000 | 1000 | 800 | 4100 |
| MZU-MBE | 1400 | 600 | 1250 | 1250 | 800 | 5150 |
| MUHI-MBILI | 800 | 500 | 1000 | 1000 | 800 | 4100 |
| MUC-COBS | 800 | 500 | 1000 | 1000 | 700 | 4000 |
| SUA | 800 | 700 | 1200 | 1800 | 800 | 4700 |

Mheshimiwa Spika, ukiangalia hali hiyo ni wazi Serikali inapaswa kuwakopesha wanafunzi wetu kiasi kisichopungua shilingi 5,000/= kwa siku ili walau wawezi kukabiliana na ongezeko la gharama za maisha wawapo Vyuoni. Kwani sasa hivi bado wanapata shilingi 2,500 ambayo imetoka tangu mwaka 2001.

Mheshimiwa Spika, tatizo la posho na mikopo lipo pia kwenye suala la elimu ya vitendo *(Practical Training).* Mfano mwanafunzi anayesoma geologia *(UDSM)* anapangwa kwenda *PT* Mkoani Mwanza kwa Sh.6,000/- kwa siku, hii ikiimaanisha ni chakula, malazi na usafiri kwa kiasi hiki, baadhi ya wanafunzi huishia kula mlo mmoja na kulazimika kulala katika mazingira duni mno. Ukweli gharama halisi ni kama ifuatavyo:-

| **MALAZI** | **USAFIRI** | **CHAKULA** | **DHARURA** | **JUMLA (Tsh)** |
|---|---|---|---|---|
| 5,000 | 1,000 | Asubuhi 600<br>Mchana 1200<br>Jioni 1200<br>Jumla 3,000 | 1,000 | 10,000/= |

Mheshimiwa Spika, kwa hali hii ni dhahiri Serikali inapaswa kuongeza posho za mafunzo kwa wanavyuo ili waweze kutumia nafasi hiyo kujiongezea ujuzi wao kielimu.

Mheshimiwa Spika, wakati vijana wetu wanakataa kulazimishwa kukubali mfumo huu wa elimu ya juu kutolewa kwa mikopo, walielezea mambo mengi kama matatizo ambayo waliyaona kuwa yatakwamisha utekelezaji wa sera hii. Moja, lilikuwa ni lile suala la *means testing,* yaani utambuzi wa wale kweli wanaopaswa kusaidiwa. Hoja yao ilikuwa ni kwamba kutokana na maandalizi duni na mapungufu ya sheria zetu pamoja na hali ya kijamii katika nchi yetu, ni wazi walengwa hasa wa sera hii yaani wasio na uwezo kujisomesha, watanyimwa haki yao. Lakini vilevile suala la kuwa na mali isiyohamishika kama dhamana *(collateral)* lilikuwa kama kuweka vigezo vya kibaguzi kwa vijana wetu ambao wengi wao kwa kawaida wanatoka vijijini. Haya yote hayajapatiwa ufumbuzi kamili hadi hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfumo wa kujua nani ana uwezo gani *means testing* wa kukopa fedha kutoka katika Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ambao umegharimu Serikali mamilioni ya fedha kwa ajili ya kuwalipa *Consultant* wa nje kama vile hapa nchini hakuna wenye uwezo huo, una mapungufu makubwa na hauendani na mazingira ya kitanzania.

Mheshimiwa Spika, vigezo vilivyoainishwa vinatia mashaka makubwa hasa ikizingatiwa mazingira ya mfumo wa kiutawala, kijamii na kiuchumi nchini mwetu. Kama baadhi ya watu walidiriki kutoa taarifa za uongo ili watoto wao wasomeshwe kama yatima huku wazazi wao wakiwa hai na wenye uwezo mkubwa, kama ilivyotokea katika shule za kimataifa za *St. Mary's,* ni wazi bila ya maandalizi ya kutosha udanganyifu kama huo utaendelea.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Wizara kuwa na programu ya *means testing*, bado tunahoji wale wanafunzi watakaopata mkopo wa asilimia 60% hiyo asilimia 40% italipwa wakati gani? Je, kama vyuo vitawapokea na wakashindwa kulipa kabla ya mitihani yao, watazuiwa kufanya mitihani na nini itakuwa hatma yao?.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na uhalali wa mikataba ya mikopo ya wanafunzi ambayo ina mapungufu makubwa, Serikali inapaswa kutoa maelezo ya kina ya mambo yafuatayo:-

Nini hatma ya mikataba ya wanafunzi wa zamani kuanzia mwaka 1994 hadi 2005, ambao walilazimishwa kujaza fumu hizo kama sharti la kurudi Vyuoni kila baada ya migomo kadhaa iliyotokea na kupelekea kufungwa kwa Vyuo hivyo.

Ni kiasi gani cha fedha ambacho Serik ali imekuwa ikipoteza kutokana na migomo kadhaa iliyopelekea kufungwa kwa Vyuo vyetu Vikuu kama vile Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kile cha Sokoine kuanzia mwaka 1994 hadi mwaka 2005.

Hadi kufikia Julai, 2005, ni kiasi gani cha fedha ambazo zilitolewa kama mkopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu nchini na kwa wastani wa shilingi ngapi kwa kila mwanafunzi?

Ni vijana wangapi walipata mikopo ya Serikali katika kipindi cha mwaka 2005/2006 kati yao ni wangapi walitoka katika Vyuo vya Umma na wangapi walitoka katika Vyuo binafsi na hilo lilikuwa ongezeko la kiasi gani cha fedha kulingana na zile zilizotolewa mwaka 2004/2005.

Ni kiasi gani cha fedha ambazo zilikwenda kwa waombaji wasio na sifa, yaani wale ambao baadaye waligundulika kuwa hawakuwepo katika Vyuo walivyodai wapo na wale waliopata mgao wa mikopo zaidi ya mara moja.

Serikali imefanya juhudi gani hadi sasa ili kurudisha fedha zilizopotea mikononi mwa wale ambao hawakuwa walengwa rasmi wa mikopo hiyo? Ni kiasi gani ambacho kimeweza kurudishwa hadi hivi sasa?

Ni kina nani walihusika na kutoa uamuzi wa kutoa mikopo kwa waombaji wote waliopata nafasi katika Vyuo vyote vya Elimu ya Juu Nchini yaani vikiwa ni Vyuo vya umma na Vyuo Binafsi bila ya kujali sifa za vyuo hivyo? Ni hatua gani zilichukuliwa kutokana na maamuzi mabovu kama hayo.

Kuanzia mwaka 1995 hadi 2005, ni wanafunzi wangapi waliokuwa na ambao wengine bado wapo katika Vyuo Binafsi wamepatiwa posho na mikopo kutoka Serikalini na ni wa vyuo gani?

Mheshimiwa Spika, Usawa wa Kijinsia, Kijiografia na wenye Ulemavu. Suala la kuboresha mfumo wa elimu nchini ili kuwezesha kutatua tatizo la idadi ndogo ya wanafunzi wanawake katika Vyuo vyetu vya Elimu ya Juu ni moja ya mafanikio ya Serikali katika miaka ya hivi karibuni. Ingawa juhudi zaidi zinapaswa kufanyika ni wajibu wetu kuwapongeza kwa juhudi zao. Takwimu zinaonyesha ni jinsi gani wanawake walivyoachwa nyuma katika Elimu ya Juu yaani asilimia 32.7% ukilinganisha na wanaume. Lakini pia ni ukweli ulio wazi kuwa katika jamii nyingi nchini mazingira bado hayaruhusu wanawake kupata elimu ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua maana halisi ya maslahi ya Taifa letu, Serikali hapo zamani ilikuwa na mipango rasmi iliyokuwa ikilenga kuboresha uwiano wa wasomi nchini kwa Mikoa mbalimbali. Hivi sasa, ni ukweli usiofichika kuwa kuna dalili zote za kuwa na Taifa lenye wasomi wa Elimu ya Juu kutoka katika baadhi ya maeneo machache tu nchini na wengine kuendelea kuwa wasindikizaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni makosa kulundika Vyuo vya Elimu ya Juu katika maeneo fulani tu ya nchi yetu, wakati wananchi wa maeneo ya pembezoni kama Kigoma, Sumbawanga, Tandahimba, Mbinga, Namtumbo, Ngara, Musoma, Kilwa, Mtama na kwengineko wanasafiri umbali mrefu mno ili kupata elimu katika Kanda ya Kaskazini - Mashariki ambapo vyuo vyote vimejikita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati akijibu suala kuhusu idadi ya wanafunzi wa Zanzibar katika Vyuo vya Elimu ya Juu, Mheshimiwa Naibu Waziri aliliambia Bunge lako kuwa suala la Elimu Juu ni suala la vigezo tu na halipaswi kuingizwa upendeleo wa aina yoyote.

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba sio kweli kuwa wahitimu walio bora hawatapatikana kama kutakuwa na upendeleo maalum. Hivi sasa katika Vyuo vyetu vya Umma na hata vile vya binafsi vinatekeleza mipango maalumu ya kuwawezesha wasichana kujiunga na vyuo hivyo hali ya kwamba wamekosa viwango vya kutosha kushindana na wenzao wanaume. Hawa wamekuwa wakitoka chuoni hapo na kuweza kufanikiwa katika soko la ajira.

Mheshimiwa Spika , historia vilevile inatuonyesha kuwa ili Taifa liweze kujenga na kulinda umoja thabiti, kama ilivyokuwa katika nchi yetu, ni lazima juhudi za makusudi zichukuliwe ili kusaidia wananchi wake walioathirika na matatizo ya kihistoria ama kimfumo, kupata elimu ya juu. Juhudi hizi zikiwemo mfumo maarufu wa *QUOTA* zimekuwa zikitumika hata katika taifa lililoendelea zaidi kiuchumi duniani yaani *USA*. Serikali yetu kuendelea kukataa ukweli wa hali ilivyo na athari zake kwa jamii yetu ni sawa na kukalia bomu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vijana wengi wa Zanzibar kushindwa kufaidika na mfumo wa Elimu ya Juu wa Serikali ya Muungano, ni wazi Serikali yetu inapaswa iache kuliangalia suala hilo kiushindani. Wote tunajua jinsi ukosefu wa Elimu ya Juu unavyoathiri maendeleo ya Visiwa vyetu ambavyo tayari vina sababu za kutosha za kisiasa na kihistoria kutoendelea. Ili kuhakikisha kuwa hatma ya maendeleo ya Visiwa vyetu vya Unguja na Pemba inapewa umuhimu unaopaswa, tunapaswa kuliangalia suala hili kwa undani zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni wajibu wa Serikali kuanzisha mfumo wa *QUOTA* ambao utawawezesha vijana kutoka katika Visiwa hivyo, kushindana wenyewe kwa mfumo maalumu ambao utabuniwa na kusimamiwa na Vyuo vyetu Vikuu vya Umma nchini. Hili litasaidia kuhakikisha sifa za wanaoingia katika vyuo vyetu bado haiathiriki lakini wanalindwa na ushindani usio wa sawa kutoka kwa wenzao wa Bara ambao ni wengi kwa idadi na historia yao haijakumbwa na matatizo kama yanayoendelea Visiwani humo kwa miaka mingi sasa. Pia hii itapunguza katika kinachoitwa kero za Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wanafunzi wenye Ulemavu. Zaidi ya hayo ndugu zetu wenye Ulemavu nao hawajafanyiwa mkakati wa kufaidi Elimu ya Juu. Utafiti unaonyesha kuwa ulemavu na umaskini ni kama watoto pacha. Hivyo basi Serikali iangalie ni jinsi gani itawasaidia walemavu walau wale waliofika Vyuo vya Elimu ya Juu kwa usafiri na pia wasipewe mikopo bali wapate ufadhili wa Serikali kwa mahitaji yao

yote yaani *fully sponsorship*. Ni muhimu kutambua kuwa kuwabebesha mzigo wa mkopo ndugu zetu hawa ni dhambi kubwa na ni kama kuwaonea ukitilia maanani kuwa ajira kwao ni ngumu mara dufu na wengi wanatoka katika familia maskini mno.

MheshimiwaSpika, Kutokuwa na Ulinganifu kati ya Wahitimu na Soko la Ajira. Ripoti ya hivi karibuni ya *Economic Research Bureau (ERB 2006)* yenye kichwa "*The Educated Unemployed*" yaani wasomi wasio na Ajira, imeonyesha kuwawahitimu wengi wa Vyuo vetu Vikuu hawapati ajira kirahisi.

Malalamiko mengi yametolewa na vijana wetu wakielezea ugumu wa kupata ajira rasmi katika maeneo kadhaa ambako ajira zipo lakini zinakwenda kwa wageni wa nje. Waajiri wamekuwa wakitowa sababu mbalimbali za kutowaajiri vijana wetu likiwemo lile la uwezo mdogo wa kujieleza na ukosefu wa uzoefu na ujuzi wa kutosha kuhimili mikiki ya ajira hizo.

Mheshimiwa Spika, vijana wetu hivi sasa wanakumbwa na wakati mgumu wa kukosa ajira huku wakiangalia wenzao wenye elimu sawa na wakati mwingine ndogo kuliko wao wanaotoka katika nchi za Uganda, Kenya, Zimbabwe, Afrika Kusini na kwingineko Ulaya wakichukua nafasi hizo wanazoamini ni zao wao. Ni wazi kuna tatizo kubwa katika mfumo wa ajira nchini mwetu. Ni ukweli usiofichika kuwa wengi wa vijana hawa kutoka nje hutumia njia zisizo rasmi kupata haki za kuajiriwa nchini mwetu. Lakini ni wazi mapungufu ambayo waajiri wanadai yapo miongoni mwa wahitimu wetu na yanaendela kukua.

Mheshimiwa Spika, ili kulishughulikia tatizo hilo Serikali inapaswa kutekeleza yafuatayo:-

Kutoa taarifa rasmi ni vipi mfumo we tu wa elimu kuanzia sekondari hadi Vyuo Vikuu unachangia tatizo hilo?

Serikali inapaswa kutilia mkazo thamani ya elimu inayotolewa na Vyuo vyetu Vikuu nchini ili iweze kuboresha thamani ya wahitimu wetu katika soko la ajira.

Serikali kutilia mkazo elimu ya vitendo kwa vijana wetu Vyuoni kwa kuwaongezea muda wa kutoka wiki sita hivi sasa hadi wiki nane hadi kumi.

Serikali kuanzisha mpango wa kuwa na wafanyakazi wanafunzi (*interns*) watakaotoka katika vyuo vyetu vikuu mara wamalizapo masomo yao. Hawa wanapaswa kupewa nafasi hizo katika idara zake zote za serikali kuendana na masomo yao na kuwa huko kwa muda usiopungua miezi sita kabla ya wao kuingia rasmi katika ushindani wa soko la ajira.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sayansi na Teknolojia. Kwa mujibu wa Dira ya Taifa. Kufikia mwaka 2025, Tanzania itakuwa imejenga jamii iliyoelimika na ya kisasa katika matumizi ya sayansi na teknolojia ili kuleta maendeleo ya haraka ya kijamii na

kiuchumi.Ufinyu wa fedha zinazotolewa kwa Bajeti ya Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, hasa fedha za utafiti na maendeleo, kuwepo kwa tafsiri finyu ya Wizara hii kwa dhana ya kuiangalia katika muktadha wa Elimu ya Juu tu wakati Sayansi na Teknolojia ni suala mtambuka na ukosefu wa utashi wa kisiasa wa kutoa rasilimali na fedha za kutosha kwa ajili ya utafiti, sayansi na teknolojia ni baadhi ya mapungufu yaliyomo katika sekta hii.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ilipitisha katika Sera ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia mwaka 1996 ikitaka serikali kutumia 1% ya Pato la Taifa katika masuala ya uendelezaji wa sekta ya teknolojia nchini. Cha ajabu miaka 10 baada ya sera hiyo kupitishwa Serikali imekuwa ikitenga 0.3% tu ya Pato la Taifa kwa Tume ya Sayansi na Teknojia *(COSTECH).*

Mheshimiwa Spika, hii imesababisha tume hii kuishia kufanya kazi za kutoa vibali vya utafiti kwa wageni wanaokuja hapa nchini kufanya tafiti kwa faida ya mataifa yao wanayotoka. Tume hii imekuwa ikikosa hata fedha za kuboresha jengo lake lililopo Kijitonyama Dar es Salaam. Hivi karibuni jengo hilo limekuwa likitegemea kupakwa rangi za kampuni moja ya simu za mkononi ambazo sio tu zinaharibu mandhari yake lakini pia zinashusha kabisa hadhi yake kama kitovu cha sayansi nchini.

Mheshimiwa Spika, wakati wenzetu wa nchi ndogo tu ya Rwanda wanatumia nguvu na juhudi kubwa kuendeleza teknolojia na kuigeuza nchi hiyo kuwa kitovu cha teknolojia katika maeneo ya maziwa makuu, sisi tunaendelea kutothamini umuhimu maendeleo ya sayansi na teknolojia. Sijui ni nchi gani tunayotaka kujenga isiyothamini umuhimu wa tafiti rasmi za kisayansi na maendeleo ya kimpangilio ya teknolojia.

Mheshimiwa Spika, Suala la Hati Idhini ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mara baada ya Bunge lako Tukufu kupitisha sheria mpya ya Vyuo Vikuu mnamo mwaka 2005, Vyuo Vikuu vyote nchini vilitakiwa kuandaa na kupitisha Hati Idhini yaani *Charter* ambazo ndizo zitakazokuwa zinaongoza shughuli za vyuo hivyo katika mazingira yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni kumekuwa na mvutano mkubwa kuhusu Hati Idhini ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Utawala wa chuo hicho bila ya kuwashirikisha wanajamii wote wa chuo hicho yaani, wanafunzi, wahadhiri, wafanyakazi na watanzania kwa ujumla, umetoa rasimu ya Hati Idhini ambayo haiwakilishi maoni rasmi ya washika dau wengine.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia kwa kauli aliyowahi kutoa kuwa uundaji wa Hati Idhini za Vyuo Vikuu vya umma ni lazima uwe shirikishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kushangaza kwa utawala wa chuo kikuu cha Dar es Salaam kuajiri kampuni ya kigeni kufanya mchakato wa kumpata makamu mkuu wa chuo. Hii inafanyika wakati wote tukijua unyeti wa chuo chetu hiki kwa maslahi na usalama wa taifa letu. Mbaya zaidi zoezi hili lilifanyika kabla Chuo Kikuu hakijapata

Hati Idhini itakayotoa maelekezo ya namna ya kumpata Makamu mkuu wa Chuo hicho na viongozi wengine wa juu wa chuo. Je, Waziri haoni kuwa ni wazi zoezi zima limekiukwa taratibu za kisheria na dhana ya ustaarabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ufupi, zoezi hili la kuanzisha la Hati ya Idhini katika chuo kikuu cha Dar es Salaam limegubikwa na matatizo mengi kama ifuatavyo:-

Rasimu ya Hati idhini ya menejimenti ya Chuo Kikuu Dar Es Salaam ina mapungufu mengi ambayo yanaenda kinyume na taswira ya Chuo hiki kama Kitivo cha usomi nchini chenye jukumu la kuandaa vijana watakaoweza kuongoza Taifa letu.

Uandaaji wa Rasimu hiyo una mw ingiliano wa kimaslahi kwa sababu Maafisa wa juu waliopaswa kusimamia zoezi hilo wamejitokeza kugombea nafasi ya umakamu wa mkuu wa chuo, ambapo Hati Idhini hiyo ndiyo inayopaswa kuelezea na kuhalalisha namna viongozi hao watakavyopatikana. Hii inatokana na ukweli kuwa mchakato mzima wa kutafuta Makamu Mkuu wa Chuo mpya kabla ya kuidhinishwa kwa Hati Idhini ya chuo.

Pamoja na Tume ya Mheshimiwa Nicolaus Kuhanga kuundwa ili kuoanisha (*synchronize*) *charters* shirikishi na ile ya menejiment, bado utawala wa chuo unapinga mawazo ya tume hiyo.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya pamoja na hitimisho. Ili kuboresha Sekta ya Sayansi na Teknolojia na Elimu ya Juu Nchini, tunapendekeza mambo yafuatayo:-

Serikali itenge kiasi cha fedha kwa kila Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Umma kwa ajili ya kufanya utafiti kila mwaka na yule anayefanikiwa kufanya utafiti bora na unaokuwa na umuhimu wa kipekee kwa maslahi ya Taifa letu apewe zawadi maalumu ikiwemo nishani ya juu ya Taifa. Kwani bila utafiti Chuo Kikuu hakitakuwa tofauti na *Secondary Schools.*

Serikali iongeze kiwango cha mgawo wa fedha katika taasisi zetu za utafiti, zile za umma na za wasomi binafsi ili kuendana na malengo ya Dira ya mwaka 2025.

Serikali ipitie upya muundo na malengo ya Tume ya Sayansi na Teknolojia ikiwemo kuunda upya uongozi wa tume hiyo ili kuboresha hali ya uvumbuzi inayo onekana kukosekana katika muundo wa sasa. *(Makofi)*

Serikali ianze kutoa fedha za kutosha kwa ajili ya kazi za utafiti katika Vyuo vyetu vya Elimu ya Juu ili kupunguza utegemezi wa wahisani ambao hulazimisha wasomi wetu kufanya tafiti zenye kulenga matakwa ya wahisani hao.

Serikali ianzishe Mfuko utakaopewa jukumu la kukusanya fedha za kutosha kuwalipa wataalamu wetu wa sekta nyeti ambao wamekuwa wakikimbilia nchi za nje kutokana na maslahi duni hapa kwetu. *(Makofi)*

Serikali kwa kupitia wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kuonzisha zoezi maalumu la kutambua wataalamu na watafiti wetu waliopo nchi za nje na kuangalia ni jinsi gani wanaweza kushiriki katika shughuli mbalimbali za kisayansi na utafiti kwa manufaa ya taifa letu.

Serikali kutenga fedha za kutosha kulikarabati jengo la Tume ya Sayansi na Teknolojia *(COSTECH)* ili kufikia hadhi inayopaswa na kusimamisha mara moja zoezi la upakaji rangi linaloendelea hivi sasa ambalo linafanywa na Kampuni binafsi ya Simu za Mikononi.

Serikali kupitia upya mishahara ya wanasayansi wetu na wataalamu wengine wa hadhi za juu na kati na vilevile kuboresha Mazingira ya kufanyia kazi zao pamoja na kuondoa tatizo la ukosefu wa vifaa na zana za kufanyia kazi na kubadili the *brain drain syndrome*, kwani takwimu zinaonyesha Tanzania ina *Ph.D* nyingi nje ya nchi kuliko ndani.

Serikali iboreshe mafao ya Wahadhiri wetu wakiwemo Maprofesa wetu ambao kutokana na uzalendo wao wamekuwa vishawishi vya kwenda nje ya nchi kupata mafao mazuri zaidi.

Serikali ilipitie kwa haraka suala la *Dual Citizenship* ili kuwezesha wasomi wetu wenye uraia wa nchi zingine kuja kulitumikia Taifa letu kwa muda bila ya kuathiri mafanikio yao waliyopata huko ughaibuni. Wengi wapo tayari kufanya hivyo kwa moyo thabiti lakini unaotambua maslahi ya wao kuwepo huko.

Serikali ianzishe mtindo rasmi wa kuwatambua na kuwazawadia wasomi wetu mbalimbali walionyesha umahiri na uzalendo wa hali ya juu katika kutekeleaza majukumu yao makubwa kama wasomi wa nchi hii kama alivyo kuwa Marehemu Profesa Chachage Sethy Chachage ambaye alifariki hivi karibuni akilitumikia Taifa letu katika masula muhimu ya hatma ya nchi yetu. Na hili lisisbubiri hadi wafariki ama wawe wamelitumikia Taifa katika ngazi za juu tu. Kama wasanii wanapata tuzo kwa nini wasomi wetu na wataalamu wasizawadiwe kwa michango yao? *(Makofi)*

Kisiwa cha Pemba ni lazima kiwezeshwa kuwa na Chuo Kikuu cha Umma.

Upanuzi - kuna haja ya kuunganisha, kufunga na kupanua baadhi ya vyuo baada ya kufanya utafiti wa kina *(study)* mfano:-

Kuunganisha Chuo cha *IFM, DIT* na *CBE* na kuwa *city polytecnic* ambacho kitachukua hadi wanafunzi 20,000.

Kuanzisha vitivo vya Elimu, Sayansi ya Chakula ( *food science*), Utalii, *Hotel Industry,* Madini, Teknolojia ya Textile na *Clothing Industry* katika vyuo Vikuu vya *SUA* Mzumbe na *MUCCOBS.*

Kufanya *Feasibility/studies* kwa ajili ya mgao mzuri zaidi wa Vyuo vya Elimu ya Juu kikanda kama vile Kanda ya Kusini, Nyanda za Juu Kusini Ziwa, Kaskazini na Kati.

Lazima tuwe na vyuo vyenye *skills* nyingi na siyo chache kama ilivyo sasa.

Tuendelee kuongeza idadi ya wanafunzi kwa mwaka kutoka 27,000 ya sasa hadi 165,000 kwa 2010.

Mwisho, Mheshimiwa Spika, tunaiomba Serikali iache mara moja mtindo wa kuanzisha Vyuo vya Elimu ya Juu kwa kutumia majengo ya Shule za Sekondari kama vile Mkwawa, Magamba na Mazengo. Kufanya hivyo maana yake ni kupunguza nafasi za Elimu ya Sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru kwa kunisikiliza na ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, nakushukuru sana kwa kuwasilisha vizuri hoja au mchango wako kuhusu hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia.

Waheshimiwa Wabunge, ninayo wachangia sasa 17. Ni dhahiri kabisa kwa utaratibu wetu hapa kwa kuwa Wizara hii inajadiliwa kwa siku moja tu haitawezekana kuwafikia wote. Lakini nitatoa kipaumbele kwa wale ambao hawajachangia na watafuatia wale ambao wamechangia mara moja katika Mkutano huu wa Nne. Kwa hiyo, ninavyoangalia hapa, tutaishia wachangiaji saba au wanane tu. Baada ya hapo itabidi mimwite Naibu Waziri wakati wa jioni. Halafu Mheshimiwa Waziri kwa saa moja kama tulivyokubaliana jana.

Waheshimiwa Wabunge, ila tu nilikuwa napenda kusema kwamba katika wachangiaji hawa tunaweza kwenda hadi saa 11.15 jioni kwa wachangiaji Waheshimiwa Wabunge. Halafu nimwite Mheshimiwa Naibu Waziri Saa 11.15 hadi saa 11.30. Halafu Mheshimiwa Waziri mtoa hoja saa 11.30 hadi 12.30, saa moja azijibu hoja. Kuanzia hapo sasa tutakuwa na muda ule wa Kamati ya Matumizi wa kiasi cha saa moja na dakika kumi na tano. Ndivyo nilivyopanga hivyo. Kwa hiyo, naomba sasa nimwite Mheshimiwa Nimrod Mkono. Halafu atafutiwa na Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji. *(Makofi)*

**MHE. NIMROD. E. MKONO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia hoja hii muhimu ya Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote ningependa kukuomba wewe Mheshimiwa Spika, uniruhusu ni-*declare my interest* kwa kuwa mimi ni Mwenyekiti wa Bodi ya Mikopo na Mambo mengi ninayoyafahamu yanatokana na uzoefu wangu kuwa Mwenyekiti wa Bodi hii. Kwa hiyo, kuna hiyo hoja ambayo ningeomba niitaje na ukiniruhusu nitaendelea kuchangia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge endelea.

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja yenyewe ina matatizo makubwa matatu. Kwanza kabisa ningependa kusema kwa kifupi historia ya Bodi ya Mikopo ilivyoanza. Bodi ya Mikopo ilianzishwa na Serikali mwaka 2004 kwa kuleta Bungeni *Bill* ambayo ilikuwa inaitwa *Government Students Loan Board*. Ndiyo mwanzo wa Bodi. Ilikuwa ni *Government Students Loan Board* na ukiangalia kwenye *Part one*, kifungu cha kwanza kinasema hiyo *bill* ilikuwa iitwe *this bill may be sighted at the Government Students Loan Board and shall come into operation in such date as the Minister may approval.*

Hiyo ndiyo ilikuwa Sera ya Serikali, *Government Students Loan Board*. Muswada ule ulipokuja Bungeni na mimi nilikuwepo, Waheshimiwa Wabunge wengi walipinga usiwe hivyo, walipinga kabisa. Muswada huo ukabadilishwa ukaitwa *Higher Education Students Loan Board*. Sasa tukianzia huko tunaweza kujua matatizo ya Bodi yanatokanaje.

Mheshimiwa Spika, Serikali kisera ilikuwa na nia ya kukopesha wanafunzi wanaokwenda katika Vyuo Vikuu vya Serikali. Lakini baada ya Waheshimiwa Wabunge kuchangia na kui-*convince* Serikali ibadilishe msimamo huo, ikaundwa Bodi ambayo Wajumbe wake wanatoka katika sehemu zote mbili, upande wa Vyuo vya Serikali na Vyuo vya Binafsi, huo ndiyo mchanganyiko.

Kwa hiyo, ukiangalia sheria ya leo tuliyonayo ambayo imekuwa msingi wa kufanya bajeti hii ya *Higher Education* inasema yule atakayepewa fedha au mkopo ni yule tu atakuwa mwanafunzi ambaye amepata *admission* kwa Chuo ambacho kiko *accredited.* Huo ndiyo msingi. Haisemi utampa mwanafunzi gani, inasema bora awe *legible*, mwanafunzi yeyote awe na umri wa miaka 70, miaka 80 bora ni mwanafunzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huko nyuma Sera ilikuwa inasema na ninarudia tena kuisoma ile *bill* ilikuwa inasemaje. Mwanafunzi ambaye alikuwa apewe mkopo wakati huo alikuwa awe Mtanzania, amepata *admission* kwenda kwenye Chuo ambacho kimekuwa *accredited* na asiwe na umri usiozidi miaka 45. Vinginevyo awe anasoma *Open University*. Kifungu hicho kiliondolewa hapa *unanimously* na Bunge hili. Bunge likasema hapana, toa hicho kipengele cha 17, ruhusu kila mtu anayetaka kwenda kusoma Elimu ya Juu apewe mkopo.

Mheshimiwa Spika, sasa ukiangalia bajeti ya leo tuliyoletewa na fedha zilizotengewa kama kweli zimetengwa kwa makusudi ya kuwasaidia wanafunzi

wanaokwenda Vyuo Vikuu vya Serikali basi tumekiuka misingi ya Sheria tuliyoipitisha katika Bunge hili. Kama hizo fedha zilizotengwa ambazo hazizidi bilioni 50 ni kwa ajili ya wanaosoma Vyuo Vikuu pekee vya Serikali, basi mimi siungi mkono bajeti hii kabisa. Itakuwa imebagua watu na ni kinyume cha sheria ambayo tuliipitisha hapa Bungeni sisi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza ilikuwa Serikali ilete Muswada mpya kurekibesha kabisa sheria nzima ilivyo kabla ya kuanza kutoa bajeti finyu kiasi cha namna hiyo, kuweza kubagua watu kinyume cha Katiba.

Mheshimiwa Spika, na hapa ningependa ninukuu Ibara ya 13 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ibara 13(2) Haki ya Usawa. "Ni marufuku kwa Sheria yoyote iliyotungwa na mamlaka yoyote katika Jamhuri ya Muungano kuweka sharti lolote ambalo ni la ubaguzi ama wa dhahiri au wa taathira yake."

Kwa hiyo kama kweli bajeti hii tunaipitisha kwamba ilenge wanafunzi walio Serikalini basi, basi tutakuwa tumekwenda kinyume na Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Na mimi sitashiriki popote.

Mheshimiwa Spika, tumeapa hapa kwamba tutalinda Katiba na Sheria tunazozitunga lazima ziende sambamba. Je, hii bajeti tunasema tunaona matamshi ya Waziri jana na juzi Mbowe magazeti yote yameandika yanasema "Lengo ni kuwapa wanafunzi wanaosoma Vyuo Vikuu vya Serikali "basi. Mimi ningeshauri tamko hilo kwanza liondolewe kabla hatujaendelea mbele. Vinginevyo kuna vile vituo ambavyo tumevikopesha fedha. Kwa mfano pale Morogoro kuna Chuo cha Waislam kwa bajeti ya leo wao hawastahili kupata fedha. Vyuo vyote vya madhehebu havitapewa mikopo, kwa nini iwe hivyo. Itakuwa inakwenda kinyume cha Katiba na ni hatari kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, Vyuo vya Serikali ni vichache sana tunavifahamu havizidi hata kumi.

**SPIKA:** Mheshimiwa unavyoendelea naona unazidi kukibonyeza chini kile chombo husikiki vizuri, kibaki hivyo hivyo.

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Ahsante sana. Nashukuru Mheshimiwa Spika. Vyuo tulivyonavyo vya Serikali ni vichache sana, vyuo vingi vimechangiwa na madhehebu ya dini. Wao wana idadi kubwa ya wanafunzi nadhani inazidi nusu ya wanafunzi ambao wanatakiwa kwenye vyuo vikuu.

Kuna shule zingine ziko Uganda, sio za Serikali lakini wanafunzi pia wamepata mikopo. Wengine wako India, China na kadhalika. Maana sheria ilitoa maagizo kila mwanafunzi anaye-*apply* apewe mkopo.

Sasa ningependa kusema pengine ingelikuwa busara Waziri atueleze vizuri kabisa kwamba mkopo huo ambao umetengewa fedha ni kwa wanafunzi wote bila kujali

wanakwenda wapi. Ikifanyika hivyo basi kidogo tulichopewa tukigawe bila kujali shule uliyopewa. Bodi itafanya kazi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu wanafunzi nchi nzima wamekuwa wameandamana, wanataka mkopo uongezwe. Sheria inasema na nitanukuu. Sheria ya Bodi ya Mkopo inasema kwa kifungu cha 16. "Bodi itatoa mkopo kwa wanafunzi ama mwanafunzi ambaye yuko *illegible*.

Mwanafunzi ambaye ana sifa za kupokea ili aweze kukidhi mahitaji yote. *"To meet all or any of the student welfare costs*" ambazo zimeorodheshwa kwenye ibara ndogo ya 16 ambayo inasema "Iweze kukidhi mahitaji ya vyakula (1), vitabu, *field practical, work experience, expenses, research* na kadhalika. Ukimpa mwanafunzi robo ya mahitaji hayo hujamfanyia kitu. Serikali lazima na fedha zipo za kutoa.

Mheshimiwa Spika, nchi hii imejaa madini. Tuna dhahabu kila mahali leo unasema wanafunzi hawana fedha lakini si uza dhahabu. Uza dhahabu halafu wape wanafunzi wasome. Bila yak u-i*nvest* kwa *education* wanafunzi Taifa limeanguka.

Mheshimiwa Spika, ningependa kabisa kwa haya machache niliyosema yazingatiwe kabla sija-*vote* la au hapana kwenye *vote* hii . Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. FATMA A. FEREJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia nikiwa mtu wa pili katika hotuba hii ya bajeti ya Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia kuhusu Makadirio na Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2006/2007. Awali ya yote napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia leo hii kuweza kusimama mbele ya Bunge lako hili Tukufu kwa mara ya kwanza kuchangia hoja hii. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo napenda nikupongeze wewe binafsi pamoja na Naibu Spika, kwa kuchaguliwa kwa wingi wa kura kuliongoza Bunge hili na kweli mnatuongoza vizuri na niseme nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge wengine kwamba kweli maamuzi yetu yalikuwa sahihi.

Mheshimiwa Spika, sitaki niwe mwizi wa fadhila napenda sana nikishukuru kwa dhati chama changu pamoja na wapiga kura wangu wa Mji Mkongwe ambao katika mazingira magumu kabisa ya Uchaguzi waliweza kunichagua kwa kura nyingi kunipa nafasi kuwa mwakilishi wao katika Baraza la Wawakilishi Zanzibar na hatimaye Baraza la Wawakilishi kuweza kunichagua kuwa Mbunge katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Napenda niwaahidi kwamba nathamini sana heshima hii ambayo wamenipa na sitawaangusha. Nitatumia juhudi, uwezo na maarifa yangu yote kuwatumikia kwa uadilifu mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu Prof. Peter Msolla, Naibu Waziri Mama Gaudentia Kabaka, Katibu Mkuu ambaye huyu

ni Mwalimu wangu Mama Katunzi, Watendaji wote wa Wizara hii ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia kwa kuwasilisha Bajeti yao hii leo. Pia napenda nimpongeze Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusiana na maoni yake juu ya bajeti hii. Napenda pia nimpongeze sana sana Mheshimiwa Mkanga ambaye ni Mwenyekiti wa Huduma za Jamii kwa kuwasilisha vyema maoni ya Kamati yake kuhusiana na Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nichangie machache sana kuhusiana na bajeti hii. Nianze na kuhusu utekelezaji wa dhana nzima ya kuongeza idadi ya Vyuo Vikuu ambavyo inapaswa iongezeke kutokana na idadi ya wanafunzi ambao watatarajiwa kujiunga na vyuo hivi. Kutokana na takwimu ambazo jana ama juzi ziliwasilishwa na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi ni dhahiri kwamba itakapofika mwaka 2010 tutakuwa na wahitimu wengi ambao watahitaji kujiunga na Vyuo Vikuu. Mimi napongeza jitihada za Wizara katika kuhakikisha kwamba wanakuwa na Vyuo Vikuu vya kutosha ili kuweza ku-*absorb* wanafunzi hawa ambao watatakiwa kujiunga na vyuo. Lakini niseme tu kwamba nina mashaka na maandalizi hayo.

Hivi karibuni tumekishuhudia Chuo cha Mzumbe kimegeuzwa kuwa Chuo Kikuu na tayari tumeshuhudia vile vile baadhi ya vyuo kama 5 vimepandishwa hadhi na kuwa Vyuo Vikuu Vishiriki. Mimi naogopa kwamba matatizo yale ambayo sasa hivi tunayakabili kutokana na mipango ya MMES na MMEM yasije yakajitokeza tena hapa katika kuendeleza Elimu ya Juu. Kwa sababu hapa itakuwa ni hatari sana. Sijui kama hii ni njia nzuri ya kuongeza idadi ya Vyuo Vikuu. Kupandisha tu hadhi vile Vyuo ama Sekondari ambazo zipo na kugeuza Vyuo Vikuu. Nafikiri ipo haja ya Wizara kutafakari zaidi ni njia gani bora ya kuongeza idadi hii ya Vyuo Vikuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme Vyuo hivi ambavyo vimepandishwa hadhi na kuwa Vyuo Vikuu Vishiriki pamoja na Vyuo Vikuu vyenyewe hivi sasa vinakabiliwa na matatizo makubwa sana ya Wahadhiri pamoja na vitendea kazi, hilo ni jambo ambalo linaonekana liko wazi kabisa halijifichi. Sasa suala ambalo hapa napenda kulisisitiza ni kwamba tunapoambiwa katika Mpango wa MMES mwanafunzi wa Kidato cha 6 anapewa *crash programme* ili akafundishe Sekondari kidogo linavumilika. Lakini napenda kuonya hapa kwamba isije ikafika siku katika Tanzania hii tukaambiwa kwamba kuna mwanafunzi aliyemaliza Shahada ya Kwanza na pengine kwa kiwango chochote kile sasa anakuwa Mhadhiri wa Chuo Kikuu hapo tutakuwa tunapoteza lengo zima la kutoa wahitimu bora katika Vyuo vyetu ambao wanasukuma mbele maendeleo ya Taifa hili. Hili napenda sana litiliwe maanani. Katika hili basi naomba Wizara itueleze kwamba hii mikakati yao ambayo imo katika bajeti hii ni kweli mikakati hii itaweza kabisa kukidhi haja katika suala hili la ku-*absorb* hawa wanafunzi kwa wingi ambao watatakiwa kujiunga na Vyuo. Naomba hapo nipate maelezo wakati Mheshimiwa Waziri anakuja kutoa majumuisho.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo napenda kuliongelea na kweli hili naliongelea kwa uchungu sana ni kuhusu masuala ya Elimu ya Juu na dhana nzima ya jinsi wanafunzi wa Zanzibar wanavyofaidika katika vyuo hivi. Nianze kwa kutoa shukrani kwamba sisi ambao tumesoma sio kwamba ni wasomi lakini tumesoma. Wengi

mnaotuona hapa akiwemo Mheshimiwa Abubakar, Khalifa, na wengine wengi ambao sasa hivi siwaoni lakini tunao katika nchi yetu tumepata elimu yetu hapa katika Serikali hii ya Muungano kupitia Chuo Kikuu Dar es Salaam na ndiyo maana nikathubutu kusema hapa leo Katibu Mkuu ni mwalimu wangu aliyenifundisha *Curriculum Development* Chuo Kikuu Dar es Salaam na nashukuru sana kama sio yeye pengine hapa nilipo nisingefika, namshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nirudi kidogo katika historia. Mimi nilijiunga chuo pale mwaka 1983 lakini nitarudi nyuma zaidi ambapo wako wengine walijiunga katika miaka ya 70, mwaka 1972. Ninavyokumbuka katika maelezo ninayoyapata pale Zanzibar kwamba katika mwaka 1972 waliingia wanafunzi kama 11 Chuo Kikuu Dar es Salaam kutoka Zanzibar. Na walipofika pale mazungumzo yalikuwepo kwamba aah mmekuja wanafunzi kidogo mna *quota* yenu ya 30% hapa ambayo hamkuhitimiza kwa maana kwamba waliokuwa labda na *qualification* za ku-*join* pale au wale ambao walikuwa wanaweza kwenda walikuwa wachache. Lakini ilikuwa ni katika nia njema kabisa ya Serikali ya Muungano kusaidia Serikali ya Zanzibar kupata wasomi ambao hatimaye watasukuma maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, bado naendelea nilipojiunga mimi na chuo mwaka 1983 nafikiri bado ilikuwepo hiyo *quota system.* Tuliingia kwa wingi sana nathubutu kusema zaidi ya wanafunzi 30 pale chuoni na kweli msiangalie jamani *qualification* tunazotoka nazo nyumbani. Wengine tumeingia pale tukiwa na 3rd *class* lakini tuliondoka na *1st* na *Upper 2nd* tuliwashinda kabisa wale ambao waliingia wao na *1st class* za *Form Six* pale. Kuna mazingira mengi ambayo yanawafanya wanafunzi wa Zanzibar wasi-*perform* vizuri mojawapo lilizungumzwa jana. Nashukuru sana na Mwenyekiti wa Kamati za Huduma za Jamii Mheshimiwa Kwaangw' kwamba mitaala inayofuata wanafunzi wa Zanzibar wanaingia *so abruptly* kufuata mitaala ya hapa wakati *Primary* wao walikuwa na mitaala yao. Pia ushirikishwaji wa Zanzibar katika kufanya mitaala ile ambao ndio wanaotahiniwa nao unakuwa ni mdogo sana. Kwa hiyo naomba sijui kama jicho la huruma lipite. Lakini basi kwa nia njema kabisa ya kudumisha Muungano wetu na kwa nia njema kabisa kama ambavyo Mheshimiwa Kikwete anaeleza kwamba: "Tunajaribu kuondosha haya matatizo ya Muungano ambayo yapo". Kweli niseme kwamba katika kujibu swali Mheshimiwa Waziri kuhusiana na kiasi gani au idadi gani ya wanafunzi waliokuwepo hapa wapo katika Vyuo Vikuu lile jibu niseme wazi kabisa kwamba halikupokewa vizuri Visiwani Zanzibar. Kwa kweli limekatisha tamaa kabisa na kwa sababu sisi ndio wawakilishi wa kule tumefuatwa na tukaambiwa jamani tuko wapi, jamani kweli tutaendelea. Ili kuendelea nchi yoyote lazima iwe na wasomi, iwe na watu walioelimika na hali yetu sisi ni kama mnavyoiona. Inawezekana tu kwenye familia tu jamani tunasaidiana, unaweza kuwa wewe ndio mwenye uwezo lakini mdogo wako naye kama hajiwezi basi ukamsaidia saidia ili na yeye ajiweze.

Kwa hiyo kwa nia njema kabisa mimi naomba Serikali iangalie tena uwezekano, si vibaya ku-*reverse* maamuzi jamani. Jana tuliona hapa tukiambiwa ilipongezwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwamba wamerudia mitaala, walipongezwa sana. Si vibaya nasema ku-*reverse* maamuzi ikiwa yale maamuzi yaliyopita ndiyo yalionekana ya busara. Kwa hiyo mimi nasema kama kulikuwa na maamuzi ya kuondosha *quota system*

ambayo ilikuwa inatenga idadi fulani ya wanafunzi wa Zanzibar kwamba hawa jamani kwa hali yao watashindana wenyewe lakini wataingia hapa chuoni na wao waelimike na kweli wanapotoka pale wana-*perform* vizuri basi ni vizuri sasa tukafiria kurudisha utaratibu huu wa *quota system,* kwa nia njema kabisa.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo kabla wakati wangu haujamalizika napenda kuligusia ni kuhusiana na suala zima la Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Niseme kwamba utendaji wa Bodi hii kwa kweli haukuridhisha wananchi, haukuridhisha walengwa. Nathubutu kusema kwamba labda umekuwa ni *failure* kabisa. Tulichokiona wanafunzi wanataka kuandamana mara kwa mara, mara kunakuwa na maamuzi haya, mara yanabadilishwa na kuweko maamuzi haya. Kwa sababu hiyo naamini kwamba Serikali kutokana na kwamba haiko sawa sawa katika mipango yake hii Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ilisababisha kukopa fedha kufidia wale wanafunzi ambao hawakutarajiwa kupewa mikopo na jambo hili limeifanya Serikali kupata hasara kwa sababu mikopo hiyo imekopwa na itahitajika kulipwa na *interests*. Mimi naomba hapa Mheshimiwa Waziri akija atueleze ni hasara gani Serikali imepata katika kupitia Mfuko huu wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kutokana na kuja kukopa hizo fedha kuwalipa watu kwa sababu mipango yenyewe haikuwa sawa sawa na mpaka sasa kusema kweli haiko sawa, hakieleweki kitu gani kinafanywa.

Mimi nashauri si vibaya kufanya *Reforms.* Kama kunaonekana kuna utendaji mbovu maana yake hawa Watendaji wa Bodi ya Mikopo hawafai, kwa hivyo tubadilishe kabisa mfumo mzima labda tuivunje hii Bodi ya Huduma ya Mikopo ianzishwe upya ipewe Watendaji wenye ujuzi katika shughuli hii ili tupate mafanikio mazima katika shughuli hii ya mikopo na ile nia ya Serikali ya kuhakikisha kwamba sasa wanafunzi wengi wasiokuwa na uwezo wanapata elimu iweze kutumia. Kimetajwa kitu *Mean testing* ngapi. Nilipouliza uliza tu niliambiwa aah !!! Mheshimiwa hii inakuwa kwamba unapewa fomu, sasa unapopewa fomu.

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana ahsante sana na naomba pia kuunga mkono hoja. (*Makofi)*

**SPIKA:** Samahani sana Mheshimiwa nilikuwa najisikia raha sana kufuatilia hoja zako unavyozipanga. Lakini nabanwa na kanuni, ningekuongeza muda.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia.

Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutukutanisha hapo wote tukiwa wazima asubuhi ya leo. Vile vile natoa pole sana kwa familia ya Prof. Chachage, Mwalimu wangu wa *Sociology of Knowledge* kwa kweli Idara ya *Sociology* imepoteza ambaye alikuwa Mwalimu mzuri sana na vile vile nadhani Taifa letu linajua jinsi alivyokuwa anafanya *analysis* nzuri ya society yetu.

Mheshimiwa Spika, mimi nitapenda kujikita zaidi na watu wataona nitakuwa *bias* lakini ni kwa sababu nimesoma pale Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na mifano mingi nitakuwa natoa itakuwa ya pale Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Napenda kuipongeza Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia kwa mikakati mbalimbali ambayo wanafanya kuhakikisha kwamba angalau wanafunzi wanaongezeka ambao watakuwa wamepata Elimu ya Juu ambao tuseme itakuwa Elimu ya Chuo Kikuu. Kutoka 0.27 ambayo sasa hivi itakuja kuwa *one something.* Napenda kuwapongeza sana. *(Makofi)*

Lakini ongezeko hilo tunaomba liendane na hali halisi ya mazingira ya mwanafunzi. Tuangalie makosa ambayo yaliyopo sasa, matumizi yaliyopo sasa ambayo yanawakumba wanafunzi. Kwa mfano pale Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuna wanafunzi wengi sana unakuta kozi moja wanafunzi labda 1,000. Lakini zile *lecture room* unakuta inaweza ku-*accommodate* labda wanafunzi 500 tu. Kwa hiyo unakuta tumekaa mle ndani tumebanana. Kwa hiyo mazingira sio mazuri kwa mwanafunzi kusoma. Kwa hiyo hicho kitu pia kiangaliwe kwamba tunaongeza wanafunzi lakini tuhakikishe kwamba na madarasa pia yanaongezeka. Vile vile wahadhiri Wizara ihakikishe kwamba nao wanaongezeka pia. Tusiongeze idadi ya wanafunzi halafu tukawa hatuna walimu wa kutosha. Tuhakikishie kwamba na *facilities* za mwanafunzi kusoma pia zinapatikana. Isiwe tena watu wanasoma Sayansi kwa vitendo badala ya kusoma kwa vitendo wanasoma kwa nadharia. Kwa hiyo naipongeza lakini izingatie hayo.

Mheshimiwa Spika, pale Chuo Kikuu tulikuwa tunasoma kwa mtindo wa *semester system*. Ile *semester system* ni mpango mzuri sana ambao unawasaidia wanafunzi kuweza kuwapunguzia kama mzigo kwa sababu tunasoma wiki 17. Katika zile wiki 17 kuna kama wiki 3 za mwisho ambazo wiki 2 zinakuwa za mtihani na wiki moja inakuwa ni ya maandalizi. Lakini bahati mbaya sana ile wiki ya maandali hatuipati kwa sababu madarasa ni kidogo, walimu wanakuwa wanajitahidi tuhakikishe kwamba tunamaliza zile *course work*. Kwa hiyo unajikuta wiki ile ya mwisho ya maandalizi bado tunaendelea kutengeneza *course work*. Zile wiki 2 za mtihani yaani unaingia kwenye mtihani kama bado hujaweza kujiandaa vizuri kuingia kwenye chumba cha mtihani. Kwa hiyo naomba hilo Wizara iliangalie kuna upungufu sana wa madarasa.

Kwa upande wa Mpango wa Semina. Katika Vyuo Vikuu vyote nadhani wanaendesha *seminar system. Seminar system* inamsaidia mwanafunzi katika kufanya *argumentation.* Unakuta chumba cha kutosha wanafunzi 25 ili kila mmoja apate nafasi labda ya *urge* mambo ambayo amekuwa amefundishwa. Wanaingia wanafunzi kama 50 au 65 matokeo yake sasa inakuwa kwanza ni kero kwa wanafunzi wenyewe hata kwa mwalim ambaye anaweza kusimamia ile semina. Matokeo yake mnakuwa mmepewa maswali na kuna *seminar system* ambayo kuna mwanafunzi mmoja mmoja angeweza kusimama simama na kuweza kulielezea lile swali jibu lake kutokana na vitabu mbalimbali alivyosoma. Matokeo yake mwalimu anasema kila mtu aje ameandika swali lake. Kwa hiyo hapo ndiyo kuna matatizo, kuna neno moja wanafunzi wanalitumia kudesa. Muda umekuwa haukutosha, wanafunzi wamekuwa wamekopiana lile swali wamekwenda kukusanya na kitu kingine unaingia mle ndani unakuta kwa kutaka maksi 5 ambazo zinamsaidia kuongeza *course work* yake. Kwa hiyo ukiingia katika semina kuna

maksi 10, 15 za mahudhurio na 5 za kazi. Naomba suala hilo pia liangaliwe. Naiomba Wizara iangalie uwezekano wa kuthaminisha elimu yetu Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika ripoti mbalimbali ambazo wanazisoma za kuondoa umaskini unakuta sana sana kinachoelezewa elimu imekuwa kiasi gani katika Mpango wa MMES na MMEM. Mimi sijaona kama ni kitu muhimu zaidi kuliko Elimu ya Juu. Kweli ina umuhimu wake lakinina elimu ya juu lazima ielezewe tuonyeshe kiasi gani tumepanda katika Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, tunataka kujua Serikali ina mipango gani na mikakati gani madhubuti kuhakikisha kwamba Elimu ya Juu nayo inaboreshwa. Tunataka kuona mwanafunzi amemaliza Chuo Kikuu anaweza ku-*urge* kitu yaani *logically* kabisa kama ni Kiingereza au Kiswahili kuliko sasa hivi tunakuwa tunapata shida sana vijana katika soko la ajira na watu wengi waliosoma nje ndio unakuta kwamba Mashirika mbalimbali wanachoka kwa sababu tu wana cheti cha kutoka labda chuo chochote kilichoko Uingereza, unakuta wengine wanatoka Uganda na Kenya. Kwa hiyo sisi tunabaki nyuma wakati tumesoma.

Mheshimiwa Spika, pamoja na tatizo la wahitimu ambalo lipo tuna tatizo pia la wahadhiri wa vyuo vyetu. Walimu wengi wanaofundisha pale vyuoni wamemaliza *Masters* na wala hawajafaulu vizuri ni kutokana na kwamba mpango unaonekana labda sio mzuri wa kuhakikisha kwamba walimu wa Vyuo Vikuu wanapatikana. Walimu wengine ni wale wa *PH.D.* za *online* ambao wanafundisha pale Chuo Kikuu. Kwa hiyo inabidi tuangalie sana kama kweli tuna mpango wa kuongeza ubora wa elimu tuhakikishe kabisa na wahadhiri wanaofundisha wanafunzi kuwa bora.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo napenda kuongelea ni malazi kwa wanafunzi ni tatizo kubwa sana. Sasa nadhani kuna wanafunzi kama 15,000 ambao kabla ya wale ambao hawajamaliza kuna wanafunzi zaidi ya 15,000 lakini vitanda vya kulala sidhani kama vinafika 8,000 pamoja na kwamba kuna Mabibo Hostel pale. Mimi nitatoa *experience* ambayo ninayo. Kwa mfano Hall 2 wanakaa wanafunzi 360. Lakini kwa upande wa kaka zangu wanaosoma *Engineer* wana kituko kimoja. Wanakuwa labda wanafunzi 4 chumba kimoja wana *share* hivyo vitanda viwili ambavyo vipo. Kwanza ni hatari kwa sababu ya maradhi na magonjwa ya ngozi. Mtu anakwenda kusoma labda wanapangiana masaa wewe lala masaa manne nikirudi nakuamsha ukasome na mimi nipate nafasi ya kulala. Yule mwenzake anakwenda kukesha darasani mpaka asubuhi na wale wanasoma kuanzia asubuhi mpaka saa 12.00 jioni. Kwa hiyo tunaomba hili liangaliwe *accommodation* kwa kweli hili ni tatizo pale chuoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika suala hilo la *accommodation* pia mabweni mengi pale *University of Dar es Salaam* yale ya pale *campus* kwa kweli yamechakaa. Mfumo wa majitaka na majisafi kwa kweli sio mzuri. Unaweza ukatoka darasani ukakuta maji yamejaa mpaka mlangoni kwako au saa nyingine mpaka chumbani, saa nyingine ni maji ambayo yanatoka vyooni.

Kwa hiyo tunaomba sana kama kuna fedha za kufanya marekebisho yafanyike, hali ni mbaya. Kwa upande mwingine Hall 2 na Hall 5 ni yale marefu ambayo hata ukipita kwa mjini kwa mbali ukiwa baadhi ya sehemu unayaona yanaonekana kwamba yana *crack* na yanaweza kuanguka na kuna watu wanasema utafiti umefanyika inaonekana kwamba hata miaka 5 inaweza isifike. (*Makofi)*

Tatizo lingine yale mabweni ni kwamba haya lift ya uhakika. Mwanafunzi anaamka asubuhi anakesha amebeba kila kitu kwamba asirudi mchana hata dakika moja kwa sababu atapanda juu mpaka ghorofa ya 11 anarudi saa 5.00 usiku baada ya kumaliza kusoma ili alale kesho asubuhi aamke mapema na vitu vyake aondoke. Kwa hiyo tunaomba sana hili suala pia liangaliwe.

Suala lingine ambalo napenda kuliongelea ni kwamba nadhani kila mtu anafahamu kwamba kazi ya Chuo Kikuu ni kufanya *research*, kufundisha na kufanya *Consultation.* Lakini sasa hivi Chuo Kikuu chetu cha Dar es Salaam tunaona kwamba kinafanya kazi zaidi za kutengeneza vitega uchumi.

Kuna *bookshop* pale ilikuwepo lakini sasa hivi imegawanyishwa sehemu mbili. Sehemu moja kuna mwekezaji ameweka Benki ya *CRDB* pale. Sasa kama *bookshop* inageuzwa sehemu ya biashara bora hata yule mtu angekuja kuuza vitabu basi amekuja kufanya benki. Kwa hiyo ina maana hata uendelezaji wa ile *bookshop* kwa kweli utakuwa wa matatizo na elimu tunaendelea kuibomoa sisi wenyewe.

Kwa upande mwingine napenda kuongelea ile *Mlimani City.* Nilipomaliza pale 2004 *Mlimani City* ilikuwa bado haijaanza kujengwa. Wakati tunapitapita nikaona watu wanajenga nikajua kwamba kwa sababu chuo kina matatizo ya mabweni na madarasa sasa hivi labda wameamua kuongeza mabweni na madarasa. Lakini kuja kusikia tunajenga *Mlimani City* na pale kutakuwa na *Five Star Hotel* inawezekana kutakuwa na *cassino* kutakuwa na kuna maduka mbalimbali.

Vile ni vitu ambavyo ni tofauti na taaluma. Na siku hizi wanafunzi wanaosoma pale Chuo Kikuu ni miaka chini ya 18, sio kama zamani walikuwa wanaingia watu wazima tu kwamba tutasema hawa ni watu wazima wanaweza wakaji-*contro*l wenyewe, lakini pale ni watoto chini ya miaka 18. Kuna watoto wa miaka 17 mpaka 21 ndio wanaoingia mwaka wa Kwanza .

Kwa hiyo naomba Serikali iwe inaangalia mbele, iwe na uzalendo Kwa sababu pale ilikuwa ni eneo la ku-*expand* Chuo Kikuu na kwa nini wasimpe huyu mwekezaji sehemu nyingine. Kwa hiyo naona hilo ni tatizo kubwa sana tuwe wazalendo na tuache ubinafsi fedha peke yake sio kigezo cha kututatulia matatizo yetu. Tuwaelimishe Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho ningependa kukizungumzia kama muda bado unaniruhusu ni kuhusu uwiano wa mahitaji. Sasa hivi Chuo Kikuu kimekuwa

na uanzilishi wa Idara nyingi yaani inajihusisha na mambo badala ya kitaaluma zaidi imejihusisha zaidi na masuala ya utawala. Kuna Idara nyingi sana zimeanzishwa zikiwemo Idara ya *Research* na Uchapishaji vitabu halafu kuna Idara ya *Consultancy*.

Vitu hivi vinaonekana vinatakiwa viende pamoja lakini vinawekwa tofauti tofauti kiasi kwamba katika kila Idara lazima kuwe kuna gari, ofisi sasa naona kama ni gharama kubwa badala ya kuongeza Idara ya Utafiti na Idara ya *Consultancy* ingekuwa kitu kimoja kwa sababu unafanya utafiti unaweza kufanya pia na *Consultancy* kuliko kufanya Idara zikawa tofauti tofauti. Hiyo ni kuongeza tu gharama ambazo mimi naona kama hazina maana.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ningependa kuongelea ni kuhusu masuala ya wafanyakazi pale Chuo Kikuu.

Pale Chuo Kikuu nadhani kila mtu anajua kwamba kuna wafanyakazi wa aina mbalimbali. Kuna Wahadhiri na vile vile kuna wafanyakazi ambao ni wa *administration* au waendeshaji wa pale Chuo Kikuu. Ni dhahiri kwamba mishahara yao haiwezi kulingana kutokana na labda na tofauti ya elimu zao au tofauti ya kazi zao. Lakini kwa sasa hivi inaonekana kwamba kuna ubaguzi katika kuongeza maslahi ya wafanyakazi.(*Makofi*)

Kulikuwa na matatizo mbalimbali ambapo kukaundwa Kamati husika ili kuhakikisha kwamba wanaangalia maslahi ya wafanyakazi pale Chuoni. Ikaonekana kwamba wahadhiri angalau wamesikilizwa kilio chao wameongezewa mshahara kama nusu ya maombi yao, asilimia 50 waliongezewa Januari. Baadaye Julai wataongezewa asilimia 50 iliyobakia, kwa maana hiyo watakuwa wametimiziwa asilimia 100.

Je Serikali inasemaji kwa wale ambao ni wafanyakazi wengine kwa sababu kazi zao wanazifanya pamoja. Kwa hiyo naomba sana Serikali iangalie hili na tunaomba majibu jioni wakati mna *summaries* hotuba yenu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, naomba na mimi nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja iliyoko mbele yetu, kwanza kwa kukupongeza wewe kwa kazi yako nzuri na Mheshimiwa Naibu Spika kwa jinsi mnavyotuongoza Wabunge na tunaamua maamuzi ambayo yana heshima ya uwakilishi ambao umetuweka humu ndani, tunakuombea kwa Mwenyezi Mungu aweze kukuelekeza vizuri ili tuweze kuendelea vizuri katika miaka hii mitano.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nichukue nafasi hii kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake pamoja na watendaji wote wa Wizara hii ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia kwa kazi nzuri wanayoifanya kuhakikisha

kwamba sasa hapa ndipo tunatafuta wataalam ambao wataweza kuiongoza nchi yetu katika nyanja za utaalam.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuongeza Chuo Kikuu kingine hapa Dodoma, ambacho sasa kitakuwa nafikiri itasaidia sana kuhakikisha kwamba wanafunzi watakaomaliza kidato cha sita wanachukuliwa moja kwa moja kutoka shule hizo ili waweze kujiunga na vyuo vikuu hivyo.

Mheshimiwa Spika, katika kuongelea hotuba hii ya Wizara ya Elimu ya Juu mimi nitaongelea masuala mawili ya kuhusu uboreshaji wa huduma ya elimu ya juu pamoja na upatikanaji wa wanafunzi kuingia katika vyuo hivi. Katika elimu ya sekondari kwanza tulianza katika kuboresha elimu ya msingi MMEM, wameweza kuboresha sana maeneo ya shule za msingi. Tunasema kwamba wanafunzi hawafaidiki na elimu yao kwa ajili ya kukaa chini na kuandika migongo imeinama. Lakini kwa sasa kutokana na utawala mzuri wa Chama cha Mapinduzi, sasa tatizo hili katika shule za msingi limekwisha na mahali pengine imebaki sehemu chache sana.

Mheshimiwa Spika, sasa tumeingia tena kwenye mpango mwingine wa MMES, kwa kuboresha shule za sekondari baada ya kuboresha shule za msingi wanafunzi sasa wanakwenda kwenye shule za sekondari. Kama tumeamua shule za msingi na za sekondari kuboreshwa kiasi hicho ninaomba sasa ndugu zangu wa vyuo vikuu mjindae. Kwa sababu maamuzi ya MMES ni kwamba kila kata tuwe na sekondari. Kama umeamua kila kata tuwe na sekondari, kata katika nchi hii ni nyingi sana ambazo zitatoa wanafunzi wa kidato cha sita ambao wanatakiwa sasa watoke pale waingie katika vyuo vikuu. Nikuombe Mheshimiwa Waziri uje na mkakati maalum na endelevu kuhakikisha sasa hawa watanzania watakapotoka katika shule za sekondari watafikiaje katika kupata elimu ya juu ya sayansi na teknolojia ili na wenyewe wawe sawa na wanadamu wengine katika nchi nyingine za dunia.

Mheshimiwa Spika, kama atakuja na mkakati huo basi nahakika kwamba tutakuwa na wataalam wazuri vyuo vikuu. Vyuo vikuu ndiyo tunapata wahandisi wazuri, madaktari na watalaam ambao wanawezesha kuja kuiongoza nchi yetu hii, katika mikakati ambayo tunasema kwamba ya kukuza uchumi katika nchi yetu. Nitaomba nianze kuzungumza juu ya uboreshaji wa huduma ya elimu ya juu. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri lengo la kuchukua wanafunzi katika vyuo vikuu kwa mwaka huu anataka kusema kwamba atachukua wanafunzi 68,029, ni wengi. Lakini naomba nichukue nafasi hii kutoa pendekezo langu.

Mheshimiwa Spika utaratibu ambao umekuwa ukitumika wa kuwachagua watoto wa kujiunga na vyuo vikuu naomba uangaliwe upya. Sasa hivi tuna Mikoa 26 na huko Mikoani kuna sekondari nyingi katika mgawanyo wa nafasi hizi nikuombe kupitia wewe, Mheshimiwa Waziri aangalie kutoa nafasi sawa kutoka Mikoa ni za kuwachukua wanafunzi hawa wanaomaliza kidato cha sita. Kigezo kizuri cha kuwachukua wanafunzi ningeomba Mheshimiwa Waziri ajaribu kuwa na mahusiano mazuri ya karibu na Mheshimwa wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi anapotoa matokeo ya *form six* ninafikiri sasa inafikia wakati waziri

uchukue wanafunzi ili kuepusha lawama za rushwa, tatizo mojawapo ambalo linawasibu sana wanafunzi wa kike ya ngono ili aweze kupata nafasi kuingia chuo kikuu.

Lakini Waziri huyu atakapochukua matokeo ya *form six, division one* na *two*, angalie kwamba mwanafunzi huyu aliyepata *division two* ya *point ten* ambaye alikosa *point* moja tu apate *division one*, achukue fursa hii basi kuwachukua moja kwa moja wanafunzi hao ili waweze kuorodheshwa katika vyuo vikuu hivi, hapo utakuwa umepunguza lawama, kwamba mtoto wa fulani amechaguliwa kutokana na vigezo vya kufaulu kwake ndiyo vimemfanya aingie chuo kikuu. Itakuwa vizuri atakapofanya hivyo mapema basi aandae maeneo ya kwamba wanafunzi fulani wakutoka *form six* na bado kuna sehemu nyingine ya wafanyakazi akatenga nafasi hizo zikajulikana mapema ili kuwapa mwanya ambao watoto wa wakulima ambao wako vijijini wamekosa kuingia chuo kikuu mapema wakatafuta vyuo vingine ambavyo vitawasaidia.

Mheshimiwa Spika, nitaomba tu nitoe mfano sasa hivi. Watoto wengi wamemaliza *form six* tangu mwezi wa tatu mpaka sasa hivi hatujajua kwamba vyuo vikuu hivi vimechukua wanafunzi wangapi, na ninategemea kwamba vyuo vikuu huenda vikaanza mwezi *October* au Septemba vikafunguliwa. Lakini mpaka sasa hivi hatujajua hatima ya hao watoto wangapi wamechaguliwa kuingia vyuo vikuu na wangapi wameachwa hatujajua kwamba watatafuta saa ngapi vyuo vingine. Lakini la muhimu zaidi ili wizara hii iwaweke sawa wanafunzi itakuwa imepunguza na msongamano na watoto sasa kuhangaika mara achukue Chuo Kikuu cha Tumani au cha Mzumbe au wapi. Lakini Mheshimiwa Waziri mtakapojipanga kwa sababu vyuo vikuu vyote viko chini yako basi utusaidie sisi wazazi ambao tuna watoto kama hawa kutupangia mapema kwamba watoto wenye vigezo hivi vya kuingia vyuo kikuu uwe unatutolea mapema ili tuweze na sisi kujipanga vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie suala la bodi ya mikopo. Naomba nichukue nafasi hii nizungumze kwa dhati kabisa nimpongeze sana Mheshimiwa Mkono katika kutusaidia kuhakikisha migomo ambayo ilikuwa anajitokeza mara kwa mara ya kuhusu mikopo ya wanafunzi imepungua. Sisemi kwamba imeisha lakini imepungua nimpongeze Mheshimiwa Mkono kwa kazi nzuri ambayo yeye ameenda pale kutoa utaratibu ambao umesaidia kidogo katika utoaji wa mikopo hii. Lakini utaratibu wa utoaji wa mikopo hii, ninaomba Mheshimiwa Waziri uangaliwe upya. Ni kweli bajeti uliyopewa ni ndogo lakini kama ni ndogo tugawie maeneo yote ya Mikoa yote. Nimwombe Mheshimiwa Waziri katika kuhakikisha kwamba basi hii mikopo ninayoigawa kwa wanafunzi iende kwenye maeneo mengi. Kuna watoto wengine mara nyingi mikopo inaishia Dar es Salaam, watu wa Pwani, karibu karibu na Wizara pale. Nimwombe basi hata hiki kidogo kilichopo Mheshimiwa Waziri kigawiwe kwa watoto wengine ambao wako mbali na maeneo hayo.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri juzi tu ndiyo zimetokea *form* za kujaza za watoto hawa wa kupewa mikopo, naomba nichukue nafasi hii kwa masikitiko makubwa wakati Mheshimiwa Waziri ukijua kwamba vyuo vyako havijatangaza kwamba imechukua wanafunzi wangapi. Leo unatoa *form* za wanafunzi wajaze kuomba mikopo, wanaomba mikopo kwa chuo gani.

Nimwombe Mheshimiwa Waziri ili bodi yako hii ijipange vizuri baada ya wewe kuhakikisha kwamba umewachukua wanafunzi wa kuingia hivyo vyuo basi bodi ya mikopo iwasiliane na wewe kuhakikisha kwamba vyuo vyako vya Serikalini vingapi ambavyo vitahitaji mikopo utakuwa umeirahisishia sana.

Mheshimiwa Spika, nashukuru baada ya kuona wanafunzi wengi walikuwa wamepitwa baada ya kutangaza mwisho wa kurudisha fomu za mikopo tarehe 15. Lakini naona Serikali imeliona mapema ikaongeza muda, nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kuliona hili mapema kuna watoto wengi sana vijiji kule walikuwa wamepitwa na wakati hawakuweza kujaza. Lakini sasa nakuhakikishia kwamba kwa muda uliongeza wameweza kujaza niwaombee tu sasa sijui huko katika mgao wako sijui kama watafanya lakini *inshallah* Mwenyezi Mungu atawasiadia wanaweza kupata.

Mheshimiwan Spika, vyuo vikuu ndiyo mahali ambapo ni pa kuwekeza sana, na urithi wa mtoto sasa hivi ni elimu. Elimu tumejitahidi kwamba MMEM na MMES, tumeimarisha sasa tunakwenda kwenye vyuo vikuu. Hapa ndipo tunapotafuta wataalam. Sera ya awamu ya nne inasema kwamba ili tuwawezeshe watanzania ninaomba tuwawezeshe katika elimu. Tujipange vizuri kuhakikisha kwamba watoto wetu hawa tunawapa elimu ya kutosha ambayo sasa itakuwa imepunguza kulalamika wanakosa ajira katika nchi yao. Kwa sababu kama tunatoa ma-*engineer* hakutakuwa na haja ya kutoa tena ma-*engineer* kutoka nchi za nje. Kama tutakuwa tumetoa madaktari hatutaagiza tena madaktari kutoka nchi za nje. Hivyo suala la ajira tutakuwa tumelipunguza sana kwa kutumia vyuo vikuu vyetu hivi. Hivyo ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri aje na mkakati endelevu ya kuhakikisha kwamba vyuo vikuu hivi vinaongezewa bajeti ya kutosha ya kuhakikisha kwamba tunaimarisha watoto wetu katika maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, kama tutawekeza katika elimu kwa hawa watoto wetu, wataheshimiwa katika nchi yao. Watasema nimetoka katika Chuo Kikuu cha Dar es salaam, atakuwa ameheshimika kwamba amepata elimu katika nchi yake na hawatakata tamaa tena kwamba ajira hawatapa. Lingine katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 25 amesema kwamba tayari wanafunzi 42,729 wameshakopeshwa mikopo. Mikopo hii ni mfuko ambao kama ni *revolving fund*, ambao unatakiwa watu warudishe ili watoto wengine asome. Nitamwomba Mheshimiwa Waziri ingawaje katika ukurasa wa majumuisho katika hotuba yake anasema kwamba kuna maazimio ambayo wamesema kwamba watakusanya hizi pesa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia (*Makofi*)

**MHE. MARGRETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika awali ya yote napenda kukushukuru kunipa nafasi ya kuweza kuchangia lakini zaidi ya hapo nakushukuru sana kwa kuniwezesha leo kusoma hotuba kwa niaba ya kamati yangu hapo mbele hapo. Kwa sababu ni tangu jana ulihakikisha maandalizi ya mimi na hali yangu yanakamilika na basi umeweza kunipa nafasi na ninadhani sikukuangusha nimeisoma vizuri.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na shukrani hizo kwako zaidi ninayemshukuru asubuhi hii ni Mheshimiwa Mwenyekiti Omar Kwaangw' ambaye kwa kweli tangu wiki iliyopita alinihimiza kwamba unapaswa kusoma hapo mbele. Nikamwambia Mwenyekiti mbona mimi siwezi, akaniambia hapana. Kwa hiyo namshukuru sana kwamba ameonyesha ni ya kutoa nafasi kijinsia na kihali. Kwamba nakupa nafasi wewe endelea tuone kama unamudu au vipi. Kwa hiyo imenipa moyo na namshukuru sana na nitaendelea kumtii na kumshauri.

Mheshimiwa Spika, zaidi niende ndani ya hoja ambayo iko mbele yangu nashukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Prof. Peter Msolla, Naibu wake Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, Katibu Mkuu Dr. Naomi Katunzi watendaji wa Wizara na taasisi nyingi tu ambazo zimo chini ya hii Wizara, kwa kuandaa hotuba hii kwa ujumla wao na katika kuisoma mimi nimeona inatoa matumaini kwa watanzania kwamba sasa nadhani tumejizatiti kuongeza wanafunzi katika taasisi zetu pamoja na matatizo ambayo yapo na yataendelea kuwepo. Kwa sababu ni ukweli kabisa huwezi kukosa matatizo lakini tu ni kwa namna gani unavyoyatatua ndiyo inakuwa *challenge* kwetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nijielekeze katika maeneo machache. Moja mikopo ya wanafunzi. Mimi nimefarijika sana kwa sababu nilikuwa kwenye Kamati pia nilipata ufafanuzi wa vigezo ambavyo vimeelekezwa vitakavyoweza kumwezesha mwanafunzi kupata mkopo. Sasa hapa kigezo ambacho mimi ninajikita nacho ni hiki cha mwanachuo ataweza kupata mkopo, kama ni mlemavu ataweza kupata mkopo au wazazi wake wanaulemavu na ni maskini wakipato. Hilo mimi nimefarika nalo sana kwa sababu ni ukweli usiofichika sana kwamba wazazi wenye watoto wenye ulemavu au wazazi wenye ulemavu kwa kweli ni maskini na kiasi fulani wanashindwa hata kumudu maisha yao ya kila siku.

Lakini pamoja na faraja na shukrani hizo labda ningependa kufahamu, kwa sababu wanachuo wenye ulemavu kama hotuba ya Waziri anayesubiri ilivyojielekeza wanamahitaji mengi licha ya haya ya kisomi. Lakini wanamahitaji mengi ya msingi; kwa mfano mlemavu wa viungo. Mwingine atahitaji hata nyezo ya kuweza kujimudu, *Bajaj*, *calliper,* viatu ili aweze kusogea kufika kwenye ma-*lecture rooms*. Wasioona watahitaji *brail machine,* wa kumtafsiria na vitu vingine ili aweze kumudu hayo masomo.

Sasa ninauliza je, katika kupata mikopo na mambo haya hayo niliyoyanzunguza kwa mfano hawa wanachuo hawa watakopeshwa nayo? Au mkopo utaishia kwenye mambo tu ya mule darasani. Kwa mfano nimesikia kwamba the *highest* atakayepata mkopo wa juu itakuwa labda ni *60 percent* ya yale mahitajio au mwingine 40 *percent*. Sasa hawa wenzangu ambao hata hiyo 60 ni ndani ya darasa lakini yale mengine ya kuwasaidia kuweza kufika darasani hawana uwezonayo haya yatakuwakuwaje, yatawekwawekwaje, watapata fedha za mikopo au itakuaje?

Mheshimiwa Spika, kwa mfano haya ninayoyazungumzia viungo hivyi nini, vyuo vilikuwa vinajitahidi kutoa sijui kwenye hela za kutoka kwenye hela zao za *development* halafu wanawasaidia. Sasa kwa mtindo huu wa mikopo itakuwaje? Hilo naomba msaada,

lakini kimsingi kama atashindikana, mimi ninavyofahamu wanachuo wenye ulemavu wanaoweza kufika vyuo vikuu ni wachache.

Sasa katika uchache huo mimi ninaishauri Serikali kwa kweli iwahudumie, kwa sababu kama ni mateso, kama ni kujitahidi, kama ni kujikongongoja inafikia mahali mtu unashindwa. Kwa hiyo ninaomba kabisa wanafunzi wenye ulemavu ambao wamekidhi vigezo vya kuingia vyuo vikuu ambao ni wachache kwa kweli wahudumiwe na Serikali nadhani watajisika amani pamoja na kwamba mimi nilisoma lakini nilichangia kidogo, na nilikwenda kama mwalimu sasa wenzangu wanakwenda *fresh from school* kwa kweli wasaidiwe ndiyo ushauri wangu.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo jingine ambalo napenda nizungumzie hapa ni jitahada ya Serikali katika kupanua elimu ya juu, hongera sana kwa sababu inaendelea kuhamisisha taasisi mbalimbali kuanzisha vyuo hivi ili taasisi hizo ziweze kuisaidia Serikali katika utoaji wa elimu ya juu. Lakini pamoja na jitihada hizo za uhamasishaji mimi naona mpaka sasa hivi gharama za elimu ya juu hasa katika vyuo vingine vinavyoanzishwa tunavyovihimiza kwamba waanzishe vyuo hivi, gharama ni kubwa mno. Gharama ni kubwa kiasi kwamba mimi naogopa ni wanafunzi wachache wenye wazazi wanaojimudu kifedha ndiyo watakaoweze hata kufaidika na matunda hayo ya upanuzi wa elimu ya juu.(*Makofi*)

Sasa hapo ushauri wangu ni kwamba Wizara na Serikali kwa ujumla iendelee kutoa maelekezo kwenye taasisi hizo mpya ili ziweze kupunguza gharama katika masomo la sivyo tutajenga matabaka ndani ya nchi kutokana na uwezo wa watu na hili si lengo letu. Lengo letu ni kwamba tufike ili tuweze kuihudumia jamii tukiwa na hali ya elimu inayotakiwa hasa katika ulimwengu huu ambapo elimu sasa inachukua nafasi.

Mheshimiwa Spika, suala jingine ni kuhusu ujenzi wa Chuo Kikuu kipya kitakachojengwa hapa Dodoma jina sijui. Hili ni jambo jema sana kama hotuba ilivyosema na hata Kamati yetu tulilifurahia sana na wananchi wamelifurahia sana, hasa wa Mkoa wa Dodoma kwamba sasa linaonyesha picha kwamba Makao Makuu yanaanza kusogea sogea kwa njia moja au nyingine na ninaamini watakuwa mstari wa mbele kushirikiana na Serikali kuhakikisha kwamba jambo hili linafanyika kwa haraka iwezekanavyo kama ambavyo Mungu atatujalia. Lakini kwa sababu ni majengo na ni chombo kipya, hapa ushauri wangu ni uleule wa siku zote. Mimi nitaendelea kusema tu kwa sababu katika kusema ndiyo unaelimisha, unatambulisha na unahabarisha. Ninaiomba Serikali, kwa sababu majengo ni mapya na nia ni kupanua elimu ya Chuo Kikuu watu waweze kwenda hapa mazingira muafaka katika chuo hiki yaweze kuzingatiwa ili wanachuo na wahadhiri wenye ulemavu watakaoweza kuja kufundisha ama kusoma hapa waweze kupata nafasi ahueni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sipendi kuona wengine waendelee kupata matatizo mimi niliposoma chuo kikuu kwanza nilipokwenda tu waliniuliza wewe umekuja kusoma utweza haya mazingira pale *registration office*, nikawaambia kuna nini, wakasema ngazi nyingi sasa, nikawauliza hivi sasa mnaniambia ni *postpone* nitakapo *postpone* miaka miwili hizo ngazi nitakuta zimebomolewa? Wakagwaya, *that was challenge* niliumia nikawaambia mimi nitajitahidi kwa uwezo wangu nitakaposhindwa basi. Nikajikongoja

kwa shida sana, tena afadhali wenzangu waliopita baadaye wakawa wananunuliwa sijui *bajaj* marekebisho yakafanyika lakini enzi zile *nothing was their* ni wewe unahangaika na Mungu wako, lakini nilimudu kwa shida sana. Sasa sipendelei wengine waje waendelee kupata taabu hizi na kumbe walipata mtu wa kuikumbusha Serikali kwamba jamani twende hivi. *(Makofi)*

Ninaomba Wizara kwa sababu ndiyo inatoa sera wote watakaojenga majengo upya ya vyuo hivyo wa *accommodate* hali hizo ninazozisema. Kuna chuo kile cha ramani watachora wanajua ninayoyasema mimi nafupisha tu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi leo sikuwa na la kusema sana ni hilo hilo Jimbo langu basi niweze kulisemea ili nalo liweze kufaidika kwa sababu mengine yote yataongelewa na wenzangu. Baada ya kusema haya nashukuru sana napenda kuunga mkono hoja hii mia kwa mia. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Margreth Mkanga wakati wote umekuwa ni kielelezo. Watu wengi tunajima kutumia vipaji nyetu kwa sababu kama wewe umeweza kufanya yote hayo je, sisi wengine ambayo Mwenyezi Mungu ametupa kila moja.

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI:** Mheshimiwa Spika, *Bismillah Rahman Rahim,* kwanza naomba nichukue nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa kunipa nafasi hii na mimi leo kuwa mchangiaji katika hoja hii iliyopo mbele yetu. Nisingekuwa na mengi ya kuzungumza kwa vile ni mmoja katika wajumbe wa Kamati ambayo ilijadili hotuba hii au ilijadili Wizara hii kikamilifu mpaka leo ikafikia hapa kuja kutolewa maelezo. Lakini kwa jinsi nilivyo huwa na sahau-sahau kabla sijaenda mbali ningeomba nitumie nafasi hii kuunga mkono hoja hii kwa asilimia zote.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo naomba nitoe pongezi maalum kwako kwa jinsi ya uamuzi uliochukua juzi na jana wa kuangalia shughuli za mambo zinavyokwenda na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi iliyopita kwa kukaa nyuma ambapo kwa muda wote nimekuona ukiangalia. Pengine labda kama pangefanyika kosa ungesema, lakini kwa bahati nzuri hapakutokea kosa. Kwa hivyo nakupongeza wewe binafsi pamoja na mtoa hoja wa jana kwa jinsi ya hatua mlivyozichukua, hongereni sana.

Baada ya hayo nilikuwa na machache ya kuzungumza, kwanza ningezungumza kuhusu suala la *Institute of Marine Science*, Taasisi ya Sayansi za Bahari kilichoko Zanzibar. Katika ukurasa wa 11 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, nyota pili kutoka chini naomba kunukuu: “Moja katika utekelezaji wa mambo yake ni kuendelea na ujenzi wa awamu ya kwanza ya sehemu ya Buyu Zanzibar. Ambako ndiko kutakuwa na makao mapya ya Taasisi ya Sayansi za Bahari.”

Mheshimiwa Spika, kama alivyozungumza mchangiaji mmoja aliyepita hapa kuhusiana na chuo hiki ni kwamba kwa kweli ninamasikitiko, ni miaka mingi kilikua ni kilio cha chuo hiki; na kwa juhudi kubwa zilizofanywa katika awamu zilizopita mpaka ikafikia kiwango cha kufikiwa muafaka wa kuanzishwa kwa taasisi ile, naona inastahili kila hali ya kuona sasa zile juhudi ambazo zimechukuliwa na Waheshimiwa Wabunge na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ambayo nampongeza sana Mheshimiwa Rais wa

Zanzibar kwa juhudi ambazo amezichukua za kutoa vibali na kila hali ya fursa ili ipatikane kuendelezwa chuo kile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa imefika wakati wa kwamba tuanze ujenzi wa Chuo kile. Kwa bahati, katika awamu iliyopita nilikuwa ni Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es salaam. Nilikuwa nashuhudia, nimesema, nimesema na kuomba kuchangia katika kuhakikisha Chuo hiki na hatua tumeiona, tunashukuru sana. Lakini nasikitika kwamba bado Serikali naweza nikasema kwamba haijatia mkazo wa kuona kwamba Chuo hiki kinajengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka ulopita, Chuo hiki kilitengewa shilingi milioni 400 na kwa taarifa hapa na taarifa ya Kamati ni kwamba gharama ya ujenzi huu unahitaji shilingi bilioni 5.2. Sasa awamu hii, walivyoona sijui kama zote zitapelekwa, lakini imetengewa shilingi milioni 800. Kwa taarifa ni kwamba mkandarasi bado yuko *site,* anadai malipo yake, hajapewa hata senti moja ya kuweza kuwezesha kujenga Chuo hiki.

Mheshimiwa Spika, sasa, hapa kweli tuna nia ya kusema kwamba tumalize Chuo hiki na ikiwa kama Serikali imepanga, tuseme kutoa hizo shilingi milioni 800, ijaliwe kwamba kila mwaka iwe inatoa shilingi milioni 800 kwa awamu hii au kwa miaka mitano, 8 x 5 ni 40. Sasa itakuwa ni bilioni 4, bado hatujafikia kiwango cha kumlipa mkandarasi na kujenga chuo kile na kukamilika.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali haioni kwamba sasa hivi ipo haja ya mkakati maalum wa kuona kwamba sasa hivi inatafuta nyenzo za kuweza kufanikisha kumalizika kwa ujenzi wa chuo hiki? Kwa sababu mifano ipo, hivi sasa kuna taarifa kwamba kuna ujenzi wa kumbi za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambao kila ujenzi unagharimu zaidi ya bilioni 1.3.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu kimeweza kutafuta mikopo kupitia *Tanzania Elimu Authority (TEA)* na kikapata kujenga ukumbi ule kwani haiwezekani Serikali ikatafuta utaratibu wa kutafuta hela kwa njia nyingine na kufanikisha ujenzi wa *Institute* hii na ikamalizika kwa muda ambao umepangwa na vile vile tukaondokana na hii, pengine huenda ikaja ikawa aibu ya kujakutakiwa fedha wakati mkandarasi huyu atakapotaka fedha zake za kumaliza kazi zake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningeshauri sana hapa Wizara na Serikali, kutafuta mpango mwingine wa kuweza kuhakikisha kwamba Chuo hiki kinapatiwa fedha za kutosha na mkandarasi huyu aweze kulipwa ili Chuo hiki kimalizike kwa muda ambao umepangwa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni kuhusu Sayansi na Teknolojia ambayo kwa mujibu wa hotuba katika ukurasa 32 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri naomba kununukuu, amesema: “Katika mwaka 2006/2007, Idara ya sayansi na teknolojia inatarajia kutekeleza yafuatayo, kati ya hayo, ni kukamilisha utungaji wa Sera ya Taifa ya Utafiti.”

Mheshimiwa Spika, sasa ninalotaka kuzungumzia hapa ni suala la utafiti. Tukikubaliana kwa kweli nchi zote, maendeleo ya nchi yanategemeana na shughuli za kufanya utafiti. Nakumbuka kulikuwa na azimio au azma ya kwamba kuwe na kasma ya si chini ya asilimia moja ya pato la nchi kupelekwa katika tafiti na mpaka hivi sasa sijui kama tumefikia lengo hilo, lakini inavyoonyesha ni dhahiri kwamba bado Serikali haijachukua mkakati wa kufanikisha shughuli hizi za kuendesha shughuli za utafiti kufuatana na kuimalisha na kukuza shughuli za teknolojia. Ningeiomba sana Wizara kutilia mkazo kufikiria suala hilo lingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ambalo ningezungumza katika muda huu, ni suala la kuiendeleza Zanzibar. Mheshimiwa Waziri katika kujibu maswali, nakumbuka mara mbili katika kipindi hiki, alizungumzia kwamba katika kutekeleza na kuisaidia Zanzibar, si tu kuisaidia, lakini ni jukumu la Zanzibar kuona kwamba nayo inapiga hatua ili kuondoa ile lamawa, alisema kwamba, Zanzibar inawakilishwa vizuri katika shuguli zote zinazohusiana na Elimu ya Juu. Akatamka kwamba katika *Commission* ya Vyuo Vikuu kuna wawakilishi wawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa najua kwamba katika wawakilishi wawili, hapa katika Bunge lako Tukufu, tulichagua mjumbe wa kuwa katika Bodi hii ya Vyuo Vikuu. Nasikitika kwamba tokea tumechaguliwa, mimi ambapo pengine ndiye mjumbe huyo anayetajwa kwamba ndiyo katika hao wawili, mpaka kufikia leo, sijasikia taarifa yoyote, sijahudhuria kikao chochote, sijatajwa kwa suala lolote, licha ya kuuliza kwamba kuna nini. Sasa ikiwa hii ndiyo hali ya kusema kwamba kuna wawakilishi Zanzibar ambao wako katika suala la Vyuo Vikuu na suala hili na tunafikia hatua hii.

Mheshimiwa Spika, naomba sana kama Mheshimiwa Waziri alisahau, leo tunamkumbusha kwamba ipo kila haja ya kuona kwamba ile *quarter system* ambayo ilikuwepo, iwe inafikiriwa kwa dhati kabisa. Nazungumza haya kutokana na maelekezo au salaam nilizozipata baada ya baadhi ya wananchi kuniambia kwamba sasa mbona Waziri anasema kwamba hakukuwa na utaratibu huu, na kwa kweli baada ya kukaa katika muda wa Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, nilikuwa nachunguza na kuona hali ya wanafunzi kutoka Zanzibar, kwa kweli ilikuwa ni hali ya chini kabisa. Kwa hiyo, kuna kila haja ya kuona kwamba tunapanga mkakati maalum wa kuona kwamba tunaifikiria Zanzibar, Wazanzibar tuna akili ya kufahamu.

Mheshimiwa Spika, mimi nimemaliza Udaktari baada ya kusoma Darasa la 12, lakini nimesoma na watu wa *form six* na nimemaliza kuwa Daktari mpaka nikapata *degree* ya pili na ya tatu kutokana na kumaliza *form four* na natokea Zanzibar.

Kwa hiyo, natoa ushauri sana kwamba hapa Mheshimiwa Waziri pamoja na Serikali ifikirie ili kupunguza hili tatizo na suala la kuona kwamba labda Zanzibar tunawekwa nyuma kuhusiana na taaluma ya Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, sitopenda nipigiwe kengele ya pili, baada ya hayo maelezo machache, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia zote. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie japo kidogo kuhusu Wizara hii nyeti ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naungana na wenzangu kwa kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wa Wizara hii kwa kazi yao hii ya matayarisho ya bajeti hii ambayo iko mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia, labda ningeomba nimkumbushie tu Mheshimiwa Waziri kwamba katika ukurasa wake wa saba alisema katika miaka ya 1990 kulikuwa na Vyuo Vikuu viwili na vya Ufundi vitatu, lakini nataka kumhakikishia kwamba kulikuwa na chuo kingine cha nne cha Ufundi cha Karume kule Zanzibar. Kwa hiyo, tulikuwa na vyuo vya Ufundi vinne kikiwemo *Karume Technical College* kilichoko Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo namwomba hata kwenye jedwali lake kiambatanisho namba tano, akiingize mle ili kuwa na takwimu sahihi ya wanafunzi ambao wanasoma katika vyuo hivyo kikiwemo na kile cha Arusha ambacho amekisahau kwa bahati mbaya, nafikiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, kama walivyosema wenzangu ni Wizara muhimu sana katika maendeleo ya nchi yetu na ndiyo inayosimamia uzalishaji wa wataalam wetu.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengi sana wameshasema matatizo ya vyuo. Vyuo vyetu tulivyo navyo vina matatizo mengi. Kwa kweli hata kuhesabu, haina mashaka hauwezi ukayamaliza. Lakini moja alilozungumzia Mheshimiwa Magdalena Sakaya, ni kuhusu Chuo Kikuu kile cha Dar es Salaam na mimi nimesikia kwamba kuna kampuni ya *Mlimani City* ambayo imeshaanza kujenga pale. Imepewa eneo la kujenga Hoteli kama *Shopping Centre*. La kuongezea ni kwamba watatumia lile eneo kwa muda wa miaka 50. Sasa muda wa miaka 50 hata wale vijana pale, nafikiri watakuwa wameishazeeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya miaka 50, ndio Chuo Kikuu inakuwa mali yake. Lakini kingine najiuliza kwani nini akapewa kujenga hoteli pale? Wale ni wanafunzi, hawana hata pesa. Sasa itakuwaje wanafunzi? Ina maana ile *concentration* yao kwanza haitakuwepo. Kwa hiyo, nashauri Wizara, basi akimaliza hayo majengo, Serikali iyanunue. Wanafunzi wayatumie kama madarasa na sehemu ya kulala, kuliko ilivyo sasa hivi na wawatafutie eneo lingine.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaingia kwenye sehemu ambayo nataka kuizungumza ya elimu ya Ufundi, pia nataka kuzungumza kuhusu bajeti zinazotolewa kwenye vyuo vyetu hivi.

Mheshimiwa Spika, bajeti kwa kweli safari hii wamejitahidi kwa sababu wameongeza kutoka asilimia 40 mpaka asilimia 85. Lakini pamoja na hivyo kuna Chuo Kikuu cha Mzumbe, nafikiri wao wame-*shoot down,* wamepunguza kama bilioni moja

kutoka bilioni 8.9 mpaka bilioni 7.7, kiasi cha bilioni 1.2. Kwa kweli hii si sahahi kwa sababu wao wameishajiwekea majukumu yao na sijui kwa nini ikawa hivyo.

Namwomba Mheshimiwa Waziri atakaposimama kwenye majumuisho ya hii Wizara atueelezee vizuri, kwa sababu ilikuwa ni vyema akaachia hasa zile bilioni 8.8 zao kama kuna sababu nyingine, kwa sababu lengo hasa ni kuongezea pesa, mimi nahisi bajeti kwenye vyuo vyetu ni ndogo sana ukilinganisha na hali halisi, ndio maana hata elimu inayotolewa kidogo, kama walivyozungumza wenzangu, mtu ana-*graduate,* lakini anakuwa bado hajiamini na soko linakuwa la wasiwasi.

Mheshimiwa Spika, niipongeze pia Serikali kwa kupitia pia Wizara hii kwa kuweza kuruhusu taasisi na mashirika ya dini kuanzisha vyuo binafsi vinavyotoa mafunzo haya ya elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, lakini sina uhakika wa jinsi gani ubora wa elimu katika taasisi hizi inavyopatikana kwa sababu vimeanza karibuni. Lakini ingekuwa ni vizuri pia vikawa vinafuatiliwa, kwa sababu tusije tukawa na watu wenye *degree* nyingi lakini kwa kweli ni kama darasa la 12. Kwa hiyo, ni vizuri pia wawafuatilie kwa karibu, kwa sababu nasikia kuna Chuo kimoja hapo *IMTU,* kiliwahi ku-*cheat* hata wale ma- *lecturers* wake, wakaambiwa wao wana ma-*doctor* wakati watu wamemaliza *Diploma* ya *Medicine*. Kwa kweli watu hawa wanataka kufanya biashara, lakini ni vyema Wizara ikawa karibu nao ili kuhakikisha kwamba wanatoa taaluma inayofaa na ina manufaa kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, suala la majengo kwa wanaoanzisha vyuo hivi vya binafsi, kwa kweli lazima viendane na hadhi, isiwe kama mabanda ya shule tu. Chuo Kikuu unakikuta kina mabanda unafikiri kwenye mnada wa ng'ombe. Sasa haiwezekani. Majengo yaendane na hadhi ya Chuo Kikuu au taasisi husika. Kwa hiyo, iwe ni sera mojawapo kwamba majengo yawe katika *standard* fulani na walimu wanaotakiwa, wawe wenye sifa fulani. Lakini pia kwa sababu sisi kuna vijana wetu wanamaliza Vyuo Vikuu hapa hawana ajira, basi wapewe *priority* kwamba Watanzania wawe ma-*lecturers,* badala ya kuchukua watu kutoka nje kule wanakuja hapa na wengine hatujui hata uhakika wao, wana-*cheat* huko na nini…

Mheshimiwa Spika, inatokea hata mitihani kunakuwa na migogoro. Badala ya kutoa mitihani aliyosomesha, anatoa mfano wa kwenye kitabu, ukimwambia ai-*solve,* inamshinda. Kwa kweli naiomba Wizara iwe *serious* kabisa katika mambo haya. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, pia nina ombi lingine kuhusiana na vijana wale wenye vipaji maalum ambao wengine wamebahatika kuwa na elimu, lakini wengine hawana elimu ambao kwa kweli wanakuwa wanatengeneza mazuri sana lakini wanataka msaada. Kuna vijana wenye vipaji wanatengeneza kwa mfano magobole na bunduki. Badala ya Serikali kuwakamata na kuwasweka ndani, basi kuwe na kijiji au kituo maalum cha kuwawezesha wawe wanatengeneza hizi silaha ili Taifa baadae linaweza likatumia tukawa tunatumia silaha zetu wenyewe na tunaweza tukauza nchi za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hilo Mheshimiwa Waziri atakaporudi wakati ana-*summarize,* namwomba anielimishe kama itakuwa ni wazo sahihi au vipi.

Mheshimiwa Spika, nataka sasa nijikite kwenye elimu ya ufundi ambayo kwa kweli wenzangu hawajaizungumzia sana. Vyuo vyetu vya ufundi kwa kweli vilikuwa vimesahaulika na nahisi havina mtetezi. Kwa muda mrefu tangu vianzishwe kwa kweli ule msimamo, mfumo mzima wa utoaji wa elimu hasa ile mitihani ya mwisho, ina matatizo. Kwa maana hiyo, watu wengi, vijana wengi kwa kweli tumewapoteza na niliwahi kuzungumza wakati wa hotuba ya Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vijana wa *FTC* kwa mfano, wanapojiunga na elimu hiyo, ni wananfunzi ambao wanakuwa na *division one* au *division two*. Lakini wanakuwa wanashindwa kuendelea kulingana na utaratibu mbaya uliopo, kwanza, masharti magumu, lazima a-*pass* masomo yote tena kwa *average B* na mitihani inatungwa na Baraza la Mitihani.

Mheshimiwa Spika, sasa hilo kwa kweli, siyo usahihi na nilisikia tu, lakini nimesoma kwenye bajeti sijaona kwamba labda kuna mabadiliko haya kwamba wanaanzishiwa kozi ya Shahada ya Uhandisi yaani wote wawe na *Diploma in Engineering,* lakini siajaona. Kama ni kweli, naomba Mheshimiwa Waziri aje anielimishe juu ya hilo kama ipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kuzungumzia pia Elimu ya Juu ya Uhandisi inayotoka kwenye vyuo hivi hivi, *DIT* na Mbeya. Utaratibu bado ni ule ule mbovu, kwa kweli utaniwia radhi kama nimekosea lugha. Lakini utaratibu si mzuri kwa sababu ya utahiniwaji wao yaani upewaji wa vyeti, inategemea na ku-*pass* na mtihani wa Taifa. Sasa mtihani wa Taifa ambao uko kwenye Wizara ya Elimu na jana nili-*comment* kwa maandishi, nikawaomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, basi wasilishirikishe Baraza hili katika kutunga mitihani kwa sababu limechangia kwa kiasi kikubwa kupoteza wataalam wetu na hata pato la wakulima, pesa za wakulima zimekuwa zikipotea, unajua kumsomesha mwananfunzi katika fani ya *Engineering* ni pesa nyingi. Lakini matokeo anafeli, hapati cheti na kwa maana hiyo hana uwezo wa kuendelea mbele.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri abadilishe huu utaratibu uliopo sasa hivi na waweze kutahiniwa mitihani yao kulingana na mitaala ya taasisi zao kama ilivyo vyuo vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba wameshaanza Chuo cha Ufundi cha Dar es Salaam *(DIT)* pale na sasa hivi nafikiri wana mitaala, wanachukua *PAC* ya *Engineering*. Watakuwa wanachukua *Bachelor* ya *Engineering*. Sasa naomba hata vijana wa Mbeya wale kwa sababu ni chuo pekee ambacho kinatoa mafunzo haya kwa sasa na chenyewe kitoke kwenye mfumo ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini lingine, naomba kwamba kwa kuwa vyuo vingi vinavyoanzishwa wanakuwa hawaanzishi hii *Fuculty* ya *Engineering* kwa sababu ni ghali sana. Sasa kuna vyuo vyetu hivi, viwe *upgraded*. Kwa mfano *Mbeya Technical* ni chuo ambacho kimekaa vizuri hata majengo. Kwa nini kisiwe *Polytechnical,* hata wa *degree* mpaka *PhD* baadae ya Ufundi kwa sababu ufundi kwa kweli nafikiri ndio msingi wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nikisema hapa kila unachokiangalia mara nyingi ni cha ufundi. Kila utakachofanya ni ufundi kinagusa. Kwa hiyo, tuwatayarishe wenzetu kwa kuongezea vyuo kama hivyo ili wapate nafasi. Ukiangalia sasa hivi tunajiunga kwenye *East Africa Community* na ukiangalia takwimu ya ushiriki wa vijana wetu kwenye vyuo ni ndogo sana hata haijafikia yaani watu 100 kwa mtu 0.27. Kwa kweli uwiano ni mdogo sana. Wenzetu kule Kenya wanakaribia kwa watu 100 kwa wawili. Sasa wakija hapa sijui tutakuwa wapi. Kwa hiyo, tutayarishe vyuo vyetu, tuvi-*upgrade* na tuondoe urasimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimezungumza kuhusu ufundi kwa sababu naona ndiyo kichocheo cha maendeleo katika nchi zilizoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumze kidogo suala la Mfuko wa Mikopo ya Wanafunzi. Kwa kweli wanafunzi na mimi nilipitia mle, mikopo ndio tulianza kupata sisi. Mikopo kwa kweli tunaishukuru Serikali imejitahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sijui, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir kama unaweza kuchangia kwa kifupi kuzitumia dakika 10 hizi.

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, zinanitosha.

**SPIKA:** Sawa sawa! Ahsante sana! *(Makofi)*

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, na mimi nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kwa mchana wa leo ili kuchangia juu hotuba ya bajeti ya Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa. Namshukuru Naibu Waziri na nawashukuru watendaji wake wote kwa hotuba yao hii waliyoitoa. Vile vile naishukuru sana Kamati ya Huduma za Jamii kwa taarifa ambayo wameitoa asubuhi ya leo.

Mheshimiwa Spika, kabla sijapoteza wakati mwingi kama muda hauruhusu, nina machache ambayo nataka kuyazungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la kwanza ambalo nataka kulizungumza ni kuhusu suala la sera ya elimu tuliyonayo nchini hasa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sera ya Elimu ya Juu kwa kweli ukiangalia, Tanzania Bara na Tanzania Visiwani, tuna sera mbili tofauti ambazo zinamlenga mtu mmoja, lakini ni sera tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Zanzibar sera yao kuanzia elimu ya msingi au elimu ya lazima, inaanza darasa la kwanza mpaka *form two* yaani wanaelekea *form four* sasa hivi. Lakini Tanzania Bara sera yao kuanzia darasa la kwanza mpaka la saba. Lakini

tunamlenga mtu yule yule mmoja, wakati huo huo mitaala ambayo wanaitumia katika Elimu ya Juu ni Mitaala ya aina moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tatizo lipo hapa, kuwa mtu unamwandaa katika sera tofauti au mitizamo tofauti, lakini hatima yake ni kuwakutanisha pamoja, kitu ambacho kitakuwa kigumu kwao. Hili ni tatizo ambalo tunaliona kuwa kama hatutabadilisha sera zetu au mitaala yetu, tunaweza tukafikia mahala tuanaachana mbali kama hivi sasa tulivyo katika elimu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ipo haja kuangaliwa upya sera na mitaala ilingane na hiki kitu kimoja tulichonacho katika Jamhuri ya Muungao wa Tanzania. Kama sote tunaingia katika soko moja la Afrika Mashariki au sote tunaingia katikasoko moja la *SADC* au katika nchi tofauti, kwa sababu tukiachana tofauti tofauti, kuna hali ambayo tunaizungumza kila wakati kuwa Zanzibar tuko nyuma kielimu na kama tuko nyuma kielimu, ipo haja kuangaliwa upya mtizamo huu tulionao hivi sasa ili tuhakikishe kuwa tunaboresha elimu kulingana na wakati tulinao hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nataka kuzungumzia ambalo Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, kali-*rush* kidogo kuhusu suala zima la *Science Marine,* Zanzibar. Hili ni suala kwa kweli ni kilio kikubwa kweli. Kimeanza miaka 15 iliyopita na hili kama hatutoliangalia linaweza likaleta tofauti tofauti kuhusu hivi Vyuo vyetu Vikuu vyiliyoko Tanzania Bara na vilivyoko Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kwa nini *Science Marine* inachukua muda mwingi sana kutoa fedha yake ili kuhakikisha kuwa kinaendelezwa na ukilinganisha na vyuo vingine vinapata fedha mara moja ambavyo vikianzishwa. Kwa hiyo, tuliangalie hili suala kuwa lazima hivi sasa Serikali itumie Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, tuhakikishe kuwa inapata mikopo kuendeleza kile Chuo kule Zanzibar, kwa sababu bilioni 6.3 ambayo si rahisi Wizara kupata fedha hizi kwa wakati mmoja. Lakini naamini kuwa hicho kima ambacho watakipata hivi sasa cha fedha ambayo wanaitumia kwenye bajeti shilingi milioni 800, wanaweza wakalipa mkopo kwa hiyo mifuko ambayo inawea ikatoa mkopo kwa ajili ya kujengwa chuo kila ili kuhakikisha kwamba chuo kile kinaimarishwa kule Buyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nataka kuzungumzia ni kuhusu Chuo Cha Mwalimu Nyerere ambacho kiko Kivukoni. Hiki ni Chuo kwa kweli kizuri na mwaka jana tu kimepandishwa daraja kuwa ni chuo ambacho kinaweza kikatoa hata *degree*. Lakini sasa matatizo yaliyopo pale, kwa kweli kile chuo lazima tukiangalie kwa mtizamo wote tulionao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Huduma za Jamii ilipotembelea, iliona uhalisi wa kile chuo kilivyo, ni chuo ambacho kinahitaji ukarabati wa hali ya juu. Kipindi kilichopita chuo kilitengewa shilingi milioni 100 kwa ajili ya ukarabati. Fedha hiyo ilikuwa ni ndogo sana kwa ajili ya ukarabati. Chuo kile kina hali mbaya sana ukilinganisha na hali tuliyo nayo hivi sasa na chuo kile kama hakitofanyiwa ukarabati wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, bahari inaweza ikakikumba chuo kile cha Mwalimu Nyerere pale Kivukoni. Bahari inakula sana ufukwe wa chuo kile, kwa hiyo, lazima tuwe waangalifu au tunaweza tukakikosa kile chuo katika kuhakikisha kuwa tunaendeleza chini yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine katika chuo kile, kimetenga eneo mahsusi Zanzibar Ukanda wa Bububu pale, lakini kwa kweli hakuna nia au hakuna mpango wowote wa kuendeleza viwanja vile. Wamepewa ili kuendeleza *campus* ya chuo cha Kivukoni yaani wawe na chuo kingine kule Zanzibar. Lakini hakuna ishara, hakuna dalili wala hakuna hatua yoyote ambayo Serikali imetenga fungu maalum kuhakikisha kuwa wanajenga chuo kingine pale Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashauri kuwa ipo haja hivi sasa, tuhakikishe kuwa tunaweza kufanya hiyo hali au kuhakikisha kuwa tunaanza ujenzi wa chuo hicho. Lakini hatutoanza ujenzi huo kama hakuna nia madhubuti kwa sababu *Science Marine* imeshaanza, mafundi wako kwenye *site,* lakini bado hawajalipwa. Kwa hiyo, inaonyesha kuwa mwelekeo unakuwa ni mdogo sana.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo natakata kulizungumza, ni kuwa lazima Watanzania tuwe na utamaduni wa kukarabati vyuo vyetu. Tuwe na utamaduni wa kuhakikisha kuwa miundombinu ya vyuo, miundombinu ya sehemu zote tofauti inakarabatiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli ukiviangalia vyuo vina hali mbaya kwa kulinganisha na nchi zingine ambazo unaweza ukatembelea, ukilinganisha na Tanzania tulivyo, vyuo vyetu kwa kweli vina hali mbaya. Kwa hiyo, lazima tuwe na utamaduni wa kuhakikisha kuwa tunakarabati vyuo vyetu na tunatenga fungu maalum ambalo linaweza likahakikisha kuwa kuwa tunafanyia ukarabati vyuo vyetu au miundombinu iliopo katika vyuo, la sivyo kwa kweli hali ni mbaya na inasikitisha kwa wanafunzi ambao wanasoma katika vyuo vyetu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nataka kuzungumzia ni kuhusu hali ya utafiti tulio nao. Fedha ambazo zinatengwa kwa ajili ya utafiti ni ndogo. Ukiangalia, ni ndogo au haipo kabisa au ni ya kutegemea nchi wahisani. Asilimia 95 ya fedha za utafiti wa Tanzania, basi ni wahisani na asilimia tano ndio za ndani. Kwa hiyo, hili ni jambo ambalo kwa kweli linafanya utafiti wetu kuwa wa kubahatisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo lazima tuwe waangalifu sana. Katika elimu ya juu kama hakuna utafiti, hakuna elimu ambayo inaweza ikapatikana ambayo ni ya uhakika. Kwa hiyo, lazima tuhakikishe kwamba elimu itakuwa haina maana kama hakuna utafiti wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kuzungumzia suala lingine la Tume ya Sayansi na Teknolojia. Hii ni Tume ambayo tayari imeundwa na sheria ya Bunge namba 7, ilianzishwa mwaka 1986 na kazi yake kubwa ni kutoa ushauri wa kitaalam na vile vile kutoa mwanga kwa watu ambao ni wabunifu wa mambo ya sayansi.

Mheshimiwa Spika, lakini suala zima ambalo nchi za Kiafrika zimekubaliana, waitenge asilimia moja mpaka asilimia tatu ya bajeti yake ili kuhakikisha kuwa sayansi na teknolojia inakua katika nchi hizo.

Mheshimiwa Spika, lakini ukiangalia katika nchi yetu, suala hilo kwa kweli hatujalifikia wala hatuna lengo la kuhakikisha kuwa tunafikia asilimia hiyo. Lakini je, kuna azma gani ya kuhakikisha kuwa sayansi na teknolojia nchini kwetu inakua?

Kwa hiyo, lazima tuhakikishe kuwa maagizo au maamuzi ambayo kwa kweli tunaamua katika nchi jirani, tunayafikia ili tuhakikishe na sisi tuanapiga hatua katika sayansi na teknolojia. Suala zima ambalo hivi sasa lipo ambalo linashughulikiwa au Tume yetu inalishughulikia kuhakikisha kuwa inafanikisha, imeanzisha mfuko rasmi ambao unaitwa *UMISATE*. Huu ni mfuko ambao kwa kweli umewekwa, lakini je, unamsaidiaje mwananchi wa kawaida? Je, Serikali inachangiaje katika mfuko huu?

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri atueleze kuwa katika mfuko huu, mwananchi wa kawaida anasaidiwaje wale wabunifu, wanasaidiwaje kuhakikisha kuwa sayansi na teknolojia inakua katika nchi yetu?

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache nasema naunga mkono hoja na nasema ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, kwa kweli umetusaidia sana. Hii inatuwezesha kumalizia jioni saa 11.00 na Mbunge wa Kisesa, Mheshimiwa Luhaga Mpina, baada ya hapo nitamwita Naibu Waziri saa 11.15, kwa robo saa. Mtoa hoja ataingia saa 11.30 hadi saa 12.30. Halafu Kamati ya Matumizi kuanzia saa 12.30 jioni hadi kuahirisha Bunge, ambacho ni kipindi cha kutosha kabisa cha saa moja na robo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ningeomba tutambue kwamba kwa muda kama wa saa mbili hivi, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais alikuwa ndiyo Kiongozi wa Shughuli za Bunge humu ndani. Mambo haya lazima kuyataja, kwa sababu si hapa, unaweza baadaye… Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

Matangazo, nawakumbusha Waheshimiwa Wabunge Wajumbe wa Tume ya Huduma kwamba tunakutana leo saa 7.30 mchana kwenye *Board Room* ya Spika. Ni kikao muhimu sana. Tume ya Huduma za Bunge leo saa 7.30 mchana.

Nakumbusha pia Waheshimiwa kwamba kesho asubuhi, kutakuwa na yale mashindano yetu ya mbio kwa rika mbali mbali kuanzia saa 12.00. Sasa mgeni rasmi ni Mheshimiwa Waziri Mkuu, asije akajikuta wakati wa kuwapokea, yuko peke yake. Kwa hiyo, tujitahidi ili tuweze kutimiza hilo. *(Makofi/Kicheko)*

Baada ya hilo, kesho saa 3.00 asubuhi tunayo semina inayoelezea Utekelezaji wa Programu ya Maji Vijijini kwa Tanzania nzima, itakayotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Maji na wataalam wake. Ni semina muhimu sana kama mnavyofahamu suala la maji,

basi tafadhalini sana tuweze kuhudhuria semina hiyo ya maji hapo kesho saa 3.00 asubuhi kwenye ukumbi wetu ule wa zamani wa Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lakini, si hivyo tu, Jumapili saa 5.00 asaubuhi, kutakuwa na semina itakayotolewa na Tume ya Haki za Binadamu ambayo inahusu shughuli, mafanikio na matatizo ya sekta hiyo ya haki za binadamu. Hili nalo ni zito sana, Waheshimiwa Wabunge kila wakati mnazungumzia. Ni vizuri Jumapili saa 5.00 asubuhi kwenye ukumbi huo huo, tukawepo ili kuchangia katika semina hii.

Waheshimiwa Wabunge, nimeelezwa kwamba viongozi wa Tume ya Haki za Binadamu wanapenda sana kupata maoni yetu na tutapata taarifa muhimu hapo zinazohusu haki ya binadamu. Kwa hiyo kesho saa 3.00 asubuhi, Semina ya Programu ya Maji, Utekelezaji wa Maji wa Programu ya Maji Vijijini. Keshokutwa, Jumapili saa 5.00 asubuhi ukumbi huo huo, shughuli, mafanikio na matatizo ya Tume ya Haki za Binadamu. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, muda wa kusitisha shughuli za Bunge umefika, kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 mchana, Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyotangaza wakati wa asubuhi tutakuwa na msemaji mmoja tu sasa wa mwisho kwenye hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia. Baada ya hapo nitamwita Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara hiyo ili aanze kujibu hoja kwa robo saa. Saa 11.30 jioni nitamwita mwenyewe mtoa hoja kwa saa moja ili saa 12.30 jioni tuingie katika kamati. Kwa hiyo, sasa namwita Mbunge wa Kisesa, Mheshimiwa Luhaga Mpina. *(Makofi)*

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, niungane na wenzangu kwa kumshukuru Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia pamoja na watalaam wake katika maandalizi ya bajeti hadi hapa ilipofikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimefahamishwa kwamba kwa mara ya kwanza kabisa, kwamba leo hii tunao marais wa vyuo vyetu vikuu wanne waliohudhuria katika bajeti hii. Nimeambiwa na wazoefu kwamba hii ni mara ya kwanza kwa marais wengi namna hii kuhudhuria katika bajeti hii. Kama ulivyotangaza tunaye Rais wa *DARUSO,* Bwana Magesa Mwita, tunaye Rais wa *CDTI* Tengeru, Bwana Daniel Ole Porukwa na tunaye Kayombyo Majogoro, Rais wa Wanafunzi wa Mzumbe. Hii inaonesha kwamba kasi mpya hii iko mpaka vyuoni sasa. Vijana wanahitaji kujua nini Serikali yao inafanya juu ya elimu.

Mimi nianze kwa kuchangia moja kwa moja katika kipengele cha Bodi ya Mikopo. Bodi ya Mikopo katika vyuo vyetu *meal allowances and accomodation* mpaka sasa hivi ni shilingi 2,500 kama alivyojadili ndugu yangu dada yangu Mheshimiwa Susan

Lyimo, asubuhi kwamba toka mwaka 2001 kiwango hiki ni kile kile cha shilingi 2,500 pamoja na mabadiliko yote ambayo yamekuwa yakijitokeza lakini kiwango kimebaki shilingi 2,500 fedha ambazo haitoshelezi kabisa mahitaji ya vijana wetu wanapokuwa masomoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika *policy* ya bodi kuna mahali wamesema kwamba kiwango ni shilingi 2,500 halafu wakasema *subject to be revised* lakini sasa bado sijasikia sasa kuwa *declared* ni kiasi gani? Kama iko *revised* sasa ni kiasi gani? Labda Waziri atakaposimama kujibu hoja aseme kwamba kama iko *reserved* sasa ni kiwango gani cha vijana wetu watapewa kama *meal allowance and accommodation*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kiwango hiki ni kidogo sana, mfano, vijana walio nje ya vyuo wanalazimika kupanda magari kila siku kusafiri kwenda chuoni ni kama shilingi 800 kila siku mwanafunzi analipa kwa ajili ya usafiri. Sasa ukichukua ile hesabu ya shilingi 2,500 halafu ukatoa shilingi 800 utaona fedha itakayobaki vijana wetu tunayowapa. Tunasema tunawawekea mazingira mazuri kweli kwani hawawezi wakapata hata yale mahitaji yao ya msingi. *(Makofi)*

Kuna suala la *tuition fee, practical training and research* sasa hivi bodi imefikia uamuzi wa kutoa 60%. Kama wenzangu walivyojadili hii 60% hawa watu wameshaingia vyuoni wakiwa na uhakika na bodi hii kwamba ilikuwa ikiwalipia kwa asilimia 100. Vijana wengi wanatoka katika mazingira magumu kwa wazazi wao wasiokuwa na uwezo, wengi tunahangaika nao kule hata kusoma tu sekondari shilingi 20,000 kwa kila mwanafunzi ni kazi kwao. Lakini leo hii sasa mtoto huyu amekuwa *registered* Chuo Kikuu akawa *assured* kwamba atakopeshwa na bodi asilimia 100 lakini *unfortunately* anaambiwa kwamba sasa bwana sisi tunalipa asilimia 60 basi. Kwa hiyo, Wizara inatakiwa iliangalie hili kwa sababu bila kufanya uangalizi wa hali ya juu katika hili na kama *cost sharing* itakuwa ni asilimia 40 ni fedha nyingi watoto wengi wataacha masomo ya Chuo Kikuu. Hawawezi ku-*manage* kulipa asilimia 40 ya vyuo vyetu. Kwa hiyo, nasema kwamba Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia ni lazima waangalie upya, ni lazima wapitie upya unapoamua kusema asilimia 60 unategemea nini kitatokea? Sasa tunasema tunaboresha mazingira ya watoto wetu lakini wakati huo huo tunawafanya wasiwe chuoni kabisa.

Nimepitia sera za bodi za wanafunzi wenye ulemavu, bodi yetu haikuwazingatia vijana wenye ulemavu wanapokuwa Chuo Kikuu. Vijana hawa wenye ulemavu mahitaji yao ni makubwa zaidi kuliko mahitaji ya mtu mwingine. Baiskeli zao wanazotumia, mashine za kuchapa wanaita mashine za kuchapa nundu ni gharama kweli kweli, vitabu vyao ni gharama kweli kweli. Sasa wanaingia mikopo mikubwa mno kuliko mwanafunzi mwingine wa kawaida. Kwa nini wanafunzi wetu hawa tunawahukumu kwa ulemavu walionao? Kweli Serikali yetu inashindwa kutoa *grants* kwa watoto hawa walemavu nako tunasema fedha hatuna! Mimi naomba kwamba lazima Serikali sasa iangalie na Wizara iangalie hili ili vijana wetu wapewe *grants,* wapate hayo mahitaji. Sasa kilema huyo ambaye ni mlemavu namsema leo hii anamaliza masomo anadaiwa shilingi milioni sita au milioni 10 na kitu na mshahara anakwenda kuajiriwa sasa hivi sijui *TGS D* sasa hivi sijui ni 120,000/= ndiyo analipwa sasa akatwe hizo milioni 10 na kitu atazimaliza saa

ngapi? Tunawasaidia kweli? Nasema kwamba Wizara iangalie hilo iwaone vijana wetu kwamba na wao wanahitaji kusaidiwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, umekatiza baina ya Spika na mzungumzaji. Kwa leo nakuacha hivyo hivyo labda utajifunza. *(Kicheko)*

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Halafu kitu kingine ambacho bodi inafanya kuna mambo ambayo yamefanyiwa *research* na wataalam wetu *academically* yakakubalika, lakini kama bodi ya mikopo imekuja kwenye *practical training* Chuo Kikuu cha *UCLAS* huwa ni wiki tisa, *practical training*, *UDSM* wiki 8 na *DTI* wiki 10. Sasa lakini bodi yenyewe inasema kwamba sisi tunatoa mikopo kwa ajili ya *practical training* wiki sita. Kwa hiyo, tayari una-*impair*. Inapunguza *competence* kwa sababu kama watalaam wali-*assess* wakasema kwamba ili uwe *qualified* kuwa *engineer* ni lazima uende *practical training* wiki 8 sasa wewe unampeleka wiki sita tayari *competence* ya utalaam wetu unaishusha. Sasa maamuzi mengine basi yangeheshimu research, yangeheshimu watalaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo sasa ningeomba nichangie upungufu wa vifaa vya kujifunzia mashuleni mfano, *library*. Mimi nimesoma Mzumbe nimeondoka mwaka 2003 lakini hali ya vyuo vyetu tunafurahi tunafikiria kuanzisha vyuo vingine vikuu lakini sasa hii furaha ya kuanzisha Vyuo Vikuu ingeenda sambamba na kuboresha Vyuo Vikuu tulivyonavyo. Kwa sababu kama tutajali tu vijana wana *graduate* lakini wanakuwa hawako *competent* kwenye *market* tunapowapeleka tunashindwa kumuda ushindani. Sasa Chuo Kikuu cha Mzumbe mimi nimekuwa hapo kama nilivyosema na mpaka sasa hivi nimefanya *research* hakuna mabadiliko yoyote, ile *library* ya Chuo Kikuu cha Mzumbe ina uwezo wa kuchukua wanafunzi 200 tu lakini wanafunzi walioko hapo na wanaoitegemea *library* hiyo ni 2,000 sasa fikiria 200 kwa 2000 inakwendaje!, *CDTI Tengeru* Waziri wa Maendeleo ya Jamii ananisikia, *library* yake ina uwezo wa kuchukua wanafunzi 50 lakini waliopo pale ni 1,000. Sasa fikiria 50 kwa 1000 vijana wetu wanayo mazingira magumu sana ya kujifunzia. Kuna upungufu mkubwa sana wa vitabu katika vyuo vyetu vikuu. Kama nilivyosema nimekuwepo mimi Mzumbe pale na mpaka sasa hakuna mabadiliko yoyote kuna kitabu cha *management* kinaitwa *Gupta* ni *copy* mbili tu chuo kizima. Wanafunzi wanaosoma *management* pale ni wanafunzi 600 lakini wanatumia vitabu viwili vya *management*. Kuna vitabu kama *Hongreen* zipo *copy* mbili tu kipindi kile mimi natangazwa kuwa Mbunge, ma-*graduate* wenzangu wakawa wanapiga simu wakawa wananitania kwamba wewe Mpina si tuliyekuwa tunagombania *Hongreen* juzi,juzi. Ukipewa *assigment* inabidi uhakikishe kwamba unaingia *library* saa moja uwe umeshajipanga pale na kuhakikisha kwamba hakuna anayekupita ili uwahi vile vitabu. Ni mazingira mabovu kweli ya wanafunzi ya kujifunzia. Lazima Wizara iangalie, iweke fedha za kutosha mambo mengine tunajilemaza tu unasema huna fedha, huna fedha hata ya kununulia vitabu inawezekana kweli? Haiwezekani, Wizara iseme sasa ni lini inakwenda kununua vitabu katika vyuo vyetu vya kutosha, ni lini inakwenda kupanua maktaba katika vyuo vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *Information Technologies, Computer, Internet cafe*, katika vyuo vyetu vikuu havina *facilities* za mawasiliano za kutosha. Mtu akikaa kwenye

*internet cafe* huwezi kumtoa. Kwa mfano vyuo vingine kuna *internet cafe* hazizidi hata 20 sasa uta-*access* vipi *information?* Ukitoka pale huna uwezo mzuri wa ku-*compete* kwenye *labour market*. Majengo ya vyuo vyetu vikuu yamechakaa sana. Nimesoma kwenye mapendekezo kila *University* inasemaje, lakini kwenye ukarabati wa majengo sijaona kwamba Wizara inasemaje katika majengo mabovu ambayo yameharibika sana katika vyuo vyetu.

Nenda katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, uende bweni namba mbili na namba tano. Lile bweni mpaka limefika mahali linaanguka lenyewe, siku yoyote linaweza likaanguka vijana wetu wakapoteza maisha. Lakini sasa bado tunasema kwamba hatuna fedha. Ukienda Mzumbe bweni la Mirambo limechakaa siku chache litaanguka. Limepata nyufa na wakati wowote litaanguka. Lakini bado tunasema tu kwamba hatuna fedha.

Kuna mambo mengine madogo madogo kwenye vituo vyuo vyetu tumeshindwa kuyaweka sawa kwa mfano suala la afya. Suala la afya kwenye vyuo vyetu bado hatujaliweka sawa. Nenda Chuo Kikuu cha Mzumbe, mganga aliyopo pale ni *clinical officer* anahudumia watu 2,000. Vifaa vilivyopo pale haviwezi kugundua aina ya ugonjwa. Ukienda asubuhi ukapima una malaria, unaambiwa kwamba huna malaria, ukienda jioni unaambiwa kwamba huna malaria. Sasa hata hapa tunasema kwamba hatuna fedha. Mimi niseme kwambaWizara yetu iviangalie vyuo vyetu, ujenzi wa vyuo vikuu vipya uwe sambamba na uboreshaji wa utoaji wa huduma ya elimu katika vyuo vyetu vikuu. Suala la mganga kuwa na *clinical officer* katika Chuo Kikuu wakati *AMO* wana-*graduate* kila siku kwa nini wasiende wakasimamie afya za vijana wetu? *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. IDDI M. AZZAN:** Mheshimiwa Spika, kuhusu Bodi ya Mikopo ambapo hivi sasa wanatoa 60% badala ya 100% kama ilivyokuwa mwanzo, hii itawaumiza sana watoto hasa wale wa walalahoi, Wizara/Serikali haioni umuhimu wa kuweka mpango ambao utawasaidia watoto wa walalahoi angalau wao wapate mkopo kwa 100%.

Mheshimiwa Spika, alama za kuingia Chuo Kikuu ni *Principal 4.* Lakini ili upate mkopo kwa mwanafunzi wa masomo ya *Arts* lazima awe na *Principal 10* na wa Sayansi *Principal 6.* Hii itawafanya wengi washindwe kupata mikopo hiyo na hasa wanafunzi wa kike. Kwa nini mikopo hiyo isitolewe kwa wanafunzi wote hata wale waliopata *Principal 4?*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza niwapongeze watendaji wa Wizara Katibu Mkuu, Naibu Waziri na Waziri kwa bajeti nzuri yenye malengo ya kuleta maendeleo katika Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ukilinganisha na nchi za jirani ina wanafunzi wachache sana kwenye vyuo vikuu ukilinganisha na rika husika. Sasa hivi kuna mipango

mikubwa sana ya kuongeza wanafunzi wanaohitimu elimu ya sekondari, je, Wizara hii imejiandaa namna gani kuwapokea katika vyuo vikuu?

Mheshimiwa Spika, kwa sasa kuna upungufu mkubwa sana wa shule za sekondari na vyuo vya ufundi. Kwa nini sasa baadhi ya shule hizo/vyuo hivyo vinageuzwa kuwa vyuo vikuu/vyuo vikuu vishirikishi? Napendekeza Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia wajenge vyuo vipya badala ya mtindo wa sasa wa kubadilisha shule za sekondari kuwa vyuo.

Mheshimiwa Spika, katika Tanzania, idadi ya wanafunzi wa kike ni asilimia 33.5 ya wanafunzi walio vyuoni. Hii ni asilimia ndogo sana ukizingatia kuwa idadi ya wanawake katika Tanzania ni zaidi ya asilimia 50. Napendekeza mikakati ya kuwawezesha wanawake kujiunga na chuo kikuu iongezwe.

Pia ningependa kuelezwa, je, sasa hivi kuna harakati/mikakati gani ya kuongeza wanafunzi katika vyuo vikuu? Katika sekondari mnatumia njia gani kuwaelewesha juu ya hii mikakati?

Mheshimiwa Spika, mikopo imekuwa kero kwa wanafunzi na Watanzania kwa ujumla, utaratibu una mlolongo mrefu, fomu zinahitaji wanafunzi wajaze vyuo na kiasi wanachoomba wakati vyuo husika havijatangaza wanafunzi waliochaguliwa hasa mwaka huu, kama Serikali imesitisha mikopo kwa wanafunzi wanaosoma katika vyuo binafsi wale walio mwaka wa pili itakuwaje? Wazazi/walezi hawana uwezo je, itabidi wanafunzi wakatishe masomo?

Mheshimiwa Spika, wote tunatambua mchango wa vyuo binafsi. Kwa sasa tuna vyuo binafsi 19 na 11 vya umma. Hawa ni Watanzania, wana haki zote za kupatiwa uwezo, ili waweze kuendelea na masomo. Wizara inatambua wazi kuwa hawana vyuo vya kutosha kuchukua wanafunzi wote waliotimiza sifa/vigezo vya kujiunga. Napendekeza wanafunzi wote walio katika vyuo binafsi na vya umma wapewe Taifa. Wote ni Watanzania, wasibaguliwe.

Mheshimiwa Spika, ni jukumu la Serikali kuipatia Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia pesa za kutosha zitakazotosha wanafunzi katika pande zote mbili.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kuupongeza uongozi wa Wizara hii kwa hotuba nzuri waliyoitoa kuhusu malengo ya Wizara ambayo kwa kweli yanakidhi haja za walengwea, kwa kweli hongera sana.

Hoja yangu ni kuiomba Serikali kuimarisha Ofisi ya Mkoa wa Lindi *(OUT)* katika kupata vitabu vinavyokidhi haja za walengwa. Kumekuwepo na upungufu wa vitabu vya kusoma ili mteja afanye mtihani, lakini hakuna. Mimi binafsi nashindwa kufanya mitihani kwa sababu ya kutokuwa na vitabu vya masomo husika kama *Home Economics.*

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu peke yake ndio utakuwa mkombozi wa elimu kwa wananchi wa Lindi kwani Mkoa wa Lindi, umekosa kuwa na shule hata za sekondari kwa miaka mingi tangu zama za kale na hii imesababishwa na mfumo wa elimu tuliorithi tangu wakati wa ukoloni kwa kutokuwa na shule, Mikoa ya Kusini kwa sababu wakoloni waliwafanya watu wa Kusini kama wafanyakazi wao ni vibarua, manamba wa kukata mikonge kwa kuwachukua na kuwapeleka Tanga na kadhalika katika mashamba yao, hivyo kuifanya mkoa hii isipelekewe elimu wala barabara ili waendelee kukaa gizani na kutokujua mambo na kuwafanya *reserve*" yao ya watu na kilimo.

Katika bajeti hii haikuonyesha kusaidia Lindi (Ukurasa 37) ya kitabu cha hotuba. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuchukua majukumu ya makusudi kabisa kwa hisani yenu ya kusaidia Mkoa wa Lindi kwa kuimarisha Chuo Kikuu Huria kilichopo kwa kuongeza vitabu na zana zote zinazohitajika kwa masomo?

Mheshimiwa Spika, tunaomba mtusaidie sana, hata Chuo Kikuu Huria imekuwa shida Lindi? Mtusaidie tafadhali.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kuipongeza Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia kwa mafanikio yake ya utekelezaji wa malengo ya bajeti ya mwaka uliopita.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia suala la ujenzi wa Chuo Kikuu Dodoma, kwanza naipongeza Serikali kwa uamuzi huo na ni jambo jema lakini wasiwasi wangu ni jinsi gani chuo hiki kitakamilika hadi kufikia kuanza kwa kutoa elimu pale.

Mheshimiwa Spika, Chuo kitakamilika lini? Fedha za kuomba zinaweza kukidhi haja na kutosheleza malengo? Kwa nini Serikali imetenga fedha kidogo katika Wizara hii na hali ikijua Wizara hii ina jukumu kubwa sana ukizingatia kuwa lazima chuo kitakapokamilika lazima kuwe na walimu wenye sifa, je, Wizara imejiandaaje kuhusu walimu watakaofundisha Chuo Kikuu kipya ni walimu wangapi na wa fani zipi?

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali wa kuanzisha Vyuo Vikuu mbalimbali hapa nchini lakini napenda kuishauri Serikali iache mtindo wa kupora majengo ya shule za sekondari au vyuo vya ualimu na kuyafanya vyuo vikuu maana tunapunguza idadi ya waliokuwa wakisomea fani hiyo, pia ni usumbufu kwa wahusika. Hivyo Serikali iweke mikakati mizuri tu ya kuongeza majengo mapya na husika.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iboreshe kiwango cha fungu la fedha katika kitengo cha Tume ya Sayansi na Teknolojia. Ningependa kujua kimetengewa kiasi gani katika mwaka 2006/2007 kwa sababu majukumu yake ni muhimu katika maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa ushauri kuwa Serikali, inatoa kipaumbele katika Chuo Kikuu cha Sayansi Muhimbili na pia Wizara itekeleze ahadi zake kabla ya muda uliowekwa.

Mheshimiwa Spika, Chuo hiki cha Muhimbili kina ujenzi wa chuo kingine cha tiba, Mlonganzila. Je, Serikali inakusudia kusaidiaje ujenzi huo au inategemea fedha za kuomba wapi na kiasi gani? Naomba kuwasilisha na naunga mkono.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa natoa pongezi zangu za dhati kwa hotuba nzuri ya wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia. Ni hotuba inayoonyesha kutaka mabadiliko makubwa katika hili naomba kuchangia yafuatayo:-

(i) Kwenye baadhi ya vyuo hivi havina maendeleo ya kutosha malazi *(hostels)* na hasa kwa wasichana. Wanakosa kabisa hadi wanapanga mbali na vyuo hivyo. Katika kufanya hivyo kusoma kwao kuna kuwa kwa shida sana.

(ii) Kuweko na umuhimu wa kuwafikiria sana walemavu katika kuwatambua watu (wanafunzi) hawa ili kama atashindwa kukidhi masharti ya mkopo, wapokelewe bila vikwazo vyovyote. Hii italeta heshima ya kukitambua kitengo hiko.

(iii) Kuweko na makusudi mazima ya kuwazia chuo kingine Kaskazini cha Serikali kwa maana ya Kanda ya Ziwa. Hii itatoa mgao mzuri wa vyuo hivi nchini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja 100%.

**MHE. PROF. MARK J. MWANDOSYA:** Mheshimiwa Spika, natanguliza pongezi kwa Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia na Mheshimiwa Profesa Peter Msolla na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, sawia kwa hotuba nzuri iliyojaa takwimu na inayotoa dira ya elimu ya juu na Tanzania katika ulimwengu wa Sayansi na Teknolojia. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa Chuo Kikuu kipya Dodoma, ni wazo zuri, uamuzi mzuri, unaozingatia mahitaji makubwa ya wataalam watakaokuwa mstari wa mbele katika kusukuma maendeleo.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa Serikali kutoa majengo ya Chimwaga kuwa kitovu cha Chuo Kikuu hicho ni uamuzi wa busara na wa kimaendeleo. Kwa muda mrefu jengo hilo limekuwa ndovu mweupe *(white elephant)* na lilitumika kwa nadra sana. Kuna wakati ilikuwa kama ndoto. Nimefurahi sana kwamba ndoto hiyo imekuwa kweli.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu leo utahusu Chuo Kikuu (kitarajiwa) cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya. Mara baada kya kustaafu Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, aliwahi kutembelea kilichokuwa Chuo cha Ufundi cha Mbeya *(Mbeya Technical College)*. Alitoa tamko la kihistoria na ambalo haliwezi kusahaulika au kufutwa. Alitoa rai kwa Serikali ikifanye chuo hicho kiwe Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia, rai ya Baba wa Taifa ni nzito. Chama cha Mapinduzi, kama kumbukumbu zangu ni sahihi ikaliweka wazo la Mwalimu katika Ilani ya Uchaguzi ya

CCM kwa uchaguzi uliofuata. Pamoja na hilo, Serikali haikulifanyia kazi wazo hilo na sehemu hiyo ya Ilani. Baadaye ikatoweka katika Ilani zilizofuatwa.

Pamoja na hilo wananchi wa Mbeya chini ya uongozi wa Hayati Amon Nsekela, walianzisha Kamati ya kusukuma utekelezaji wa wazo hilo. Baadaye kukawa na kamati ndogo ambayo ilimhusisha pia aliyekuwa Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Profesa Peter Msolla, ili kuendeleza azma hiyo. Imekuwa bahati nzuri kwamba sasa wazo hilo limepata *champion* ndani ya Serikali na Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, imesisitizwa katika hotuba kwamba vyuo visibadilishwe kuwa vyuo vikuu, kwa ujumla wake hii ni sahihi. Lakini kwa vyuo au Taasisi zinazotoa vyeti vya juu au stashahada za juu au hata shahada, kuviendeleza kuwa vyuo vikuu ni *natural* na ni gharama nafuu kuliko kuanzisha vyuo vipya. Karakana na mashine za mafunzo ya vitendo ni zile zile. Kinachoongezeka ni walimu walio na ujuzi ziada. Aidha, inawezekana katika vyuo vya namna hiyo kutoa vyeti, stashahada, stashahada ya juu, shahada na mafuzo ya uzamili, katika mazingira yanayofanana. Hivyo basi, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya bado kinaweza kuendeleza stadi na fani zilizopo na kuendeleza fani mpya katika ulimwengu unaobadilika sana wa sayansi na teknolojia na mahitaji makubwa ya stadi, fani na elimu hiyo nchini.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Wizara hii ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia na watendaji wote kwa hotuba nzuri. Naomba kueleza mchango wangu katika maeneo yafuatayo:-

(i) Ongezeko la wanafunzi wa elimu ya juu kufuatana na ukubwa wa nchi na idadi ya watu bado Tanzania inapaswa kuongeza jitihada za kuongeza idadi ya wanafunzi katika vyuo vya elimu ya juu. Mpango huu lazima uende sambamba na mpango wa kuandaa wakufunzi katika ngazi mbalimbali kwa viwango vya Kimataifa kukidhi dhamira ya ongezeko la vyuo vikuu na ongezeko la wanafunzi.

Sehemu ya elimu ya sekondari imeonyesha mafanikio ya ongezeko la wanafunzi wanaopasi vizuri kidato cha tano na kwa sifa kuingia vyuo vikuu. Hivyo eneo hili la elimu ya juu lazima liwe tayari kupokea ongezeko hilo vilivyo.

(ii) Usawa, uaminifu na haki katika kuchagua wanafunzi kujiunga na vyuo vikuu.

Mheshimiwa Spika, bado yapo malalamiko ya upendeleo katika zoezi la kuchagua wanafunzi wanaostahili kuendelea na masomo chuo kikuu. Jambo hili ni aibu kwa uongozi wa Wizara husika! Ushahidi unaonekana katika rufaa zinazokatwa na wanafunzi wanaoachwa na pia kuthibitishwa kwa matokeo ya rufaa kuonyesha ukweli wa malalamiko kwa baadhi ya walalamikaji. Bado wenye alama ndogo wanapewa nafasi huku wenye alama kubwa kuachwa makusudi. Kitendo hiki ni sawa na wizi wa mitihani kama ulivyojitokeza Baraza la Mitihani la Taifa. Usimamizi wa uchaguzi/uteuzi uimarishwe na tabia za uonezu ziachwe.

(iii) Utoaji wa fedha za mikopo kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, inaonekana Bodi ya Mikopo haina mwongozo licha ya kulindwa na sheria ya mkikopo kwa wanafunzi *(Higher Education Students Loan)*. Hoja ya kutaka wanafunzi wanaotoka katika vyuo binafsi kupewa mikopo bado ni nzito kwa kuwa wote ni Watanzania wanaohitaji elimu.

Mheshimiwa Spika, fedha za *field* kwa wanafunzi hazitolewi kwa wakati na kwa mpango unaoeleweka ila kwa matokeo ya maandamano ya wanafunzi. Hivi hii ndio sera? Hivi hakuna mwongozo? Kwa nini fedha zisitengwe na kutolewa kwa wakati? Hivi hata wasomi bado hatujui umuhimu wa *Field practice?* Tuheshimu *standards* za elimu kwa manufaa ya watoto wa Tanzania fedha za *field* zitengwe na zitolewe.

(iv) Ongezeko la ujenzi wa vyuo vipya. Upo umuhimu na ulazima wa kujenge vyuo vikuu vipya na hivyo kupongeza kuanzishwa kwa chuo kikuu kipya Dodoma. Wakati wa utekelezaji wake tusiruhusu jukumu hilo jipya kumeza majukumu ya alzima ya ukarabati wa majengo na ununuzi wa vifaa vya utendaji wa vyuo vilivyo sasa. Madarasa, kumbi za mihadhara, mabweni, maabara, maktaba na nyumba za wafanyakazi katika vyuo vingi ni chakavu sana. Vyombo vya mawasiliano na kufundishia ni chakavu na vya teknolojia ya kizamani. Yote haya ni muhimu kuboreshwa sambamba na ujenzi wa vyuo vipya.

(v) Chuo cha Ualimu Chang'ombe kuwa Chuo Kikuu. Eneo la kilichokuwa Chuo cha Ualimu Chang'ombe kilipimwa kwa lengo la kutosheleza mahitaji ya chuo hicho. Hata hivyo ndani ya eneo hilo sehemu kubwa sasa imetumika kujenga Shule ya Msingi na pia Shule ya Sekondari. Je, nini hatma ya Shule hizo mbili ndani ya eneo la kinachotakiwa kuwa Chuo Kikuu bado eneo hilo litakalotosheleza mahitaji muhimu kwa madarasa, mabweni, maabara, maktaba na nyumba za walimu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Spika, mikopo ya masomo ya juu ikitolewa vizuri ikasaidia sana katika kuendeleza vizazi vyetu katika kupata elimu. Kwanza kuwapa mikopo wanafunzi na halafu kuwakatisha mitihani ya masomo ni kitendo cha hatari na ni cha kuvunja moyo.

Mheshimiwa Spika, ninachoshauri inapotolewa mikopo basi ihakikishwe wakati wote wa masomo mikopo hiyo itolewe, haicheleweshwi, mwanafunzi akopeshwe mwaka wa kwanza au kipindi cha kwanza atakapokopeshwa mkopo huo.

Mheshimiwa Spika, kuna ongezeko kubwa la vyuo vikuu nchini, hili ni jambo zuri lakini lisijekuwa ongezeko hili likawa sasa sawa na ongezeko la shule za sekondari. Je, vyuo vikuu hivi vina wahadhiri wanaostahili na majengo yanayolingana na hadhi ya vyuo vikuu? Vinginevyo kutakuwa na vyuo vikuu ambavyo havilingani na havitatolewa elimu inayolingana.

Mheshimiwa Spika, ili elimu isomeshwe kwenye vyuo vikuu, ipo haja wahadhiri na watendaji wengine katika vyuo hivyo wapewe maslahi yanayostahili vinginevyo wataalamu wetu wanaweza kuihama nchi na kufuata maslahi mengine nchi nyingine.

**MHE. DR. RAPHAEL M CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja hii kwa kusisitiza yafuatayo:-

(i) Wizara sasa iweke kauli mbiu ya kuwekeza katika rasilimali watu katika ulimwengu huu wa Sayansi na Teknolojia.

(ii) Mitaala ya masomo ilenge zaidi mahitaji ya soko lililopo kwa sasa ili kuwawezesha wahitimu kushiriki kikamilifu katika soko hili lililojaa ushindani na waweze kujiajiri zaidi badala ya kutegemea ajira.

(iii) Mikopo ya wanafunzi ilenge zaidi kwa vijana wenye uwezo wa kiakili zaidi *(brainy people)* badala ya ku-*consider* tu kila mwombaji. Ni vema wale wote wanaofaulu daraja la kwanza na hawana uwezo ndiyo wapewe nafasi ya mikopo kisha wengine wafuate. Hii itasaidia vijana wenye uwezo zaidi wapate fursa.

(iv) Kuanzishwe mkakati wa kuanzisha vyuo vikuu kwa muda maalumu ili isaidie vijana kupata elimu kwa uweiano. Pia mashirika binafsi na hasa yale ya dini yapatiwe misaada ya kuboresha vyuo vyake ili viweze kupanuka na kutoa elimu bora zaidi.

(v) Kuanzisha *research competition award of year.* Hii itasaidia na kuchochea ushindani kati ya wasomi hapa nchini kuibua na kuendeleza vipaji ikiwa ni pamoja na taaluma zao.

(vi) Kuboresha maslahi ya wahadhiri ikiwa ni pamoja na mfumo mzima wa penshini zao. Hii itasaidia sana kuwa *retair* na kuwawezesha kufanya kazi kwa ari na ubora zaidi.

(vii) Kuhusu *TEA,* izidi kutoa elimu kwa wadau wake kuhusu umuhimu wa kuchangia mfuko wa elimu.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa hatua zake za makusudi kuanzisha vyuo vikuu zaidi nchini hususan cha Mkwawa, Chang'ombe na Dodoma. Sisi wa Kanda ya Kati tumefarijika sana kwa uanzishwaji wa Chuo Kikuu cha Dodoma, ni ukombozi mkubwa sana kielimu.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mhesimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hatua yake ya kumteua Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, kuiongoza Wizara hii akisaidiwa na Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, ni watu makini wanaoweza kutusaidia kuipeleka mbele Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, wananchi wengi wanatambua michango yao katika Sekta ya Elimu nchini kwa miaka mingi hata kabla ya uteuzi wao.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, naendeleza, majadiliano ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, muda uliisha. Nina maoni mawili kuhusu ufuatiliaji wa madeni ya mikopo ya shilingi bilioni 62.5 ya wanafunzi 42,729 haya madeni yalipwe ili wapate na wengine, naomba nijue kati ya shilingi bilioni 62.5 ni wangapi wamerejesha na wangapi bado na hatua gani zimeandaliwa kuwapata wanafunzi hao na ukizingatia ajira hakuna watarudishaje?

Mheshimiwa Spika, ili twende sambamba na uelewa wa wazazi, watoe elimu itolewe kwa wazazi ni vigezo gani vya kuwawezesha wanafunzi wapewe mikopo, kwa wazazi ambao wako Mikoani hususan vijijini hawajui kitu.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana naye awe na mikakati endelevu baada ya wataalam kufuzu vyuo vikuu, wawasaidie kupata ajira, kwa hao wawekezaji wanaokuja Tanzania. Kwa kuwa ni Serikali, moja ombi langu lipokelewe.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri kwa kusimamia mradi mzuri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, hiki ni kitega uchumi kizuri kwa chuo, kwa sababu ndio mradi pekee utakaowezesha, kuendeleza upanuzi wa mabweni na madarasa nafikiri ndio lengo kuu, naomba fedha zikipatikana zipelekwe katika upanuzi wa mabweni hasa watoto wa kike.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono asilimia mia moja na apewe fedha zote na mwaka 2007/2008 bajeti iongezwe ili wanafunzi wawezeshwe katika elimu.

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wakati sasa umefika wa kufanya maamuzi ya kutumia lugha ya Kiswahili katika kutoa elimu ya juu kwa maana ya kiwango cha chuo kikuu. Kusema kuwa lazima tutumie kiingereza eti ndiyo lugha ya elimu, huku kunarudisha nyuma maendeleo ya elimu katika nchi yetu. Elimu inayotolewa kwa kutumia kiingereza ni elimu isiyokamilika kwa kiingereza sababu wanafunzi wa Tanzania ni wazungumzaji wa Kiswahili katika muda wote wa maisha.

Mheshimiwa Spika, lugha ni msamiati na kuzungumza mara kwa mara inabainika sasa hata wale waliomaliza chuo kikuu wanakuwa hawakijui kiingereza. Ni Bara la Afrika tu ambalo linatumia lugha ya kigeni katika elimu, matokeo yake tunachelewa katika maendeleo.Wenzetu wa Bara la Asia wanatumia lugha zao katika elimu. Matokeo yake sasa wanapiga hatua katika maendeleo. Wachina wanatumia Kichina chao, Malasyia chao, Thailand wanatumia Kithailand chao na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, haitatokea hata siku moja Wafaransa wakatumia kiingereza eti ni lugha ya elimu. Sisi tunatumia kiingereza kwa sababu tulitawaliwa na Waingereza.

Mtu wa kwanza wa kuzunguka dunia angani alikuwa Mrusi kwa jina Ywn Gaganini, huyu hata neno moja la kiingereza hakulijua.

Mheshimiwa Spika, wanafalsafa wote waliozungumzia elimu hawakueleza tutumie lugha gani katika elimu. Wao walielezea maana ya elimu tu kwa mfano, Plato, mwanafalsafa wa Kigiriki, aliielezea elimu kama ifuatavyo, *Education is a matter of conversion a complete turning around from the world of appearance to the world of reality.* Hapa wala hakuelezea lugha ya kutumia, bali ameelezea maana ya elimu tu.

Mheshimiwa Spika, Waingereza wenyewe katika karne za nyuma walitawaliwa na Warumi lakini wala hawakubaki na lugha ya kirumi katika elimu. Somo la aljebra asili yake ni Uarabuni, lakini wazungu hawakuchukua ni fomu tu. Ni sisi Waafrika peke yetu tunaodhani kuwa kutumia lugha ya kigeni ndio usomi. Tunachelewa katika kujiletea maendeleo. Wakati sasa umefika wa nchi yetu kuamua kutumia lugha ya Kiswahili kutoka shule ya awali mpaka Chuo Kikuu.Tujifunze kiingereza kama lugha ya kigeni tu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ili tuendelee ni lazima tupate teknolojia ya kisasa. Kwa vile hatuna, tunapaswa kuifuata popote pale inapopatikana. Hivyo inabidi tuandae mikakati ya kupeleka wanafunzi wetu katika vyuo vya nje ili wapate hiyo teknolojia tunayohitaji.

Mheshimiwa Spika,kuhusu *scholarship,* hivi sasa kuna usiri mkubwa kuhusu *scholarships.* Kwanza hazitangazwi na pia usaili wa wale wanaoomba haueleweki. Naomba Wizara inieleze kuhusu utaratibu wa kupata *scholarships.* Vile vile Wizara ieleze wazi ni vipi inapata hizi *scholarships.*

Kuhusu mikopo, kwanza pesa inayotolewa haitoshi na pia kuna mizengwe mingi ya kuipata. Hii ni haki ya kila mwanafunzi, hivyo utafutwe utaratibu unaofaa ili kila mhitaji afikie mikopo hii bila kipingamizi chochote.

Pili, mikopo hii ipatikane muda wote wa mwaka kwani vyuo ama mitaala inatofautiana kuanza kwa mwaka. Naomba Wizara itoe maelezo kuhusu suala hili.

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Spika, katika miaka ya hivi karibuni mazingira ya Chuo Kikuu cha Dara es Salaam yameboreshwa kwa viwango vya kuridhisha, barabara na majengo yamekarabatiwa na hosteli za wanafunzi za Mabibo na Ubungo zimepunguza matatizo ya malazi ya wanafunzi. Naipongeza sana Serikali kwa hatua zilizochukuliwa.

Mheshimiwa Spika, wanafunzi bado wanakabiliwa na matatizo mengi, suala la mikopo ya wanafunzi bado ni kero kubwa ambayo inawapotezea wanafunzi muda wa masomo. Wakati umefika suala hili kupatiwa ufafanuzi na utaratibu utakaoondoa ucheleweshaji na aina nyingine za usumbufu.

Mheshimiwa Spika, vyuo vinakabiliwa na matatizo ya malazi kwa wanafunzi. Tunapongeza utaratibu uliotumiwa na *NSSF* kujenga hosteli ya Mabibo. Mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii na hata watu binafsi, ihimizwe kujenga hosteli nyingi kwenye maeneo ya vyuo ili kupunguza tatizo hili kwa utaratibu utakaokubaliwa kati ya mwekezaji na vyuo au Serikali.

Suala lingine linahusu maslahi ya wakufunzi na watumishi wengine wa vyuo. Inaelekea kwamba Serikali imeshughulikia sehemu ya tatizo hili, hasa kwa wakufunzi. Suala hili lisiposhughulikiwa mapema, tutazidi kupoteza wasomi wetu ambao watatoka nje ya nchi kutafuta maslahi mazuri zaidi.Watumishi ambao sio wakufunzi wanalalamika kwamba wamesahauliwa katika uboreshaji wa maslahi ya wafanyakazi wa vyuo. Kwa kuwa huduma zao ni muhimu kwa vyuo, maslahi yao yatazamwe pia ili kuwaongezea ari ya kazi na kuboresha maisha yao.

Suala langu la mwisho ni umuhimu wa kuongeza idadi ya wanafunzi wanaojiunga na vyuo vikuu. Nchi yetu iko nyuma sana katika elimu ya juu. Inatubidi tupanue vyuo vikuu vilivyopo ili kuviwezesha kuchukua wanafunzi wengi zaidi. Hivi sasa huduma zilizopo hazikidhi hata ile idadi ndogo ya wanafunzi iliyopo. Maendeleo ya kufindishia hayatoshi, vifaa vya kufundishia havitoshi, malazi kwa wakufunzi na wanafunzi hayatoshi. Inabidi tuondoe mapungufu yaliyopo na kujenga miundombinu itakayowezesha vyuo kuchukua wanafunzi wengi zaidi. Tunapongeza hatua zinazochukuliwa za kujenga Chuo Kikuu cha Daodoma ambacho kitakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi wengi kuliko vile vilivyopo. Ifikapo mwaka 2009, asilimia 50 ya watoto watakaomaliza kidato cha sita watatakiwa kujiunga na Vyuo Vikuu. Inabidi tuhakikishe kujenga miundombinu itakaotuwezesha kuhudumia idadi hiyo kubwa ya wanafunzi. Tuwekeze katika rasilimali watu kwa kasi mpya. Naunga mkono hoja.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia kwa maandishi katika hotuba ya Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii ya Elimu ya Juu, Sayansi na teknolojia, kwa kuandaa hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuchangia kuhusu vitabu vya wanafunzi. Ukuzingatia dunia ya sasa ni ya teknolojia, utandawazi na lazima Serikali iangalie ni jinsi gani kusambaza vitabu vinavyoendana na wakati kwa mfano, nilikuta wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi wanasema kitabu kilichotolewa *Forth Edition.* Sasa hawa wanafunzi wanaweza kuwa *competent* kweli?

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika Moshi, kwa kweli chuo hiki kipo katika hali mbaya kuhusu madarasa ya kufundishia.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Ushirika kinatumia ule ukumbi wa sherehe kufundishia. Najiuliza wanafunzi 200 na *lecturer* mmoja mbele ya darasa wanaweza kweli kusikiliza na kumuelewa? Naomba Serikali itueleze ni lini watashughulikia kuhusu madarasa (kujenga) ya wanafunzi wachache katika chuo hicho?

Mheshimiwa Spika, pale ushirika hakuna *tutorial class* na vyuoni *discussion* ni za muhimu sana. Hivyo madarasa ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Tumaini University (KCMC)* wanafunzi hata kwenye vyombo vya habari vinasema utawala wa *KCMC* haitawaruhusu wanafunzi hao kufanya mitihani mpaka walipe *fees.* Wanafunzi hawa walipewa mkopo kwa *first/second term,* nini kiwazuie wanafunzi hawa wasipewe mikopo hiyo ili waweze kufanya mitihani yao?

Mheshimiwa Spika, ukizingatia hospitali nyingi zina uhaba wa madaktari na wanafunzi wengine wanamalizia ili waende *practical* ili waweze kuwa madaktari kamili kama wakicheleweshwa hii si itazidi kutuletea matatizo?

Naomba Serikali iingilie katika hapa matatizo ya *KCMC at least* itoe tamko au ku-*guarantee* hawa wanafunzi waweze kufanya mitihani yao.

Mheshimiwa Spika, naoimba Wizara, wanafunzi wa kike wanaopasi vizuri masomo ya sayansi *(PCB)* wapewe kipaumbele kuingia Chuo Kikuu kwa ajili ya kusomea udaktari. Ushahidi wa msichana mmoja aliyemaliza kidato cha sita amepata *division two* lakini wazazi hawana uwezo wa kumlipia *fees* na huyu msichana ni *bright* lakini yupo tu nyumbani hajaweza kwenda chuo na hakupata *selection,* sijui Serikali inatumia kigezo gani kufadhili wanafunzi. Naomba majibu kutoka kwa Waziri.

Mwisho kabisa naomba Serikali iongeze vyuo vingi vikuu pamoja na *lecturers* wa kutosha. Sio majengo/walimu tu pia vifaa kama kompyuta, maabara, vitabu kwa sababu tukiwa na vyuo vinavyoenda na wakati Serikali haitakuwa na gharama kubwa ya kupeleka wanafunzi kwenda kusoma nje ya nchi. Fedha hizi za kuwapeleka nje zinaweza kutumika kuboresha vyuo hapa nchini.

Vile vile Serikali iimarishe vyuo ambayo vipo mfano, Vyuo Vikuu Vishiriki, Chuo Kikuu Dar es Salaam ili vyuo hivi viweze kukidhi ubora wa teknolojia ya sasa hivi na Serikali ihakikishe inapata wahadhiri wa kutosha kwa vyuo vyote pamoja na vyuo vya ufundi.

Mheshimiwa Spika, wanafunzi wakipata elimu bora wanaweza kuwa washindani katika dunia ya utandawazi, ili waweze kujiajiri wenyewe na hatimaye kuondoa umaskini kama Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, alivyosoma kwenye hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo mheshimiwa spika naomba kuwasilisha.

**MHE. JANET B. KAHAMA:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuwapongeza Waziri na Naibu Waziri wa Wizara hii, kwa kazi nzuri wanazozifanya za kasi, ari na nguvu mpya!

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia eneo hili Tanzania halijatiliwa maanani kabisa kwa sababu bajeti ndogo kutengwa, teknolojia endelevu inatumika katika kilimo, kuhifadhi na kulinda mazingira, afya, mionzi, nishati na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia MKUKUTA hatuwezi kufanikiwa bila kushirikisha teknolojia ya miundo yote, uzalishaji - masoko na utunzaji - ugani. Vyote hivi vinategemea teknolojia endelevu.

Mheshimiwa Spika, tunao Watanzania wengi ndani na nje ya nchi waliopata utaalam katika fani hii. Teknolojia ya kemikali katika matumizi ya dawa, mashambani, hospitalini na majumbani.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu kuielewa, vinginevyo madhara hutokea kwa binadamu, mifugo na mazingira.

Mheshimiwa Spika, teknolojia katika matumizi ya mionzi ya jua *(solar energy)* ina umuhimu katika maeneo mengi yasiyo na umeme. Pia teknolojia ya matumizi ya mionzi katika *microwave,* simu za mikononi - bado zina wasiwasi, eneo hili bado linafanyiwa *research,* Bunge lililopita, majibu ya mionzi - *radius* kadhaa. Kiwango cha madhara ni kidogo sana na wataalam wetu watumieni wapo wengi.

Mheshimiwa Spika, teknolojia ni muhimu sana katika kudhibiti uchafuzi wa mazingira kama vyura vya Kihansi vilivyopungua. Kuhusu nishati nchi inakuwa jangwa kwa ukataji miti kwa ajili ya mkaa mpaka hapo, nishati mbadala ya mkaa itasaidia kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Spika, *Briqeetees* ni nishati mbadala, mkaa ipo Tanga tayari, je, ni sababu zipi bado hazijaenea Mji wa Dar es Salaam na mikoa yote? Lini Serikali itahamasisha miti, matawi yanayokatwa, yanakusanywa na makapi kuchomwa moto katika matanuri mepesi ili kupata mchanganyiko, kuna umuhimu wa kuwa na *think tank* itakayoandaa mikakati ya kunusuru jamii ya Watanzania, tumieni wataalamu!

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo, maswala ya *organic farming, genetically modified products* na *tissue culture* yote yanahitaji wataalam.

Mheshimiwa Spika, Vyuo vyote vya elimu ya juu bado vimeachwa nyuma ambapo ni tegemeo kubwa kwa vijana wetu. Chuo cha Ushirika Moshi kinadahili wanafunzi 1,500 kimepanga kujenga *hostel, theatre and lecture rooms.*

Mheshimiwa Spika, fedha walizogawiwa ni shilingi bilioni 200 tu na wao waliomba shilingi bilioni saba. Hivyo itabidi wachukue wanafunzi 500 tu, ni wachache sana na shilingi milioni 200 zitakarabati mabweni tu.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa uamuzi wa kuanzisha Chuo Kikuu kipya Dodoma. Naomba matayarisho yote yakamilike haraka ili kiweze kuanza mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia kwa asilimia mia moja.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, kwa kazi kubwa nzuri.

Mheshimiwa Spika, kufuatana na ukuzi wa teknolojia na utandawazi, uingizaji wa wanafunzi vyuo vikuu bado upo chini ya kiwango cha kasi inayotegemewa. Nashauri na ombi langu ni kuhakikisha shule zote za zamani mfano *Tabora Schools* ziwe vyuo vikuu.

Mheshimiwa Spik,a kulikuwa na mapendekezo ya kufanya kitivo cha *Mining Engineering,* Mgodi wa Dhahabu *Resolute* - Nzega watakapomaliza kwa kuwa katika kitabu cha maendeleo hakuna fedha zozote zilizotengwa. Je, mpango gani umewekwa?

Mheshimiwa Spika, Serikali iliunda kamati kwa ajili ya kuangalia maboresho ya watumishi (wanataaluma na waendeshaji) wa vyuo vikuu. Lakini baada ya kamati kumaliza na kuwasilisha mapendekezo ya marupurupu Serikalini kwa mshangao imeboreshwa 50% ya mapendekezo ya kamati na kuwaacha watumishi waendeshaji bila nyongeza kama walivyorekebisha kwa wanataaluma?

Mheshimiwa Spika, hili litaleta mtafaruku na ubaguzi. Inaweza hata kuleta migomo jambo ambalo siyo zuri. Naomba hili Wizara iingilie kati kupeleka ombi maalum Hazina na Utumishi ili walipwe kama wenzao.

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwanza ni kuhusu Elimu ya Juu, licha ya ujenzi wa Chuo Kikuu kipya cha Dodoma na kwa kuzingatia idadi ndogo ya vijana wanaojiunga vyuo vikuu nchini (0.27%) pamoja na kuwepo wengi wenye sifa lakini hawapati nafasi, nashauri yafuatayo:-

(i) Mheshimiwa Spika, ndani ya kipindi cha mwaka 2006 hadi 2010 mchakato wa kuanzisha Chuo Kikuu kingine cha Taifa uanze. Chuo Kikuu hiki kijengwe Ukanda wa Ziwa hususan Shinyanga Mjini. Eneo hili lina idadi kubwa ya vijana wanaomaliza shule

za msingi na hivi karibuni litakuwa na vijana wengi sana wanaomaliza shule za sekondari na hivyo kuhitaji elimu ya juu.

(ii) Wizara ianzishe taratibu kama za nchi za mashariki ya mbali kwa kutafuta ufadhili *(scholarships)* na makusudi kwa vijana wengi zaidi kwenda kusoma nje ya nchi hasa katika nchi zilizoendelea ili kujenga na kuimarisha hazina ya rasilimali watu, kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, mgawanyo wa fedha kwa vyuo vya elimu ya juu, wote tunajua kwamba elimu ni mhimili muhimu sana katika suala zima la maendeleo na hususan elimu ya juu ambayo ndiyo huwaandaa wanafunzi kuchukua majukumu ya uongozi wa Taifa na wataalamu wa elimu wanasema kwamba *if you think education is expensinve try ignorance,* tafsiri yake ni kwamba kama unafikiri elimu ni ghali basi jaribu ujinga. Nina hakika Watanzania hatuko tayari kujaribu ujinga, kama hivyo ndivyo basi lazima tuwekeze kwenye elimu.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Mzumbe kimepewa fedha kidogo sana ukilinganisha na bajeti ya mwaka jana. Pia Chuo cha Teknolojia cha Dar es Salaam *(DIT)* nacho kimepewa pesa kidogo sana pungufu ya zile za mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kuona kwamba bajeti ya Chuo Kikuu Mzumbe imepunguzwa kwa kiwango cha asilimia 13. Mwaka 2005/2006 chuo kilipewa shilingi 8,880,101,900/= mwaka 2006/2007 chuo kimetengewa shilingi 7,729,694,000/= ikiwa ni pungufu ya shilingi 1,150,407,900/= (13%) wakati *DIT* imepunguziwa kiasi cha shilingi 516,007,600/=.

Mheshimiwa Spika, si kawaida kwa bajeti ya mwaka wa mbele 2006/2007 kuwa ndogo kuliko ya mwaka wa nyuma 2005/2006, inashangaza sana! Kwa vyovyote vile hatua hii ya Wizara itasababisha kukwama kwa baadhi ya shughuli za vyuo husika hasa zile za kimasomo katika hali kama hii ni kweli tumenuia kukuza elimu ya juu. Naomba pia kujua sera ya elimu juu inasema ni nini juu ya utaratibu wa bajeti kwa vyuo vya elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, kama kulikuwa na sababu za muhimu za kupunguza bajeti ya vyuo hivyo, lakini kulikuwa na sababu gani za kuviongezea vyuo vingine fedha kwa kiasi cha kati ya asilimia 40 hadi 55 wakati huo huo ukipunguza ile ya Chuo Kikuu cha Mzumbe kwa asilimia 13. Kwa nini basi vyuo hivyo visingeachiwa fedha kama zilivyokuwa kwenye bajeti ya mwaka 2005/2006?

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba mimi sijaridhika na hatua ya Wizara ya kuvipunguzia vyuo hivyo bajeti na kwa msingi huo sitaunga mkono bajeti ya Wizara hii hadi Serikali itoe majibu ya kuridhisha ambayo yataonyesha ni namna gani shughuli za vyuo hazitaathirika kwa kuvipunguzia bajeti. Lakini wakati huo huo Serikali ieleze itaziba pengo hilo namna gani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upanuzi wa Chuo cha Ufundi Mbeya, naomba kujua mipango ya Serikali ya kukifanya Chuo cha Ufundi Mbeya kuwa Chuo Kikuu. Kuna dhana kwamba vyuo vya sasa visibadilishwe kwa madhumini mengine. Mimi sikubaliani na dhana hiyo kwa sababu vyuo kama Ardhi, Chang'ombe, Mkwawa na kadhalika vimebadilishwa na kuwa sehemu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa adhima ya kuimarisha elimu katika nchi. Chuo cha Ufundi Mbeya kama kikipandishwa hadhi na kuwa Chuo Kikuu basi kitaongeza wataalam wengi zaidi hasa katika nyanja ya sayansi, uhandisi na ufundi wa aina mbalimbali. Lakini pia kuanzishwa kwa Chuo Kikuu hicho kutapunguza ukosefu wa nafasi za kujiunga vyuoni kwa Watanzania wengi zaidi, pia kutaongeza ajira zaidi kwa wananchi wengi zaidi hususan wale wa mkoa wa Mbeya na mikoa ya jirani. Naomba maelezo ya kutosha kuhusu hoja hii.

Kuhusu ufujaji na wizi wa mitihani, bado kuna ufujaji na wizi wa mitihani katika vyuo vya elimu ya juu, hapa napenda kutoa ushauri mdogo, Wizara ichukue mkakati wa kutosha katika kudhibiti hali hiyo, vinginevyo tutakuwa hatuwatayarishi wanafunzi kukabiliana na changamoto za dunia.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hayo naomba tena niseme kwamba mimi sitaunga mkono bajeti hii hadi hapo Waziri atakapotoa maelezo ya kutosha hasa *item one* hapo juu.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na kuweza kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwako na Naibu Spika kwa kazi zenu nzuri za kuliongoza Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri na Naibu wake pamoja na watendaji wao wakiongozwa na Katibu Mkuu kwa kutayarisha na kuwasilisha bajeti yao katika Bunge hili vizuri.

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Juu ni sekta nyeti na muhimu sana kwa Taifa lolote ikiwemo Tanzania. Katika kipindi cha miaka 45 ya Uhuru, idadi ya wanafunzi wa elimu ya juu ni ndogo sana (0.27%) kwa Watanzania wote. Majirani zetu wana viwango vizuri zaidi ya wanafunzi katika elimu ya juu ukilinganisha na sisi katika nchi yetu. Mazingira mabaya ya vyuo vyetu yanachangia kuwa na idadi ndogo, wanafunzi ambao wanakosa sifa, ujuzi na utaalamu unaofaa kwa hao wachache wanaomaliza elimu ya juu. Naiomba Serikali iliangalie suala la elimu ya juu kwa makini sana.

Mheshimiwa Spika, mgao wa wanafunzi katika elimu ya juu ni vyema ukaangaliwa tena ili wanafunzi kutoka Zanzibar nao waweze kunufaika zaidi kuliko ilivyo hivi sasa yakiendelea hivi hivi yatawafanya wanafunzi ambao wana uwezo kutoka Zanzibar wakose nafasi. Mitaala inayotumika Bara na Zanzibar ilingane kwa vile mitihani katika Vyuo Vikuu ni ya Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, posho au mikopo inayotolewa kwa wanafunzi wa vyuo vikuu ni vyema vikaangaliwa vizuri ili kuondoa matatizo yaliyopo yanayosababisha wanafunzi hao kufanya. Maandamano au migomo isiyokuwa ya lazima. Pia naomba mikopo au posho zitolewe kwa wakati ili isiwe ni kero kwa wanafunzi hao kwani wengi wao ni masikini na hawana uwezo wa kujikimu.

Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa vyuo vikuu vipya vitaongeza idadi ya wanafunzi kuingia katika vyuo hivyo. Ni vyema mazingira ya kazi kwa wahadhiri na wanafunzi kuboreshwa ili lengo la kuongezeka kwa vyuo hivyo liweze kufikiwa.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri yenye ufafanuzi mzuri kuhusu Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia.

Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na tatu napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

Kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Dodoma ikiwemo Wilaya ya Mpwapwa tunampongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na Serikali yake kwa uamuizi wake wa busara wa kujenga Chuo Kikuu kipya hapa Dodoma. Pamoja na kwamba Chuo Kikuu hicho kitaongeza idadi ya wanafunzi pia kitaongeza idadi ya wasomi katika nchi yetu. Nchi yetu ina idadi ndogo sana ya wanafunzi katika vyuo vikuu vilivyopo. Je, ujenzi huo wa Chuo Kikuu kipya cha Dodoma utaanza lini? Je, Chuo Kikuu hicho kitafundisha vitivo gani?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa jengo la Chimwaga limetolewa na Serikali ili Chuo Kikuu kipya cha Dodoma kianze mara moja, je, *intake* ya kwanza ya wanafunzi itaanza lini na kitachukua wanafunzi wangapi?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa baadhi ya wanafunzi hugoma katika kudai haki au maslahi yao. Sasa naomba maelezo. Je, nini hasa chanzo cha migomo hiyo na Serikali imejiandaa vipi kuhakikisha kwamba migomo hiyo haitokei mara kwa mara kwa kuwalipa wanafunzi stahili zao mapema? Je, kwa kuwa Serikali inatoa mikopo ya masomo kwa vyuo vikuu vya umma, je, vyuo vikuu vya binafsi ukoje? Je, Serikali ina mpango gani wa kuchukua wasichana wengi zaidi kujiunga na vyuo vikuu vilivyopo kuliko hali ilivyo sasa ni wachache sana na wengi wasomo ya *Arts.*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Peter Msolla, Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia kwa hotuba yenye matumaini kwa Watanzania. Aidha, nawatakia uzima, furaha na utendaji bora wa milele Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nina maoni na mapendekezo yafuatayo:-

Kwanza, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 fungu 62 (a) katika ukurasa wa 77 umetamka wazi juu ya kuboresha elimu ya juu nchini na adhma ya kukifanya Chuo cha Ualimu Mtwara kuwa Chuo Kikuu Kiambata. Katika bajeti hii sioni mahali popote palipoelezea wala kutenga fedha kwa ajili ya uanzishaji wa Chuo hicho.

Pili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kilipoanzishwa kililengwa kwa watumishi ambao hawakupata nafasi ya kuwa na shahada. Lakini katika hali ya sasa vijana wenye umri mdogo wamekuwa wanajiunga na Chuo hiki na kumaliza kwa muda wa miaka minne sawa na *Conventional University*. Wanafunzi wanaohitimu wameonekana kukidhi mahitaji ya soko, ombi langu kwa Serikali ni kuwa waongeze bajeti kwa chuo hiki kutoa nafasi ya 14 na mwanya wa Watanzania wengi kupata elimu ya Chuo Kikuu kwani kwa vile Chuo hiki hakihitaji *lecture rooms* wa mabweni ni rahisi kutoa Watanzania wengi. Aidha, viongozi wa juu wa nchi kama vile Rais na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania watembelee Makao Mkuu ya Chuo na vituo vya Mikoani vya Chuo hiki wanapata nafasi. Hii itahamasisha Watanzania wengi kukiona chuo hiki kuwa sawa na Vyuo Vikuu vingine.

Tatu, Wizara inachukua hatua gani kuwaokoa walimu wa shule za Mazoezi Chang'ombe (Shule ya Msingi na Sekondari) ambao baada ya Chuo cha Ualimu Chang'ombe kuwa Chuo Kikuu Kishiriki, haki zao zingine za kiajira wamekuwa hawapati kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa maelezo kuwa wao sasa si watumishi wao huku wakiwalipa au kupata mshahara kutoka Wizara hiyo ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Spik,a nne ni kuhusu haki ya kupata vyeti, wanaomba Wizara ya Elimu ya Juu, sayansi na Teknolojia kutoa fedha kwa ajili ya maandalizi ya vyeti kwa kuhitimu kwa Chuo Kikuu Dar es Salaam. Tabia iliyozuka kuwalipisha wahitimu kwa ada ya shilingi 5000/= kwa *Provisional Result* inanyima haki ya msingi kwa wahitimu shilingi 5000/= katika hali ya kawaida ni ndogo lakini kwa vijana waliomaliza Chuo wakiwa hawana kazi ni mzigo. Aidha, vyeti vitolewe mapema mara baada ya kuhitimu kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE:** Mheshimiwa Spika, awali kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa maandalizi mazuri ya hotuba ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuchangia wachache kama ifuatavyo:

(a) Utafiti wa aina zote unaofanyika hapa nchini ni lazima ulenge katika kujenga teknolojia itakayoendeleza maendeleo ya nchi hii kama katika kilimo, tafiti za Kimataifa na hata Kitaifa inayoonyesha kuwa kuna teknolojia inayoonyesha kuwa kuna teknolojia ya *GM, tissue culture, organic farming* na kadhalika. Kwa kuwa njia hizi ni mpya, Serikali kupita Wizara hii ili wananchi waweze kuelewa teknolojia hizi kabla hazijatumika. Watu wajue mazuri na mabaya yake. Kwa mfano tunaelezwa kuwa mazao

yanayozalishwa kwa njia ya *GM* yana athari kwa binadamu kwa miaka mingi ijayo inawezekana ni kweli ama si kweli.

(b) Kuhusu mfuko wa mikopo, ni kweli fedha haitoshi ndio maana Serikali inaamua kuwakopesha wale wanaosoma katika Vyuo Vikuu vya Umma uamuzi huu hautajenga usawa kwa Watanzania wote. Ushauri wangu ni Serikali kuamua kwa nguvu moja kuongeza fedha katika mfuko huu. Hata kama uamuzi utakuwa ni kuchangia fedha toka bidhaa zetu kama mafuta, usafirishaji na kadhalika, watu wataelewa na watu wengi watapata elimu ya juu kupitia mikopo.

(c) Mheshimiwa Spika, kuhusu Vyuo vya Elimu ya Juu, naipongeza Serikali kwa juhudi yake ya kutaka kuongeza idadi ya wanachuo katika vyuo vikuu na vyuo vikuu vishiriki. Ili kutimiza azma hiyo ni muhimu kuwa na maandalizi hasa ya majengo muhimu yanayotakiwa kama *Lecture Halls, Hostels* nakadhalika.

Ukiangalia katika mgao wa fedha kwa chuo kipya Kishiriki cha Ushirika na Biashara Moshi kama unaona kuwa azma hiyo haipo. Chuo kimetengewa shilingi milioni 200 tu kwa ukarabati wa majengo ya zamani, hakuna majengo mapya yatakayojengwa.

Mheshimiwa Spika, nashauri suala hili liangaliwe upya na wapewe fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, baada ya ushauri huo mdogo naunga mkono hoja hii.

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Spika, mwanzoni nimpongeze Waziri kwa hotuba yake nzuri na ya kutia moyo lakini kuna maeneo yanahitaji mtazamo maalum ili mambo yaboreshwe.

Mheshimiwa Spika, la kwanza ni uhaba mkubwa wa walimu katika vyuo vyetu vya juu nchini, kuna umuhimu wa makusudi ili kuyafanya mazingira ya kusomesha yawe mazuri ili kuwavutia vijana wanaomaliza masomo yao vizuri kujiunga na fani hii mazingira hayo yajumuishe uwezekano wa kupata nafasi ya kuendelea na masomo ya uhazili *(MSc.)* na Shahada ya Falsafa *(Ph.D)* kwa wepesi, mishahra na kiinua mgongo bora kwa walimu. Hivi tutaweza kuwasomesha na kuwazuia *(retain)* vijana watu na hivyo kuongeza walimu katika vyuo vyeti.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili linahusu elimu ya juu kwa wanafunzi kutoka Zanzibar. Elimu ni mwanga na nyenzo kubwa ya maendeleo katika nchi. Bila ya elimu hakuna jamii au nchi yoyote inayoweza kuendelea. Kwa ajili hii, udahili wa wanafunzi kutoka Zanzibar haina budi kuongezeka. Kinyume chake tutainyonga *(strangle)* Zanzibar na kuikosesha maendeleo. Hakuna budi kufanya uchaguzi wa kina ili kujua kiini cha udahili mchache wa wanafunzi kutoka Zanzibar kwa kusudi la kuitafutia ufumbuzi tatizo hili. Vinginevyo yatakosekana maendeleo sawia kwa pande zote za Muungano hatimaye, vyuo vikuu nchini vitengewe pesa maalum kwa mahitaji ya nyenzo za lazima za wanafunzi wenye ulemavu.

**MHE. DR. ASHA-ROSE M. MIGIRO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza sana Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, Dr. Katunzi, Katibu Mkuu, wakurugenzi na watendaji wote wa Wizara hii, wamefanya kazi kubwa na nzuri katika kuandaa na kuimarisha Bajeti hii kwa ufasaha, pia nazipongeza taasisi zote za Elimu ya Juu kwa kazi za wanafunzi na uendeshaji. Taifa letu linanufaika sana na kazi wanazozifanya.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuchangia kwa kushauri eneo moja tu, hili linahusu kasi iliyopo hivi sasa ya kubadilisha hadhi za taasisi za kati au za kitaaluma kugeuzwa kuwa Vyuo Vikuu inawezekana zipo hoja nzuri za kuleta mabadiliko haya.

Lakini ni vema Wizara hii ikachukua jukumu la karibu katika maendeleo hayo au jukumu la kutoa ushauri ili kuwe na uwiano mzuri kati ya kuwa na *poverty academic institution* na taasisi za kati ambazo tunaweza kutia *professional institution* kama vile *IFM, IDM* ya zamani na nyinginezo.

Mheshimiwa Spika, uendeshaji wa Serikali unahitaji sana wahitimu wa taasisi za kati ambazo nimeziita *professional.* Nafahamu zipo mamlaka nyingine nchini ambazo zinahusika na ithibati ya mabadiliko ya vyuo hivi. Lakini naamini Wizara yetu hii ingeweza ikachukua jukumu hili la uratibu au ushauri kwani Wizara hii ina mchango mkubwa katika ujenzi wa taaluma kwa maana ya *pause academics* na vile vile *professional cadre development.*

Mheshimiwa Spika, baada ya hoja hii ndogo, naunga mkono hoja na ninashukuru Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi ya Teknolojia kwa kazi nzuri wanayofanya.

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza kwa moyo wa dhati Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, wataalam wa Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya katika kukuza vipaji vya Watanzania kwa ajili ya maendeleo endelevu ya Taifa letu.

Nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake ya bajeti na jinsi alivyoisoma katika kiwango cha uprofessa kama Waheshimiwa Wabunge walitarajia. Hongera sana.

Naomba nami niweze kutoa ushauri wangu katika kusisitiza eneo muhimu ambalo tukiweza kuliendeleza linaweza kuchangia kupata wataalamu wengi wenye ujuzi katika fani mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ushauri ni kuwa katika kuandaa Sera ya Elimu ya Mafunzo Tanzania, wataalamu wetu walishirikisha wadau mbalimbali na walitembelea nchi mbalimbali katika Bara la Afrika na nje ya Afrika. Kutokana na taarifa ya wataalamu, ilipendekezwa kuwa sera ya kuwawezesha wanafunzi na wafanyakazi kupata ujuzi wa ufundi sanifu ambao hawatapata nafasi ya kujiunga na vyuo vya ufundi ambavyo ni vya fani maalum.

Naomba kuwa kama utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo Tanzania ya mwaka 1995, ilivyobainisha kuanzishwa kwa *polytectinic* haitekelezeki sera hiyo

iangaliwe upya kwa lengo la kulifanyia mabadiliko kwa kuzingatia badiliko katika kuanzisha Vyuo vya *polytechnic* nchini.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa vyuo vya *polytechnic* ni moja, vyuo vya *polytechnic* vinatoa nafasi kwa wanafunzi wengi bila kujali rika wala umri vinatia uzoefu kazini hivyo wafanyakazi wengi wakipata nafasi ya kuendeleza taaluma zao.

Pili, vyuo vya *polytechnic* vinatoa mafunzo endelevu hivyo ni *life long learning expsience,* tatu, vyuo vya *polytechnic* vinachukua wanafunzi wa fani mbalimbali vya ufundi *(Learning can be under one roof with different specialties)* na nne, *flexibility* ni kubwa tofauti na *technical colleges* ambazo ni *final learning institutions.*

Mheshimiwa Spika, mifano ya nchi chache ambazo zimepata mafanikio makubwa kwa kuanzisha *polytechnic* ni pamoja na Kenya, Zimbabwe, Nigeria, Australia na nchi mbalimbali za Ulaya na Cuba.

Ushauri wangu haumaanishi kuwa tusipanue vyuo vya ufundi bali pamoja na kupanua na kuimarisha vyuo vya ufundi tusisahau kuanzisha vyuo vya *polytechnic* kama *all levels of technical learning under one roof* badala ya *technical colleges* ambazo ni *final specialties learning institutions under different roof.*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru wewe kwa kuniruhusu nichangie kwa maandishi. Nampongeza sana Mheshimiwa. Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia na wote.

Mheshimiwa Spika, nitajikita kwenye bodi ya mikopo kwa wanafunzi wa vyuo vikuu. Awali ya yote naomba kupongeza bodi hii kwa kutoa mikopo kwa haki na uwazi na kuzingatia anayepeleka wa kwanza kupewa na kuanza na kadhalika.

Pili, nachukua nafasi hii kuwapongeza/kuipongeza bodi ya mikopo kwa jinsi ambavyo imeweza kudhibiti migogoro ya vijana wetu. Mimi ninamini kuwa mikopo hiyo imewezesha idadi kubwa zaidi ya watu wengi vijana kwa watu wazima kuweza kusoma *Degrees* na *Diploma,* ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, naomba sasa nitoe ushauri kwa Serikali katika kuboresha bodi hii, kwanza, Serikali iongeze fedha za mikopo ili itoe kwa kiwango kinachotosheleza na sio kama sasa, pili, wahitimu wapatiwe kazi ili waweze kulipa madeni kukopa, tatu, wahisani tofauti waombwe kutunisha mfuko wa mkopo na nne, mikopo itolewe kwa wote, bila kujali umri.

**MHE.GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza Serikali kwa kuanzisha mfuko wa kukopesha wanafunzi. Pamoja na pongezi hizo kuna matatizo yanayojitokeza. Kwanza, mikopo hiyo imekuwa haitolewi kwa wakati jambo ambalo limesababisha migomo ya mara kwa mara. Nashauri mikopo hiyo itolewe mapema bila ya kuwafanya wanafunzi waingie mtaani kudai fedha hizo, pia mikopo hiyo

itolewe kwa wanafunzi wa vyuo vyote nchini bila kujali vyuo vya binafsi na vya Serikali vile vile nashauri mikopo itolewayo haina budi kukidhi mahitaji yote ya mwanafunzi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kuongeza idadi ya wanafunzi katika vyuo vyetu vikuu kuna upungufu mkubwa sana wa vyumba vya kusomea. Wanafunzi wengi hukosa nafasi hivyo hulazimika kusimama nje huku wakisikiliza mwalimu anayefundisha ndani ya chumba. Hili liangaliwe kwa umakini.

Mheshimiwa Spika, tabia ya kufunga vyuo mara kwa mara kumeshusha sana kiwango cha rlimu anachostahili kukipata mwanafunzi. Vile vile ni gharama kubwa kwa Serikali yetu kulipa walimu ambao kwa wakati huo wamekuwa hawafundishi kuzuia wanafunzi huwa wako majumbani kwao.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kuwa majadiliano kati ya Serikali na Serikali ya Wanafunzi iwe njia pekee ya kutatua migogoro hiyo na Serikali wakati mwingine ikubali kusahihishwa na ijitahidi kutatua matatizo yao haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, walimu wengi wamekwenda kufundisha nje ya nchi kwa sababu vyuo vyetu haviwalipi vizuri. Ushauri wangu ni kuwa Wahadhiri wetu walipwe mishahara inayolingana na vyuo vingine nchini hasa vyuo vyetu vya Afrika, hilo litapunguza wimbi la Wahadhiri wetu kukimbilia nje.

Mheshimiwa Spika, napongeza Serikali kwa hatua hii nzuri, maoni yangu, iwapo Serikali inafikiria kujenga Chuo Kikuu kingine kijengwe Wilayani Karagwe ili kuleta uwiano katika kutawanya maendeleo nchini. Wilaya ya Karagwe ina hali ya hewa nzuri inayofaa sana kwa kusoma na kufanya utafiti.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia Wizara hii kama ifuatavyo:-

(i)Utafiti ambao umefanywa umeonyesha kuwa Vyuo Vikuu tulivyonavyo vinayo majengo yaliyochakavu kwa kukaa muda mrefu bila kufanyiwa ukarabati. Hali hii inakwenda sambamba na upungufu wa mabweni machache ambayo yanasababisha kwa kiasi kikubwa baadhi ya wanafunzi kuishi nje. Hali hii inachangia kuwa kiasi kikubwa wanafunzi kuhusu muda wa kujisomea kutokana na mazingira wanayoishi.

Hali hii pia inachangia kwa kiasi kikubwa kushusha kiwango cha elimu kwenye Vyuo Vikuu, ni vema Wizara hii sasa yenye dhamana ijikite kwa kuomba fedha ya kutosha na yale yaliyopo yaweze kufanyiwa ukarabati mzuri wa majengo yaliyopo.

(ii) Lipo tatizo la usafiri kwa baadhi ya Vyuo na hasa vile ambavyo viko mbali na mji kama vile Chuo Kikuu cha Mzumbe ambapo wanafunzi wanapokwenda Mjini Morogoro wanajikuta wakitegemea mabasi ya watu binafsi ambayo nayo hayana muda maalum kwao.

Mheshimiwa Spika, nashauri swala la usafiri lipewe kipaumbele ili kuhakikisha Vyuo vinakuwa na usafiri wa kuaminika.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa kuleta hotuba nzuri ya bajeti yao hapa Bungeni.

Katika mchango wangu nataka kuelezea kuwa *gap* ya wanaopata elimu ya juu kati ya mikoa ya Kaskazini na mikoa ya pembezoni inazidi kuwa kubwa. Mikoa maskini inazidi kuwa na fursa finyu katika Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika, kuwepo na mpango maalum wa kutoa *scholarship* kwa makusudi ya kuwapa motisha wanafunzi wa mikoa maskini kama ilivyoainishwa katika ramani ya mikoa maskini nchini. Hawa hawawezi kushindana na wenzao ambao toka Uhuru wamekuwa na hali bora zaidi. Hili ni jambo la sera ambalo linaweza kujadiliwa na kuona jinsi gani ya kuwasaidia wanafunzi maskini zaidi ili waweze kuinuliwa.

Mheshimiwa Spika, uanzishaji wa Vyuo Vikuu vipya katika Mikoa ya pembezoni nako kunaweza kusaidia. Kulikuwa na mpango wa kuanzisha Chuo Kikuu Kishiriki Mtwara *TTC*. Mpango huu unalega lega kiasi kwamba mpaka sasa hatujaona utaratibu wowote wa kuanzisha Chuo hiki. Tukianzisha Chuo hiki kitazindua Mikoa ya Kusini ili Vyuo hivi vienee katika maeneo haya. Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia ndiyo iwe mstari wa mbele kuhakikisha vyuo vinaanzishwa katika maeneo yale ambayo bado yapo nyuma kiamaendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa matumizi ya gesi ndio kwanza yanaanza, napendekeza Kitivo cha Uhandisi kijihusishe sana katika utafiti na kuanzisha teknolojia rahisi ya namna ya kutumia gesi hii vizuri zaidi. Gesi itumike majumbani, viwandani, katika magari na kadhalika lakini taaluma yake iongezwe na Kitivo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MATHIAS M. CHIKAWE:** Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Elimu Tanzania *(TEA)* ni chombo kinachofanya kazi nzuri sana . Nashauri ile 2% ambayo inatakiwa kutolewa na Serikali kwa chombo hiki, Serikali ijitahidi kutimiza lengo hilo.

Mheshimiwa Spika, upo ugumu wa kurejeshwa kwa mikopo ambayo inachelewa kwa bodi ya mikopo ya elimu. Lipo tatizo la kupata ajira kwa wale watakaokopa na hivyo basi kushindwa kulipa madeni yao kwa wakati. Aidha, lipo tatizo la muda wa kulipa *(grace period)* ni ndefu mno.

Nashauri Serikali ifikirie utaratibu wa kuwataka wakopaji wote pale wanapomaliza vyuoni wapangiwe kazi kama kufundisha au kilimo kwa kipindi cha miaka miwili baada ya hapo deni lao lifutwe. Tuna shida ya walimu na kadhalika. Kazi hiyo ifanywe na vijana hao kulipia madeni yao (aina fulani ya *National Service)* kuliko kuanza kuwatafuta wanafanyia wapi kazi na kuanza kuwadai.

Nashauri pia mikopo hii isitolewe kwa wanafunzi wa digrii ya pili au ya tatu na vile vile isitolewe kwa wanafunzi wenye umri wa zaidi ya miaka 30. Tusomeshe vijana wetu, waliochelewa wanaweza kujitafutia taratibu zingine za kusoma.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, Serikali iweke utaratiabu wa kutoa mikopo kwa kiwango cha hali ya juu tu kwa kulingana na kiasi cha fedha kilichopo.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Mitihani kwa kushirikiana na Wizara iteue wanafunzi watakaopata mikopo kama vile inavyoteua wanafunzi wa kujiunga na kidato cha tano kwa kulingana na kiwango cha kufaulu na kulingana na kiwango cha kufaulu na kulinga na bajeti ya Serikali ya kukopesha.

Mheshimiwa Spika, watakaopata mikopo wawe tu wale waliofaulu kwa kiwango kilichopangwa na pia wapangiwe vyuo vya kwenda siyo mwanafunzi aamue tu mwenyewe. Kigezo kiwe ni kiwango cha kufaulu tu na siyo vinginevyo na mikopo iwe kwa wanafunzi wanaoingia kwenye vyuo vya hapa nchini hata kama ni vya binafsi.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote kimsingi naunga mkono hoja.

Hata hivyo, napenda kushauri jambo moja linalohusu mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu. Kwa mujibu wa Sheria Na. 9 ya mwaka 2004 ya Bodi ya Mikopo, Bajeti ya mwaka huu haitawatendea haki wanafunzi wanaosoma katika Vyuo Vikuu vya binafsi.

Kwa bajeti hii wanafunzi ambao tayari wanasoma katika Vyuo Vikuu vya binafsi na ambao mwaka uliopita walipata mkopo wa Serikali. Je, hawa kwa bajeti ya mwaka huu watawekwa katika fungu gani? Nina wasiwasi sekta ya elimu ya juu itakumbwa na misukosuko mikubwa ikiambatana kilio kikubwa cha jamii kuhusu watoto wao kushindwa kuendelea na masomo kwa kukosa fedha za kugharamia masomo yao.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu jambo hili Serikali ikaliangalia tena kwa lengo la kuhakikisha kila Mtanzania anapata haki sawa ya elimu.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, lengo la maandishi haya ni kueleza machache ambayo naamini yataboresha elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, kwanza nakubaliana na sera ya nchi inayosisitiza elimu kwa wote. Ili Watanzania wote bila kubagua jinsia, maeneo na maumbile yao, ninaposema maumbile, ninamaanisha wenye ulemavu wa viungo, kutoona na uziwi.

Mheshimiwa Spika, mikopo inayotolewa kwa wanafunzi wa vyuo vikuu, hautoi msaada wa vifaa kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimwia Spika, nashauri Serikali iangalie upya suala zima la vifaa vya wenye ulemavu vyuoni. Kuwapatia vifaa vya usafiri si mkopo.

Mheshimiwa Spika, usafiri ukiwa sehemu ya mkopo, walemavu wengi wasioweza kutembea vizuri watashindwa kuhudhuria masomo kwa wakati . Wenye uziwi wasipopata vifaa vya kusaidia kusikia, kujifunza kwao ni kugumu ukizingatia kwamba wataalam wa kutumia alama pia hawapo katika mihadhara ya masomo. Aidha, wale wasioona wakipewa vifaa vya kuwasaidia kujifunza vile vile isiwe mkopo.

Mheshimiwa Spika, kwa ufupi nashauri Serikali itoe vifaa vya kuwasaidia walemavu wanaofika vyuo vikuu, bure.

Mheshimiwa Spika, hii iwasaidia wanapopata mikopo waitumie sawa na wale wasio na ulemavu.

Mheshimiwa Spika, la pili naishauri Serikali itoe mikopo iliyo sawa kwa wanafunzi wa vyuo vikuu sawa. Izingatiwe kwamba wale walio katika vyuo binafsi vishauriwe kutopandisha ada watakavyo ili pesa zinazotolewa kwa wanafunzi zimudu kulipia mahitaji muhimu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo napenda kusema inawezekana sheria imekosewa mahali, lakini haiwezekani kabisa Serikali kumudu mahitaji yote ya mwanachuo. Kama ni hivyo, tuseme Serikali haiweza kuongeza idadi ya wasomi, bali idadi itabidi ipungue.

Mheshimiwa Spika, idadi ya wanafunzi ikipungua, nalo ni tatizo maand nchi inahitaji wataalam zaidi. Itabidi, tuige wosia wda Mwalimu Nyerere, kila mmoja wetu awe mfanyakazi Mbunge/Waziri au mwanafunzi katika ngazi yoyote, lazima ajifunge mkanda akizingatia kwamba wenzake wamejinyima kila kitu ili yeye asonge mbele. Narudia kusema kwamba Serikali haiwezi kulipa kila kitu anachohitaji mwanafunzi.

Mheshimiwa Spika, la tatu ni kuomba Serikali iweke mkakati mkubwa zaidi wa kuwawezesha wanawake wengi wasome masomo ya sayansi. Ikiwa hili litapewa uzito, ni lazima mashauriano yaanzie Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ili wasichana waangaliwe na waandaliwe vizuri tangu chekechea, msingi na sekondari. Vilevile maabara na madawa ya maabara viwepo ili wanafunzi wa sekondari wanaosoma sayansi wapate elimu kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ALI JUMA HAJI:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia afya njema, pia nakushukuru wewe kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia hotuba hii ya Bajeti ya Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimwia Waziri na watendaji wake wote ambao kwa namna mbalimbali waliwezesha kufanikisha hoja hii ambayo kwa kweli inatoa mwanga mzuri wa maendeleo ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia huko mbele tunakokwenda ambako ni kwa ulimwengu wa Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, lazima tukubali kwamba nchi yoyote duniani haiwezi kuwa na maendeleo bila kwanza nchi hiyo kuwekeza katika elimu. Elimu ni jambo moja muhimu sana katika maendeleo ya mwanadamu na nchi/Taifa uwe jumla.

Mheshimiwa Spika, tunajua kwamba serikali ina sekta nyingi na kila sekta ili ifanye kazi zake vizuri basi lazima iwe na wataalam na hawezi kuwa na wataam bila kuwa na elimu na hasa elimu ya juu. Hivyo basi ili tuwe na hao wataalam wazuri, Serikali lazima ikubali gharama ya kuwekeza katika elimu na itoe umuhimu na kuona kwamba Wizara hii inapatiwa fedha za kutosha katika kuendeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, tunampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu pale aliposema katika majumuisho ya hotuba ya Wizara yake kwamba Serikali imeipa umuhimu wa kwanza elimu na pili kilimo.

Mheshimiwa Spika, sote tunafahamu kuwa kuwekeza katika elimu ni gharama sana lakini lazima pia tukubali kwamba unapotaka kumbadili mtu au kuibadili nchi kutoka ilipo na kuingia katika ulimwengu wa sayansi na teknolojia basi pia tukubali na gharama za mapinduzi au mageuzi hayo.

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi naipongoza Serikali kupitia Wizara hii kwa kuanzisha mfuko huu kwa nia njema ya kuwasaidia watoto walio katika familia duni ili nao wawezi kumudu kugharamia na kujipatia elimu ya juu kwani wengi wao walikuwa wanashindwa kupata elimu hiyo kutokana na ukwasi wa fedha. Pamoja na nia nzuri ya Serikali kwa mfuko huu lakini bado fedha zinatengwa ni kidogo sana ukizingatia kwamba vijana wanaohitaji mkopo huo ni mkubwa sana wanafanyakazi wa mfuko hasa ukizingatia hali halisi ya kazi ngumu ya kuwahudumia wanafunzi katika mambo ya mkopo.

Mheshimiwa Spika, kama msemo wa Kiswahili usemavyo, mwanzo mgumu. Hivyo basi tunajua watendaji wa mfuko huu wamepambana na mazingira magumu na matatizo mengi kama vile migomo ya wanafunzi, uhaba wa fedha na vitendea kazi, udanganyifu wa maelezo ya baadhi ya wanafunzi ambao sio waaminifu na kupelekea hata kuchukua mikopo hiyo zaidi ya mara moja.

Mheshimiwa Spika, kutokana na matatizo hayo tunaiomba Serikali kuwaongezea fedha mfuko huu ili waweze kumudu vyema shughuli zao.

Mheshimiwa Spika, katika maoni na ushari wa Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma ya Jamii, ameeleza kwamba hadi kufikia Juni, 2006 Wizara hii ilikuwa haijapokea shilingi bilioni 5.2 kutoka Hazina (Fedha za Maendeleo) ambazo baadhi yake ni fedha za Taasisi hiyo.

Mheshimiwa Spika, namwomba pia Mheshimiwa Waziri anieleweshe fedha za taasisi hii kati ya hizo shilingi bilioni 5.2 zilitengwa wapi kwani katika kitabu cha nne hakionyeshi fedha zilizotengwa kwa taasisi hiyo kwa mwaka 2005/2006. Hivyo naomba kufahamu fedha hizo au ni maeneo tu.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kufahamua hizi shilingi milioni 800 zilizotengwa mwaka huu wa 2006/2007 zimelengwa kwenye mambo gani?

Mheshimiwa Spika, sote tunafahamu kwamba *TEA* ni chombo kilichoundwa ki-Muungano kwa mambo yote ya elimu ya juu. Mimi binafsi naipongeza sana mamlaka hii kwa kazi kubwa na uzuri wa kutoa mikopo na misaada mbalimbali kwa shule.

Mheshimiwa Spika, katika mamlaka hii mimi naomba mambo yafuatayo:-

(i) Mheshimiwa Spika, mamlaka ifanye juhudi ya kwenda Zanzibar ili kwenda kuwaelimisha wananchi wa Zanzibar juu ya umuhimu wa chombo hiki na pia kuwahamasisha katika kuchangia na umuhimu wa michango hiyo.

(ii) Mheshimiwa Spika, najua wazi kwamba mambo yanayohusu Zanzibar kwa vile chombo hichi kinatoa mikopo sasa, kwa nini chombo hiki hakiwezi kutoa mikopo (sio misaada) kwa shule zetu za Zanzibar ambazo kama Halmashauri zao au hata Wabunge wao binafsi watakuwa tayari kudhamini mikopo hiyo basi kwa nini wasikopeshwe wakati kitu kinachohitajika ni kurejeshwa tu kwa mkopo huo? Naomba hili liangaliwe kwa undani wake.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nampongeza Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia na Naibu Waziri pamoj a na watendaji wake wote kwa kuweza kuandaa hotuba hii pia na Kamati ya Huduma za jamii chini ya Mwenyekiti wake kwa ushirikiano mzuri na Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia.

Namwomba Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia kama ilivyo nchi yetu Tanzania ina mfumo wa Muungano wa Serikali mbili kwa maana Tanzania Bara na Tanzania Visiwani (Zanzibar) sasa iko haja kuona Zanzibar vyuo vikuu viongezwe Zanzibar ili Zanzibar na wananchi wake waone Muungano imara na wenye kuthamini Muungano huu.

Mheshimiwa Spika, walimu wa elimu ya juu, sayansi na teknolojia kwa kweli maisha yao ni duni kutokana na hali zao, kama Serikali inayokwenda na wakati wa

awamu ya nne, naomba kwa heshima zote Wizara ilione hili walimu hawa wa elimu ya juu wapate fedha, malazi mazuri, chakula kizuri, usafiri mzuri na maandalizi yote yawe mazuri ili hata wakati wakifanya kazi zao ziwe na uhakika ili kupata elimu bora kwa wale wanaofuzu kwenye vyuo vikuu.

Mheshimiwa Spika, bila elimu kuenea kupata wataalam wenye elimu. Nchi yetu haiwezi kuendelea kwa makusudi, naiomba Serikali ilione hili ili nchi ipate maendeleo zaidi na iendane na teknolojia za kileo.

Mheshimiwa Spika, naonga mkono hotuba hii asilimia zote.

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze sana Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia kwa hotuba yake nzuri. Naomba nitoe mchango wangu kidogo kama ifuatavyo:-

Kwanza, mwaka 2005/Septemba/Oktaba, Mheshimiwa Rais wa awamu ya tatu aliunda kamati maalum ya kuangalia ni namna gani mazingira ya kazi kwa wana taaluma na watumishi waendeshaji yanaweza kuboreshwa katika hadidu za rejea, watumishi waendeshaji walitajwa ili maslahi yao pia yaboreshwe sambamba na yale ya wana taaluma.

Kwa upande wa wanataaluma, mishahara yao iliboreshwa Januari, 2006 kwa asilimia mia moja ikiwa asilimia 50 walitakiwa wapewe Januari, 2006 na asilimia 50 nyingine wapewe Julai, 2006 na hivyo kujumuisha pia nyongeza iliyotangazwa na Utumishi kwa upande wa watumishi waendeshaji pia walitakiwa mishahara yao ipande kwa asilimia mia moja. Lakini mapendekezo hayo yalipofika Hazina yalipelekwa Utumishi kwa sababu ilisemekana hili ni suala la kisera.

Mheshimiwa Spika, mimi sijaelewa kwa nini suala linalowahusu watumishi wa sehemu moja na ambayo mapendekezo yake yamepitishwa na kamati moja yawe na sura mbili tofauti bila kuangalia athari zinazoweza kujitokeza kama vile kuleta mgawanyiko mkubwa baina ya watumishi. Hii itaweza kusababisha kutofikia matarajio ya uzalishaji wa nguvu kazi yenye ubora unaokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, tafadhali naomba maelezo.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake kwa hotuba nzuri iliyowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, pongezi kwa uamuzi wa kujenga Chuo Kikuu Dodoma. Elimu ndo inaweza kutuondoa katika dimbwi la umasikini.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Mollel aliyotueleza Rais wa awamu ya tatu ilipendekeza kuboresha mishahara na malipo mengine ya wanataaluma na watendaji wengine katika Vyuo Vikuu. Lakini Serikali imefanya uamuzi wa busara na kuwalipa

wanataaluma lakini wenzao walio katika kazi zingine za utendaji wameacha bila kulipwa kama ilivyopendekeza Kamati ya Mollel.

Mheshimiwa Spika, napendekeza mfumo wa kutoa Elimu ya Juu ndani na nje utazamwe upya ili pawepo na programu itakayotuingiza katika karne ya 21 hasa katika sayansi na teknolojia.

**MHE. USSI AMME PANDU:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Profesa Petter Msolla, kwa kuchaguliwa na Mheshimiwa Rais kuwa ndiye Waziri ambaye atamsaidia kuhusu kuendeleza maandeleo ya elimu ya juu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nataka nichukue nafasi hii pia kuwapongeza wananchi wa Jimbo langu la Mtoni, Zanzibar kwa kunichagua kuwa Mbunge wa Jimbo hilo kwa kura nyingi na mimi nawaahidi kuwatumikia kwa nguvu zangu zote.

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye hoja ya kuchangia Wizara hii napenda kwanza kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa wazo lake zuri la kuanzishwa kwa Chuo Kikuu hapa Dodoma ili nchi yetu ipate kutoa nafasi kwa wanafunzi wetu kujiunga kwa wingi na hatimaye kupata wataalam wa kutosha na wa fani mbalimbali kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuipongeza mamlaka hii kwa jinsi inavyosaidia kutoa mikopo kwa ajili ya kuboresha maendeleo ya elimu katika nchi hii na kutatua matatizo mbalimbali yanayohusu elimu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mamlaka hii ina lengo zuri la kuisaidia jamiii ya Watanzania kuhusu elimu, namwomba Mheshimiwa Waziri atakapo jibu hoja alieleza Bunge hili ni lini mamlaka hii itaweza kuwasaidia ndugu zetu kutoka Tanzania Zanzibar kufaidika na mikopo hii hasa ukiangalia kuwa Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri hii?

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia kwa nia nzuri tu iliamua kujenga Chuo kule Zanzibar, lakini jambo la kusikitisha fedha kwa ajili ya ujenzi ule umekuwa ni tatizo kubwa, hata kama fedha zimetengwa kwenye bajeti huwa hazipatikani kutoka hazina.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, wakati wa kujibu hoja alieleza Bunge hili hivi tatizo ni nini naomba kujua.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba kumpongeza Mheshimiwa Wazira wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia kwa mara ya pili na naunga mkono hoja hii kwa asilimia zote.

**MHE. RITA L. MLAKI:** Kwanza nachukua nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa kuongoza Wizara hii na hatimaye kuwakilisha Bujeti yao siku hii ya leo.

Napenda kuchangia kama ifuatavyo, Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia ni Wizara kubwa na nyeti sana kwa maendeleo ya nchi yetu. Maeneo yote mawili ni mazito, Elimu ya Juu na Sayansi na Teknolojia, kinachojulikana ni kuhamasishwa katika jamii zaidi ni Elimu ya Juu ambapo Sayansi na Teknolojia imepewa umuhimu mdogo.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Sayansi na Teknolojia ina sera nzuri lakini kama sera hizo hazitoshi kuifanikisha sekta hii basi ni afadhali zifanyiwe *amendment.* Tume ya Sayansi ambayo jukumu lake ni kuendeleza utafiti nchini ingepewa bajeti ya kutosha ili kuweze kuendeleza utafiti. Tume hiyo haifanyi utafiti yenyewe bali kuhamasisha tafiti mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, bila sayansi na teknolojia hatuwezi kuendelea kama Taifa. Dunia nzima nchi zilizoendelea zinatumia sayansi na teknolojia kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, la pili ni kuwa kuna tafiti nyingi zinafanyika lakini hazitumiki, zinachukuliwa na waliofanya tafiti hizo. Ningeomba Serikali iratibu tafiti zote na kutenga fedha maalum za kuendeleza tafiti hizo.

Mheshimiwa Spika, *ICT* pia iendelezwe kwa kusambazwa nchi nzima ili watu wapate ujuzi *(an information)* kwa ajili ya kujiendeleza kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, ni mategemeo yangu Mheshimiwa Waziri na timu yake watainua sayansi na teknolojia katika nchi yetu na tusikie *(advocacy)* kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii nami kutoa mchango wangu na nitauelekeza kwenye Taasisi ya Sayansi za Baharini iliyopo Zanzibar, Taasisi hii imeanzishwa mwaka 1978 na lengo kuu la taasisi hii ni kuendeleza shughuli za utafiti wa viumbe vya baharini.

Ni ukweli kwamba taasisi hii inakumbwa na tatizo la ukosefu wa majengo ya ofisi na maabara. Uamuzi wa Serikali wa kujenga majengo mapya kule Buyu inatia moyo lakini ni vyema ujenzi huu ukaharakishwa ili majengo hayo yamalizike mapema ili kuongeza ufanisi wa shughuli zao za ila siku.

Mheshimiwa Spika, taasisi hii kule Zanzibar ina watafiti *(Researchers)* 18 kati ya hawa ni Wazanzibari watatu tu walioajiriwa katika taasisi hii ukizingatia kwamba taasisi hii iko Zanzibar ni jambo la kushangaza kuona kwamba idadi ya watafiti wa Kizanzibari ni wachache mno kuliko mategemeo. Hali hii inatupa wasiwasi wa kwamba huenda kuna ubaguzi wa aina fulani katika ajira za watafiti au Mheshimiwa Waziri atueleze kama Zanzibar hakuna wasomi wanaoweza kufanya kazi katika taasisi hii.

Mheshimiwa Spika, ni kawaida kwa taasisi kama hizi kuchukua juhudi ya kuwaendeleza kitaaluma watendaji wake. La kushangaza hapa Taasisi ya Sayansi Baharini Zanzibar fursa za masomo zinaelekezwa zaidi kwa *academic staff* na wale wengine hawapati fursa hiyo.

Mheshimiwa Spika, *Non-academic staff* ni wengi lakini kuwanyima nafasi ya kutokuwaendeleza ni kutokuwatendea haki. Ni lazima sasa Wizara ichukue juhudi maalum ya kuwaendeleza kitaaluma *non-academic staff* ili nao waende sambamba na mabadiliko ya teknolojia na hatimaye waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba taasisi hii imeanzishwa karibu miaka 18 sasa, inasikitisha kuona kwamba kati ya watafiti wanaofanyakazi hapo hamna hata mmoja mwenye kiwango cha uprofesa. Hii ni kasoro kubwa, vinginevyo inatupa picha kwamba Wizara haioni taasisi hii kuwa ni ya muhimu kwao.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumwomba Mheshimiwa Waziri azingatie kasoro hizi na hatua madhubuti zichukuliwe ili kuongeza ufanisi wa kazi zao za kila siku.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nawaomba Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri warejee tamko lao walilolitoa kuhusiana na udhamini wa Serikali kwa wanafunzi waliofaulu kidato cha sita.

Mheshimiwa Spika, tamko lao linaenda kinyume na sheria ya mikopo ya vyuo vya elimu ya juu. Kama ilivyoainishwa na sheria inayo/iliyoidhinisha mikopo hiyo. Kutokana na sheria husika wanafunzi wote bila kujali ni wa umma au binafsi waliomba mikopo, ambapo baadhi yao walipewa nusu kwa maelezo kwamba watamalizia baada ya muda. Kipindi kirefu kimepita na wanafunzi *especially* waliopo kwenye *private universities* wako kwenye tishio la kutofanya mitihani na kufukuzwa shule.

Kwa kuzingatia kwamba sheria iko upande wa wanafunzi, je, Serikali inatoa tamko gani kuhusiana na wanafunzi wa *private universities* ambao waliomba mkopo ambao haijakamilika kwa ahadi kwamba watamaliziwa baada ya muda mfupi.

Kuhusu maslahi ya wafanyakazi vyuo vikuu, mwaka 2005 iliundwa Kamati ya Rais ya kuboresha mazingira ya kazi katika vyuo vikuu. Kamati husika ilikuwa na jukumu la kuangalia ni kwa kiasi maslahi yaliyo duni ya watumishi wa vyuo vikuu yataboreshwa.

Pamoja na mambo mengine ilikubalika kwamba kutakuwa na maboresho ya aina mbili kama ifuatavyo:-

(i) Kuboresha maslahi ya wanataaluma kwa 50% itakapofika Januari, 2006 na 100% itakapofika mwezi Julai, 2006.

(ii) Kuboresha mishahara ya wafanyakazi waendeshaji kwa 100% na kwamba mabadiliko husika yatajumuishwa kwenye bajeti ya mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa mazoezi kwa vitendo ili kuweza kupima uelewa wa wanafunzi, walimu *(lecturers)* wanapaswa kwenda kuwakagua wanafunzi wanapokuwa *field,* cha kushangaza sasa hivi hakuna fungu lililotengwa kwa ajili ya walimu kwa ajili ya kwenda kufanya usimamizi huo.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mpango gani kurejesha fungu husika kwa manufaa ya wataalamu/wahadhiri wetu?

Mheshimiwa Spika, kuhusu *housing allowances* kwa *lecturers,* kisheria walimu wote wa vyuo vikuu ambao wanakaa kwenye nyumba zao binafsi wanatakiwa kulipwa *allowance* za nyumba. Vyuo vyote vimekuwa hivyo kasoro Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, je, Serikali inatoa tamko gani kuhusiana na hilo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia hoja iliyoko mbele yetu ili nianze kujibu baadhi ya hoja zilizojitokeza leo kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge. Naomba nianze kwa kusema naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa kuhutubia hili Bunge lako, naomba na mimi niungane na wenzangu kabla ya kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, kwanza kumpongeza sana Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa ushindi wake wa kihistoria katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika Desemba, 2005. Nimpongeze pia kwa kuendeleza historia hiyo hiyo, hapo tarehe 25 Juni, 2006 wakati tulipomchagua kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, kwa kupata asilimia 99.99 ya kura zote zilizopigwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nimpongeze Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, kwa kuteuliwa na Rais na baadaye kupitishwa na Bunge lako Tukufu kwa kura nyingi sana kuwa Waziri Mkuu. Niwapongeze Wabunge wote kwa ushindi wao katika majimbo yao na katika Mikoa kwa wale wa Viti Maalum na kwa wale walioteuliwa na Mheshimiwa Rais. Pia niwapongeze Mawaziri kwa kupewa dhamana na Mheshimiwa Rais kuziongoza Wizara zao. Niwapongeze Naibu Mawaziri wenzangu kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais, nikupongeze sana mwenyewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Wenyeviti wetu Mheshimiwa Job Ndugai na Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa pamoja niwapongeze sana kwa umahiri wenu wa kuendesha vikao hapa ukumbini kwa ufanisi mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii ya pekee nami kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuniteua kuwa Naibu Waziri wa Elimu ya Juu na hivyo kumsaidia Waziri, Mheshimiwa Profesa Peter Msolla. Naomba nimshukuru Waziri wangu Mheshimiwa Msolla kwa kunishirikisha kikamilifu katika majukumu ya Wizara yetu. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu Dr. Naomi Katunzi,

wakurugenzi na wafanyakazi wote wa Wizara na Wakuu wa Taasisi zetu zilizopo chini ya Wizara yangu kwa ushirikiano wa hali ya juu wanayonipa katika kazi zangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Mara kwa kunichagua kwa kura 193 kati ya 194 na hivyo kuniwezesha kuwa mwakilishi wao hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee naomba nitumie nafasi hii pia kuishukuru sana familia yangu nikianzia na mzee mwenzangu Ndugu John Kabaka, binti yetu Robi pamoja na wengine wote walionisaidia na kunipa moyo wakati nilipoamua kuingia katika hili jukwaa la siasa, kutokana na ushauri wao ndiyo maana nimefikia hatua hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba niwapongeze ndugu zangu wa Mkoa wa Mara kwa ujenzi wa shule. Lakini naomba nitoe rai kwamba shule hizo isiwe ni kwa ajili ya watoto wa kiume tu, naomba wapeleke watoto wa kike ili nao siku moja waje wafike hapa Bungeni kama mimi nilivyofika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ambayo nilifikiri niyaseme, naomba sasa nijibu baadhi ya hoja ambazo zimejitokeza wakati wa kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri Mkuu ambazo zilihusu Wizara yangu kwanza. Hoja ya kwanza ilikuwa ni kuhusu mkopo wa wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, hoja hii itaelezwa vizuri zaidi kwa mapana na Mheshimiwa Waziri, lakini naomba nijibu hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi alisema mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu huwa ina maamuzi ya zimamoto na kutokuwa na msimamizi mzuri.

Mheshimiwa Spika, bodi ya mikopo ilianza kazi rasmi Julai, 2005 ikiwa na watendaji wachache na vifaa vichache vilivyoazimwa Wizarani kwetu. Matatizo yaliyojitokeza ni kutokana na uchache wa watendaji, vifaa na wakati mwingine shinikizo la migomo kutoka kwa wanafunzi wa Vyuo Vikuu wakipinga baadhi ya kanuni zilizokuwa zimewekwa na bodi kwa mwaka wa masomo 2005/2006. Hivi sasa bodi imepata kibali cha kuajiri watumishi 86 na tayari imekwishaajiri watumishi 29 na inaendelea na taratibu za kuajiri wengine waliobaki.

Aidha, hivi sasa bodi ina vitendea kazi vya kutosha ikiwa ni pamoja na vya kubaini uwezo wa wanafunzi wanaohitaji mikopo yaani *min testing* na kanuni za utoaji wa mikopo zimerekebishwa. Hivyo ni tegemeo la bodi kuwa matatizo ya mwaka 2005/2006 hayatarudiwa. *(Makofi)*

Hoja ya pili ilikuwa inatoka kwa Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, iliyokuwa inazungumzia kwamba bajeti inayotolewa kwa Wizara ni ndogo hasa katika Vyuo vya *DUCE, MUCE* na *MUCCoBS*. Hii ni kweli na inatokana na ufinyu wa bajeti kwa ujumla wa nchi nzima na hata hivyo Serikali itaongeza bajeti katika taasisi hizo kutegemeana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ni mapendekezo ya kuongeza posho ya chakula ya wanafunzi ya shilingi 2500 hadi shilingi 5,000 iliyokuwa imependekezwa na wanafunzi wa Chuo Kikuu. Hoja hiyo, imejitokeza sasa hivi wakati anachangia Mheshimiwa Luhaga Mpina, pia. Lakini naomba niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba baada ya matatizo tuliyoyapata ya kuonekana kwamba fedha hii haitoshi Wizara yangu iliunda Tume ambayo ilifanya utafiti katika migahawa yote ya Chuo Kikuu na ile inayozunguka Ubungo na baada ya kupata huo utafiti tulibaini kwamba kwa kutwa mwanafunzi atatumia shilingi 2,800 lakini hata hivyo Wizara yangu iliongezea kwa kuona kwamba kuna *inflation* inaendelea tutaongeza na sasa watapewa shilingi 3,500. *(Makofi)*

Hoja nyingine iliyojitokeza ni kuhusiana kigezo kilichotumika kujenga Chuo Kikuu kipya Dodoma hoja ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba. Wazo la kuanzisha Mamlaka ya Kustawisha Makao Makuu, ilizingatia kuwa Dodoma ni katikati ya nchi yetu ya Tanzania hivyo ni rahisi kufikiwa na watu kutoka pande zote za nchi. Pia Dodoma ni miongoni mwa mikoa yenye taasisi chache sana za elimu ya juu. Kuna Chuo cha Mipango tu ndiyo chuo cha elimu ya juu na Chuo cha Elimu ya Biashara.

Mheshimiwa Spika, tatu hii ni njia moja ya kuongeza kasi ya ukuaji wa Makao Makuu, nne, ikumbukwe kwamba uwezo wa Serikali kifedha ni mdogo na ujenzi wa Chuo Kikuu ni gharama kubwa. Hivyo ni vigumu kujenga Chuo Kikuu katika kila mkoa kwa wakati mmoja. Hata hivyo kwa kadri uwezo wa kifedha utakavyokuwa ukiongezeka Serikali itaendelea kujenga Vyuo Vikuu katika mikoa mingine ambayo haijapata fursa hii. *(Makofi)*

Aidha, wawekezaji wengine katika elimu ya juu watashauriwa kuwekeza katika Mikoa mingine lakini hata hivyo katika kila Mkoa kuna *centre* ya Chuo Kikuu Huria ambayo pia ni *centre* ya elimu ya juu.

Mheshimiwa Mariam Mfaki, alitoa angalizo kwamba katika ujenzi wa Chuo Kikuu tuangalie pia na upanuzi wa miundombinu. Hii ni kweli na hii itafanyika na kutokana na hali halisi ya hatua tuliyofikia tutakuwa na watalaam ambao wataangalia masuala ya barabara, tutawasiliana na Wizara zinazohusika kuangalia masuala ya barabara, maji, umeme na huduma za afya pamoja na mengine ambayo yanahitajika. Kwa hiyo, hilo litaangaliwa.

Mheshimiwa Spika, katika hilo hilo la Chuo Kikuu Mheshimiwa Herbert Mntangi, alizungumzia kuhusu ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, imefikia wapi ya ujenzi wa Chuo Kikuu. Kwa kweli hatua ni nzuri tunatarajia kwamba ifikapo Septemba, 2007, tutaanza udahili wa Chuo Kikuu cha Dodoma ambacho bado hatujakitafutia jina. Kutokana na muda sitaeleza hatua zote lakini tuchukue kwamba tuko katika hatua za mwanzo lakini nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo asubuhi tumepata hoja kadhaa na naomba kwa kweli sitaweza kuzijibu zote nitagusia chache. Hoja ya kwanza ni kutoka kwa Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis,

Mheshimiwa Charles Keenja na Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya. Hawa walizungumzia kuhusu maslahi na mafao ya walimu wa vyuo vikuu na hata maoni ya kambi ya upinzani wamegusia hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba Serikali ilishaunda kamati kuanzia Oktoba, 2005 ya kuangalia maboresho ya maslahi ya mishahara ya wataalam wa vyuo vikuu vya umma na kuyawasilisha mapendekezo hayo kwa Mheshimiwa Rais, Januari, 2006. Hata hivyo Serikali ilishaongeza mishahara ya watalaam kwa asilimia 50 na kwa bajeti hii tumemalizia ile asilimia 50. Sasa tunaendelea kuwasilisha mapendekezo kuhusiana na wale ambao siyo wana taaluma yaani wale *administrative staff* ambao mambo yao yanashughulikiwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine iliyojitokeza ni hii ya Chuo Kikuu Kiambata cha Elimu Mtwara, ambayo imetolewa na Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mbunge wa Tandahimba na tunasema kwamba mwaka 2003/2004 Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kilipewa jukumu la kufanya upembuzi yakinifu wa uanzishwaji wa Chuo Kikuu Kiambata cha Elimu Mtwara. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilitayarisha ripoti ya upembuzi huo na kuwasilisha ripoti Wizara zinazohusika. Kwa kifupi ni kwamba tulikuwa tunasubiri kwa sababu chuo hiki kipo chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na kiko chini ya sheria inayohusiana na Wizara hiyo.

Kwa hiyo, tulikuwa tunasubiri kwanza sheria ibadilishwe ili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kiweze kuingia na kuweka mabadiliko yoyote yanayohitajika ili kiweze kuwa Chuo Kiambata. Kwa hiyo, hili linashughulikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu kutumia vitabu vya zamani kwa Chuo cha Biashara Moshi, tumemuuliza Mkuu wa Chuo kwa sababu yupo hapa kwa kweli chuo kile kimepata vitabu vingi sana na ni vipya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, siyo kweli kama Mheshimiwa Lucy Owenya aliyezungumzia kwamba Chuo cha *MUCCoBS* kina vitabu vilivyochakaa na Mheshimiwa Luhaga Mpina, amezungumzia vyuo vyetu vina vitabu vilivyochakaa. Ukweli vitabu ni ghali na kuchakaa vitabu ni kawaida. Lakini juhudi inafanyika ya ku-*replace* hivi vitabu kila mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naona muda unayoyoma na kama nilivyosema sitaweza kujibu yote lakini naomba nimjibu Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, aliyezungumzia kuhusu uanzishwaji wa *polytechnics* sambamba na upanuzi wa *Technical Colleges.*

Mheshimiwa Spika, nakubaliana sana na Mheshimiwa Perofesa Philemon Sarungi kuwa vyuo vya elimu ya ufundi vilivyo chini ya Wizara havina fani mchanganyiko yaani *multiple skills,* hii inatokana na ukweli kwamba utoaji wa elimu yaani *technical education* hauko chini ya Wizara yangu tu bali utoaji wa elimu hiyo upo pia kwenye Wizara za Viwanda na Biashara *(CBE),* Wizara ya Fedha *(IFM),* kwa hiyo, inabidi tukae tuangalie jinsi ya ku-*compromise* ili tuweze kutoa kitu kinaitwa

*polytechnical education.* Lakini hata hivyo, vyuo vyetu vinatoa elimu ya ufundi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga hoja mkono hoja kwa mara ya pili. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu waungane nami kuishukuru Serikali ya Awamu ya Nne ikiongozwa na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa azma yake ya kujenga Chuo Kikuu kipya hapa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uamuzi huu wa Serikali unajali mwamko na mahitaji ya wananchi wetu kuhusu upatikanaji wa nafasi za elimu ya juu nchini na hasa ukizingatia kwamba ni asilimia chini ya 50 tu ya wale wenye sifa za kujiunga na elimu ya juu ndiyo wanapata nafasi.

Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele yenu na kutoa mchango wangu katika hoja hii. Kwa mara nyingine nichukue fursa hii kuwashukuru wananchi wa jimbo langu la Kilolo, kwa imani kubwa waliyonipa na waliyoitoa kwangu. Aidha, namshukuru mke wangu, Violet na familia yangu yote kwa kunipa moyo katika kutekeleza wajibu wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo napenda kuwatambua Waheshimiwa Wabunge 74 waliochangia hoja mbalimbali kuhusu Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia wakati wa kujadili hotuba za bajeti zikiwemo Wizara za Fedha, Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, hotuba ya Waziri Mkuu na hotuba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi pamoja na Wizara ya kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama Naibu Waziri alivyosema kuna wengine waliotoa maoni yao kwa kuzungumza hapa Bungeni na wengine kwa maandishi. Naomba sasa kuwatambua Waheshimiwa Wabunge hao kama ifuatavyo:-

Wale waliochangia kwa kusema katika hotuba ya Bajeti kwanza ni Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Ephraim Madeje, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Charles Kajege, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa na Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir. *(Makofi)*

Kwa wale waliochangia katika hotuba ya Waziri Mkuu, ni pamoja na Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Babati Ali Abeid, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Ibrahim Sanya, Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Aziza Ally na Mheshimiwa Ruth Msafiri. *(Makofi)*

Waliochangia kwenye Wizara yangu walikuwa tisa ambao ni Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa na Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, Naibu Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa maandishi kwenye Wizara yangu ni hawa wafuatao, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Mheshimiwa Gedfrey Zambi, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Janet Kahama, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mheshimiwa Idd Azzan na Mheshimiwa Ruth Msafiri. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Juma Njwayo, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Mathias Chikawe, Mheshimiwa James Lembeli, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Aloyce Kimaro, Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Rita Mlaki, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Cynthia Ngoye, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, Mheshimiwa Charles Kajege, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Matha Umbulla na Mheshimiwa Stephen Galinoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, michango ya Waheshimiwa Wabunge niliowataja ilikuwa ni mizuri sana. Aidha, siyo rahisi kujibu kwa kina na kutosheleza hoja zote za Waheshimiwa Wabunge 74 waliochangia. Ninaahidi kwamba baadhi ya hoja ambazo sitapata muda wa kuzijibu tutaweza kuzijibu kwa maandishi na kumtumia kila Mbunge kwa ajili ya rejea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati ya Huduma za Jamii tutayazingatia ipasavyo na kutokana na ushauri na maoni ya Kamati tutapenda kuzungumzia machache ambayo hayajatajwa na Mheshimiwa Naibu Waziri.

Kuna mmoja ambaye amechangia kwa bahati mbaya tuliruka jina lake ni Mheshimiwa Luhaga Mpina ambaye amechangia hapa mwisho, samahani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja nyingi na kama nilivyoeleza kwamba itakuwa vigumu kuzijibu zote lakini tutachagua zile ambazo tutaweza kujibu kwa wakati huu kulingana na muda uliopo.

Mheshimiwa Spika, ya kwanza, ilitoka kwa Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, aliuliza kwamba ni nini hatua zinazochukuliwa katika utekelezaji wa ahadi za Rais, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, katika kujenga Chuo Kikuu kipya angalau kimoja

kizuri. Lakini akaongezea kwamba Serikali iangalie uwezekano wa kufungua Chuo Kikuu kingine Mbeya kwenye Chuo Kikuu cha Ufundi.

Mheshimiwa Spika, waliochangia katika hili ni pamoja na Mheshimiwa Victor Mwambalaswa pamoja na Mheshimiwa Benson Mpesya na Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya. Asubuhi wakati nikiwasilisha hoja yangu nilisema kwamba tunatekeleza maagizo ya Rais, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, wakati ule alipotembelea Wizara yangu tarehe 1 Februari, 2006 kwamba katika kupanua elimu ya juu tusigeuze vyuo vingine vya kati au *secondary schoools* viwe vyuo vikuu. Hii ni taasisi ya elimu ya kati. Lakini vile vile tunafahamu kwamba huko nyuma Baba wa Taifa Marehemu Mwalimu Julius Nyerere, alishatamka wazi wazi na ipo kwenye maandishi kwamba alitaka aone kwamba kile Chuo kinajengwa kiwe Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa sababu kuna kauli mbili, ya Rais aliyepo madarakani na vile vile kwa ajili ya kumheshimu Baba wa Taifa, Marehemu Mwalimu Julius Nyerere, tunafikiri kwamba hili wazo tumelipokea, tutafanya mawasiliano na Serikali tuone uwezekano wa kujenga chuo hiki kifikie ngazi ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango mwingine ulitoka kwa Mheshimiwa Susan Lyimo kwamba Serikali inaongeza vyuo vikuu lakini hakuna mpango/ mkakati wa kuongeza idadi ya wanataaluma. Analosema ni kweli na hili jambo ni la kihistoria huko nyuma miaka ya 1990 kwa muda wa miaka 10 vyuo vikuu vilizuiliwa kuajiri wanataaluma kwa sababu maalum, tulikaa kipindi cha miaka 10 kwa hiyo, haikuwezekana kabisa kuajiri watu wowote kulikuwa na pengo lakini miaka ya hivi karubuni kama mitano, sita iliyopita vyuo vikuu vimeanza kuruhusiwa kuajiri wanataaluma wengine. Katika mwenendo huu tuna mategemeo kwamba mikakati itafanywa, tutapata vijana wahitimu ili kusudi wapelekwe kwenye masomo ili waweze kufaulu na waweze kuwa walimu wazuri. Hivi tunavyoongeza idadi ya wanafunzi katika vyuo vikuu hawa hawa ndiyo tutakaotokana nao ili kusudi waweze kujiunga na vyuo vikuu na wawe walimu. Lakini kwa mfano Chuo Kikuu hiki kipya cha Dodoma tayari baadhi ya wahisani wameonyesha dalili ya kutaka kutusaidia pamoja na vifaa vingine na walimu kwa muda huu wa mwanzoni tunapoanza. Kwa hiyo, mikakati ya kuwapata wanataaluma ipo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine samahani, naona niliwaruka watu wengi, nilimruka kutokumtambua Mheshimiwa Nimrod Mkono, ambaye ndiye aliyekuwa mchangiaji wa kwanza. Nakuomba radhi sana lakini tunatambua mchango wako. *(Makofi)*

Vile vile tulipata michango mingine kutoka katika majadiliano yaliyokuwepo leo hapa asubuhi la kwanza ilikuwa ni hati, idhini ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambalo lilitolewa na Mheshimiwa Susan Lyimo kwamba mpaka sasa baada ya kupitisha ile Sheria Na. 7 ya mwaka 2005 ya kuanzisha Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania. Vyuo vyote vilipewa muda wa miezi 18 kufikia Desemba, mwishoni mwaka 2006 viwe vimetengeneza chata zao. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilianza huo mchakato kukawa na maoni kidogo tofauti na hatimaye Baraza limeunda Kamati Teule ambayo ndiyo

inapitia hizi zote na itapeleka kwenye mapendekezo kwenye Baraza la Chuo mwezi wa tisa mwaka huu na hatimaye watakuwa wamewahi ule muda wa kufikia Desemba. Ninaamini kwamba hili litatekelezwa.

Vile vile Mheshimiwa Lucas Selelii aliuliza juu ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Madini, *Golden Pride* kilichopo Nzega kwamba haoni maendeleo yoyote kuna kitu gani? Nia ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam cha kuanzisha Chuo Kikuu Kishiriki cha Madini cha *Golden Pride* ipo pale pale. Hata hivyo, kasi ya utekelezaji wa mradi huu imekuwa ni ndogo kutokana na sababu nyingi zikiwemo mabadiliko ya mara kwa mara ya uongozi wa *Exit Tanzania Limited.* Uendelezaji wa sehemu zingine za machimbo hivyo kutokuwa na uhakika ni lini mradi wa Kimarekani wa milioni 20, lini mradi huu wa *Golden Pride Project* utamalizika? Tatizo lingine ni ukosefu wa fedha, kiasi cha fedha kinachohitajika ni dola milioni 20 kuanzisha mradi huu. Juhudi bado zinafanyika na *Golden Pride* ili kuweza kuona uwezekano wa kuanzisha chuo hicho.

Mheshimiwa Spika, mchangiaji mwingine alikuwa ni Mheshimiwa Usi Ame Pandu, ambaye alisema lini mamlaka ya elimu itaweza kusaidia Tanzania na Zanzibar kufaidika na mikopo kutokana na mfuko wa elimu. Nasikia kwamba Zanzibar tayari imeshawasilisha maombi yake na kiasi kinachohitajika ni shilingi bilioni 4.2. Lakini wakati huo huo kiasi ambacho mamlaka ya elimu inacho ni kiasi cha shilingi bilioni 4.2 hivyo hivyo. Hata hivyo, uongozi wa mamlaka utawasiliana na wale walioweka hayo maombi.

Mheshimiwa Spika, kuna mmoja vile vile ambaye nilimsahau, nazidi kukumbushwa, kuna Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, alichangia. Vile vile Mheshimiwa Fatma Mikidadi, naomba samahani ya kutokuwataja hapo mapema. *(Makofi)*

Vile vile kulikuweko na swali ambalo liliulizwa na huyo huyo ambaye nimemtaja, anasema kwa nini Mamlaka ya Elimu Tanzania haitoi mikopo kwa shule za Zanzibar pamoja na kwamba uwezo wa kulipa upo? Taarifa tuliyopewa ni kwamba Zanzibar bado haijaomba fedha zozote kutoka Mamlaka ya Elimu Tanzania kwa ajili ya shughuli hizo.

Mheshimiwa Spika, kulikuwepo na swali la *Mlimani City Project* ambayo iko Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kwamba ujenzi wa *project* hauendani na yale yanayotarajiwa na Chuo Kikuu. *Mlimani City Project* ni *project* ambayo wawekezaji wake wametoka Botswana na mradi huo unaendelea mpaka sasa na wamefika kiasi cha kuezeka. Utakuwa na vitu vingi, kutakuwa na *conference facilities,* kutakuwa na *shopping mall,* kutakuwa na *science parks* pamoja na hoteli.

Mheshimiwa Spika, dhana ya kwanza ya mradi huu ni uwekezaji ili kusudi faida watakayoipata kutokana na mradi huu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kiweze kujenga *facilities* ikiwa ni pamoja na mabweni, pamoja na *lecture thietres,* mabaara na vitu vingine. Hiyo ndiyo dhana yake.

Swali lingine, ni kwamba liliulizwa swali na Mheshimiwa Rita Mlaki, kwamba Sayansi na Teknolojia inapewa umuhimu kidogo sana. Sayansi na Teknolojia kwa kweli

haipo mahali pamoja. Hivi mahali pengi kwa mfano, Vyuo vyote vilikuwa vinahusika na mambo ya Sayansi na Teknolojia, *University of Dar es Salaam, College of Education of Engineering and Technology* kule *SUA*. Kuna miradi mbalimbali inayohusisha wakulima sehemu mbalimbali. Kuna ugunduzi hata wa madawa pale *SUA,* chanjo kwa mfano za kuzuia ugonjwa wa kideli kwa kuku, wagundua mashine za kutengeneza mihogo, wamegundua trekta ndogo vile vile na vitu mbalimbali vinafanyika. Lakini pengine kinachokosekana ni ile kutokueleza watu wakaweza wakafahamishwa sababu nini kinachofanyika. Kwa hiyo, kuna *RND institutions* nyingi ambazo zinahusika na hili.

Kulikuwa na swali la kusema wananchi walio wabunifu hao wanatambulikaje na mfano uliotolewa na Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, ni kwamba kuna vijana ambao wanatengeneza bunduki, badala ya kupongezwa wanashikwa na kutiwa ndani. Nafikiri ukishikwa na kutiwa ndani kwa sababu ya kutokufuata sheria maana yake mpaka ukafikie hapo, ni lazima kuwe na utaratibu maalum. Lakini wale wabunifu wa vitu vingine ambavyo vina manufaa sana kwa watu. *Commission of Science and Technology* huwa inatoa tuzo kwa wale ambao wameshinda. Kwa hiyo, wanatambuliwa kwa ajili ya kazi hizo.

Mheshimiwa Spika,suala lingine lilikuwa ni swali lililoulizwa na Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, ambaye amesema vyuo vya elimu ya ufundi vimesahaulika na havina mtetezi. Ningependa kulieleza Bunge lako kwamba hapana havijasahaulika. Mwaka jana ilipitishwa Sheria ya *NACTE* Na. 9 ile ilikuwa mwaka 1997 na sasa hivi vyuo viko chini ya mamlaka hayo na wameanzisha hata programu mpya na kama tulivyoeleza huko nyuma hata kile chuo cha Mbeya kimebadilishwa kutoka *Technical College* na kuwa *Mbeya Institute of Science and Technolodge,* kwa hiyo, vina mtetezi.

Vile vile Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, aliuliza juu ya Chuo cha *Mwalimu Nyerere Memorial Academy* ni kweli chuo kile kwa mwaka 2005 hakikupata fedha za kutosha kilipata milioni 100. Lakini kwa mwaka huu tumetengewa shilingi bilioni 1.25. Kwa hiyo, matengenezo yatafanywa. *(Makofi)*

Vile vile limezungumzwa sana juu ya ubora wa majengo kwamba majengo mengi katika vyuo vikuu ni mabovu. Napenda kusema kwamba ni kweli kuna majengo ambayo ni mabovu. Lakini jitihada zimekuwa zikifanyika na pale ambapo fedha zinapatikana marekebisho ama ukarabati umekuwa ukifanyika na hata mwaka jana tu, vyuo vikuu tisa vilitengeneza ukarabati katika majengo yake na wengine walijenga hata majengo mapya zaidi. Lakini tatizo kubwa ni ukosefu wa fedha. Kwa hiyo, kila inapopatikana fedha ukarabati huu utaendelea ili kuboresha mazingira ambayo vijana wetu wanasomea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile mchana huu imezungumzwa juu ya mazingira ambayo sio mazuri kwa vyuo vikuu na hili limechangiwa vizuri sana na Mheshimiwa Luhaga Mpina, baadhi ya maelezo hayo yameshaelezwa na Naibu Waziri na akauliza vile vile juu ya mambo ya mikopo, posho ya chakula imeshaelezwa. Lakini vile vile aliulizia kwamba je, wale wanaoendelea na masomo ambao kwa mwaka jana walielekezwa kwamba mikopo itakuwa kuwaje. Naomba awe na subira kidogo nitatoa maelezo juu ya

hilo. Lakini vile vile aliuliza uhalali wa kujenga chuo kipya wakati vyuo vingine vina hali ambayo siyo nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa kutoa maelezo ya ziada kwa nini Serikali imeamua kujenga Chuo Kikuu kipya hapa Dodoma. Serikali ya Awamu ya Nne ya Jamhuri ya Muungnao wa Tanzania imekwisha tangaza azma yake ya kuanzisha Chuo Kikuu Dodoma. Lengo ni chuo kitatarajiwa kuanza masomo yake ifikapo Septemba, 2007 na kuwa na uwezo wa kudahili wanafunzi 40,000 pindi ujenzi utakapokamilika. Hoja za kuanzisha chuo kingine cha Serikali nchini imejengwa kutokana na mazingira yafuatayo:-

Kwanza, ongezeko kubwa la wanafunzi wanaohitimu masomo ya sekondari na kuwa na stahili ya kujiunga na elimu ya juu. Hii imezungumzwa sana pamoja na mpango wa *MMES* kwamba miaka michache ijayo tayari tutakuwa na wimbi la vijana wenye sifa hiyo.

Pili, kutayarisha mazingira yanayokidhi changamoto zinazojitokeza kutokana na matokeo ya mpango wa *MMEM* na *MMES.* Tatu, ongezeko la mahitaji ya elimu ya juu, nne, ufinyu wa nafasi katika vyuo vilivyopo kwa sasa hivi, tano, idadi ndogo ya rika la wasomao vyuo nchini ukilinganisha na nchi jirani. Niliona wengi walipochangia leo bado wanatumia ile takwimu ya zamani ya mwaka 1997 kwamba *participation rate* ya Tanzania katika elimu ya juu ni 0.27. Nilipotoa hoja asubuhi hii nilieleza kwamba tumeshapanda tumetoka hiyo 0.27 ya mwaka 1997 na sasa tumefikia 1.2. *(Makofi)*

Ongezeko la nia ya kuwa na jamii iliyoelimika ni muhimu kwa kuongeza chuo kingine kipya. Vile vile kuna changamoto ya utandawazi, sayansi na teknolojia na mambo mengine. Kutokana na uzito wa hoja hizo kwa maendeleo ya Taifa letu, Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia imeunda kikosi kasi ambacho moja ya hadidu za rejea ni kufanya tathmini na upembuzi yakinifu juu ya mpango wa kuanzisha Chuo Kikuu Dodoma kwa kuanzia na jengo la Chimwaga ambalo Serikali imetoa. *(Makofi)*

Kwa kuanza Chuo Kikuu siyo kwamba tumesahau mahitaji mengine ya ukarabati na kuboresha mazingira katika vyuo vikuu vilivyopo. Sasa hivi tuko katika majadiliano na Benki ya Dunia ili kuweza kupata fedha kiasi cha dola milioni 150 kwa ajili ya kukarabati majengo tuliyonayo, kupanua miundombinu tuliyonayo, kupeleka kwenye mafunzo wana taaluma na kuendeleza mahsusi somo la *ICT.* Kwa hiyo, hilo halijapuuziwa, tuna matarajio mazuri kwamba tutapata hizo fedha ili kusudi tuweze kupanua na kuboresha na miundombinu tuliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja zilizochangiwa ambazo nyingi tumezijibu na kama nilivyosema itakuwa ni vigumu kuzijibu kila moja. Mengi yamekwishajibiwa na kama nilivyosema mengine tutayajibu kwa maandishi na kumfikishia kila Mheshimiwa Mbunge. Kulikuwa na moja ambalo lilizungumzwa na Mheshimiwa Susan Lyimo kwamba wanafunzi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na hata Mzumbe wanakosa nafasi za kufanyia mitihani na hivyo kulazimika kufanya mitihani siku za Jumamosi au Jumapili, hii siyo sababu ya kweli.

Mheshimiwa Spika, kinachotokea ni kwamba wanafunzi wa namna hii huwa wanafanya *common courses* sasa wanaweza kuwa wengi sana na kupata wote kwa siku moja inakuwa siyo rahisi, hivyo wao wenyewe kwa kukubaliana wanamweleza mwalimu anayehusika na hatimaye wanachagua siku ambayo wanaona kwamba ni muafaka ili kusudi waweze kufanya mtihani huo. Tatizo ni huo wingi wa wanafunzi na kwamba ni *course* anafundisha mwalimu mmoja hawezi kutunga mitihani mingi kwa wakati mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile kulizungumzwa juu ya kwamba hata walimu wengine wanapata shahada zao *online*. Sasa sielewi *concept* hiyo kama tunaielewa sawa sawa. Maana yake *online* inawezekana kwamba siyo dhambi, lakini ungesema wanapata shahada kutoka Chuo ambacho hakitambuliki, hilo linaeleweka. Sasa hivi wewe unaweza kukaa hapa mka-*organize lecture* ikawa inatolewa New York, ninyi mmekaa hapa, *which is also moreless online,* wewe ukawa uko hapa.

Lakini vile vile unaweza kuwa umekaa hapa unapata *instructions* kutoka mbali kabisa na unaendelea na masomo yako na wewe unawasiliana nao na unaendelea na masomo yako. Lakini wale ambao wanapata shahada zao kutoka kwenye vyuo ambavyo havitambuliki hao ndiyo tunaona kwamba hiyo ni kasoro na bahati nzuri tunayo *Accreditation Committe* ya *Tanzania Commission of Universities* ambayo inashughulikia wale wote wenye vyeti ambavyo havitambuliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu leo asubuhi nimesema kwamba mwaka huu uliokwisha, *TCU* ilipokea maombi ya tathmini ya vyeti 82. Katika vyeti 82 ni vyeti 60 ndiyo vimeonekana kwamba ni halali. Kwa hiyo, kazi mojawapo ya *TCU* ni hiyo na wanafanya kazi hiyo kwa bidii zao zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile kumezungumzwa umuhimu wa kuanzisha Vyuo Vikuu katika kila Kanda. Nafikiri majibu ambayo alitoa Naibu Waziri yanaendana na hilo ombi na kama alivyoeleza kadri uwezo unavyozidi kupatikana tutapeleka hivi vyuo katika mikoa ambayo kwa kweli haina vyuo vikuu vyovyote ambavyo ni *residential.* Mikoa hii mara nyingi iko pembeni, kama vile Mtwara, Sumbawanga, Kigoma na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, sehemu hizi zitapewa upendeleo maalum, kila inapotokea nafasi ya kuweza kujenga mahali pengine. Kulikuwa na jambo ambalo lilizungumzwa, nafikiri na Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji, anasema kwamba alionyesha malalamiko yake makubwa juu ya bodi ya mikopo kwamba utendaji wake hauridhishi. Nafikiri Naibu Waziri ameeleza, sababu ambazo hiyo bodi ya mikopo kwa kuanzia ilipata matatizo ikiwa ni pamoja na upungufu wa wafanyakazi, kutokuwa na vifaa muhimu na alishauri kwamba hiyo bodi ivunjwe. Sasa nafikiri kwamba kila kitu kipe muda wake kwanza kabla hujafikia azma kama hiyo. *(Makofi)*

Vile vile kulitolewa maombi juu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam juu ya mabweni kwamba naomba sehemu hizo ziweko na *liftm* hasa *hall number five and six.*

Nilipotembelea pale mwezi Mei, 2006 waliniambia kwamba tayari wameshaliweka hilo kwenye bajeti na kwamba watajitahidi kupata *lift* kwa ajili ya vijana.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile, tulizungumzia juu ya watu kubebana, badala ya chumba cha watu wawili au wanne wanalala mara mbili ya hilo, hili sio tatizo la chuo chenyewe, haya ni matakwa ya wanafunzi wenyewe. Mara nyingi wengine kwa ajili ya kuokoa fedha walizonazo, wanakubaliana mmoja anasema wewe nitaku-*accommodate,* wanakuwa pale ni mapatano yao, sio kwamba haya yanatoka mahali pengine. Lakini uongozi wa chuo daima wamekuwa wakijitahidi sana kujaribu kurekebisha hali hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza hayo, naomba sasa nichukue nafasi hii kueleza yafuatayo kuhusu bodi ya mikopo. Juzi wakati najibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Susan Lyimo, nilitoa jibu kwa ufupi na hivyo inaelekea kwamba halikueleweka, hivyo naomba nichukue nafasi hii nitoe maelezo ya ziada kama ifuatavyo, nikianzia na historia ya bodi ya mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uchangiaji katika elimu ya juu kwa kupitia bodi ya mikopo kuna historia iliyoanza huko nyuma kabisa. Kwanza kabisa utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu, ni utekelezaji wa sera ya uchangiaji yaani *cost sharing policy* ya mwaka 1999. Bahati nzuri hii *policy* mimi nilikuwa ni Mwenyekiti wa Kamati hiyo, kwa hiyo, nakumbuka yale yote yaliyopo na nitayanukuu baada ya muda kidogo. Lakini kabla ya mwaka 1988, Serikali ilikuwa ikigharamia gharama zote za elimu ya juu, ikiwa ni pamoja na posho ya elimu ya juu, nauli na fedha za tahadhari.

Kipindi cha kuanzia mwaka 1988, kulijitokeza migogoro ya wanafunzi katika vyuo vya elimu ya juu ambayo sehemu kubwa ilikuwa ni malalamiko yaliyohusu huduma duni, ikiwa ni pamoja na chakula kwenye *cafeteria,* katika elimu ya vyuo vya elimu ya juu na katika kukabiliana na migogoro hii, Serikali iliona ni vyema kujiondoa katika uendeshaji wa *cafeteria* za vyuo vikuu na badala yake wanafunzi walipewa fedha taslim ili waweze kujipatia chakula kutoka kwa waendeshaji binafsi ya *cafeteria* hizo.

Mheshimiwa Spika, hata baada ya wanafunzi kupewa fedha za kujinunulia chakula palijitokeza madai ya fedha kwamba hazitoshi na wakati huo uwezo wa Serikali kugharamia kila kitu ulikuwa unazidi kupungua. Hivyo katika hatua inayofuata, ulikuja uchangiaji wa gharama za elimu juu, kutokana na sababu za kibajeti za kugharamia elimu ya juu, ikilinganishwa na mahitaji Serikali iliamua kuwa wanafunzi wa elimu ya juu, wachangie gharama za elimu yao. Hii ni kwa sababu mhitimu wa elimu ya juu, hunufaika zaidi kuliko jamii na Serikali ambayo inamgharamia elimu hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uchangiaji gharama za elimu ya juu ulipangwa kufanyika kwa awamu tatu, kuanzia mwaka 1992,/1993, hii ilikuwa ni awamu ya kwanza ambapo wanafunzi walitakiwa kuchangia nauli ya kuja na kurudi toka chuoni, fedha za tahadhari yaani *quotion money* na michango ya wanafunzi, hizi ni *student union fees.* Gharama hizi hazikuwa kubwa sana na kila mwanafunzi aliweza kumudu yeye mwenyewe. *(Makofi)*

Awamu ya pili ya uchangia ilikuwa ni mwaka 1994/1995, ambapo ilihitaji kila mwanafunzi achangie gharama za chakula na malazi. Sababu ya kutoa hili ni kwamba huyu mwanafunzi hata kama asingekuwa chuoni angekuwa huko kwake nyumbani, bado yeye angehitaji kulala na kula. Kwa hiyo, wakasema hii gharama, afadhali iwe ndio mchango wa mwanafunzi, kwa hiyo, gharama ya chakula na malazi. Gharama hizi kidogo zilikuwa kubwa kuliko zile za kwanza na ilidhihirika kwamba si kila mwanafunzi angemudu gharama hizo, kwa kutambua uwezo mdogo wa kiuchumi wa wanafunzi pamoja na wazazi na walezi wao, Serikali ilianzisha utaratibu wa kutoa mikopo kuwawezesha wanafunzi wenye uwezo kitaaluma na ambao hawana uwezo kiuchumi kunufaika na elimu ya juu kuwapatika mkopo.

Mheshimiwa Spika, awamu ya tatu ya uchangiaji ilianza kutekelezwa mwaka 2005/2006, kupitia bodi ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu iliyoanzishwa kwa Sheria Na. 9 ya mwaka 2004. Mikopo ililenga pamoja na mambo mengine kuwawezesha wanafunzi waliofaulu vizuri zaidi, lakini hawana uwezo wa kujiunga na elimu ya juu. Faida nyingine za mikopo kwa wanafunzi ilikuwa ni pamoja na yafuatayo:-

(1) Kuwafanya wanafunzi wawe na uwezo wa kuwajibika kuhusu mambo yanayowahusu hususan matumizi ya fedha na mali ya umma.

(2) Kuwezesha hosteli na *cafeteria* za Vyuo Vikuu kuendeshwa kibiashara na kupunguza matumizi ya ziada.

(3) Kuongeza ushindani kitaaluma miongoni mwa wanafunzi. Katika awamu hii mwanafunzi alihitajika kugharamia pamoja na gharama za awamu ya kwanza na ya pili, gharama za ada ya mafunzo, mafunzo kwa vitendo, utafiti, vitabu na viandiko pamoja na mahitaji maalum ya vitivo. Uzoefu uliojitokeza katika kutekeleza awamu ya tatu ya uchangiaji, kupitia bodi ya mikopo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, waliokopesha mwaka 2005/2006 sio wote waliolengwa na sheria ya mikopo na kanuni zake, hii ilitokana na uchanga wa bodi na kutopatikana kwa wakati chombo cha kutambua uwezo wa kiuchumi wa muombaji. Kwa mujibu wa sheria ya mikopo, mkopo unapaswa kutolewa kwa mwanafunzi mhitaji na mwanafunzi mhitaji kwa kanuni za mikopo ni yule ambaye ni yatima, ni mlemavu au mwenye wazazi maskini na walemavu, anayetoka katika familia yenye mzazi mmoja maskini, anayetoka katika makundi yaliyotenzwa na anayetoka familia yenye kipato duni.

Mheshimiwa Spika, kuibuka kwa dhana kuwa mkopo ni ruzuku, ambayo matokeo yake ni shinikizo la kila mwanafunzi kutaka kukopeshwa asilimia 100 hata katika maeneo ambayo walikuwa wamelipiwa wenyewe. Pia na udanganyifu wa wanafunzi kwa kujiandikisha zaidi ya chuo kimoja, kubadili majina, kubadilisha akaunti, kuomba mkopo wakati ameshalipiwa na mzazi ama mlezi, shirika na kadhalika, yote haya yalikuwa ni baadhi ya matatizo, sasa nini taratibu za utoaji wa mikopo katika mwaka wa masomo 2006/2007?

Kwanza ningependa kutamka kwamba *style* ya utoaji mikopo kwa mwaka 2006/2007, kwa wanafunzi wanadailiwa katika vyuo vya elimu ya juu yaani vyuo vya umma na binafsi utazingatia sera ya elimu ya juu ya mwaka 1999 na sheria ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, ambayo ni Na. 9 ya mwaka 2004.

Kwa mujibu wa sera ya elimu ya juu Ibara ya 6.3.2(vi) , mwanafunzi anayestahili kupata mkopo ni yule aliyefaulu katika kiwango cha juu na ningependa kunukuu: "*Full or passion sponsorship shall be awarded to academically outstanding student, these awards shall be offered by the government through the Ministries responsible for Higher Education or Parastatal Organization Trusts,Foundations, Professional Boards, Non Governmental Organizations and all individual, their warding authority shall be signed on which disciplines for example science, medicine and all other groups.*"

Mheshimiwa Spika, *these warding authority would sign on which their award should be given. Awarding authorities and institution may establish their warding criteria and procedures.*

Mheshimiwa Spika, hivyo kutokana na maelezo hayo hapo juu, Serikali itaendelea kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu katika vyuo vikuu vya umma na binafsi kwa utaratibu ufuatao:-

(1) Kwa kuwa Serikali haina uwezo wa kusomesha kila mtoto kwa elimu ya kiwango cha chuo kikuu, inatulazimu tutumie uwezo mdogo tulionao sasa hivi. Kwa sasa msisitizo utakuwa ni kuwasomesha watoto waliofaulu vizuri zaidi yaani wavulana katika kiwango cha daraja la kwanza na wasichana katika kiwango cha daraja la kwanza na la pili, ili kuandaa wataalam wengi zaidi kwa maendeleo ya Taifa. Ningeomba kusisitiza hapa kwamba mikopo hii ni sawa na *scholarship* ambazo duniani kote hutolewa kwa wanafunzi waliofanya vizuri zaidi. Hata tunaletewa *scholarship* hapa kutoka Uingereza, Newzealand na Australia, wanatuambia wanataka vijana waliofaulu kwa kiwango hiki, kwa hiyo ndiyo hali ya ushindani.

(2) Uwezo mdogo uliopo, utumike kusomesha watoto katika kiwango cha elimu ya juu ya Chuo Kikuu kwa Shahada ya Kwanza tu, kwa sababu ya ukosefu wa uwezo.

(3) Ikitokea kwamba nafasi katika Vyuo Vikuu vya Umma imejaa lakini bado kuna wanafunzi waliofaulu vizuri na wamekosa nafasi, Serikali itawagharamia ipasavyo wanafunzi husika katika vyuo vikuu binafsi nchini. Kwa maana nyingine hii inatoa nafasi ya kupanua uwigo wa udahili. *(Makofi)*

(4) Kwa kuwa taratibu za udhamini zimekiukwa na kusababisha wanafunzi wasiostahili kupata udhamini wa Serikali, wanafunzi hao wataendelea na udhamini huo hadi wamalize masomo yao. *(Makofi)*

Hata hivyo, kuanzia sasa Serikali itahakikisha kwamba wanafunzi watakaodhaminiwa na Serikali ni wale tu wenye stahili hiyo kwa mujibu wa Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo hayo hapo juu ni dhahiri kwamba kigezo kilichowekwa ni kile cha kufaulu vizuri yaani *out standing academic performance* na ni dhahiri kwamba Serikali itawagharamia wanafunzi waliofaulu vizuri katika Vyuo Vikuu vya Umma na binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kauli hii inasahihisha ile kauli ambayo niliipata muda mfupi sana kuieleza na kwa hiyo, nafikiri kwamba litakuwa limeeleweka wale waliokuwa wanasema kwamba wale wanaosoma kwenye Vyuo Vikuu binafsi hawatagharamiwa, hapana wana nafasi ya kuchukua mikopo sawa na wengine ili mradi awe amefaulu kwa kiwango hicho ambacho kimetajwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo napenda nimalizie kwa kuwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao na naomba tuendelee kushirikiana ili kuboresha Elimu Juu, Sayansi na Teknolojia nchini kwa lengo ya kukuza rasilimali watu kwa ajili ya maendeleo endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja hiyo ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia kuamua kwake itabidi tuingie katika Kamati ya Matumizi.

## KAMATI YA MATUMIZI

## MATUMIZI YA KAWAIDA

### FUNGU 68 - WIZARA YA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

Kifungu 1001- *Administration and General* ... ... 2,634,943,800/=

**MWENYEKITI:** Tutaorodhesha, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa keti, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, keti, Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji, keti, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbi, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi na Mheshimiwa masolwa Cosmas Masolwa. Nimefunga orodha hapo kwa kifungu hiki, sasa tunaanza, nitakuwa nachanganya changanya ili tupate Wabunge wa Upinzani na wa CCM.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, katika hotuba yetu ya upinzani tuliomba na naomba nitumie kifungu cha 68, programu 10, *sub vote 1001,* kifungu kidogo zaidi cha 250 100. Tulikuwa tumeomba Waziri atueleze ndugu zetu ambao wana ulemavu na huwa wanapata shida sana katika kujiendeleza, lakini kwa bahati nzuri wanafikia kiwango cha kuingia Chuo Kikuu. Lakini wanapofikia hatua hiyo inakuwa vigumu sana kwa sababu yanayohitajika kuwawezesha kushiriki ni ghali sana na mathalani, chombo cha kuandikia tu *brailer* ni shilingi 500,000. Mkichukua na asiyeona tena hata kwa kutembea tu ile fimbo, ni karibu dola 20 mpaka 40, sasa haya yanakuwa ni ghali sana na tuliomba Waziri atusaidie kwamba hawa kwa sababu wana uwezo lakini Mwenyezi Mungu hawakuwajalia kwa maana ya viungo na mara nyingi hata wazazi huwa hawapendi wasome, hata jamii huwa haipendi kuwasaidia sana kwa sababu ya utamaduni, tulitaka wapate *full sponsorship* yaani wapate ufadhili kamili wa Serikali. *(Makofi)*

Sasa tulitaka Waziri atuambie je, hawa watashiriki vipi na mpango gani? Nime-*check* kitabu hiki, nime-*check* kitabu cha nne, sikuona kinachowasaidia katika kuwaingiza na fomu zinazozungumziwa zinazungumzia sisi wa kawaida ambao tunaweza tukatafuta njia nyingine, lakini si kwa njia ya hawa. Kwa hiyo, tulitaka kwa uhakika hawa wenzetu wanaweza kupata msaada wa namna gani wa *full sponsorship*.

**WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale katika *Loan Board* hii haiji katika fungu la kawaida, inakuwa kwenye *Loan Board* na hiyo ni kifungu kingine kabisa na wala hakiko katika sehemu hii.

Kifungu hiki kipo katika *Higher Education* na huko ndiko kwenye mikopo, sasa hawa katika mikopo inatambua kabisa kwamba wale watakaofikiriwa na kupewa kipaumbele, ni pamoja na wale yatima, wale ambao ni *disabled or from disabled poor parents,* ama anatoka kwa mzazi mmoja ambaye hana uwezo, ama anatoka *from marginalize and disadvantage groups* na haya tunayafahamu *or* hizo fomu za *low income*.

Kwa hiyo, wale walemavu wamewekwa hapa lakini mahitaji ya walemavu kama ulivyosema ni makubwa, kwa mfano, *trycycle* ambayo inaendeshwa kama kipikipiki. Ile ni gharama sana, lakini kuna vingine kama vile *hearing edges* zile si gharama kubwa lakini kuna wale vile vile vipofu, zile zinaitwa nini…

**WABUNGE FULANI:** *Brailing Machine. (Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** *Brail machine* nazo zile ni gharama. Bodi inawajibu wa kuweza kuwafikiria juu ya maombi hayo kulinga na hali halisi. Lakini sehemu zingine vifaa kama hivyo vimekuwa vikitolewa kwenye vyuo ili kusudi yule anapomaliza anaondoka kwa sababu ni vitu vya mafunzo, basi aweze kutumia vile vingine anapokuja pale. Kwa hiyo kuna *alternative* hizo na kwa kuwa ni jambo la bodi, nitalipeleka kwenye bodi kusudi waweze kuliangalia.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi, ni fungu hilo hilo *sub vote 1001, item* 250100.

Mheshimiwa Waziri wakati anaeleza hapa ametoa maelezo mazuri kidogo kuhusu mikopo, lakini mimi ningependa kupata ufafanuzi kwa sababu zifuatazo, kuna hiki kitu kinaitwa hii *min test,* hii inasema kuwa unapewa asilimia 40 halafu unajieleza wanajaribu kukuchunguza. Lakini la msingi hapa kwamba ni *timing* ni kitu muhimu sana. Tuchukulie mfano labda wa mara hii, mwisho kupeleka maombi haya inaweza ikafikia labda tarehe 31 Julai na kuingiza wanafunzi chuoni inaweza ikawa ama ni kati ya mwezi Agosti au kati ya mwezi Septemba.

Sasa ikiwa kwa mfano yamekwenda maombi 20,000 ya watu wanaotaka kuingia Chuo Kikuu kwa kupewa mikopo hii. Hivi ni *mechanism* gani itatumika ikiwa kweli tunataka kutenda haki kufanya *vetting* ya hawa watu kwa sababu kitakachotegemewa hapa ni fomu yake aliyojaza na Waziri amekiri sasa hivi hapa alipokuwa akitoa maelezo kuwa uko uwezekano wa watu kufanya *cheating*.

Sasa tutajuaje kuwa huyu aliyeomba anastahili kweli kupewa na huyu hastahili kupewa ikiwa hatukutoa muda wa kutosha katika jambo hili? Tungependa atupe maelezo na ni kwa nia nzuri kwa sababu hii ni *whisper* ambayo watu wanayazungumza vibaya, tungependa atupe maelezo ambayo yatamsaidia yeye na yatawasaidia wananchi kuelewa kulikoni hasa.

**WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mweyekiti, napenda kutoa ufafanuzi kwa Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, *min testing* hii ni *software,* ni chombo cha kwenye kompyuta ambacho tayari kimeshakuwa *designed,* ili kuweza kufanya tathmini ya taarifa iliyojazwa kwenye fomu. Ni kweli kwamba safari hii majibu ya mitihani ya *fomu six* yalichelewa, matarajio yangu ni kwamba huko tunakokwenda kuanzia mwaka kesho, kwa sababu tulikuwa tunakwenda tunamaliza hii *double court* kwamba watafanya mitihani yao mapema, ili mitihani hiyo iweze kusahishwa, ili vijana wapate nafasi ya kuweza kuomba kwenye Vyuo Vikuu na Vyuo Vikuu viweze kukaa mapema ili majibu ya kuchaguliwa ama hapana yaweze kutolewa kwa muda muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taratibu zake kwa bahati mbaya udanganyifu sisi wote ni wanadamu, lakini hii sio taratibu ya mara ya kwanza *min testing* ilikuwepo siku nyingi wale watu wanaofahamu hata zamani ilikuwa kama umeshindwa kulipa ada kulikuwa na utaratibu wa kwenda kutoka kijiji kwa sababu wale ndio wanaokufahamu, una kuku wangapi, una ng'ombe wangapi, una shamba ngapi, itakwenda kwa sub chief, itakwenda kwa *DC.*

Sasa wote hawa watakuwa ni waongo, hiyo itakuwa ni bahati mbaya kwa sababu kila mmoja anajaza kwa nafasi yake anapeleka juu. Sasa kila mmoja kama atakubali

kufanya hivyo, basi hiyo itakuwa ni bahati mbaya. Lakini tunategemea kwamba hilo halitakuwa tatizo kubwa, kama lipo basi tutakabiliana nalo linavyozidi kuja. *(Makofi)*

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, wakati natoa hotuba yangu nilizungumzia suala la waandisi wanaochukua Stashahada ya Juu kutahiniwa au kutungiwa mitihani na Baraza la Mitihani la Taifa. Sasa nilitaka Mheshimiwa Waziri anielezee kuna utaratibu gani, huu utaratibu utaisha mpaka lini? Kwa sababu miaka ya nyuma nikiangalia umezua zogo sana kwenye vyuo kama hivi *Dar es Salaam Technical*, *Mbeya Technical* na mwaka jana nafikiri kuna wanafunzi walifukuzwa kwa ajili ya kugomea mitihani kama hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa utaratibu huu utaisha mpaka lini na ni sababu gani zimepelekea kuwa wawe wanatungiwa mitihani hiyo na wakati ni taasisi ambayo zinajitegemea, naomba maelezo tu hayo basi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Utaisha mpaka lini au utaendelea mpaka lini au?

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utaendelea mpaka lini?

**WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi kwa Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri anachozungumzia ni lile jambo ambalo lilikuwepo pale *Dar es Salaam Institute of Technilogy* pale kulikuwa na kozi za aina mbili tofauti, iko ya hiyo Stashahada ambayo ilikuwa ni *Diploma* na hii toka mwanzo sheria ilipoanzishwa walikuwa chini ya *National Examinations Council*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii kozi imekuwa *phased out* kwa sasa hivi lakini ikaja kuanza hii nyingine ambayo ni *equivalent to Bachelors* ya *Engineering.* Sasa hawa wako chini kama utaratibu wa vyuo vingine vyovyote. Vyuo Vikuu vyote haviendi chini ya utaratibu wa *National Examination Council,* wanatunga mitihani yao, wanairatibu na kutoa mitihani na kusahisha na kila kitu. Sasa ile imeshakwisha, pale sasa *DIT* wataanza sasa kutoa mitihani yao wenyewe na kusahisha na kutoa majibu.

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri na kuna chuo hicho cha Mbeya ambacho nafikiri na wao wanachukua *course* kama hiyo. Je, kule kuna utaratibu gani kwa sababu ni kuangalia malengo ya Baraza la Mitihani kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kuna programu hiyo ya kuendelea kuwatungia mitihani wahandisi wa Stashahada ya Juu, sasa na ukiangali Stahashahada ya juu ni hiyo *Mbeya Technical,* sasa utaratibu huko *Mbeya Technical* ukuoje?

**WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutuoa ufafanuzi wa swali la pili la ndugu Masolwa Cosmas Masolwa kama ifuatavyo, Vyuo vyote hivi viwili viko chini ya utaratibu mmoja

isipokuwa hii ya Dar es Salaam itatangulia kumaliza *phasing out* ya ile *Diploma* na wale wanaendelea, lakini wataendelea kutahiniwa wale wa kule Mbeya watandelea kutahiniwa na *National Examination Council* mpaka watakapotoka kwenye *line. (Makofi)*

**MHE. FATMA ABDULHABIB FEREJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante najielekeza katika *vote 68,* programu ya 10, *sub vote 1001* kifungu kidogo 250100. Wakati nachangia hoja ya Wizara hii leo hii niliuliza swali na nilimtaka Mheshimiwa Waziri atueleze ni kiasi gani cha hasara Serikali imepata kutokana na utendaji mbovu wa bodi ya mikopo kwa kulazimika kukopa fedha ili kulipa gharama ambazo hazikutarajiwa au ambazo hazikuwa *budgeted for?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu hili sijajibiwa, naomba maelezo.

**WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi kwa Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli aliuliza hilo swali lakini nilikiri hapa kwamba kwa muda tuliokuwa nao ilikuw si rahisi kuweza kujibu kila mmoja. Lakini Bodi ya Mikopo ilipoanza mwaka jana ilitegemewa kutoa mikopo kwa wanafunzi 33,000 na fedha zilizokuwa zimetengwa ni shilingi bilioni 32.5 lakini kufika Januari ikaonekana kwamba wahitaji walikuwa wengi zaidi na ndiyo maana ikalazimika kutoa mikopo kwa wanafunzi 42,729 kwa kukopa zaidi fedha shilingi bilioni 30 na hivyo kufikia kiasi cha jumla ya shilingi bilioni 62.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama fedha za ziada zilizokopwa zile ndiyo unaweza kuzifanyia hesabu kwa sababu hizo zimekopwa na riba yake ni 15% zile shilingi bilioni 30, kwa hesabu za haraka naweza kusema ni shilingi milioni 450.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *Vote 68, Program 10, Sub Vote 1001,* Mshahara wa Waziri, Kifungu namba 250100.

Mheshimiwa mwenyekiti, katika hoja zetu ambazo tuliziwasilisha kwa Waziri kwamba tunaomba atutolee tamko ilikuwa ni hii mojawapo ya Mikopo kwa Wanafunzi ambapo wale *private* walipewa mikopo nusu wameshindwa kumalizia kwa sababu mikopo hiyo ilisitishwa, wengine wamekataliwa kufanya mitihani, wengine wamefukuzwa na wengine wako kwenye hatihati ya kufukuzwa. Kwa hiyo tunaomba Mheshimiwa Waziri atoe tamko je, anasemaje juu ya hilo?

**WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ufafanuzi kwa Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, juu ya mikopo ya wanafunzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyofahamu sijapata taarifa yoyote kwamba wanafunzi wowote ambao wamekataliwa kufanya mitihani au wamefukuzwa chuoni,

isipokuwa kilichojitokeza wanafunzi wa Mzumbe kama majuma matatu yaliyopita waliandamana kuja hapa kwa kusema kwamba Bodi ilikuwa haijawapa mikopo.

Baada ya kuwasiliana na uongozi wa Chuo tuliwaambia warudi wakaendelee na Chuo kiwape hiyo *cooperation* na kwamba baada ya kuulizia tuliaambiwa kwamba baadhi yao wale kwa kweli walikuwa wamejiandikisha kama *private candidates* kwamba wangekuwa wamejilipia wenyewe lakini tukawaambia kama ipo kesi waende kwenye Bodi ya Mikopo watasikilizwa.

Lakini vile vile juzi tulipata malalamiko kutoka kwa wanafunzi wa *KCMC* ambao nao walitaka kuja hapa Bungeni ili kusudi waeleze masikitiko yao kwamba hawajapewa mikopo. Wao wamesema wanayo barua kabisa waliyoandikiwa na Bodi ya Mikopo kwamba wangelipiwa malipo yote katika malipo ya shilingi milioni 3.6 walikuwa wamelipwa shilingi milioni 2.5 kwa hiyo walikuwa wanadai shilingi milioni 1.1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwashauri waende kwenye Bodi ya Mikopo na barua hiyo ya ushahidi siku ya jumatatu kule Dar es Salaam na ninawashukuru makundi yote mawili wamekuwa wasikivu na wamefuata maagizo na kama ni kweli walikuwa wameahidiwa basi taratibu zitafuatwa na watalipwa fedha zao. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimwia Waziri kwa majibu yanayotosheleza kabisa. Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi karibu.

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni programu hiyo hiyo ya 10 *Sub Vote 1001* Kifungu 250100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipomwandikia Mheshimiwa Waziri asubuhi niliuliza tu kitu kidogo kwamba watumishi wa vyuo vikuu hasa wanataaluma mishahara yao imeongezwa kwa 100%, 50% Januari wakalipwa mwezi huu wanatakiwa walipwe 50% nyingine. Watumishi Uendeshaji hawakulipwa chochote mpaka hivi sasa je, yako maelezo ya tofauti hizi? Maana tukitaka *productivity* iende vizuri katika sehemu hizi ni bora uboreshaji wa maslahi ya watumishi katika vyuo hivi ukaenda sambamba na zile za wanataaluma, nitaomba maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili linahusu hii Sheria ya utoaji mikopo, sheria hii mwaka 2004 ilipokuja ilikuja kama *Government Students Loan Scheme* lakini baadaye ikakataliwa ndani ya Bunge ndiyo ikaitwa *Higher Education*. Tukafikiri kwamba Sheria ile sasa ingebadilishwa ndiyo ingeleta zile tofauti ambazo zimekuwepo, nampongeza Waziri amekubali kwamba sasa wameliona hilo watatoa mikopo kwa wanafunzi wanaokwenda vyuo vyote, kwa hiyo, tutakuwa na kitu kinachoitwa *Public Private Partnership* wote watapata.

Lakini ili hili liende vizuri na asilete mkanganyiko ule ambao ulikuwa unapingana na sehemu ya tatu ya Katiba ya nchi hii naomba Waziri atoe tamko kama yuko tayari sasa kuibadilisha sheria hii kuileta Bungeni na kuifanyia marekebisho maana ilivyo sasa haifai kwa matumizi yake ya sasa. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nadhani la muhimu ni kutoa ufafanuzi katika hatua ya Kamati, kudai jambo libadilishwe sheria ni nje ya utaratibu kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri hebu toa ufafanuzi tu kuhusu hayo mawili.

**WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi kwa maswali mawili ambayo ameuliza Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hili la mishahara ya waendeshaji katika vyuo vikuu bila shaka wakati tunaanza kutoa majibu Mheshimiwa alikuwa hajafika lakini Naibu Waziri ametolea maelezo hayo ya kwamba jambo hili limeshafikishwa Serikali liko katika Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na tumeahidiwa kwamba linafanyiwa kazi ili kurekebisha hali hii. La pili, juu ya Sheria ya Mikopo, asubuhi nilipotoa hoja yangu nimelieleza kabisa kwamba tumegundua kwamba kuna vipengele vinavyopingana na tumeshatoa tayari nia ya kutaka kuisha hili kwa hiyo hili tunategemea kwamba litaletwa katika Bunge la mwezi wa 10 mwaka huu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, ikiwa ni kubishana tu katika hatua hii basi nakupa nafasi hii ya mwisho, unaruhusiwa mara mbili tu.

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina sababu ya kubishana, ni ufafanuzi mzuri unaohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi waendeshaji pamoja na wanataaluma wa vyuo hivi wote ni watumishi wanaofanya kazi chini ya *Institutions* moja moja ambazo zimetajwa kwa vyuo vikuu, lakini wakati Rais alipoteua Tume mwezi Oktoba na Novemba, 2005 aliteua Tume ile ifanye kazi kwa maslahi ya watumishi wote wa Vyuo Vikuu *irrespective* kama ni wanataaluma au ni watumishi uendeshaji.

Naomba ufafanuzi kwa nini hazina ilipoandika barua ikakubali yale malipo ya wanataaluma yatekelezwe na kupeleka Utumishi yale malipo ya watumishi uendeshaji, ni ufafanuzi huo tu unaotakiwa.

**MWENYEKITI:** Siwezi kuendeleza kitu kama malumbano kwa sababu Waziri kisha jibu liligundulika na linafanyiwa kazi na Wizara ya Utumishi, kwa hiyo, tofauti hiyo hivi sasa Serikali inairekebisha. Kwa hiyo, kama kulikuwa na *oversight* na inarekebishwa kuendelea kudai maelezo jibu litakuwa ni lile lile kwamba Serikali inarekebisha. *(Makofi)*

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa jambo nililotaka kusema ndiyo hili nililopewa maelezo fasaha sina la kusema. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *Vote 68, Program 10, Sub Vote 1001,* Kifungu 250100, mimi nahitaji tu ufafanuzi kutokana na maelezo ya Mheshimiwa Waziri inanisikitisha jinsi ambavyo inaonyesha Serikali ina *skip* wajibu wake katika elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ya Mheshimiwa Waziri yanasema kwamba watadhamini wanafunzi wa kiume waliopata *division one* na wanafunzi wa kike waliopata *division one* na *two.*

Sasa mimi naomba anieleze kuhusiana na wale wavulana waliopata *division two* na wasichana ambao wamepata *division three* ambao kwa viwango vyetu sisi wamefaulu na kwa kuzingatia vile vile kwamba Tanzania ni nchi ambayo ina watu maskini sana hawawezi ku-*afford* kujilipia *private universities.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba atoe tamko la Serikali kwamba wanafunzi wetu wajue sasa tunakwenda wapi tukipata *division two* au *three, what next*. Nashukuru.

**WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ufafanuzi kwa Mheshimiwa Halima Mdee, juu ya hatma ya wale ambao watakuwa nje ya hayo madaraja mawili, lakini kwa kulieleza hilo pengine nitoe takwimu tu kwa mwaka huu uliokwisha vijana waliomaliza kidato cha sita walikuwa ni kama 21,000 wale waliofaulu kati ya Daraja la I na la III walikuwa ni 11,900 ambayo ni 86.7% au vinginevyo. Sasa katika hawa, hawa wa daraja la II ni wengi sana na daraja la III ndiyo usiseme.

Kwa hiyo, hakutakuwa na upungufu wowote kwa hawa wanaojaza nafasi ya elimu ya juu na hii ndiyo maana ya *outstanding academic performance* kwa maana ya kwamba kile unacholipa ni lazima kiwe na *value* lakini hawa hawakataliwi, vyuo vikuu vina nafasi yake ya kudahili watu hata kushuka chini zaidi. Lakini kwa ajili ya mikopo taratibu ni tofauti. Nafikiri nimeeleweka. *(Makofi)*

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona maswali yangu ambayo nilitaka kupata ufafanuzi yameshapatiwa, kwa hiyo, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ili pia na mimi nipate ufafanuzi kutoka kwa Waziri kwa yale ambayo nataka kuyazungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilichangia kwa maandishi leo asubuhi katika hotuba hii ambayo Mheshimiwa Waziri aliitoa asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja langu kubwa ambalo nililisema nilitaka maelezo Wabunge wenzangu wayasikie lakini pia na Watanzania wayasikie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu Mzumbe pamoja na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam zimepunguziwa bajeti zake, Chuo Kikuu cha Mzumbe kimepunguziwa bajeti kwa 13%, mwaka jana kilipewa shilingi bilioni 8.8, mwaka huu kikapangiwa shilingi bilioni 7.7 ikiwa ni pungufu ya shilingi bilioni 1.1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini *DIT* kilipewa shilingi bilioni 3.7 mwaka huu kikapewa shilingi bilioni 3.2 ikiwa ni pungufu ya shilingi milioni 516. Sasa mimi nilisema katika utaratibu wa Bajeti ninavyoelewa tuna bajeti kwenda mbele hatubajeti kurudi nyuma *unless* kuwe na sababu za msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia hapa tulikuwa tunazungumza kwamba tunataka tusukume maendeleo ya elimu katika nchi hii, wamezungumza wenzangu katika taarifa mbalimbali kwamba tunataka tuwamotishe walimu, tuwamotishe pia wafanyakazi wa vyuo hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi ninavyoelewa kwa kupunguza bajeti za vyuo hivi kwa vyovyote vile kutakuwa na athari katika uendeshaji wa vyuo hivi kwa sababu kuna shughuli ambazo zilikuwa zimepangwa wakitegemea kwamba hizi pesa zitapatikana na kwa kupunguzwa maana yake kwa vyovyote vile ni lazima program za vyuo hivi ziharibike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nilikuwa naangalia vyuo vingine vimeongezewa hela kwa kati ya 40% mpaka 85% kama vyuo vingine vimeweza kuongezewa pesa kwa kiasi hicho kulikuwa na sababu gani ya kupunguza pesa za vyuo hivyo kurudi nyuma na mimi ningefikiri kwamba afadhali zingebaki vile zilivyokuwa mwaka jana kuliko kuzipunguza kwenda chini zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atoe maelezo wananchi wayasikie na wanapoona kwamba pengine vyuo hivi vinashindwa kuchukua wanafunzi wengi zaidi na shughuli zinakwama basi waelewe kwamba ni sababu zipi hasa za msingi ambazo zimesababisha hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Godfrey Zambi, naomba unionyeshe hizo takwimu unazitoa wapi.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazo ninaweza kukupatia kwa sababu ninazungumza vitu ambavyo nina hakika navyo.

**MWENYEKITI:** Hilo siyo suala, huwezi kunijibu hivyo, mimi nataka kujua takwimu unazitoa wapi unaniambia unazo mfukoni, zinatoka wapi? Kwenye kitu gani? Inaitwaje hiyo? *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni takwimu ambazo nimezipata ambazo ni bajeti ya Chuo Kikuu cha Mzumbe, zipo kwenye kitabu cha Mzumbe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba mimi naliwakilisha Bunge kwenye Bodi ya Mzumbe, kwenye Bodi iliyopita labda niseme hili suala liliwahi kuzungumzwa na Chuo kiliwahi pia kuomba kwa Waziri kwamba awaeleze hali hii

inatokana na nini, lakini Mheshimiwa Waziri na mimi kwa sababu nilimuuliza kwamba alieleze hakusemea lolote juu ya suala hili.

**MWENYEKITI:** Sasa hapo nimekuelewa, *source* ya *information* ni muhimu tunapojadili mambo haya.

**WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kufafanua hoja mbili alizozitoa Mheshimiwa Godfrey Zambi, kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa vyuo hivyo viwili alivyovitaja Chuo Kikuu cha Mzumbe na *Dar es Salaam Institute of Technology* kwa muda mrefu vyuo vikuu vimekuwa vikilalamika kwamba bajeti wanayoipata hailingani na mahitaji halisi ya kuendesha vyuo hivi, kukawa na taratibu mbalimbali lakini moja iliyokubalika kujaribiwa ni kitu kinachoitwa *student unit cost* na ikaamuliwa kwamba ili tuweze kujua matokeo ya *student unit cost* tuchague *Institutions* mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ambayo inafanya *Liberal Arts* na nyingine ambayo inafanya mambo ya Sayansi, kwa hiyo hawa walipewa fedha wakati ule na zikawa nyingi kuliko ile bajeti kulingana na idadi wanafunzi waliokuwa nao. Ule muda wa kujaribu umekwisha tarehe 30 Juni, 2006 sasa tunarudi kule tulikokuwa na tathmini ya matokeo yake ndiyo inafanywa sasa kwa hiyo, upungufu huo kwa kweli umetokana kwa sababu ya hiyo.

Lakini niongezee tu kwamba wala siyo hapo tu, mahali kwingi wamepata fedha pungufu zaidi ikiwa ni pamoja na Wizara yenyewe, mwaka jana *Operational Budget* ya Wizara ilikuwa ni shilingi bilioni 41.5, mwaka huu tumepata shilingi bilioni 37, *4.5 less* tumejaribu kuandika Hazina hatujafanikiwa kwa hiyo, asione kama ile ni sehemu tu ya Mzumbe ndiyo imeathirika zaidi bali ni vyuo vyote. *(Makofi)*

**MHE LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *Vote 68, Program 10, Sub Vote 100,* Kifungu kidogo 250100. Nilivyoandika mchango wangu kwa maandishi sikuzungumzia vitabu vichakavu nilikuwa na maana *Library* za vyuo viwe na vitabu *latest Edition* mfano mzuri tu ni kitabu cha *Organisation Behaviour* kule Ushirika sasa hivi kiko *17th Edition* lakini pale wanasoma *Second Edition.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri anielewe kwa hilo sikuwa na maana kitabu kichakavu.

Kingine nilichotaka kupata maelezo ni kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumza kwamba wanafunzi walikuwa wanapewa *pocket money* ya shilingi 2,500 baada ya utafiti wakaongezea ikawa 3,500. Sasa ina maana wanafunzi hao baada ya kutoa matumizi watabaki na shilingi 700, shilingi 700 inabidi watoe shilingi 500 kwa ajili ya malazi sasa wanabaki na shilingi 200.

Je, Mheshimiwa Waziri anaona shilingi 200 inaweza ikawatosha hao wanafunzi ukizingatia wanafunzi wa kiume na wa kike wana matumizi tofauti hapo hapo

Mheshimiwa Waziri anasema ile *shopping mall* inajengwa pale sasa sijui hao wanafunzi kwa hiyo, shilingi 200 hiyo *shopping mall* itakuwa na *special price* kwa wanafunzi? Tunaomba ufafanuzi.

Kitu kingine ni kwamba Mheshimiwa Waziri amesema kuhusu mabweni ya wanafunzi, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilipokea wanafunzi 15,349 mwaka 2005 na vitanda viko 7,800 kwa vyovyote vile wanafunzi wanakuwa *forced* ku-*share,* wanafunzi wanataka kulala wawili wawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwomba Mheshimiwa Waziri atueleze kuna mikakati gani ya kuhakikisha wanaongeza hosteli za wanafunzi? Tunaomba ufafanuzi. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ufafanuzi wa hayo matatu yaani vitabu siyo vichakavu ila vilipitwa na wakati ni vya zamani halafu na hii posho ya 3,500 na mabweni.

Moja tu nisaidie ni *common knowledge,* Mradi wa *Mlimani City* siyo maana yake kuwapatia wanafunzi sehemu ya kununua nyanya na vitunguu na kadhalika, mradi wa *Mlimani City* ni *Investment Program* ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, maana yake kuwezesha Chuo chetu Kikuu kiwe na miradi ya uwekezaji itakayoongeza nguvu sasa kwa Chuo chenyewe. Karibu Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ufafanuzi wa maswali matatu ya Mheshimiwa Lucy Owenya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vitabu kwa kawaida vyuo vyote vinajitahidi sana kuagiza vitabu ambavyo viko *up to date* na inawezekana kitabu kimoja tu katika *Library* kubwa yote ile angekuwa ameangalia na vitabu vingine lakini ameangalia kimoja tu. Lakini vile vile siku hizi *Library* katika hii dunia ya utandawazi *Library* haihitaji iwe kubwa, haihitaji vitabu vyote, kuna *internet,* unatafuta kwenye *internet.* Kwa hiyo, hiyo siyo sababu ya kufikiri kwamba hawa watu wako *out dated,* hapana bali wana njia nyingi.

Kuhusu *allowance* pengine nifafanue tu kwamba baada ya kufanya utafiti katika *cafeteria* mbalimbali Dar es Salaam gharama iliyoonekana halisi ilikuwa ni shilingi 3,050 siyo ile ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameitaja kwamba 2,800/= ni shilingi 3,050/= na hiyo ndiyo ilifikishwa katika sehemu mbalimbali katika majadiliano ni kwa ajili ya chakula na malazi. Lakini baada ya kufikiria kwamba huku mbele tunaweza tukapambana na *inflection* ikakubalika kuongeza mpaka shilingi 3,500/= na hiyo ndiyo iliyofanyiwa *Scientific Analysis* ikaonekana kwamba inatosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mabweni, vyuo vikuu vinaendelea kujitahidi kujenga mabweni yaani *hostel* kwa ajili ya wanafunzi lakini kusema kweli uwezo wa Serikali hautakuwa wa kasi sana kwa hilo. Tumekuwa tukitumia Taasisi za fedha nyingine kama *PPF* na nyingine na wengine mtakuwa mashahidi wa zile *hostel* zilizopo

Mabibo kule Dar es Salaam ambazo zina *host* wanafunzi wengi sana na hali kadhalika vyuo mbalimbali vinakwenda na jitihada hiyo hiyo ya kuanza kujenga mabweni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pengine nitumie nafasi hii kuwaomba wale Watanzania wenye uwezo kwenda kuwekeza katika ujenzi wa *hostels* katika ardhi za Vyuo Vikuu kwa mikataba maalumu kwa maana ya kwamba unajenga, unatumia na baadaye una - *transfer* kwa Chuo baada ya wewe ku-*recover* fedha zako. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbi, maswali yake yamejibiwa kwa hiyo, ameniandika hapa kwamba hana haja ya kuuliza.

Kwa hiyo Mheshimiwa Susan Lyimo, halafu tutamalizia na Mheshimiwa Grace Kiwelu. *(Makofi)*

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi niko katika *Vote 68 Program 10 Sub Vote 1001* Kifungu kidogo 250100, mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati natoa hoja zangu asubuhi ya leo nilieleza kwa masikitiko makubwa umuhimu wa *teaching practice* katika vyuo vyetu vya Elimu ya Juu hasa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mpaka sasa hivi wanafunzi wa mwaka wa kwanza na wa pili wako katika vituo vyao vya kufanyia *teaching practice* bila uratibu wa aina yoyote kwa sababu eti walimu hawajapatiwa fedha.

Sasa naomba Mheshimiwa Waziri aeleze ni lini walimu hao watapatiwa fedha hizo ili waweze kwenda kuwaratibu wanafunzi hao kwani madhara ya kutokuwa na uratibu kwa wanafunzi wale ni mkubwa ikiwa ni pamoja na kutokuhudhuria kwenye vipindi, lakini pia wanaweza wakafanya matatizo mengine katika shule hizo ili baadaye wakose nafasi hizo.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atuambie ni lini walimu wa Chuo Kikuu watapatiwa fedha za kwenda kuwa *assess* wanafunzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili nilikuwa naomba pia kuulizia kuhusu suala la *charter* ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Ni kwa nini Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimekuwa na *charters* mbili wakati ni chuo kimoja, kwa nini kuwe na *charter* na *charter* ya Utawala na *charter* shirikishi ambayo ina wadau kama wanafunzi na wafanyakazi, lakini pia nataka kujua ni sababu zipi zilizopelekea Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuajiri kampuni binafsi kufanya mchakato wa Makamu Mkuu wa Chuo wakati kuna maprofesa waliobobea ambao wangeweza kufanya shughuli hizo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi juu ya maswali madogo aliyouliza Mheshimiwa Susan Lyimo, kuhusu tatizo la walimu kutokwenda ku-*supervise* wanafunzi ambao wako kwenye *teaching practice.*

Mheshimiwa Spika, undani wake kusema kweli kwa sasa hivi hapa sina lakini niahidi kwamba tutalifuatilia tuone kuna matatizo gani, lakini moja ya tatizo ambalo linaweza kujitokeza kwa wakati kama huu na ambalo ningeweza kutoa ushauri kwa vyuo vikuu kwamba ni lazima tu-*singlenize academic semisters* wakati kama huu kama kuna wanafunzi wako masomoni hii ni *June - July* na ni mwisho wa *financial year.*

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kabisa wanaweza kupata matatizo ambapo fedha zinakuwa hazijatolewa bado, lakini sina hakika undani wake nasema tunaweza tukalifuatilia hilo. *(Makofi)*

Kuhusu *charter* nafikiri nilikwisha jibu nilipokuwa naeleza hapa mara ya kwanza kwamba taratibu za kutoa *charter* kwa kweli kimsingi ziko chini ya *management* ya chuo na *management* ya chuo inapitia katika vyombo vyake halali pamoja na ushirikishaji halafu ndiyo vinapelekwa kwenye *council* na nimesema haya yalijitokeza na baadaye *council* ikaamu kwa sababu kulikuwa na *charter* mbili ikaamua iunde kamati maalum ili kusudi ipitie maoni ya hizo *charter* mbili na hatimaye ifikishe kwenye Baraza la Chuo mwezi Septemba. *Deadline* ya kila chuo kuwa kime- *develop charter* yake ni mwishoni mwa mwezi Desemba, 2006. Ninaamini hili litafanyika.

Kuhusu mchakato wa kumpata *Vice Chancellor,* mimi naona kidogo kama tunaingia ndani kwa sababu kila chuo kina utaratibu chini ya sheria hii tuliyonayo namba 7 ya mwaka 2005 inaeleza taratibu watakazozitumia unakuwa na *search committee* na wanatangaza vile vile watu wanaomba halafu kwenye *search committee* kule kunakuwa na *interviews* halafu hatimaye ndiyo wanatoa mapendekezo kwa Mwenyekiti wa Baraza ambaye hatimaye wakishakubaliana kwenye Baraza wanapendekeza kwa *chancellor* ambaye yeye ndiye hatimaye anatoa uteuzi. Sasa kama kungekuwa na matatizo hapo katikati nafikiri *is the learning process* kwa sababu katika vyuo vingine wamefanikiwa kufanya hivyo bila kuwa na matatizo yoyote. Nina imani hata hili litatekelezeka. *(Makofi)*

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini pia nilikuwa nataka kupata ufafanuzi kwa suala dogo. Kwa sababu Mheshimiwa Waziri amesema kwamba suala la fedha za Wahadhiri hao bado hazijapatikana na kwa kuwa wanafunzi walioko kule wanakaa kwa wiki sita na sasa hivi ni wiki ya tatu imeisha na wanafunzi wale kama hawatatathminiwa ina maana kwamba itabidi warudie zoezi hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri, gharama hizo zitalipwa na Serikali au ni watu gani? Kwa sababu wanafunzi wale itabidi tu kwa vyovyote wafanye tena *practical training* kwa sababu hawajafanya na hiyo ndiyo *requirement* ya ku-*graduate.*

**WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ningependa kusahihisha kidogo jibu la Mheshimiwa Mbunge. Mimi sikusema kwamba fedha hakuna. Nilisema sielewi undani wa tatizo na napenda kurudia hivyo. Lakini nikasema inawezekana *timing* ya kufanya hayo mafunzo kwa

vitendo imekuja wakati ambapo Chuo hakina fedha. Kwa hiyo, sikusema hilo ambalo Mheshimiwa Mbunge amelitamka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pamoja na hilo lingine ambalo ameliuliza nafikiri bila kuwa na uhakika wa hali yenyewe kamili, itakuwa ni vigumu mimi kueleza nini kinatakiwa kufanyika baada ya hapo. *(Makofi)*

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Niko kwenye *Vote 68, Programme 10, sub-vote 1001,* kifungu kidogo 250100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maoni ya Kambi ya Upinzani yaliyotolewa asubuhi kuna mambo ambayo tulikuwa tunataka kupatiwa majibu hasa katika mikopo. Yapo mambo yaliyojibiwa na mengine bado inawezekana kutokana na muda, lakini kupitia vifungu tunamwomba Mheshimiwa Waziri, atupatie majibu.

La kwanza tulitaka kujua ni kiasi gani cha fedha zilizokwenda kwa waombaji ambao walikuwa hawana sifa, waliomba mikopo hiyo kupitia Vyuo ambavyo walikuwa hawamo na ni wangapi walipata mikopo hiyo mara mbili? Naomba majibu.

**WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa ufafanuzi kwa Mheshimiwa Grace Kiwelu, juu ya maswali yake mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hapa itakuwa vigumu sana kuweza kutoa idadi ya wale waliodanganya, kwa sababu mambo haya yanakuja kudhihirika baadaye. Kwa hapa siwezi kuwa na *data* ambazo ni *up right*. Hivyo hivyo, kwa wale waliopata mikopo mara mbili sina takwimu kamili za kuweza kumpa. Lakini tukizipata tutahakikisha kwamba tunampelekea Mheshimiwa Grace Kiwelu kwa ajili ya taarifa yake. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitisha na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts ... ... ...150, 452,000/=*
Kifungu 1003 - *Policy and Planning … … … 577,165,800/=*
Kifungu 2001 - *UNESCO Commission* … … ... ... 322,005,700/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo hapo vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 3001 - *Higher Education ... ... ... 150,947,659,500/=*

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nataka nisahihishe, wakati nikichangia nilipokuwa napeleka mahesabu ya mkopo au gharama za ujenzi wa *Institute of Marine Science* nilisema kwamba 8 x 5 = 48 nikasema kwamba ni bilioni 4, lakini usahihi wake ni kwamba 8 x 5 ni bilioni 4 kwa milioni 40. Baada ya masahihisho hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia *Vote 68, Programme 30, sub-vote 3001,* kifungu kidogo 260800 - *Training Expenses*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia hoja hii nilitaka Mheshimiwa Waziri anifafanulie kuhusu lile suala la *quota system* kuhusu wanafunzi kutoka Zanzibar ambapo ilizungumzwa kwamba utaratibu huo ulikuwa upo na ukafa kidogo kidogo mpaka ikafikia hatua kwamba hakuna. Sasa mbali ya kwamba katika maelezo yake hapo nyuma alipokuwa akijibu swali hapa Bungeni alisema kwamba kulikuwa na baadhi ya wanafunzi ambao hupendelea kusoma katika Vyuo vilivyokuwa karibu nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Tanzania Bara kuna vyuo vingi nadhani vile vile Wazanzibar wangependa kuongeza taaluma yao kuja Tanzania Bara. Kwa hiyo, ningemwomba Mheshimiwa Waziri anipe maelezo. Je, suala hili litazingatiwa au litafikia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa ufafanuzi kuhusiana na swali la Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge anazungumzia suala la kuwa na idadi maalum ya wanafunzi kutoka Tanzania Zanzibar kujiunga na Vyuo Vikuu vya Tanzania Bara. Lakini kabla sijatoa maelezo ningependa kusahihisha na pengine tuhitaji ushahidi. Kwa bahati nzuri mimi nimekuwa *Membe*r wa *University of Senate* ya *University of Dar es Salaam* kwa muda mrefu, lakini vile vile nimekuwa kwenye *Admission Committees*. Nimekuwa kwenye *Joint Admission Board* ambayo inaunganisha vyuo vyote, hata siku moja sijawahi kusikia jambo hili la *quota system,* halikuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo baada ya Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji kuzungumzia hili nimekwenda kucheki. Profesa Luhanga ambaye ni *Vice Chancellor of University of Dar es Salaam* na yupo *Chief Administrative Officer* wako hapa na walimu wengine wote wamethibitisha kwamba jambo hili halijawahi kutokea. Kwa hiyo, nafikiri halipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa kuwa linazidi kuulizwa kila wakati sielewi muafaka wake utafikia wapi? Lakini kwenye elimu kwa kweli ukianza kusema *quota system*. Kwa sababu leo hii baada ya Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji kuzungumzia hili, amekuja Mheshimiwa Esther Nyawazwa akaomba wapewe *quota* kwa ajili ya Mikoa ya Shinyanga na Mwanza. Sasa tukiendelee namna hii tutafika wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri kupata nafasi katika elimu ya juu tuendelee kutumia utaratibu uliopo ambao ni *competitive* ya ushindani ndiyo tuweze kupata vijana wazuri zaidi. *(Makofi)*

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nataka kupata maelezo machache tu. Kwanza kabisa wakati nachangia hoja hii asubuhi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nimrod Mkono kifungu gani?

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote 68, programme 30, sub-vote 3001,* kifungu kidogo cha 250100 mshahara wa Waziri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, mshahara wa Waziri haupo hapo. *(Kicheko)*

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani kidogo. Nasema kifungu ni hicho hicho, lakini nataka kupata ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, bado nataka useme ni kifungu gani? Wenzako walizungumzia kwenye Mshahara wa Waziri wakamaliza. Wewe umesubiri sasa tuko kwenye *Higher and Technical Education.* Sasa unasemaje hapo?

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 280500.

**MWENYEKITI:** *Transfer and Subsidy - Institute at the same Level of Government*.

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** *Okay,* sawa.

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi cha fedha kilichotengwa hapo kinaonekana kuwa ni shilingi 146,744,617,700. Nataka kupata ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kwamba kiasi hicho sasa hakitakuwa na ubaguzi ule wa zamani. Nataka kupata ufafanuzi tu kwamba watakaopewa mikopo ya hizo fedha utakuwa ni chini ya utaratibu tulionao mpaka leo, hadi hapo sheria mpya itakapokuja mwezi Oktoba, 2006. Nataka kujua tu kama nimempata vizuri Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Labda Mheshimiwa Waziri arudie tu, lakini ndivyo alivyosema katika ufafanuzi tena mrefu kabisa. Mheshimiwa Waziri rudia tu kwa faida ya Mheshimiwa Nimrod Mkono. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ufafanuzi kwanza kwamba hiki kifungu kinahusu ni nini. Hiki kifungu 280500 - *Transfer and Subsidy - Institute at the same level of Government*,

hiki ni kifungu kinachohusu *OCs* za Vyuo Vikuu vyote, kinahusu mishahara ya Walimu wa Vyuo Vikuu pamoja na wafanyakazi wengine.

Mheshimiwa Spika, kifungu hiki vile vile kinajumuisha Mamlaka ya Elimu Tanzania na kifungu hiki kinahusu mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema utoaji wa mikopo utazingatia ushindani wa kitaaluma na haubagui. *(Makofi)*

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sheria hii ya *Higher Education Students Loans* imetoa *criterion* ya kutoa mikopo chini ya kifungu cha 16 na 17 na kwamba Bodi inapotoa mikopo hiyo ina *obligation* na ikishindwa kufanya hivyo inaweza kushitakiwa chini ya Sheria hii.

Suala langu ni hivi, kwa kuwa pia Mheshimiwa Waziri anayo mamlaka ya kufanya *regulations* ambayo inaweza kusema sasa ni *competition* na hizo *regulations* hazijatokea. Je, haitakuwa jambo la hatari sana kuweza kutoa mikopo kwa hisia tu kwamba sheria inayokuja mwezi Oktoba, 2006 itarekebisha jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, hao wanafunzi wanaoomba sasa mikopo watumie sheria hii kama ilivyo ama wangojee mpaka mwezi Oktoba, 2006. Nataka kupata ufafanuzi tu.

**MWENYEKITI:** Lakini Mheshimiwa Nimrod Mkono kwanza hujasema kama wewe ndiye Mwenyekiti wa Bodi ya Mikopo. Ni vizuri Waheshimiwa Wabunge wote waelewa hivyo au umekwishatolewa?

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Suala langu hili nililizungumza asubuhi ambapo nili-*declare my interest.* Mimi ni Mwenyekiti wa Bodi ya Mikopo, kwa hiyo, na-*declare interest* na asubuhi nilisema hivyo, nazidi pia ku-*declare interest* yangu. Nataka kupata ufafanuzi tu.

Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kutoa huo ufafanuzi wa kwanza kwamba kuna sheria inakuja mwezi Oktoba, 2006 ambayo imeniridhisha na kutoa wasiwasi wangu niliokuwa nayo asubuhi ya leo, hiyo nimeisema. Lakini sasa swali langu ni hivi *pending* ya hiyo sheria kuja. Je, Bodi itumie mwongozo upi? Maana yake ya leo ni *horror* hauko kwenye *regulation,* unapingana na sheria hii iliyopo. Je, mpaka hapo sheria itakapokuja tutumie sheria gani kwenye Bodi ya Mikopo?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpongeza Mheshimwia Nimrod Mkono kwa kushinda ile kesi ya *City Water,* nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kisha-*declare interest,* tunajua ndiye Mwenyekiti wa Bodi ya Mikopo. Mheshimiwa Waziri amefafanua kabisa utaratibu huu wa mikopo. Maelezo mengine anayotaka ni *administrative,* atakwenda ofisini kwa Waziri wake atampa maelekezo ya nini cha kufanya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nina hakika hata mimi nilielewa kwamba utaratibu uliopo haukwamishi utoaji mikopo. Ndiyo maana sasa tuharakishe hapa kupitisha hizi fedha ili vijana wetu waweze kupata mikopo yao. *(Makofi)*

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi nipo kwenye *Vote 68, programme 30, sub-vote 3001,* kifungu kidogo 260800. Nafikiri mimi sitakuwa na mbali na Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji. Lakini nahitaji kupata ufafanuzi zaidi. Kwa kweli elimu ni mwanga na ni nyenzo ya maendeleo katika jamii yoyote ile au katika nchi yoyote. Ikikosekana elimu hakuna maendeleo. Nimesema *sub-vote 3001,* kifungu kidogo cha 260800 - *Training Expenses*. Elimu ni mwanga na nyenzo ya maendeleo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge nakuomba uende kwenye hoja. Hapa unatafuta kupata ufafanuzi. Hutuchangii mada katika hatua hii, ni kutafuta kupata maelezo na ufafanuzi. *(Makofi)*

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Namshukuru Mwenyezi Mungu jana nilitimiza kuwa na umri wa miaka 59. Kwa *best of my knowledge* nakumbuka hii *quota system* ilikuwepo huko nyuma. Lakini *quota system or otherwise* tunataka maendeleo ya Zanzibar. Elimu ya Juu ni chombo cha Muungano na bila ya maendeleo kuwa sawia upande huu na upande huu ni kero moja hiyo. *Quota system or otherwise,* tunaangalia kwamba kuna udahili zaidi kwa wanafunzi wa Zanzibar mtaupataje? Ikiwa haiwezekani kwa sababu za kihistoria au za mvutano wa kisiasa, *marks* zao kidogo hazifiki sawasawa, kwani wanafunzi wasichana mnawachukuaje? Si kuna *mechanism* ya kuweza kuwachukua na baadaye wanakuja ku-*perform* vizuri zaidi hata kushinda wanaume, iko *syste*m hiyo. Kwa nini hatuwezi kufanya *system* hiyo kwa Wazanzibari? *That is one*. *(Makofi)*

La pili, kuongeza idadi ya walimu katika Vyuo Vikuu. Tumeambiwa watafundishwa vijana wetu zaidi ili baadaye waje wachukue nafasi zile. Kweli tutawafundisha. Lakini *the other problem is to retain them* kuweza kuwashikilia wabakie hapa nchini, ku-*retain them*. Ikiwa hakuna maslahi bora kwa walimu ni bure.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, hili la pili, naomba sasa utulie, kwa sababu sasa unaanza kuzungumza hoja. Hili la *quota system,* mimi ningependekeza Mheshimiwa Waziri Mkuu katika yale majadiliano wanayokuwa nayo na Mheshimiwa Kiongozi wa Zanzibar hebu jaribu kuliangalia hilo, maana yake Waziri amekwisha kujibu kwa ukomo wake kwa sera ilivyo sasa. Kwa sababu wenzetu kutoka Zanzibar inaelekea lina kero, lina historia na lina hivi. Kwa nini basi Mheshimiwa Waziri Mkuu lisiingie katika mjadala huo hata kama halitaitwa *quota system*. Lakini ni namna fulani ya kuwezesha labda wanafunzi wengi wa kutoka Zanzibar waweze kupatikana, nadhani ndiyo lengo. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwa umetabasamu nadhani umekubali. *(Kicheko)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani maelezo ya Mheshimiwa Waziri yanatosha kwamba tusigawe nchi katika masuala ya Elimu ya Juu kwa utaratibu wa *quota system* haitatusaidia.Ukitaka upendeleo maalum kwenye Elimu ya Juu utapata watu ambao kwa kweli hawafai kupata *degree* hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nasema bado sisi ni maoni yetu kwamba maelezo ya Mheshimiwa Waziri ni sahihi na kwa sasa hivi huo ndiyo msimamo wa Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, nakupa nafasi ya mwisho.

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli huo ndio msimamo wa Serikali. Lakini wakati tunazungumzia maendeleo ya wananchi ni lazima tuangalie kwa macho mawili kwa sababu kwa njia tunayokwenda tutainyonga Zanzibar kukosa viongozi wa kesho na wataalamu wa kesho. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, hoja yako inakuwaje sasa? Hebu kaa kwanza. Inaelekea wewe ni mtaalam wa *quota system*. Hebu uelezeni umma wa Watanzania uielewe. *Quota* maana yake nini? Maana yake ni kuchukua mtu yeyote tu, unafanyaje hiyo. *(Kicheko)*

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi si mtaalam wa *quota system.* Lakini nasema tuwe na *mechanism* aidha, *it is quota system or otherwise*. Tuangalie kwamba kuna udahili zaidi wa wanafunzi kutoka Zanzibar, kwani wanafunzi wa kike tunawachukuaje? Si iko *mechanism* ya kuwachukua wanakuwa hawana kile kiwango cha *marks* ambacho kinahitajika, lakini mnawachukua.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani msimamo umeishatolewa na Serikali. Tutaendelea kujadiliana.

*(Kifungu kilichotajwa hapo hapo kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 3002 - *Technical Education ... ... 10,492,655,300/=*
Kifungu 3003 - *Science and Technology ... ... 2,485,335,900/=*

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

Kifungu 1001 - *Administration and General ... ... 63,000,000/=*
Kifungu 1003 - *Policy and Planning ... ... 4,300,000,000/=*

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 3001 - *Higher Education… … … … 30,835,945,000/=*

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi tena katika kuchangia suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia *Vote 68, sub-vote 3001 - Higher Education,* kifungu kidogo cha 2225 kuhusu *Institute of Marine Science.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia hoja nilitaka nielezwe ni namna gani uendelezaji wa Chuo hii cha *Marine Science* kilichoko Zanzibar ambacho mpaka sasa hivi mkandarasi yuko kwenye *site* na hajalipwa. Kwa mujibu wa *Vote* hii ni kwamba safari hii kimetengewa shilingi milioni 800 na nikasema kwamba shilingi milioni 800 ikiwa kama zitalipwa kila mwaka mkandarasi huyu atafika shilingi bilioni 4 na gharama za ujenzi wa Chuo ni zaidi ya shilingi bilioni tano. Sasa nataka kupata ufafanuzi, je, Mheshimiwa Waziri ili kufanikisha ujenzi huu anatwambia nini kuhusu upatikanaji wa fedha hizo ili kufanikisha ujenzi wa Chuo hicho? Ahsante sana.

**WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ufafanuzi kwa Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, juu ya kifungu hicho 2225. Ujenzi wa *Institute of Marine Science.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kazi imekuwa ni ya muda mrefu. Kulijitokeza matatizo mengi kwanza kwa upatikanaji wa kiwanja kilikuwa Unguja Kaskazini baadaye kikaja kupatikana mahali pengine na hatimaye mwaka jana kwa mategemeo ya kupata fedha zilizokuwa zimetengwa zilikuwa shilingi milioni 400. Mkandarasi alipewa akaanza kujenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya hizo fedha hazikuweza kupatikana. Pamoja na kufuatilia Hazina na siyo hizo tu, kulikuwa na fedha zingine jumla kwa Wizara tu peke yake ilikuwa bilioni 5.2. Baadhi ya Vyuo vingine ambavyo navyo ujenzi wao uliathirika ni pamoja na Mzumbe, *SUA, University of Dar es Salaam* na sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka huu na kwa kuona umuhimu huo na baada ya kuzungumza na Waziri wa Fedha, katika hizi shilingi milioni 800 ambazo zimetengwa, tayari shilingi milioni 400 zimeshapelekwa ili kusudi kazi iweze kuendelea. Sasa kwa kushirikiana na uongozi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam tutajitahidi kuweza kutafuta fedha nyingine. Lakini hakuna uhakika wa kusema fedha hizo zitapatikana hivi karibuni. Tumeandika miradi kwa ajili ya upanuzi wa Vyuo Vikuu na iwapo tutafanikiwa, basi nafikiri kwamba sehemu ya fedha hizo zinaweza kwenda kwenye hicho chuo cha *Marine Science* Zanzibar. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, *Sub-vote 3001- Higher Education.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge hujamaliza. Kifungu kidogo kipi, siyo *sub-vote,* ni suala lipi, inaendelea mpaka ukurasa 112.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nimetaja kifungu chote.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, haiwezi kuwa fungu lote. Jamani msaidieni Mwenyekiti wakati wa Kamati ya Matumizi, taratibu zinajulikana. Mheshimiwa Mbunge, lazima kuna suala mahsusi ambalo unataka kuuliza, haiwezekani unataka tu *Higher Education* kama sera. *(Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kuuliza hakikuorodheshwa hapa, lakini inahusu fedha ambazo zitatumika kukijenga Chuo Kikuu cha Dodoma. Sasa kama kitajengwa mbona fedha zake hazimo katika orodha ya *University* zote ambazo ziko chini ya *Higher Education*. Hilo ndilo swali langu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, nimelielewa swali lako, ni vizuri tu Mheshimiwa Waziri alifafanue. Ni swali lingine juu ya hili.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali juu ya hilo ni kwamba hakuna fedha iliyowekwa hapa itayotumika kuanza kukijenga hicho Chuo Kikuu cha Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa kuwa hicho Chuo Kikuu cha Dodoma inaonekana kuna maneno mengi yatazungumzwa hapa. Chuo labda kitaitwa jina la Mheshimiwa Rais wa Kwanza vitu kama hivyo. Yeye aliamini mambo ya elimu bila kulipia, bila mikopo. Je, hicho Chuo pia pamoja na matatizo tuliyoelezwa na chenyewe kitafuata utaratibu wa mikopo?

**MWENYEKITI:** Hili la pili, siliruhusu kwa sababu ni kabla ya wakati wake kabisa. Mheshimwa Waziri toa ufafanuzi katika hilo la kwanza tu, fedha za kujenga Chuo Kikuu Dodoma zinaonyeshwa wapi?

**WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kufafanua swali alilouliza Mheshimiwa John Cheyo, juu ya fedha za ujenzi wa Chuo Kikuu hapa Dodoma ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo la kujenga Chuo Kikuu hapa Dodoma lilikuwa katika Ilani ya Uchaguzi mwaka 2005 na katika kuanza kufanya kazi hizi fedha maalum kwa ajili ya ujenzi hazikuwa zimetengwa. Lakini kulikuweko na *funds* ambazo zilitafutwa kwa ajili ya kazi za awali kwa mfano kufanya upembuzi yakinifu ambao unaendelea mpaka sasa. Lakini hauko kwenye bajeti ya huu mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyoelewa kwamba jitihada zinafanywa kupata wahisani kusaidia ujenzi wa Chuo hiki. Lakini mpaka sasa hizo fedha hazijapatikana

pamoja na kwamba wahisani karibu wawili wameonyesha dalili za kuchangia katika ujenzi huo. Lakini itawekwa katika bajeti ya Wizara kuanzia mwaka huu.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako Tukufu ndilo linaloidhinisha matumizi yote ya Serikali na hili sio jambo jipya, limo ndani ya hotuba ya Waziri. Leo itakuwaje Waziri atuambie kuna fedha baadaye itapatikana, itapatikana kutoka wapi na kwa ruhusa ya nani? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninavyoelewa Waziri ameteleza tu kidogo. Ndiyo! Matumizi kama haya kwa kawaida huanzia wazo lenyewe kulijenga, kutafuta wataalam na kadhalika yanakuwa katika kitabu cha pili ambacho tayari tumekipitisha.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 3002 - *Technical Education ... ... ... ...4,000,000,000/=*
Kifungu 3003 - *Science and Technology ... ... ..3,050,000,000/=*

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitisha Bajeti ya Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia fungu namba 68 ya mwaka 2006/2007 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila ya mabadiliko yoyote

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu sasa liyakubali Makadirio hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, kwa mwaka 2006/2007 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Matangazo tu, naomba kukumbusha kwamba kesho saa 3.00 asubuhi ni Semina kwa Wabunge wote kuhusu Utekelezaji wa Programu ya Maji Vijijini.

Kwa hiyo, pamoja na kuwa saa 12.00 jioni itakuwa ni mashindano ya mbio za Wabunge kulingana na umri wao. Nawatakia kila kheri wote muweze kufanya vizuri ili tuweze kuhudhuria katika semina ambayo itafanyika katika ukumbi wetu wa zamani, saa 3.00 asubuhi.

Mbio ni saa 12.00 asubuhi. Kila kitu kimepangwa vizuri tu. Mbio ni saa 12.00 asubuhi Mgeni rasmi ni Mheshimiwa Waziri Mkuu atapokea wakimbiaji saa 1.00 asubuhi pale mahali petu pa kawaida. Halafu saa 3.00 asubuhi ndiyo Semina ya Wizara ya Maji kuhusu Utekelezaji wa Programu ya Maji Vijijini.

Sasa Jumapili saa 5.00 asubuhi ni Semina ya Shughuli ya Mafanikio na Matatizo ya Tume ya Haki za Binadamu Tanzania. Hii nayo ni Semina muhimu sana ambayo ni vizuri Waheshimiwa Wabunge tukahudhuria ili tuweze kujifunza maendeleo ya nchi katika eneo hili la Haki za Binadamu. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo na kwa kuwa muda uliosalia hautoshi kuendelea na wala hakuna shughuli zozote. Orodha ya shughuli za leo zimekwisha kabla ya muda wake. Kwa hiyo, naliahirisha Bunge hadi Jumatatu ijayo, saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 01.39 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatatu,*
*Tarehe 24 Julai, 2006 saa tatu asubuhi)*